JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TUME YA MABADILIKO YA KATIBA



Trial Version
www.nuance.com

BANGO KITITA LA RANDAMA YA RASIMU YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

FRBRUARY, 2014

YALIYOMO

YALIYOMO i

UTANGULIZI WA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO i

SURA YA 1 - JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA 1

SEHEMU YA KWANZA - JINA, MIPAKA, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA 1

Ibara ya 1: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1

Ibara ya 2: Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 9

Ibara ya 3: Alama za Sikukuu za Taifa 18

Ibara ya 4: Lugha ya Taifa na Lugha za Alama 19

Ibara ya 5: Tunu za Taifa. 22

SEHEMU YA PILI - MAMLAKA YA WANANCHI, UTII NA HIFADHI YA KATIBA .. 23

Ibara ya 6: Mamlaka ya Wananchi, Utii na Hifadhi ya Katiba 23

Ibara ya 7: Watu na Serikali 25

Ibara ya 8: Ukuu na Utii wa Katiba 28

SURA YA PILI 31

MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWELEKEO WA 31

SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA 31

Ibara ya 10: Malengo Makuu 31

Ibara ya 11: Utekelezaji wa Malengo ya Taifa. 44

Ibara ya 12: Sera ya Mambo ya Nje. 46

Trial Version
www.nuance.com

SURA YA TATU 48
SEHEMU YA KWANZA – MAADILI YA UONGOZI NA WATUMISHI WA UMMA ... 48
Ibara ya 13: Dhamana ya Uongozi wa Umma. 48
Ibara ya 14: Kanuni za Uongozi wa Umma. 51
Ibara ya 15: Zawadi katika Utumishi wa Umma. 53
Ibara ya 16: Akaunti nje ya nchi na Mkopo. 55
Ibara ya 17: Wajibu wa kutangaza Mali na Madeni. 56
Ibara ya 18: Mgongano wa Maslahi. 58
Ibara ya 19: Matumizi ya Mali ya Umma. 60
Ibara ya 20: Utekelezaji wa Masharti ya Maadili. 61
SEHEMU YA PILI - MIIKO YA UONGOZI WA UMMA 62
Ibara ya 21: Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma. 62
Ibara ya 22: Marufuku ya baadhi ya Vitendo. 68
SURA YA NNE 70
SEHEMU YA KWANZA – HAKI ZA BINADAMU 70
Ibara ya 23: Uhuru, Utu na Usawa Binadamu. 70
Ibara ya 24: Haki ya Kuwa hai. 71
Ibara ya 25: Marufuku Kuhusu Ubaguzi. 72
Ibara ya 26: Haki ya kutokuwa Mtumwa. 77
Ibara ya 27: Uhuru wa Mtu binafsi. 78
Ibara ya 28: Haki ya Faragha na Usalama wa Mtu. 79

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 29: Uhuru wa Mtu kwenda anakotaka. 80
Ibara ya 30: Uhuru wa Maoni. 82
Ibara ya 31: Uhuru wa Habari na Vyombo vya Habari. 85
Ibara ya 32: Uhuru wa Imani ya Dini. 87
Ibara ya 33: Uhuru wa Mtu kujumuika na kushirikiana na Wengine. 89
Ibara ya 34: Uhuru wa kushiriki shughuli za Umma. 90
Ibara ya 35: Haki ya kufanya kazi. 91
Ibara ya 36: Haki za Wafanyakazi na Waajiri. 91
Ibara ya 37: Haki ya Kumiliki Mali. 93
Ibara ya 38: Haki ya Uraia. 94
Ibara ya 39: Haki ya Mtuhumiwa na Mfungwa. 94
Ibara ya 40: Haki ya Watu walio chini ya Ulinzi. 97
Ibara ya 41: Uhuru na Haki ya Mazingira safi na Salama. 98
Ibara ya 42: Haki ya Elimu na Kujifunza. 100
Ibara ya 43: Haki ya Mtoto. 101
Ibara ya 44: Haki ya Wajibu wa Vijana. 104
Ibara ya 45: Haki za Watu wenye Ulemavu. 105
Ibara ya 46: Haki za Makundi Madogo katika Jamii. 107
Ibara ya 47: Haki za Wanawake. 109
Ibara ya 48: Haki za Wazee. 111

Trial Version
www.nuance.com

SEHEMU YA PILI - WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI NA MIPAKA YA HAKI ZA BINADAMU 112

Ibara ya 49: Wajibu wa Raia. 112

Ibara ya 50: Wajibu wa Kushiriki Kazi 113

Ibara ya 51: Ulinzi wa Mali ya Umma. 116

Ibara ya 52: Haki ya Wajibu Muhimu 117

Ibara ya 53: Hifadhi ya Haki za Binadamu. 119

Ibara ya 54: Usimamizi wa Haki za Binadamu. 120

Ibara ya 55: Mipaka ya Haki za Binadamu. 122

SURA YA TANO 124

URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO 124

Ibara ya 56: Uraia wa Jamhuri ya Muungano. 124

Ibara ya 57: Uraia wa Kuzaliwa. 126

Ibara ya 58: Uraia wa Kuandikishwa 128

Ibara ya 59: Hadhi ya Watu wenye Asili au Nasaba na Tanzania 130

SURA YA SITA 134

MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO 134

Ibara ya 60: Muundo wa Muungano. ..... **Error! Bookmark not defined.**

Ibara ya 61: Vyombo vya Utendaji vya Jamhuri ya Muungano. 157

Ibara ya 62: Mamlaka ya Serikali ya Muungano. 158

Ibara ya 63: Mambo ya Muungano 160

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 64: Nchi Washirika.....163
Ibara ya 65: Mamlaka ya Nchi Washirika. 164
Ibara ya 66: Mahusiano kati ya Nchi Washirika. 168
Ibara ya 67: Mawaziri Wakaazi. 170
Ibara ya 68: Mamlaka ya Wananchi. 171
Ibara ya 69: Wajibu wa Kulinda Muungano.....173
SURA YA SABA 175
SEHEMU YA KWANZA - SERIKALI, RAIS, MAKAMU WA RAIS NA BARAZA LA MAWAZIRI..... 175
Ibara ya 70: Serikali ya Jamhuri ya Muungano 175
Ibara ya 71: Rais wa Jamhuri ya Muungano.....178
Ibara ya 72: Madaraka na majukumu ya Rais.....179
Ibara ya 73: Utekelezaji wa madaraka ya Rais. 186
Ibara ya 74: Rais kuzingatia ushauri. 190
Ibara ya 75: Rais kushindwa kumudu majukumu yake. 191
Ibara ya 76: Utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla ya kumaliza muda wake. 193
Ibara ya 77: Utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo. 195
Ibara ya 78: Uchaguzi wa Rais.....198
Ibara ya 79: Sifa za Rais. 199
Ibara ya 80: Utaratibu wa uchaguzi wa Rais. 203
Ibara ya 81: Malalamiko kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Rais. 206

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 82: Kiapo cha Rais na muda wa kushika Madaraka. 209
Ibara ya 83: Haki ya kuchaguliwa tena. 210
Ibara ya 84: Madaraka ya kutangaza vita. 212
Ibara ya 85: Madaraka ya Raia kutangaza hali ya hatari. 214
Ibara ya 86: Mamlaka ya kutoa msamaha. 219
Ibara ya 87: Kinga ya Mashtaka dhidi ya Rais. 221
Ibara ya 88: Bunge Kumshtaki Rais. 223
Ibara ya 89: Maslahi ya Rais. 232
Ibara ya 90: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano. 233
Ibara ya 91: Upatikanaji wa Makamu wa Rais. 234
Ibara ya 92: Sifa za Makamu wa Rais. 235
Ibara ya 93: Kiapo cha Makamu wa Rais. 237
Ibara ya 94: Wakati wa Makamu wa Rais kushika Madaraka. 238
Ibara ya 95: Bunge kumshtaki Makamu wa Rais. 239
Ibara ya 96: Upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi 242

SEHEMU YA PILI - BARAZA LA MAWAZIRI LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO 243

Ibara ya 97: Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri. 243
Ibara ya 98: Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri. 244
Ibara ya 99: Waziri Mwandamizi. 246
Ibara ya 100: Kazi na Mamlaka ya Waziri Mwandamizi 247

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 101: Sifa za Mawaziri na Naibu Mawaziri. 248
Ibara ya 102: Kiapo, Muda na Masharti ya Kazi ya Waziri na Naibu Mawaziri. 250
Ibara ya 103: Utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni. 251
Ibara ya 104: Mwanasheria Mkuu wa Serikali. 253
Ibara ya 105: Katibu Mkuu Kiongozi 257
Ibara ya 106: Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu. 260
Ibara ya 107: Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu 262
Ibara ya 108: Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri 263
SURA YA NANE 264
UHUSIANO NA URATIBU WA SERIKALI 264
Ibara ya 109: Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali. 264
Ibara ya 110: Malengo ya Tume. 266
Ibara ya 111: Majukumu ya Tume. 268
Ibara ya 112: Sekretarieti ya Tume. 271
SURA YA TISA 273
BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO 273
SEHEMU YA KWANZA..... 273
KUUNDWA NA MADARAKA YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO 273
Ibara ya 113: Kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano. 273
Ibara ya 114: Muda wa Bunge. 275
Ibara ya 115: Madaraka ya Bunge. 276

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 116: Mipaka ya Bunge katika kutumia madaraka yake. 279
Ibara ya 117: Madaraka ya Bunge Kutunga Sheria. 280
Ibara ya 118: Utaratibu wa Kubadilisha Katiba. 282
Ibara ya 119: Utaratibu wa Kubadilisha Masharti mahsusi. 283
Ibara ya 120: Utaratibu wa Kutunga Sheria. 284
Ibara ya 121: Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu mambo ya Fedha. 286
Ibara ya 122: Madaraka ya Mkuu wa Nchi Kuhusu Muswada wa Sheria. 290
Ibara ya 123: Kupitishwa Kwa Hoja za Serikali. 293
SEHEMU YA PILI - WABUNGE 294
Ibara ya 124: Uchaguzi wa Wabunge. 294
Ibara ya 125: Sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge. 296
Ibara ya 126: Utaratibu wa Uchaguzi wa Bunge. 306
Ibara ya 127: Kiapo na Masharti ya Kazi ya Bunge. 306
Ibara ya 128: Kupoteza Sifa za Ubunge. 308
Ibara ya 129: Haki ya wapiga kura kumwajibisha Mbunge. 311
Ibara ya 130: Uamuzi wa Suala kama Mtu ni Mbunge. 313
Ibara ya 131: Tamko Rasmi la Wabunge kuhusu Maadili ya Uongozi. 314
SEHEMU YA TATU - UONGOZI WA BUNGE 315
Ibara ya 132: Spika na Mamlaka ya Spika. 315
Ibara ya 133: Ukomo wa Spika. 317
Ibara ya 134: Naibu Spika. 319

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 135: Sifa za Mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika. 321
Ibara ya 136: Utaratibu wa Uchaguzi na Kiapo cha Spika na Naibu Spika. 323
Ibara ya 137: Katibu wa Bunge.....325
Ibara ya 138: Sekretarieti ya Bunge. 326
SEHEMU YA NNE - UTARATIBU WA SHUGHULI ZA BUNGE 327
Ibara ya 139: Kanuni za Kudumu za Bunge.....327
Ibara ya 140: Rais kulihutubia Bunge. 327
Ibara ya 141: Mikutano ya Bunge. 328
Ibara ya 142: Uongozi na Vikao vya Bunge. 329
Ibara ya 143: Akidi ya Vikao vya Bunge. 330
Ibara ya 144: Kamati za Bunge. 330
SEHEMU YA TANO - MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE 331
Ibara ya 145: Uhuru wa Majadiliano bungeni. 331
Ibara ya 146: Mipaka ya Majadiliano bungeni.....333
SEHEMU YA SITA - TUME YA UTUMISHI WA BUNGE 334
Ibara ya 147: Tume ya Utumishi wa Umma. 334
Ibara ya 148: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma. 335
Ibara ya 149: Mfuko wa Bunge. 338
SURA YA KUMI..... 339
MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO 339
SEHEMU YA KWANZA - MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA 339

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 150: Kuanzishwa kwa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano. 339
Ibara ya 151: Misingi ya Utoaji Haki. 340
Ibara ya 152: Uhuru wa Mahakama. 342
SEHEMU YA PILI - MUUNDO WA MAHAKAMA 344
Ibara ya 153: Muundo wa Mahakama.....344
Ibara ya 154: Mahakama ya Juu. 345
Ibara ya 155: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Juu. 346
Ibara ya 156: Mamlaka ya Mahakama ya Juu. 347
Ibara ya 157: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu. 350
Ibara ya 158: Uteuzi wa Jaji Mkuu. 351
Ibara ya 159: Uteuzi wa Naibu Jaji. 354
Ibara ya 160: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu. 355
Ibara ya 161: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu. 356
Ibara ya 162: Muda wa kuwa madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Kuu. 357
Ibara ya 163: Utaratibu wa Kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu. 359
Ibara ya 164: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu. 362
Ibara ya 165: Mahakama ya Rufani. 366
Ibara ya 166: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Rufani. 368
Ibara ya 167: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani. 368
Ibara ya 168: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani. 370

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 169: Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. 372
Ibara ya 170: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. 374
Ibara ya 171: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani. 375
Ibara ya 172: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani. 376
Ibara ya 173: Muda wa kuwa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani. 376
Ibara ya 174: Utaratibu wa Kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. 379
Ibara ya 175: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani. 382
Ibara ya 176: Msajili Mkuu wa Mahakama. 383
Ibara ya 177: Majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama. 385
Ibara ya 178: Mtendaji Mkuu wa Mahakama. 386
Ibara ya 179: Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama. 387
SEHEMU YA TATU - TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA NA MFUKO WA MAHAKAMA..... 388
Ibara ya 180: Tume ya Utumishi wa Mahakama. 388
Ibara ya 181: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma. 390
Ibara ya 182: Uanachama katika Vyama vya Siasa. 395
Ibara ya 183: Mfuko wa Mahakama. 396
SURA YA KUMI NA MOJA..... 397
UTUMISHI WA UMMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO 397
Ibara ya 184: Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma. 397
Ibara ya 185: Ajira na Uteuzi wa Viongo wa Taasisi katika Serikali. 401

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 186: Tume ya Utumishi wa Umma. 402
Ibara ya 187: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma. 404
Ibara ya 188: Mamlaka na Majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma. 404
SURA YA KUMI NA MBILI..... 408
UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIASA 408
SEHEMU YA KWANZA - UWAKILISHI WA WANANCHI..... 408
Ibara ya 189: Ushiriki katika Uchaguzi na Kura ya Maoni.....408
SEHEMU YA PILI - TUME HURU YA UCHAGUZI..... 413
Ibara ya 190: Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi. 413
Ibara ya 191: Kamati ya Uteuzi.....419
Ibara ya 192: Ukomo wa kushika nafasi ya Madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi.....422
Ibara ya 193: Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi. 427
Ibara ya 194: Malalamiko kuhusu Uchaguzi. 432
Ibara ya 195: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi. 433
Ibara ya 196: Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi. 434
SEHEMU YA TATU: USAJILI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA SIASA 436
Ibara ya 197: Usajili wa Vyama vya Siasa. 436
Ibara ya 198: Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa. 439
SURA YA KUMI NA TATU 442
TAASISI ZA UWAJIBIKAJI 442
SEHEMU YA KWANZA: TUME YA MAADILI YA UONGOZI NA UWAJIBIKAJI 442

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 200: Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji. 442
Ibara ya 201: Uteuzi na Sifa za Wajumbe. 444
Ibara ya 202: Kamati Maalum ya Uteuzi. 446
Ibara ya 203: Majukumu ya Jumla ya Tume.....447
Ibara ya 204: Muda wa kukaa madarakani kwa Mjumbe wa Tume.....453
Ibara ya 205: Kuondolewa Madarakani kwa Mjumbe wa Tume. 454
Ibara ya 206: Uhuru wa Tume.....457
Ibara ya 207: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali. 458
SEHEMU YA PILI: TUME YA HAKI ZA BINADAMU 459
Ibara ya 208: Tume ya Haki za Binadamu.....459
Ibara ya 209: Kamati ya Uteuzi.....463
Ibara ya 210: Kazi na Majukumu ya Tume. 467
Ibara ya 211: Muda wa kukaa madarakani kwa Kamishna wa Tume. 474
Ibara ya 212: Kuondolewa Madarakani kwa Kamishna wa Tume.....475
Ibara ya 213: Uhuru wa Tume.....478
Ibara ya 214: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali. 479
SEHEMU YA TATU: MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI 480
Ibara ya 215: Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. 480
Ibara ya 216: Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. 481
Ibara ya 217: Kazi na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. 482

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 218: Muda wa kukaa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.488

Ibara ya 219: Kuondolewa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.....489

Ibara ya 220: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali. 493

SURA YA KUMI NA NNE..... 494

MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO..... 494

Ibara ya 221: Mfuko Mkuu wa Hazina. 494

Ibara ya 222: Masharti ya kutoa Fedha za matumizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina. 495

Ibara ya 223: Utaratibu wa kuidhinisha Matumizi ya Fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina.497

Ibara ya 224: Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya Fedha kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuanza kutumika. 500

Ibara ya 225: Mfuko wa Matumizi ya Dharura. 501

Ibara ya 226: Mishahara ya baadhi ya Watumishi kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina.....504

Ibara ya 227: Deni la Taifa.....507

Ibara ya 228: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa.....508

Ibara ya 229: Mamlaka ya Serikali za Nchi Washirika kukopa.....509

Ibara ya 230: Masharti ya kutoza kodi.....511

Ibara ya 231: Vyanzo vya Mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano. 511

Ibara ya 232: Ununuzi wa Umma.....513

Ibara ya 233: Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano. 514

Ibara ya 234: Benki za Serikali za Nchi Washirika. 515

SURA YA KUMI NA TANO..... 516

Trial Version
www.nuance.com

ULINZI NA USALAMA WA JAMHURI YA MUUNGANO 516

Ibara ya 235: Usalama wa Taifa. 516

Ibara ya 236: Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa. 518

Ibara ya 237: Kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa. 521

Ibara ya 238: Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa. 524

Ibara ya 239: Kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. 526

Ibara ya 240: Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. 527

Ibara ya 241: Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu. 529

Ibara ya 242: Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. 532

Ibara ya 243: Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano. 533

Ibara ya 244: Misingi ya Utendaji wa Jeshi la Polisi. 533

Ibara ya 245: Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi. 535

Ibara ya 246: Uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi. 536

Ibara ya 247: Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi. 536

Ibara ya 248: Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa. 537

Ibara ya 249: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa. 538

Ibara ya 250: Usalama katika Nchi Washirika. 539

Ibara ya 251: Utaratibu wa kujiuzulu katika Utumishi wa Umma. 540

Ibara ya 252: Masharti kuhusu kukabidhi Madaraka. 543

Ibara ya 253: Baadhi ya Watumishi wa Umma kutoshika nafasi za Kisiasa. 547

Ibara ya 254: Ufafanuzi. ..... **Error! Bookmark not defined.**

Trial Version
www.nuance.com

Ibara ya 255: Jina la Katiba na kuanza kutumika. 560

Ibara ya 256: Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 Sura ya 2. 560

SURA YA KUMI NA SABA 561

MASHARTI YATOKANAYO NA MASHARTI YA MPITO 561

SEHEMU YA KWANZA - MASHARTI YATOKANAYO 561

Ibara ya 257: Matumizi ya Baadhi ya Masharti ya Katiba Sura ya 2 561

SEHEMU YA PILI - MASHARTI YA KIKATIBA NA SHERIA ZA NCHI 562

Ibara ya 258: Kuendelea kutumika Masharti ya Katiba. 562

Ibara ya 259: Kuendelea kutumika Sheria za Nchi. 563

SEHEMU YA TATU - UTUMISHI WA UMMA 568

Ibara ya 260: Kuendelea kuwepo kwa Rais madarakani. 568

Ibara ya 261: Kuendelea kuwepo kwa Makamu wa Rais madarakani. 569

Ibara ya 262: Kuendelea kwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu Mawaziri. 569

Ibara ya 263: Kuendelea kwa Watumishi wa Umma. 570

SEHEMU YA NNE - BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO 574

Ibara ya 264: Kuendelea kwa Ubunge na Uongozi wa Bunge. 574

Ibara ya 265: Kuvunjwa kwa Bunge. 575

SEHEMU YA TANO - MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO 577

Ibara ya 266: Kuendelea kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu. 577

Ibara ya 267: Kuendelea kwa Mashauri yaliyopo Mahakamani. 578

Trial Version
www.inuka.com

SEHEMU YA SITA - MASHARTI YA MPITO 580

Ibara ya 268: Muda wa Mpito. 580

Ibara ya 269: Utekelezaji wa Masharti ya Katiba Mpya. 582

Ibara ya 270: Kamati ya Kusimamia muda wa Mpito. 585

Ibara ya 271: Kufutwa kwa Masharti yatokanayo na Masharti ya Mpito. 587

Trial Version
www.nuance.com

UTANGULIZI WA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

KWA KUWA, sisi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yetu jamii inayoheshimu na kuzingatia misingi ya utu, uhuru, haki, usawa, udugu, amani, umoja na mshikamano katika nyanja zote za maisha yetu;

NA KWA KUWA, tunaamini kuwa misingi hiyo inaweza tu kutekelezwa katika jamii yenye mfumo wa demokrasia na utawala bora ambayo Serikali yake inasimamiwa na Bunge lenye Wabunge waliochaguliwa na wanaowakilisha wananchi, na Mahakama huru zinazotekeleza wajibu wa kutoa haki bila woga wala upendeleo wowote, na kuhakikisha kuwa haki za binadamu zinalindwa na kudumishwa na kwamba wajibu wa kila mtu unatekelezwa kwa uaminifu;

NA KWA KUWA, tunatambua umuhimu wa kutunza mali ya Mamlaka za Nchi na ya pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu, ubadhirifu na kuhimiza matumizi bora na endelevu ya rasilimali na maliasili zetu pamoja na kulinda na kuhifadhi mazingira yetu kwa mustakabali wa maisha ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;

NA KWA KUWA, tunatambua umuhimu na faida za kujenga, kukuza na kuendeleza amani, umoja, urafiki na ushirikiano miongoni mwa Watanzania, mataifa mbalimbali ya Afrika na dunia kwa ujumla;

NA KWA KUWA, azma ya kujenga Umoja wa Bara la Afrika inadhihirishwa na Muungano wa iliyokuwa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar;

NA KWA KUENDELEZA DHAMIRA YETU HIYO, ni muhimu:

(a) kulinda, kuimarisha na kuudumisha Muungano wa nchi za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar;
(b) kujenga Taifa huru na linalojitegemea;
(c) kuimarisha na kuendeleza utawala wa sheria;

Trial Version
www.nuance.com

(d) kukuza na kuendeleza maadili, uwajibikaji na uwazi;
(e) kujenga umoja na mshikamano utakaowezesha kutimiza malengo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, kimazingira na kulinda urithi kwa ujumla;
(f) kujenga na kuendeleza ukuu wa mamlaka ya watu;
(g) kujenga na kuendeleza utii wa mamlaka ya Katiba; na
(h) kuimarisha na kudumisha uzalendo kwa Taifa miongoni mwa Watanzania;

NA KWA KUZINGATIA, urithi tulioachiwa na Waasisi wa Taifa letu wa kujenga nchi yenye umoja wa watu wake ambao hawabaguani kwa misingi ya ukabila, dini, rangi, jinsi au ubaguzi wa aina nyingine yoyote;

NA KWA KUZINGATIA, uzoefu wa zaidi ya Miaka Hamsini ya Uhuru wa Tanganyika, Miaka Hamsini ya Mapinduzi ya Zanzibar na Miaka Hamsini ya Muungano wa Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, na umuhimu wa ushiriki mpana na bayana wa wananchi katika utungaji wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

HIVYO BASI, KATIBA HII YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA ILIYOPENDEKEZWA NA BUNGE MAALUM LA KATIBA imetungwa na **SISI WANANCHI WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA** kupitia **KURA YA MAONI** kwa madhumuni ya kujenga jamii kama hiyo, na kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaongozwa na Serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia na utawala wa sheria, kujitegemea na isiyofungamana na dini.

Trial Version
www.nuance.com

SURA YA 1 - JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA

SEHEMU YA KWANZA - JINA, MIPAKA, ALAMA, LUGHA NA TUNU ZA TAIFA

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 1: Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi na Shirikisho lenye mamlaka kamili ambalo limetokana na Muungano wa nchi mbili za Jamhuri ya Tanganyika na Jamhuri ya Watu wa Zanzibar, ambazo kabla ya Hati ya Makubaliano ya Muungano ya mwaka 1964, zilikuwa nchi huru. (2) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Shirikisho la kidemokrasia linalofuata mfumo wa vyama vingi vya siasa, usawa wa binadamu, kujitegemea,	Sababu ya kuweka Ibara hii ni kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuwepo, inaimarishwa na kudumishwa, na kuhuuisha Muungano. Aidha, lengo la Ibara hii ni kuainisha aina na hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni Muungano wa Shirikisho lenye Mamlaka Kamili (*Sovereign Federal State*). Hatua hii ina lengo la kuimarisha Muungano kwa kuipa Mamlaka ya Kidola Jamhuri ya Muungano na	Kifungu cha 9(2)(a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 kimeielekeza Tume katika kutekeleza masharti ya sheria kuongozwa na misingi mikuu ya kitaifa na maadili ya jamii ya kuhifadhi na kudumisha kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuondoa utata wa aina na muundo wa Muungano ambao umesababisha kuvunjwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Serikali zote mbili mara kadhaa. Sababu nyingine ya kupendekeza aina

Tigiveraun www.tigiveraun.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na lisilofungamana na dini.	kubainisha utambulisho, uwezo na mamlaka ya Nchi Washirika katika Muungano. Vile vile, lengo la Ibara hii ni kuainisha mfumo wa utawala wa Jamhuri ya Muungano na kupanua misingi muhimu ya nchi ikilinganishwa na iliyyo katika Ibara 3 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inayoeleza kuwa, "Jamhuri ya Muungano ni nchi ya kidemokrasia na ya kijamaa isiyo kuwa na dini, yenye kufuata mfumo wa vyama vingi vya siasa". Lengo jingine ni kuonyesha kuwa Hati ya Muungano ya 1964 ndio chimbuko la Muungano wa Tanzania na kadri ambavyo	hii ya Muungano ni kuhifadhi asili, taswira na hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jumuiya ya kimataifa kwa mujibu wa Kifungu cha 2 cha Mkataba wa Montevideo wa mwaka 1933 unaohusu Haki na Majukumu ya Nchi (*Montevideo Convention on Rights and Duties of States*) "*the federal state shall constitute a sole person in the eyes of international law*" inayomaanisha nchi yenye muundo wa shirikisho katika sheria za kimataifa ni dola moja. Kumekuwa na mijadala miongoni mwa Watanzania kuhusu aina ya Muungano uliopo Tanzania iwapo ni shirikisho au la. Katika medani ya kisiasa mjadala juu ya jambo hili ulijitokeza mwaka 1983 mpaka 1984 kwa uwazi na kwa nguvu wakati wa zoezi la wananchi kutoa
	(3) Hati ya Makubaliano ya Muungano iliyorejewa katika ibara ndogo ya (1), ndio msingi mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba hii, kwa kadri itakavyorekebishwa, itakuwa ni mwendelezo wa Makubaliano hayo.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		imekuwa ikibadilika kwa haja na madhumuni ya kukidhi mabadiliko ya wakati na utekelezaji. Pia, ni kwa madhumuni ya kuipa hadhi ya kikatiba Hati hiyo ya Muungano kwa kuihamisha kutoka kwenye Ibara ya 98 (1) (a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ikisomwa pamoja na Nyongeza ya Pili, Orodha ya Kwanza na badala yake kuingizwa ndani ya katiba kama ibara inayosimama yenyewe.	maoni juu ya mapendekezo ya Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM juu ya Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 na Katiba ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, 1979. Zoezi hilo lilidumu miezi tisa na lilikamilika kwa kufanyika kwa Mabadaliko ya Tano ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1984 na kutungwa kwa Katiba ya Zanzibar ya Mwaka 1984. Hali hiyo ilipewa jina la "Kuchafuka kwa Hali ya Hewa" na ilisababisha aliyekuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu Mwenyekiti wa CCM, Aboud Jumbe Mwinyi, kujiuzulu. Kwa mujibu wa Kumbukumbu za Kikao

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			cha Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi katika Mkutano wa Tano, ambao ulikuwa maalum, uliofanyika Dodoma Januari 24-30, 1984, Mwalimu Nyerere alitamka kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ukiangalia kwa jicho la Zanzibar ni wa shirikisho lakini ukiangalia kutoka upande wa Tanzania Bara ni Serikali moja. Mwalimu alikuwa akimjibu Makamu Mwenyekiti wa CCM, Makamu wa Rais na Rais wa Zanzibar Sheikh Aboud Jumbe Mwinyi aliyesema kuwa Muungano wa Tanzania umeunda Shirikisho (*Federation*) na sio Serikali moja (*Unitary State*). Mfumo wa shirikisho unaopendekezwa katika Rasimu hii unaendeleza hadhi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni Nchi na ni dola moja lenye

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mamlaka kamili yenye serikali tatu. Shirikisho hili linatokana na muungano wa hiari wa Tanganyika na Zanzibar ambazo zilikuwa Jamhuri zenye mamlaka kamili kabla ya kuungana tarehe 26 Aprili 1964. Kwa kawaida nchi ambazo zimeingia katika muungano zinaweza kuchukua moja kati ya sura hizi tatu zifuatazo: i. Muungano wa Serikali Moja (*Unitary State*); ii. Muungano wa Shirikisho (Federation); na iii. Muugano wa Mkataba (*Confederation*) Kwa vyovyote vile, mfumo wa shirikisho unakuwepo pale ambapo nchi mbili au

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			zaidi zimeungana na hazikuunda serikali moja. Kwa maana hiyo shirikisho (*Federation*) linamaanisha mfumo wa utawala wa nchi wenye sifa zifuatazo: (1) Kunakuwa na ngazi mbili za serikali zinazotawala eneo moja la nchi na raia wale wale; moja ikisimamia mambo ya muungano (shirikisho) na nyingine mambo yasiyo ya Muungano (yasiyo ya shirikisho); (2) Kila ngazi ya serikali, yaani ile ya shirikisho na ile ya nchi washirika inakuwa na mamlaka kamili na maeneo ya utendaji na uhakikisho wa kikatiba wa uhuru wa kutoingiliana baina ya serikali hizo katika maeneo waliyo na madaraka nayo bila ya kushauriana. Mfumo huu ni tofauti na ule wa dola moja lenye serikali moja (unitary state)

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ambapo serikali kuu inaweza kuamua kuzinyang'anya serikali za chini yake madaraka kadri inavyoona inafaa; (3) Katika muundo huu, serikali ya muungano ndiyo yenye mamlaka juu ya masuala yote yaliyokubaliwa kuwa ya muungano (shirikisho). Serikali za nchi washirika zinakuwa na mamlaka ya kikatiba ya kushughulikia mambo yasiyo ya muungano katika maeneo yao ya utawala; na (4) Katika muungano wa shirikisho mamlaka kuu ya kidola (*sovereign powers and functions*) yapo chini ya serikali ya shirikisho (muungano). Ingawa katika mfumo huu wa muungano wa shirikisho kunakuwa na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			serikali zaidi ya moja kwa mujibu wa Ibara ya 2 ya Mkataba wa Montevideo wa Haki na Majukumu ya Nchi (*Montevideo Convention on Rights and Duties of States*) katika sheria za kimataifa na mahusiano ya kimataifa nchi inayofuata mfumo wa muungano wa shirikisho huchukuliwa na kuhesabiwa kuwa nchi moja. Sura ya shirikisho la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa ni nchi yenye mamlaka tatu na serikali tatu inajidhihirisha katika masharti yaliyomo katika Ibara za 61, 63, 64, 65, 66, 67, 70, 71, 72, 110, 111,117, 119, 156 na 235. Miongoni mwa mifano ya nchi zinazofuata muundo wa muungano wa shirikisho ni nchi za Ethiopia, Marekani, Nigeria, Ujerumani, India na Brazil. Hata

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			hivyo Muungano wa Tanzania ni tofauti na miungano ya shirikisho iliyotajwa kwa sababu ni wa hiari na usiotokana na ubeberu au ukoloni na ulihusisha nchi mbili zilizokuwa jamhuri kamili kabla ya kuungana. Kwa aina hii ya Muungano wa hiari huwezi kufuta kuwepo kwa utambulisho wa nchi washirika zinazounda au zilizounda Muungano.
Ibara ya 2: Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni eneo lote laTanganyika likijumuisha sehemu yake ya bahari na eneo lote la Zanzibar likijumuisha sehemu yake ya bahari.	Lengo la Ibara hii ni kutambua eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ukamilifu na kuiweka Tanzania katika ramani ya kimataifa na kuweka bayana mipaka na nchi jirani. Ibara hii pia inalenga kuhamasisha Watanzania kujenga tabia ya kutambua na kulinda	Umuhimu wa kubainisha eneo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuridhia kiu ya wananchi waliotaka kuwepo kwa ufafanuzi thabiti kuhusu eneo na mipaka ya nchi. Kufanya hivyo, kutatunza historia ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuondoa utata na hisia kwamba mipaka ya nchi hizi mbili inabadilika.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		mipaka ya nchi yao. Maelezo hayo yasomeke pamoja na Ibara za 49, 51 na 235 za Rasimu ya Katiba.	Baadhi ya nchi ambazo zimeweka mipaka yake katika katiba zao ni pamoja na Kenya, Msumbiji, Sudan ya Kusini na Ethiopia. Lakini pia nchi za Uganda na Siera Leone zimekwenda mbali zaidi kwa kutumia vipimo vya kisasa vya Global Positioning System (GPS) kuweka mipaka yao katika katiba za nchi. Katika kuweka vifungu vya mipaka katika Katiba zao, nchi ya Msumbiji inayopakana na Tanzania Ibara ya 6 ya Katiba yake inatamka: *"1. The territory of the Republic of Mozambique is a single whole, indivisible and inalienable, comprising the entire land surface, maritime zone and air space delimited by the national boundaries."* *"2. The breadth, limits and legal order*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			of Mozambique's territorial waters, the exclusive economic zone, the contiguous zone and seabed rights shall be fixed by law." Pia, sababu ya mapendekezo haya ni kubainisha mipaka ya Jamhuri ya Muungano inayotambulika na mikataba mbalimbali ya kimataifa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Sheria za Bahari wa mwaka 1982 (*United Nations Law of the Sea Convention*) kama ulivyoainishwa katika sheria ya *Teritorial Sea Exclusive Economic Zone Act*, Sura ya 238 na *Deep Sea Fishing Authority Act*, Sura ya 389 ya Sheria za Tanzania. Kwa undani zaidi, Sheria ya *Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act*, Sura ya 238 inatamka katika Kifungu cha 3 kwamba:-

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			"The breadth of the Territorial Sea of the United Republic shall comprise those areas of the sea extending up to 12 nautical miles measured from the coastal low-water line as determined under Section 5 of this Act." Kwa mujibu wa Kifungu cha 5 cha Sheria hii, msingi wa kupima bahari ya Jamhuri ya Muungano umeelezewa kuwa ni: *"The baseline from which the breadth of the Territorial Sea of the United Republic is measured shall be the low-water line along the coast of the United Republic including the coast of all islands, as marked on a large scale chart of map officially recognized by the Government of the*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			United Republic." Kutokana na Sheria hii bahari yote ndani ya kilomita 12 za bahari inachukuliwa kuwa ni maji ya ndani na si ya kimataifa. Kifungu cha 4 kinaeleza kuwa: *"The internal waters of the United Republic of Tanzania include any areas of the sea that are on the landward side of the baseline of the Territorial Sea of the United Republic."* Sheria ya Deep Sea Fishing Authority Act, Sura ya 389 inabainisha katika Kifungu cha 2 kwamba: 1. *This Act shall apply to Tanzania Zanzibar as well as Mainland Tanzania.* 2. *The Act shall be construed as being*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			in addition to and not in derogation of the Territorial Sea and Exclusive Economic Zone Act, 1989 and shall for all intents and purposes compliment that Act." Mikataba ya Kimataifa ya Mipaka ya Tanzania na Mataifa jirani ni kama ifuatavyo: a) **Mpaka wa Tanzania na Burundi** [*Protocol between the Belgium and British governments relative to the Tanganyika-Ruanda-Urundi border (5 August 1924); Anglo-Belgium Agreement (2 November 1934)*]. b) **Mpaka wa Tanzania na Rwanda** [*Treaty between Belgium, Great Britain and Northern Ireland concerning the Boundary between Tanganyika and*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Ruanda-Urundi (22 November 1934)]. c) **Mpaka wa Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo** *[Convention between German and Belgium (11 August 1910); Protocol signed by Great Britain and Belgium (5 August 1934)*]. d) **Mpaka wa Tanzania na Kenya** ***[****Agreement between Great Britain and German respecting Zanzibar, Heligoland and the Spheres of Influence of the two countries in Africa (1 July 1890); Agreement between Great Britain and German respecting Boundaries in East Africa from the mouth of Umba River to Lake Jipe and Kilimanjaro (25 July 1893); Protocol of*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Agreement between the British and German governments respecting the Jassin and Umba valley Boundary (14 February 1900); Draft Agreement respecting the Boundary between the British and German Territories in East Africa from mount Sabino to Lake Jipe (4 July 1914); British Mandate for East Africa (20 July 1922)]. e) **Mpaka wa Tanzania na Msumbiji** *[Declaration of Spheres of Influence between Portugal and German (30 December 1886); Anglo-Portuguese Treaty (11 June 1891)]*. f) **Mpaka wa Tanzania na Uganda** [*Anglo-German*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Delimitation of Spheres of Influence in East Africa: Exchange of Notes (29 October - 1 November 1886); Anglo-German Agreement (1 July 1890); Anglo-German Agreement (14 may 1910)]. g) **Mpaka wa Tanzania na Zambia** [*Agreement between Great Britain and Germany relative to the Boundary of the British and German spheres of interest between Lake Nyasa and Tanganyika (23 February 1901)];* na h) **Mpaka wa Tanzania na Malawi** [*Anglo-German Agreements (1 July 1890 and 23 February 1901), na Protocol (11*

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			November1898). Serikali ya Tanzania (wakati huo "Tanganyika") iliridhia mikataba hii yote ya mipaka isipokuwa eneo la mpaka wake na Malawi katika Ziwa Nyasa.
Ibara ya 3: Alama za Sikukuu za Taifa	(1) Alama za Taifa zitakuwa ni: (a) Bendera ya Taifa; (b) Wimbo wa Taifa; na (c) Nembo ya Taifa, kama zitakavyoainishwa katika sheria za nchi. (2) Sikukuu za Kitaifa zitakuwa ni: (a) Siku ya Uhuru wa Tanganyika, itakayoadhimishwa tarehe 9 Disemba;	Madhumuni ni kuhakikisha kuwa Alama na sikukuu za kitaifa zinapewa hadhi ya kikatiba na kutambulika kuwa ni vielelezo vya utaifa na alama kuu za dola na watu wake.	Wananchi wengi katika maoni yao walipendekeza kuwa alama na sikukuu za kitaifa zitambuliwe bayana katika katiba kwa madhumuni ya kubainisha utaifa, kujenga uzalendo, mshikamano na umoja wao. Sababu nyingine ni kuondosha utata au kutoeleweka kwa uhakika ni zipi alama za taifa kwa mitizamo ya kiitikadi au mawazo ya makundi ndani ya Tanzania. Uzoefu umechukuliwa katika nchi kadhaa za eneo letu na mabara mingine juu ya suala hili zikiwemo Kenya,

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) Siku ya Mapinduzi ya Zanzibar, itakayoadhimishwa tarehe 12 Januari; (c) Siku ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, itakayoadhimishwa tarehe 26 Aprili; na (d) Sikukuu nyingine zitakazoainishwa na sheria za nchi. (3) Kila Sikukuu ya Kitaifa itakuwa ni siku ya mapumziko.		Venezuela, Msumbiji na Namibia ambazo zimeweka alama za taifa na Sikukuu za kitaifa katika katiba zao. Kwa mfano, Katiba ya Msumbiji kwenye Kifungu cha 13 kinaeleza: "*The symbols of the Republic of Mozambique shall be the national flag, emblem and national anthem*."
Ibara ya 4: Lugha ya Taifa na Lugha za Alama.	(1) Lugha ya Taifa ya Jamhuri ya Muungano ni Kiswahili na itatumika katika mawasiliano rasmi ya kitaifa na kiserikali.	Ibara hii ya Rasimu imelenga kuitambua kikatiba lugha ya Kiswahili kuwa ni lugha ya Taifa na umuhimu wake katika	Dhamira ya kukifanya Kiswahili kuwa lugha ya taifa ina historia ndefu. Tanganyika ilitangaza nia hiyo toka mwaka 1963, na hata baada ya

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), lugha ya Kiingereza au lugha nyingine yoyote inaweza kutumika kuwa lugha rasmi ya mawasiliano ya kiserikali pale itakapohitajika. (3) Serikali itaweka mazingira yatakayowezesha kuwepo kwa mawasiliano mbadala zikiwemo lugha za alama, maandishi yaliyokuzwa na nukta nundu kwenye sehemu muhimu za umma na katika vyombo vya habari vinavyotangaza habari zake kitaifa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum.	kuwaunganisha Watanzania na kujenga umoja na utaifa kama ilivyopendekezwa na wananchi wengi. Pia, ni kujenga msingi kuwa lugha ya taifa ni kwa ajili ya kuimarisha mawasiliano baina ya wananchi, dola kwa wananchi wake na pia kuimairisha utamaduni, mila na desturi zao. Kadhalika, Rasimu ya Katiba imeitambua lugha ya alama kwa lengo la kuwawezesha wananchi wenye ulemavu na wenye mahitaji maalum kuwa na haki ya kupata habari na taarifa mbalimbali za kitaifa na kimataifa ili kujenga misingi ya usawa na haki ya mawasiliano.	kuundwa Jamhuri ya Muungano suala hilo limebaki kuwa la kisera bila ya kupewa nguvu ya Kikatiba. Hata wananchi wengi waliotoa maoni walitaka Kiswahili kiwe lugha ya kitaifa na hili litiwe ndani ya Katiba kwa ajili ya kukienzi na kukitukuza. Tanzania ndiyo mhimili na chimbuko la Kiswahili lakini juhudi za kukiendeleza na kukienzi Kiswahili zimeshamiri ngazi ya kimataifa ambapo Kiswahili kina sifa ya kuwa lugha pekee ya Kiafrika iliyo na hadhi katika mashirika ya kimataifa. Kwa mfano, Kiswahili ni Lugha Rasmi ya EAC na AU jambo lililoungwa mkono si na Tanzania peke yake, lakini pia na aliyekuwa Rais wa Msumbiji, Mheshimiwa Joachim Chisano, aliyekuwa Rais wa Nigeria, Mheshimiwa Olesugun Obasanjo na Mwenyekiti wa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		Kujenga msingi kwa Serikali kuwajibika kuweka miundo mbinu na kutoa elimu na vifaa ili kuwawezesha wananchi wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata haki hiyo kikatiba sawa na wananchi wengine kwa jumla. Ibara hii inaweza kusomwa sambamba na Ibara ya 10 (3) (b), inayoelezea juu ya Malengo Makuu, Ibara ya 11 na Ibara 45 juu ya haki ya watu wenye ulemavu.	Kwanza wa AU Bw. Alpha Konare. Kiswahili pia kinafundishwa katika zaidi ya vyuo vikuu 150 katika bara Asia, Marekani na Ulaya. Ni lugha ya Kiafrika inayotumika zaidi na mashirika ya maendeleo ya nchi nyingi. Pia Kiswahili kimetumika katika harakati za ukombozi barani Afrika. Halikadhalika idhaa kadhaa maarifu duniani kwa mfano Idhaa ya Kiswahili ya Uingereza (BBC), Deutsch Welle, Radio ya Umoja wa Mataifa, Radio Iran, Radio ya Ufaransa na Radio Japan International hutumia Kiswahili katika matangazo yao. Kwa sasa kuna juhudi za kukifanya Kiswahili kuwa moja ya lugha za Umoja wa Mataifa jambo ambalo litapata msukumo zaidi iwapo nchi iliyojitoa katika kukienzi na kukiendeleza itakitumia katika

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mawasiliano yake rasmi.
Ibara ya 5: Tunu za Taifa.	Jamhuri ya Muungano itaenzi na kuzingatia Tunu za Taifa zifuatazo:	Haja ya kuweka Ibara hii ni kujenga mwafaka miongoni mwa Watanzania kuhusu mambo yanayowaunganisha na kuwatambulisha kama taifa. Vivyo hivyo, ni kujenga moyo wa kujithamini na kuthamini misingi muhimu ya maadili na taratibu mbalimbali katika taifa letu na kurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine.	Tunu za Taifa ndiyo mtima na fahari ya Taifa. Wananchi walitaka ibara hii kiwepo hasa walipokuwa wakizungumzia kumomonyoka kwa maadili na kupungua kwa uzalendo. Umuhimu wa kujumuisha Tunu za Taifa ni kuwezesha ziote mizizi na ziweze kuenziwa na kurithishwa vizazi baada ya vizazi. Uzoefu unaonyesha kuwa nchi kadhaa zimeingiza Tunu za Taifa katika Katiba zao kusisitiza sifa za msingi zinazowaunganisha wananchi kama vile Ghana na Kenya. Kwa mfano, Ibara ya 10 (2)(a) ya Katiba ya Kenya inajumuisha Tunu zifuatazo:
	(a) utu; (b) uzalendo;		
	(c) uadilifu;		
	(d) umoja;		
	(e) uwazi;		
	(f) uwajibikaji; na		
	(g) lugha ya Taifa.		

Final Version
www.nuru.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			(a) patriotism, national unity, sharing and devolution of power, rule of law; and participation of the people." Ibara cha 10 (2)(b) cha Katiba hiyo ya Kenya inataja Tunu za Taifa zifuatazo; *"human dignity, equity, social justice, inclusiveness, equality, human rights, non-discrimination and protection of the marginalized"*. Eneo hili la Katiba linapaswa kusomwa kwa pamoja na Utangulizi wa Rasimu hii na Ibara za 7, 8, 9, 10, 11, 13, 184 na 235 za Rasimu hii.
SEHEMU YA PILI - MAMLAKA YA WANANCHI, UTII NA HIFADHI YA KATIBA			
Ibara ya 6: Mamlaka ya Wananchi, Utii na Hifadhi ya Katiba	Jamhuri ya Muungano ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia inayozingatia haki ya kijamii, na kwa hiyo:	Madhumuni ya Ibara ni kuweka wazi kikatiba kuwa wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na	Kutambua kuwa wananchi ndiyo msingi na chimbuko la mamlaka yote ya nchi na kuifanya Serikali iwajibike kwa wananchi kwa kuhakikisha kuwa

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) wananchi ndio msingi wa mamlaka yote, na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi ambao kwa umoja na ujumla wao wanaimiliki na kuipatia Katiba hii uhalali; (b) lengo kuu la Serikali litakuwa ni maendeleo na ustawi wa wananchi; (c) Serikali itawajibika kwa wananchi; na (d) Wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.	mamlaka yake kutoka kwa wananchi, ambao kwa umoja na ujumla wao, wataimiliki na kuipatia Katiba uhalali. Aidha, ni kuweka dhana kuwa lengo kuu la Serikali ni kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi na kwamba Serikali itawajibika kwa wananchi; na wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.	inasimamia maendeleo na ustawi wa wananchi wake na kutengeneza mazingira ya kikatiba yatakayowezesha wananchi kushiriki shughuli mbalimbali za nchi. Aidha, Ibara hii inafanana na Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 inayotambua mamlaka ya wananchi na wajibu wa serikali na ndiyo Ibara iliyowapa wananchi uhalali wa kushiriki moja kwa moja katika kufanya mabadiliko ya Katiba ya 1977. Katiba za Kenya, Uswisi na Marekani zina vipengele vya namna hii. Ikumbukwe kwamba katika nadharia ya demokrasia, mamlaka na sauti ya mwisho ni ya umma (*popular control of public power*). Katika muktadha wa Rasimu hii, Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 7, 10

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			(3), 11, 78, 119, 124 na 129 za Rasimu.
Ibara ya 7: Watu na Serikali	(1) Muundo wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake, katika uendeshaji na utekelezaji wa shughuli zake, utazingatia azma ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa. (2) Kwa madhumuni ya masharti ya ibara ndogo (1), mamlaka ya nchi na vyombo vyake vinawajibika kuelekeza sera, sheria na shughuli zake zote kwa lengo la kuhakikisha kwamba: (a) utu, heshima na haki nyingine za binadamu zinalindwa, zinathaminiwa, zinahifadhiwa na kudumishwa kwa kuzingatia mila na desturi za Watanzania na mikataba mbalimbali iliyoridhiwa na Jamhuri ya Muungano; (b) sheria za nchi zinasimamiwa	Lengo la Ibara hii ni kusisitiza Umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa, kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi kwa kulinda haki za binadamu na kuakisi maslahi ya wananchi katika sera, sheria na shughuli zote za serikali, kuhimiza usawa na ulinganifu wa haki, fursa na manufaa kama misingi ya utendaji na kukuza umakini na uwajibikaji katika shughuli za serikali; na matumizi na ulinzi wa rasilimali za taifa.	Suala la ardhi na rasilimali za nchi ni miongoni mwa maeneo yaliyotolewa maoni kwa wingi na wananchi. Dai lao kuu ni kuitaka Katiba iweke masharti kuhakikisha Serikali na vyombo vyake inalinda na kuhifadhi haki za binadamu na rasilimali za Taifa ikiwemo rasilimali kuu ya ardhi. Pia, Ibara hii inaendeleza masharti yaliyopo katika Ibara ya 27 ya Katiba ya 1977 inayoweka wajibu wa kulinda mali asili na kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu nchini. Taarifa nyingi zinazotathmini utendaji wa serikali, zikiwemo zile za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu wa Serikali, zimeonyesha upungufu mkubwa katika usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji

www.tlc.or.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na kutekelezwa; (c) shughuli zinazofanywa zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kwamba utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na kutumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine; (d) ardhi ikiwa rasilimali kuu na msingi wa Taifa inalindwa, inatunzwa na kutumiwa na wananchi wa Tanzania kwa manufaa, maslahi na ustawi wa kizazi cha sasa na vizazi vijavyo; (e) maendeleo ya uchumi wa Taifa		wa katiba, sera, sheria na mipango ya nchi katika ngazi zote za serikali jambo linalodhibitiwa kwa kuhimiza umakini na ushiriki wa wananchi katika masuala ya kitaifa.

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yanapangwa na kukuzwa kwa ulinganifu na kwa pamoja na kwa namna ambayo inawanufaisha wananchi wote;		
	(f) kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya kazi, na kazi maana yake ni shughuli yoyote ya halali inayompatia mtu kipato chake;		
	(g) kunakuwepo fursa na haki zilizo sawa kwa wananchi wote, wanawake na wanaume, bila ya kujali rangi, kabila, nasaba, itikadi, dini au hali ya mtu;		
	(h) aina zote za dhuluma, vitisho, ubaguzi, unyanyasaji, rushwa, uonevu au upendeleo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	zinaondolewa nchini; (i) utajiri wa rasilimali na maliasili za Taifa unaelekezwa katika kuleta maendeleo, kuondoa umaskini, ujinga na maradhi; na (j) nchi inaongozwa kwa kufuata misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na kujitegemea.		
Ibara ya 8: Ukuu na Utii wa Katiba	(1) Katiba hii ni sheria kuu katika Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii. (2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), endapo masharti ya sheria yoyote yatatofautiana na masharti ya Katiba hii, masharti ya sheria	Lengo ni kuondoa utata kuhusu ukuu wa Katiba katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia, ni kuondoa utata wa mipaka ya mamlaka kati ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba za Nchi	Umuhimu wa Ibara hii ni kubainisha hadhi na ukuu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya mfumo wa shirikisho. Pia, Ibara hii inadhamiria kubatilisha sheria, kanuni, maamuzi na mienendo inayokwenda kinyume na masharti ya Rasimu hii.

Final Version
www.katiba.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hiyo yatakuwa batili na yatatenguka kwa kiwango kile kinachotofautiana na masharti ya Katiba hii.	Washirika. Aidha, Ibara hii inatambua ukuu wa wananchi,mmoja mmoja na ujumla wao, inaipa Katiba ukuu juu ya mamlaka na sheria zote. Hivyo, Katiba hii ndiyo sheria kuu ya nchi na ipo juu ya sheria na mamlaka zote za nchi. Pia, Rasimu inaelekeza kwamba maudhui ya katiba hii yabebwe katika Katiba, sheria, sera na mipango ya Nchi Washirika. Kadhalika, madhumuni ya Ibara hii ni kuhakikisha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inafuata utawala wa kikatiba kwa kusisitiza ukuu, uhifadhi na utii wa Katiba. Aidha, Ibara hii inaweka wajibu wa kukuza uraia kwa kuhimiza	Ukuu na utii wa katiba unaainishwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar 1984 ingawa haya hayazingatiwi kwa ukamilifu. Katiba za Ethiopia, Ujerumani, Uswisi na Australia zina vifungu vinavyohusu ukuu na utii wa katiba kama msingi wa taratibu zote za kuendesha nchi. Vifungu hivyo vinawafanya wananchi na mamlaka za nchi kuwajibika kuiheshimu, kuilinda, na kuitii Katiba; pamoja na kuhakikisha kuwa uamuzi wowote ambao hauwiani au kwenda sambamba na masharti ya Katiba kuwa ni batili.
	(3) Mtu yeyote, chombo, taasisi, jumuiya na wakala wowote wa mamlaka ya nchi na mamlaka binafsi zinao wajibu wa kuzingatia masharti ya Katiba hii na sheria za nchi na kuzitii.		
	(4) Sheria yoyote, mila, desturi au uamuzi wowote wa chombo cha dola, ofisa wa Serikali au mtu binafsi ni sharti ufuate na kuendana na masharti yaliyomo kwenye Katiba hii na kwamba sheria, mila, desturi au uamuzi wowote ambao hautawiana au kwenda sambamba na masharti ya		

www.tanzlii.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Katiba hii utakuwa batili. (5) Serikali itaweka utaratibu wa kuwawezesha wananchi kuifahamu, kuilinda na kuitii Katiba.	uelewa wa katiba miongoni mwa raia. Suala hili pia limo katika Ibara 64(3) ya Katiba ya mwaka 1977. Ibara hii ya Rasimu ya Katiba isomwe pamoja na Ibara za 10, 11, 12, 64, 69, 110, 111, 117, 156, 167, 231, 233, 234 na 235 za Rasimu hii.	
Ibara ya 9: Hifadhi ya Utawala wa Katiba	(1) Mtu au kikundi cha watu hakitachukua au kushikilia mamlaka ya nchi isipokuwa kwa mujibu wa Katiba hii. (2) Kitendo chochote kinachokiuka masharti ya ibara ndogo ya (1) ni batili na ni kitendo cha uhaini kama itakavyoelezwa katika sheria za nchi.	Madhumunii ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kushika madaraka ya nchi kwa mujibu wa Katiba ikiwemo kwa njia ya uchaguzi. Kukiuka Katiba na kuchukua madaraka ya nchi kwa nguvu ni kitendo cha uhaini. Hivyo, Ibara hii inajenga utamaduni wa kutii, kutetea na kulinda utawala wa Kikatiba	Historia ya Bara la Afrika baada ya uhuru na hata siku za karibuni (mfano huko Mali, Ivory Coast, Jamhuri ya Afrika ya Kati na Sudan ya Kusini) imeshuhudia mapinduzi ya kijeshi na utawala wa kiimla dhidi ya serikali zilizochaguliwa na watu. Nchi zilizopitia mapinduzi ya kijeshi au utawala wa kiimla kama Togo, Ghana, Nigeria, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Benin na Zaire

Trial Version
www.wincap.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		miongoni mwa wananchi.	zimeshuhudia matendo makubwa ya uuaji, dhulma na ubadhirifu. Katiba za nchi nyingi duniani zimeweka Ibara za aina hii ili kuzuia kupora madaraka kinyume na misingi ya kidemokrasia na katiba. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 63, 69, 78, 91, 235, 239 na 241 za Rasimu hii.
SURA YA PILI **MALENGO MUHIMU, MISINGI YA MWELEKEO WA SHUGHULI ZA SERIKALI NA SERA ZA KITAIFA**			
Ibara ya 10: Malengo Makuu	(1) Lengo Kuu la Katiba hii ni kulinda, kuimarisha na kudumisha haki, udugu, amani, umoja na utengamano wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano kwa	Madhumini na malengo ya Ibara hii ni kuweka misingi ya wananchi kufikia ndoto, dira, vipaumbele na matarajio yao kama mtu mmoja	Chemchemu ya malengo na misingi mikuu ya taifa kuwekwa katika katiba za nchi ni Katiba ya Uhuru ya Ireland ya mwaka 1916 walipojiondoa kutoka ukoloni wa Kiingereza. Walitaka Katiba

Final Version
www.liane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuzingatia ustawi wa wananchi na kujenga Taifa huru lenye demokrasia, utawala bora, maendeleo endelevu na kujitegemea.	mmoja na pia kama jamii na taifa. Kuweka misingi na vigezo imara vya kuwawezesha wananchi kuwajibisha serikali na viongozi wao kwa jumla.	hiyo isionekane kuwa imejikita katika kuunda na kusimamia vyombo tu, bali pia iwe inatoa fursa kwa wananchi kuweza kuota, kutamani na kutarajia tunu na ustawi wao. Pia ilikuwa ni kujenga utamaduni mpya ambao unatoa nguvu kwa wananchi kuiagiza Serikali yao juu ya mambo ya ustawi na maendeleo ambayo wanataka serikali isimamie kwa ukamilifu wake, na kuwa na sauti juu ya mipango na sera za Serikali. Pia wananchi wa Ireland walitaka viongozi na Serikali wasiwe mabwana na badala yake wawe ni watumishi wa umma. Katiba nyingine zenye misingi mikuu ni Ghana, India, Nigeria, Papua New Guinea, Uganda na pia Katiba ya
	(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), lengo hilo kuu litaendelezwa na kuimarishwa katika nyanja zote kuu, ikijumuisha nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni na kimazingira.	Ni kuweka misingi ya kikatiba kuongoza muelekeo wa sera, sheria na shughuli za kitaifa. Halikadhalika ni kutoa na kuweka fursa ya kufaidi haki.	
	(3) Katika kutekeleza malengo ya Taifa ya:		
	(a) kisiasa, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili -		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i) kuhakikisha kuwa inazuia, inapinga na kuondoa dhuluma, vitisho, ubaguzi, unyanyasaji, rushwa, uonevu na upendeleo miongoni mwa wananchi kwa misingi ya itikadi, asili ya mtu, sehemu anayotoka, nasaba, kabila, jinsi, dini au imani yake;		Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 na Katiba ya Zanzibar ya 1984.
	(ii) kuhakikisha uwepo wa amani na kujenga utamaduni wa kuenzi, kuheshimu na kudumisha amani, umoja na utengamano, ushirikiano na uvumilivu wa kisiasa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa madhumuni ya kukuza maendeleo ya kijamii na kiuchumi;		
	(iii) kuhakikisha uwepo wa ulinzi, usalama na ustawi wa watu na mali zao, na kuepuka kufanya jambo lolote litakalohatarisha au kwenda kinyume na lengo hilo;		
	(b) kijamii, Serikali inachukua hatua zinazofaa ili -		
	(i) kuhakikisha kwamba heshima ya binadamu inahifadhiwa na kudumishwa kwa kufuata mila, desturi na Kanuni za Tangazo la Dunia		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuhusu Haki za Binadamu na mikataba mingine ya kimataifa iliyoridhiwa na Tanzania;		
	(ii) kuhakikisha kwamba Serikali na vyombo vyake vyote vya umma vinatoa nafasi na fursa zilizo sawa kwa raia wote, bila ya kujali itikadi, jinsi, rangi, kabila, dini, nasaba, hali ya mtu au mahali alipo;		
	(iii) kujenga utamaduni wa kuwepo ushirikiano, maelewano na maridhiano, uvumilivu na kuheshimu mila, desturi na imani ya dini ya kila		

Trial Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mtu;		
	(iv) kuhakikisha kuwa msaada na hifadhi ya jamii inatolewa kwa watu wasiojiweza, wazee, wagonjwa, watoto na watu wenye ulemavu;		
	(v) kuwezesha upatikanaji na utoaji wa huduma ya msaada wa kisheria kwa wananchi wasiokuwa na uwezo wa kumudu gharama za uwakili;		
	(vi) kuweka utaratibu unaofaa kwa ajili ya kufanikisha utekelezaji wa haki ya mtu kujipatia elimu na kuwa huru		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kupata fursa sawa ya kutafuta elimu katika fani anayoipenda hadi kufikia upeo wowote kulingana na stahili na uwezo wake;		
	(c) kiuchumi,Serikali inachukua hatua zinazofaa ili -		
	(i) kuwaletea wananchi maisha bora kwa kuondoa umaskini;		
	(ii) kuhakikisha kwamba shughuli za Serikali zinatekelezwa kwa njia ambazo zitahakikisha kuwa utajiri wa Taifa unaendelezwa, unahifadhiwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	unatumiwa kwa manufaa ya wananchi wote kwa jumla na pia kuzuia mtu kumnyonya mtu mwingine;		
	(iii) kuweka mazingira bora kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza vyombo vya uwakilishi wa wakulima, wafugaji na wavuvi;		
	(iv) kuweka mazingira bora ya kufanya biashara na kukuza fursa za uwekezaji;		
	(v) kuweka mazingira bora kwa ajili ya kukuza kilimo, ufugaji na uvuvi kwa kuhakikisha kuwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wakulima, wafugaji na wavuvi wanakuwa na ardhi na nyenzo kwa ajili ya kuendeleza shughuli zao;		
	(vi) kuweka mazingira bora ya uzalishaji wa mazao kwa wakulima, wafugaji na wavuvi, utafutaji na uendelezaji wa masoko ya mazao yao;		
	(vii) kuweka utaratibu mzuri wa upangaji na usimamiaji wa mizania ya bei za mazao na pembejeo;		
	(viii) kuimarisha na kuendeleza uwekezaji wa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ndani, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, maeneo ya ufugaji na vifaa vya uvuvi;		
	(ix) kuhakikisha kunakuwa na upatikanaji wa fursa na nafasi za wazi kwa watu wote na kuanzisha shughuli za kiuchumi na kukuza mazingira yaliyo bora kwa ajili ya kuhamasisha sekta binafsi katika uchumi;		
	(x) kuhakikisha kuwa kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi anapata fursa ya kufanya kazi, kwa maana ya kufanya shughuli yoyote halali		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	inayompatia kipato;		
	(xi) kuhamasisha uwekezaji wa pamoja baina ya raia na wasio raia katika miundombinu ya uchumi, uvunaji wa rasilimali na maliasili za Taifa;		
	(xii) kuweka utaratibu wa usimamizi wa kiuchumi na uandaaji wa mipango, kuwezesha malengo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kutekelezwa;		
	(xiii) kuwezesha na kuendeleza matumizi ya sayansi na teknolojia na kukuza ubunifu katika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	shughuli za kiuchumi na maendeleo ya Taifa kwa jumla;		
	(d) kiutamaduni, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili-		
	(i) kulinda na kuhifadhi urithi wa asili, malikale na sehemu zenye umuhimu wa kihistoria au kidini ili kuepuka uharibifu, udhalilishaji, wizi au utoroshaji nje ya nchi;		
	(ii) kulinda, kuhifadhi na kuendeleza tamaduni za watu wa jamii mbalimbali ambazo zinaendeleza na kukuza utu na hadhi yao kwa namna ambayo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	haikinzani na Malengo Muhimu, Misingi ya Mwelekeo wa Shughuli za Serikali na Sera za Kitaifa;		
	(iii) kutambua, kulinda na kuendeleza lugha ya Kiswahili; na		
	(e) kimazingira, Serikali itachukua hatua zinazofaa ili-		
	(i) kuhakikisha kuwa ni haki na wajibu wa kila mtu kulinda na kudumisha mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo;		
	(ii) kuhakikisha kuwa taasisi za umma na asasi za		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kiraia zinawajibika kusimamia utekelezaji na uzingatiaji wa matakwa ya kisheria katika kulinda na kuhifadhi mazingira; (iii) kuhakikisha kuwa wananchi wa Tanzania ndiyo wenye haki ya kumiliki rasilimali za kijenetiki za Tanzania kwa manufaa ya Taifa.		
Ibara ya 11: Utekelezaji wa Malengo ya Taifa.	(1) Malengo ya Taifa yaliyoainishwa ndani ya Katiba hii yatakuwa ni mwongozo kwa Serikali na mamlaka nyingine na kwa kila mwananchi katika matumizi au kutafsiri masharti ya Katiba hii au sheria nyingine yoyote na katika utekelezaji wa uamuzi wa kisera	Madhumuni na Malengo haya ya Taifa ni kuhakikisha kuwa Serikali na mamalaka zake zimepewa mwongozo wa kisera na mwelekeo wa kiutendaji ambao itabidi kusimamia kwa niaba ya wananchi na kutoa fursa kwa wananchi kuweza kuipima serikali	Kuwepo kwa Ibara hii katika Katiba ni kujaribu kujenga umoja, maridhiano na mwafaka wa kitaifa juu ya malengo makuu ya jamii na sera za nchi ili kuepusha mkanganyo na ushindani wa ilani na mikakati ya vyama na sera za kitaifa katika utendaji wa Serikali.

Draft Version www.tanzlii.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa madhumuni ya kujenga jamii iliyo bora, huru na makini. (2) Serikali itatoa taarifa Bungeni si chini ya mara moja katika kila mwaka, kuhusu hatua zilizochukuliwa na mamlaka ya nchi ili kuhakikisha utekelezaji wa malengo ya Taifa yaliyoainishwa katika Katiba hii.	yao. Pia, ni kuweka mwongozo wa dhamira ya malengo ya taifa yaliowekwa katika katiba hii. Halikadhalika, vyama vya siasa vitakavyoshika madaraka vitawajibika kufuata bila kujali sera na ilani ya chama binafsi bali kuongozwa na malengo haya makuu ambayo yatakuwa ni ya kitaifa.	Kuwepo kwa sharti la Kikatiba la Serikali kutoa taarifa kila mwaka ni kuhakikisha kuwa haipuuzi wajibu huo na haiwanyimi wananchi haki ya kujua maeneo hayo makuu, ambayo ni msingi wa taifa, yamesimamiwa vipi mwaka hadi mwaka. Kuhakikisha kwamba malengo haya yanakuwa ndiyo mwongozo kwa Serikali, mamlaka nyingine zote na wananchi kwa ujumla katika kutekeleza maamuzi yaliyo makini kwa lengo la kujenga jamii iliyo bora. Ibara hivi vimekuwemo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya 1977 na kuwa ya mwanzo kufanya hivyo kwa nchi za Afrika Mashariki. Katiba za nchi nyingine zenye Ibara kama hivi ni Philipines, Uganda, Sudan Kusini, Ghana, Kenya na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Namibia.
Ibara ya 12: Sera ya Mambo ya Nje.	(1) Sera ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Muungano inalenga na kuzingatia maslahi ya Taifa na mamlaka kamili ya nchi na kwamba sera hiyo inatekelezwa kwa uwazi ili- (a) kukuza ujirani mwema, ushirikiano wa kikanda na wa kimataifa; (b) kukuza maendeleo na ushirikiano wa kiuchumi wenye tija kwa Taifa na raia wake; (c) kuunga mkono na kuendeleza jitihada za kuimarisha Umoja wa Afrika, sera ya	Kuweka bayana misingi mikuu ya Sera ya Mambo ya Nje na falsafa yake na kuwapa nafasi wananchi kuelewa namna nchi yao inavyojihusha katika mambo ya nje na ushirikiano na mataifa mengine. Kulinda maslahi ya kitaifa na yale ya dola ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutambua nafasi, msimamo na wajibu wa taifa katika mahusiano yetu na taasisi na nchi tunazoshirikiana au kuhusiana nazo. Vile vile kukuza umoja wa Afrika na kujenga utangamano katika Bara la Afrika kuwa ni msingi	Kwakuwa palikuwa na ombwe juu ya Tanzania inavyoshirikiana na mataifa mengine palionekana kuwa na haja ya Ibara hii kwa mara ya kwanza katika Katiba ya Tanzania. Tanzania imekuwa ikiingia katika mahusiano ya makundi na jumuiya mbalimbali na wakati mwingine kujitoa bila ya wananchi kujua msingi wa uamuzi kama huo. Pia, ni kuweka wazi suala la Mambo ya Nje kuwa ni suala la Muungano kwa kupewa hadhi yake katika katiba na kuwawezesha Nchi Washirika kujua nafasi zao katika suala hili la Mambo ya Nje ambapo Serikali ya Jamhuri ya Muungano inatekeleza kwa niaba yao. Sababu nyingine ni kudhihirisha mamlaka kamili ya dola katika medani

Final Version www.bunge.go.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutofungamana na upande wowote na ushirikiano na nchi zinazostawi duniani;	mkuu wa sera yetu ya mambo ya nje.	ya kimataifa. Mifano ya nchi ambazo zimeweka suala la Sera ya Mambo ya Nje katika Katiba zao ni:, Ghana, Kenya, Siera Leone, Sudan Kusini, Switzerland, Uganda and Venezuela.
	(d) kuheshimu sheria za kimataifa;		
	(e) kuzingatia mikataba ya kimataifa na ya kikanda yenye maslahi kwa Jamhuri ya Muungano na kutatua migogoro ya kimataifa kwa njia ya majadiliano, usuluhishi, maridhiano au mahakama;		
	(f) kukuza uzingatiaji wa haki za binadamu na uhuru wa watu;		
	(g) kupambana na makosa ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kimataifa ya jinai; na		
	(h) kuheshimu uhuru wa mataifa mengine.		
	(2) Bunge litatunga sheria, pamoja na mambo mengine, itakayoelekeza na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje.		
SURA YA TATU			
MAADILI NA MIIKO YA UONGOZI NA UTUMISHI WA UMMA			
SEHEMU YA KWANZA – MAADILI YA UONGOZI NA WATUMISHI WA UMMA			
Ibara ya 13: Dhamana ya Uongozi wa Umma.	(1) Madaraka anayopewa kiongozi wa umma:	Ibara hii imewekwa ili kuwawezesha watu wanaotaka	Sababu moja wapo ya kuweka Ibara hii ni kurudisha, kuyahuisha na kuyapa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) ni dhamana na atatumia madaraka hayo na kutekeleza wajibu wake kwa: (i) kuzingatia masharti ya Katiba hii; (ii) kuheshimu wananchi; (iii) kukuza hadhi ya Taifa na kulinda heshima ya ofisi anayoitumikia; na (iv) kukuza imani na heshima ya ofisi kwa wananchi; (b) yanatoa wajibu kwa kiongozi kuwatumikia wananchi. (2) Dhamana ya uongozi na heshima kwa kiongozi wa umma	kugombea au ambao watapata fursa ya kuteuliwa kujua masharti ya Utumishi au Uongozi wa umma ambayo wataingia na wananchi wanaotaka kuwatumikia. Kufanya marekebisho, kuinua hadhi, taswira na sifa ya ofisi ya umma kwa kuweka misingi bora ya viwango, vigezo na uadilifu katika kutumikia umma. Pia kuweka wazi vigezo ambavyo kila anayetaka kujiunga au kuchaguliwa katika utumishi wa umma atapaswa kuvimiza kwa ukamilifu.	nguvu ya kikatiba maadili ya uongozi yaliyokuwa katika Azimio la Arusha na Ahadi za TANU kama ambavyo wananchi wengi walivyotaka wakati wa utoaji wa maoni ya wananchi na katika Mabaraza ya Katiba. Eneo hili ni jipya katika Katiba ya Tanzania ingawa tumekuwa na miongozo, sheria, Tume ya Maadili ya Viongozi na Sekretariati ya Maadili ya Viongozi. Utekelezaji wa yote haya umekuwa dhaifu kwa kukosa nguvu za kikatiba. Wananchi wengi walilalamikia na kuchukizwa na mmomonyoko wa maadili ya umma uliokithiri, rushwa na ufisadi. Watu walizungumzia juu ya haja ya kudhibiti wizi, ufisadi, umangimeza, uzembe, kuweka mbele maslahi binafsi,

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	itazingatia mambo yafuatayo:		utumiaji mbaya wa madaraka na kiburi kwa viongozi na watumishi wa umma. Kwa hali hiyo, Tume ikaona haja ya kukisikiliza kilio cha wananchi. Katiba ya Phililipines ya mwaka 1987 iliweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma kama njia ya kuzuia rushwa na matumizi mabaya ya madaraka. Katiba hiyo imeainisha misingi ya maadili ya uongozi na uwajibikaji. Halikadhalika, Katiba ya Afrika Kusini ya mwaka 1994 ina misingi ambayo inawafanya viongozi wa umma kuwajibika katika kuwatumikia wananchi waliokuwa na matumaini makubwa kwa serikali katika kuboresha maisha yao baada ya miongo kadhaa chini ya Serikali ya kibaguzi. Vilevile Katiba ya Nigeria inaeleza: "*A public officer shall not put himself*
	(a) uteuzi kwa misingi ya mwenendo wa mtu, uwezo, sifa au uchaguzi uliyo huru na wa haki;		
	(b) uwezo pasipo upendeleo katika kufanya uamuzi na kuhakikisha kwamba uamuzi haufuati udugu, ukabila, udini, upendeleo, rushwa au ubaguzi wa aina yoyote;		
	(c) utoaji wa huduma pasipo upendeleo na kwa kufuata maslahi ya umma kwa kuonyesha -		
	(i) uwazi, ukweli na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uaminifu katika utekelezaji wa kazi za umma; (ii) wajibu wa kutangaza maslahi binafsi ili kuepuka mgongano wa maslahi; (d) uwajibikaji kwa umma katika kufanya uamuzi na katika utendaji; na (e) uadilifu, nidhamu na kujituma katika kutoa huduma kwa umma.		*in a position where his personal interests conflict with his duties and responsibilities*." Katiba hiyo inakwenda mbali zaidi kwa kueleza: "*Without prejudice with the foregoing paragraph a public officer shall not receive or be paid the emolument of any public office the same time as he receives or is paid the emulments of any other public office*."
Ibara ya 14: Kanuni za Uongozi wa Umma.	(1) Kiongozi wa umma, akiwa katika kazi za ofisi au kazi binafsi au wakati amejumuika na watu wengine, atahakikisha kwamba	Ibara inakusudia kutenganisha maslahi ya umma na yale ya binafsi, kutunza hadhi na heshima ya ofisi ya umma na kuweka	Sababu moja wapo ya kuwekwa Ibara hii ni kuweka utumishi wa umma wenye heshima na hadhi stahiki. Vile vile kuondoa rushwa, ufisadi na mgongano

Final Version
www.nlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mwenendo wake:	vigezo na viwango vya utumishi juu ya mwenendo wa utumishi wa umma.	wa maslahi ambao kwa sasa umejaa katika mfumo wa utawala. Kwa sababu hiyo Tume imependekeza maadili ya viongozi wa umma na miiko ya viongozi wa umma yawekwe katika katiba mpya. Aidha, Sekretairieti ya Maadili ya Viongozi ibadilishwe kuwa Tume kamili yenye mamlaka ya uwezo wa kusimamia maadili ya viongozi. Rasimu hii inapendekeza kuwepo kwa Tume ya Maadili na Uwajibikaji ili kusimamia suala la maadili ya uongozi.
	(a) hauruhusu kutokea mgongano wa maslahi kati ya maslahi binafsi na maslahi ya utumishi wa umma;		
	(b) hauhatarishi maslahi ya umma kwa ajili ya maslahi binafsi; au		
	(c) haushushi hadhi ya ofisi anayofanyia kazi.		
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kusimamia utekelezaji wa		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	masharti yanayohusu kanuni za uongozi wa umma.		
	(3) Wadhifa wa "Kiongozi wa umma" kama ulivyotumika katika Sehemu hii utajumuisha viongozi wa kuchaguliwa na kuteuliwa kama watakavyoainishwa kwenye sheria za nchi.		
Ibara ya 15: Zawadi katika Utumishi wa Umma.	(1) Kiongozi wa umma wakati anapotekeleza shughuli za kiserikali, akipewa zawadi, zawadi hiyo itakuwa ni mali ya Jamhuri ya Muungano na ataiwasilisha kwa Katibu Mkuu Kiongozi kupitia kwa Katibu Mkuu wa Wizara au kiongozi wa taasisi ya Serikali inayohusika, akiainisha:	Ibara hii inaweka namna ya kushughulikia zawadi hizo na njia bora zaidi ya kudhibiti matumizi mabaya ya ofisi kwa kujipatia zawadi kupitia ofisi ya umma na ambapo hiyo itamfanya kiongozi kuweza kutenganisha dhima binafsi na dhima ya umma kuhusiana na zawadi anazopewa akiwa mtumishi wa umma.	Kujenga utamaduni wa kuhifadhi zawadi zinazotolewa kwa viongozi ili zihifadhiwe kama vile Makumbusho ya Butiama ambayo yametunza zawadi zote alizopewa Mwalimu Nyerere lakini pakiwa na upungufu mkubwa wa taarifa juu ya zawadi walizopewa viongozi wetu wakuu wengine. Kupunguza ushawishi wa kudai au kupewa zawadi viongozi au watendaji

Trial Version www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) aina ya zawadi; (b) thamani ya zawadi; (c) sababu ya kupewa zawadi; na (d) mtu au mamlaka iliyotoa zawadi hiyo. (2) Neno "zawadi" kama lilivyotumika katika Ibara hii linajumuisha kitu chochote chenye thamani atakachopewa Kiongozi wa umma katika utekelezaji wa shughuli za umma. (3) Bunge litatunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine, thamani,	Kujenga utamaduni wa viongozi wetu wa kupeleka zawadi kutunzwa ili ziweze kuhifadhiwa katika sehemu za makumbusho kwa faida ya vizazi vya leo na vijavyo na namna ya kutumia zawadi ambazo zinaweza kuharibika haraka kwa asili yake kwa maslahi ya umma.	na kuathiri maamuzi yao yalalie zaidi ya maslahi ya taifa kwa kuweka maslahi yao binafsi mbele. Tabia ya baadhi ya viongozi kudai zawadi kwa wananchi imekera watu wengi na kutolewa maoni na watu kadhaa wa kadhaa wakati wa kukusanya maoni ya Katiba. Baadhi ya nchi ambazo zimeweka ibara kama hizo katika Katiba zao ni Nigeria ambapo ibara 6 (3) inaeleza: "*Any gift to a public officer on any public or ceremonial occasion shall be treated as a gift to the appropriate institution represented by the public officer*"

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kiwango, aina na uhifadhi wa zawadi kwa Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 16: Akaunti nje ya nchi na Mkopo.	Kiongozi wa umma - (a) hatafungua au kumiliki akaunti ya benki nje ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kwa namna ambayo sheria za nchi zinaruhusu; na (b) hataomba au kupokea mkopo au faida yoyote kwa namna au mazingira ambayo yanashusha hadhi au heshima ya utumishi wa umma.	Ibara hii inakusudia kusisitiza uadilifu na uzalendo katika utumishi wa umma; kupunguza uwezekano wa kutorosha na kuficha fedha nje ya nchi, kupiga vita ufisadi, ubadhirifu na kulinda hadhi ya ofisi ya umma.	Sababu ni kuzuia vitendo ambavyo vimeanza kuota mizizi ndani ya nchi kwa viongozi wa umma kutojali maslahi ya taifa. Wizi na ufisadi umekua ukionekana kuwa ni jambo la kawaida na hata watu kutunzwa na kusifiwa kwa wizi, uporaji na ubadhirifu wa mali ya umma. Halikadhalika, kumekuwa na matukio katika ngazi ya kanda na Bara la Afrika kama vile kufungua akaunti nje ya nchi katika sehemu ambazo inaruhusiwa kuficha fedha kama vile Switzerland, Jersey Island na Island of Man kwa jina maarufu Offshore Accounts na kusababisha kudhoofika vyombo vya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ndani vya fedha na kudhihirisha viongozi wetu kukosa imani kwa wananchi. Nchi ya Venezuela imeweka vifungu imara katika katiba yao kukabili tatizo hilo.
Ibara ya 17: Wajibu wa kutangaza Mali na Madeni.	(1) Kiongozi wa umma atalazimika kutangaza na kuwasilisha, ndani ya siku thelathini baada ya kupata uongozi na baada ya kuacha uongozi, mali na thamani yake na madeni yake katika Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.	Ibara hii itasimamia utekelezaji wa tunu ya uwazi na uadilifu; na kuhimiza uaminifu katika jamii na uongozi na pia kuwezesha wananchi kujenga imani kwa viongozi wao. Kuondoa uwezekano wa viongozi wa umma kujilimbikizia mali kinyume cha sheria.	Ibara hii imelazimika kuingizwa kwenye Rasimu ya Katiba kwa sababu ya uzoefu wa wazi wa matukio kadhaa ambapo viongozi wameonekana kutajirika kwa njia zisizo halali mara tu wanapoingia madarakani na bila ya kuwepo taratibu za kuwawajibisha. Wananchi walitoa maoni kuwa matukio kama ya EPA, Richmond, taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali na taarifa za kibunge, tume zilizoundwa pamoja na kesi zilizo mahakamani ni ushahidi wa madai hayo.
	(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Kiongozi wa umma atalazimika kutangaza na kuwasilisha taarifa ya mali na madeni:		

Trial Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) yake binafsi; (b) ya mwenza wake wa ndoa; na (c) ya watoto wake walio chini ya umri wa miaka kumi na nane, mara moja kila mwaka kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji. (3) Bunge litatunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine: (a) ngazi au orodha ya viongozi wa umma wanaopaswa kutangaza mali na madeni yao; na (b) utaratibu wa kuwasilisha		Katika uzoefu kwenye eneo hili kuna Katiba kadhaa ambazo zimeweka wajibu huu wa kutangaza mali na ni pamoja na Philipines ambapo kwenye Ibara ya 12: "All *members of the Senate and the House of Representative shall upon the assumption of office make full disclosure of their financial and business interest….*"

Trial version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	taarifa ya mali na madeni kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kwa mujibu wa Katiba hii.		
Ibara ya 18: Mgongano wa Maslahi.	(1) Kiongozi wa umma hatashiriki katika kufanya uamuzi wa jambo au shughuli yoyote ambayo ana maslahi nayo yeye binafsi, mwenza wake, mtoto wake, jamaa yake, rafiki au mtu yeyote wa karibu.	Ibara hii inakusudia kuwazuia viongozi wa umma kujinufaisha kwa namna yoyote wakati wa utumishi wao na kupiga vita ubinafsi na upendeleo kwa kutumia nafasi zao. Aidha, inasisitiza utii, uadilifu na umakini katika kazi anayoitumikia na kuepusha kutokea mgongano wa maslahi.	Tume imependekeza kuwepo kwa Ibara hii ili kupigana na tabia inayoota mizizi ya viongozi kujiongezea maslahi na marupurupu, hasa wale wa kisiasa wakiwemo Wabunge. Uzoefu unaonesha kuwa nchi nyingine, zikiwemo Namibia na Nigeria zina ibara kama hizi. Ibara ya 42(1)(2) ya Katiba ya Namibia inakataza viongozi wa umma kutumia nafasi zao kujinufaisha na kujitengenezea maslahi yao na kutumia nafasi au taarifa wanazozipata ili kujinufaisha kibiashara.
	(2) Kiongozi wa umma hatazungumzia kitu chochote katika Baraza la Mawaziri, Bunge, Kamati au chombo kingine chochote rasmi ambacho ana maslahi nacho ya moja kwa moja au vinginevyo, isipokuwa tu kama atatoa taarifa ya		

Final Version
www.uandi.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mgongano huo wa maslahi katika chombo hicho.		
	(3) Itakuwa ni marufuku kwa Kiongozi wa umma kushiriki katika uamuzi unaohusu kuongeza au kuboresha maslahi kwa namna yoyote ile yanayohusu wadhifa alionao, na endapo atashiriki, basi masharti hayo mapya yataanza kutumika kwa kiongozi wa umma atakayekuja baada ya kiongozi husika kuondoka au kumaliza muda wa kukaa katika nafasi ya madaraka, iliyompatia fursa ya kushiriki katika kuamua maslahi husika.		
	(4) Masharti ya ibara ndogo ya (3), hayatamhusu kiongozi wa umma		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ambaye kutokana na asili ya nafasi ya madaraka au aina ya kazi zake anapaswa kushiriki katika upangaji wa mishahara au maslahi mengine ya watumishi wa umma.		
	(5) Kiongozi wa umma hataruhusiwa kushika nafasi za madaraka zaidi ya moja au kutumikia Mihimili ya Dola zaidi ya mmoja kwa wakati mmoja.		
Ibara ya 19: Matumizi ya Mali ya Umma.	Kiongozi wa umma hataruhusiwa kutumia au kuruhusu kutumika kwa mali yoyote ya umma, zikiwemo zilizokodishwa kwa Serikali, kwa madhumuni ya kujipatia yeye binafsi au kumpatia mtu mwingine manufaa yoyote.	Ibara hii inakusudia kudhibiti matumizi mabaya na haramu ya mali ya umma kwa manufaa binafsi. Pia kujenga tabia, nidhamu na utamaduni wa kuheshimu, kuhifadhi na kutunza mali ya umma.	Kumejitokeza matumizi mabaya ya mali za serikali na watu kujiuzia rasilmali za umma kama vile nyumba, viwanda, migodi, mashamba makubwa na mali nyingine. Jambo hili wananchi walilizungumzia sana. Wakati mwingine uuzaji huo wa rasilmali na mali umesababisha migogoro mikubwa.

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Vilevile mali za serikali zimekuwa zikikodishwa nje ya utaratibu na hivyo siyo tu kuikosesha serikali mapato lakini pia kuitia hasara kwa kulipa huduma ambayo haitolewi kwa mfano ukodishaji wa mitambo na kuwapangia hoteli viongozi wa umma. Ibara hii inatakiwa isomwe pamoja na ibara za 7, 49 na 51 za Rasimu hii.
Ibara ya 20: Utekelezaji wa Masharti ya Maadili.	(1) Bunge litatunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine: (a) utaratibu wa utwaaji wa mali za viongozi wa umma zilizopatikana kwa kukiuka sheria; (b) utaratibu wa kumwajibisha	Kuifanya sehemu ya Maadili ya Viongozi kuwa na meno ya kisheria na kukaziwa kikatiba. Pia sehemu hii inakusudia kuwadhibiti na kuwawajibisha viongozi wa umma wanaokiuka maadili na miiko ya uongozi. Kujenga utamaduni na misingi ya	Ibara hii imevuka daraja ambalo halikuweza kuvukwa chini ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za kusimamia maadili zilizokuwepo. Hii inaifanya Serikali na vyombo vya kutunga sheria kulazimika kutunga sheria za usimamizi na urasimishaji wa jambo hili na kama

Final Version www.ilirene.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Kiongozi wa umma aliyekiuka maadili na Miiko ya Uongozi; na (c) uanzishaji wa mitaala inayohusu Katiba, maadili na uraia, shuleni na vyuoni.	uelewa na wajibu wa vijana katika masuala ya kikatiba na kimaadili.	vile Rasimu hii ilivyotangulia kuweka Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji. Sababu nyingine ni kuzuia vitendo vya kujitwalia mali na rasilmali za umma na kupiga vita uroho na uporaji wa mali hizo.
	(2) Masharti yaliyoainishwa katika Sehemu hii ya Sura ya Tatu yatatumika pia kwa watumishi wa umma baada ya kufanyiwa marekebisho stahiki.		
SEHEMU YA PILI - MIIKO YA UONGOZI WA UMMA			
Ibara ya 21: Utii wa Miiko ya Uongozi wa Umma.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, kiongozi wa Umma atapaswa kuheshimu na kutii maadili ya viongozi wa umma, ikiwemo Miiko ya Uongozi.	Ibara hii ipo kwa ajili ya kuainisha maadili na makatazo yanayohusu viongozi wa umma. Pia kuainisha uwajibishwaji wa viongozi hao ikiwa ni pamoja na kusimamishwa	Sehemu hii imekuja kuitikia kilio cha wananchi wengi waliosema kuwa hawaoni hatua imara za kisheria kuchukuliwa dhidi ya viongozi wanaokiuka maadili. Wananchi walidai

Final Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		uongozi watakapokabiliwa na shutuma za kukiuka au kuvunja maadili. Halikadhalika kuweka misingi imara ya kutenganisha biashara na shughuli binafsi na uongozi ili kuepuka mgongano wa maslahi na ukiukwaji wa maadili.	vitendo vya hujuma ya mali ya umma, kufanya biashara wakiwa katika uongozi vimekithiri na wakataka katiba ilisimamie hilo na sheria ziende mbali kudhibiti vitendo hivyo. Hivyo, umeonekana umuhimu wa kujenga utamaduni wa uongozi na uwajibikajiwa pamoja na kupiga vita utumiaji wa nafasi ya uongozi kufanya vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia au wa aina nyingine yoyote. Aidha, sababu nyingine ni kuzuia viongozi wa umma kutumia nafasi zao kujinufaisha wao binafsi. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 52(3)(4) na (5) na Ibara 102 ya Rasimu inayozungumzia uwajibikaji wa pamoja wa Baraza la Mawaziri.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Miiko ya Uongozi inayorejewa katika ibara ndogo ya (1), itakuwa kama ifuatavyo:		
	(a) Kiongozi wa umma hatopaswa -		
	(i) kuvunja au kukiuka masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano;		
	(ii) kutoa au kupokea rushwa;		
	(iii) kujilimbikizia mali kinyume cha sheria;		
	(iv) kusema uongo au kutoa taarifa zisizo za ukweli;		
	(v) kutoa siri za Serikali		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kinyume cha sheria;		
	(vi) kutumia wadhifa, nafasi au cheo chake kwa manufaa yake binafsi, familia yake, ndugu, jamaa au marafiki zake au mtu yeyote aliye na uhusiano naye wa karibu;		
	(vii) kufanya vitendo vya uzembe, uvivu, ubaguzi, kiburi, dharau au unyanyasaji wa kijinsia.		
	(b) Kiongozi wa umma atapaswa kuheshimu na kuendeleza -		
	(i) dhana ya uwajibikaji wa pamoja kwa viongozi wanaohusika; na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(ii) maadili na Miiko ya Uongozi wa Umma, ikijumuisha:		
	(aa) kuwa na tabia na mienendo inayokubalika katika jamii;		
	(bb) kuheshimu, kutunza na kulinda mali za umma; na		
	(cc) kutambua, kuheshimu na kuzingatia Kanuni za Maadili na Mienendo ya Watumishi wa Umma, Kanuni za Kudumu za Watumishi wa Umma, nyaraka za umma na		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	miongozo mbalimbali ya Serikali kuhusu viongozi na watumishi wa umma.		
	(iii) kutenganisha biashara na shughuli binafsi na masuala yanayohusiana na uongozi.		
	(3) Kiongozi wa umma ambaye anatuhumiwa kwa makosa ya:		
	(a) kimaadili;		
	(b) udhalilishaji wa mtu au wa kijinsia; au		
	(c) wizi au ubadhirifu wa mali za umma,		
	atasimamishwa kazi hadi suala lake		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	litakapoamuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi au taratibu nyingine zinazowahusu viongozi wa umma.		
Ibara ya 22: Marufuku ya baadhi ya Vitendo.	(1) Mtumishi wa umma aliye katika ajira ya kudumu hataruhusiwa kuingia katika ajira nyingine yoyote ya kudumu yenye malipo ya mshahara.	Ibara inataka kutenganishwa utumishi wa umma na siasa. Pia inaweka masharti ya kikatiba kuzuia mtumishi wa umma kufanya ajira nje ya ajira ya Serikali na kupata mshahara. Hii inakusudia kuzuia mgongano wa maslahi kwa mtumishi wa umma.	Watoa maoni wengi walitaka watumishi wa umma wanaotaka kugombea nafasi za kisiasa kwanza wasite katika utumishi wao wa umma ili kuepuka kufanya upendeleo katika kujitengenezea mazingira ya kushika nafasi hizo za kisaisa. Halidhalika, kumekuwa na tabia yakuchanganya shughuli za kisiasa na za umma kama vile mawaziri kuwa na nafasi za juu katika chama cha siasa. Kuwepo kwa ibara hii kutasaidia kudhibiti uwajibikaji na hivyo kuongeza ufanisi. Ibara hii isomwe na Ibara ya 125 cha
	(2) Mtumishi wa umma haruhusiwi kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya madaraka katika chama cha siasa au nafasi ya madaraka ya kisiasa ya aina yoyote chini ya Katiba hii.		
	(3) Endapo mtumishi wa umma ataamua kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika-		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) nafasi ya madaraka ya kisiasa ya aina yoyote chini ya Katiba hii; au (b) uongozi wa ngazi yoyote katika chama cha siasa, mtumishi huyo atachukuliwa kuwa utumishi wake umekoma tangu siku ya kuteuliwa kuwa mgombea, kuchaguliwa au kuteuliwa kushika nafasi ya madaraka ya kisiasa au uongozi katika chama cha siasa.		Rasimu hii.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA NNE			
HAKI ZA BINADAMU, WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI			
SEHEMU YA KWANZA – HAKI ZA BINADAMU			
Ibara ya 23: Uhuru, Utu na Usawa Binadamu.	(1) Binadamu wote huzaliwa huru na wote ni sawa. (2) Kila mtu anayo haki ya kuheshimiwa, kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake.	Madhumuni na lengo ni kuweka haki ya msingi ya kutambuliwa, kuheshiwa na kuthaminiwa utu wa mwanadamu katika Katiba. Pia ni kusisitiza uhuru, utu na usawa wa kila mwanadamu. Haki hii ambayo inahusu uhai, inajenga msingi wa kudai haki nyinginezo ambazo zitakuwa zinakiukwa.	Ni muhimu kwa Katiba kutambua na kulinda utu wa mwanadamu ambao ni chemchemu, kiini, kitivo na ndiyo msingi wa haki zote za binadamu. Haki hii inayohusu utu haiwezi kuondolewa kwa hali yoyote ile. Pia Ibara hii inatekeleza masharti ya mikataba mbalimbali ya kimataifa kuhusu haki za binadamu. Ieleweke kwamba nchi ya kwanza duniani kufanya utu wa binadamu kuwa ni haki inayolindwa kikatiba ni Ujerumani. Kwa Bara la Afrika, Katiba ya Jamhuri ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ilikuwa ya kwanza kulinda haki ya utu wa mwanadamu
Ibara ya 24: Haki ya Kuwa hai.	Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata hifadhi ya maisha yake kutoka katika Serikali na jamii kwa mujibu wa sheria za nchi.	Ibara hii inaweka masharti ya kulinda na kuthamini uhai wa mwanadamu na usiondolewe kinyume na masharti ya kikatiba na sheria za nchi.	Sababu ya msingi ni kuhakikisha kuwa hakuna mtu wala chombo chenye mamlaka ya kutoa uhai wa mtu mwingine na hivyo kulindwa kikatiba. Halikadhalika Ibara hii inapanua maana ya uhai na hivyo kuweka msingi wa namna uhai huo unavyoweza kuwekewa mazingira ya kila mtu kuishi na kufaidi kikamilifu haki hii. Mahakama za Tanzania zimekwenda mbali zaidi kupanua dhana hiyo ya haki ya kuishi ikiwa ni pamoja na kuishi katika mazingira safi na salama. Kesi hizo ni pamoja na *Joseph D. Kessy and Others v. City Council of Dar es Salaam. High Court of Tanzania,* Dar es Salaam,

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			9 September 1991 (**Lugakingira J**) na pia ile ya *Festo Balegele and 794 others (Applicants) v. DSM City Council (Respondent) High Court of Tanzania at Dar es Salaam, Misc. Civil Cause No. 90 of 1991*. (**Rubama J**).
Ibara ya 25: Marufuku Kuhusu Ubaguzi.	(1) Watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanayo haki ya kulindwa na kupata haki sawa mbele ya sheria. (2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kubaguliwa na mtu, mamlaka ya nchi au mamlaka yoyote inayotekeleza madaraka yake chini ya sheria yoyote au katika kutekeleza kazi au shughuli yoyote ya mamlaka ya nchi. (3) Ni marufuku kwa sheria yoyote iliyotungwa na mamlaka yoyote	Ibara inalenga kuhakikisha usawa mbele ya sheria ili kuakisi dhamira ya taifa ya kujenga jamii yenye usawa. Pia ni kuweka katazo la kubagua raia katika hali yoyote. Inaweka haki ya kusikilizwa na kujitetea na kuondoa hali ya mtu kutumia nafasi yake kumkomoa mtu mwingine. Ibara pia inakusudia kuzuia vitendo vya ubaguzi kwa kutumia tofauti za watu kama kigezo cha kuwadunisha au kuwanyima haki	Ni kupiga marufuku ubaguzi na vitendo vyote vya kutesa na kutweza binadamu. Vilevile ni kutekeleza wajibu unayowekwa na mikataba mbali mbali ya kimataifa na sera za kibaguzi zinazolenga kuzuia utesaji wa binadamu za ndani ya nchi. Inajenga pia wajibu chanya kwa serikali kusimamia haki hii kuhifadhi na kutekeleza haki.

Ticlvision www.ticlvision.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika Jamhuri ya Muungano kuweka sharti lolote ambalo ni la ubaguzi ama wa dhahiri au kwa taathira yake.	au fursa. Kuchukua hatua za upendeleo maalum kwa kutoa nafuu kwa makundi au watu kutokana na kutengwa kwao.	
	(4) Haki ya raia, wajibu na maslahi ya kila mtu na jumuiya ya watu yatalindwa na kuamuliwa na mahakama na vyombo vinginevyo vya mamlaka ya nchi vilivyowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
	(5) Kwa madhumuni ya masharti ya Ibara hii, neno "kubagua" maana yake ni kutimiza utashi, haki au mahitaji mengineyo kwa watu mbalimbali kwa kuzingatia utaifa wao, kabila, mahali walipotokea, maoni yao ya kisiasa, rangi, dini, jinsi, ulemavu au hali yao katika jamii kwa namna ambayo watu wa		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	aina fulani wanafanywa au kuhesabiwa kuwa dhaifu au duni na kuwekewa vikwazo au masharti ya vipingamizi ambapo watu wa aina nyingine wanatendewa tofauti au wanapewa fursa au faida iliyoko nje ya masharti au sifa za lazima.		
	(6) Neno "kubagua" lilivyotumiwa katika ibara ndogo ya (2), halitafafanuliwa kwa namna ambayo itaizuia mamlaka ya nchi kuchukua hatua za makusudi zenye lengo la kurekebisha matatizo mahsusi katika jamii.		
	(7) Kwa madhumuni ya kuhakikisha usawa mbele ya sheria, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu unaofaa na unaozingatia misingi kwamba -		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) wakati haki na wajibu kwa mtu yeyote vinapohitajika kufanyiwa uamuzi na mahakama au mamlaka nyingine inayohusika, basi mtu huyo atakuwa na haki ya kupewa fursa ya kusikilizwa kwa ukamilifu na pia atakuwa na haki ya kukata rufani au kupata nafuu nyingine ya kisheria kutokana na uamuzi wa mahakama au mamlaka nyingine inayohusika;		
	(b) ni marufuku kwa mtu aliyeshtakiwa kwa kosa la jinai kutendewa kama mtu aliyehukumiwa kwa kutenda kosa hilo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	isipokuwa tu kama itathibitika mahakamani kuwa anayo hatia ya kutenda kosa hilo;		
	(c) ni marufuku kwa mtu kuadhibiwa kwa sababu ya kitendo chochote ambacho wakati alipotenda kitendo hicho hakikuwa ni kosa chini ya sheria; (d) ni marufuku kwa mtu kupewa adhabu ambayo ni kubwa kuliko adhabu iliyokuwapo wakati kosa linalohusika lilipotendeka;		
	(e) kwa ajili ya kuhifadhi haki ya usawa wa binadamu, heshima ya mtu na		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	faragha itahifadhiwa katika shughuli zote zinazohusu upelelezi wa tuhuma na uendeshaji wa mashtaka ya jinai na katika shughuli nyingine ambazo mtu anakuwa katika kizuizi cha mamlaka ya nchi au katika kuhakikisha utekelezaji wa adhabu; na		
	(f) ni marufuku kwa mtu kuteswa, kufanyiwa ukatili au kupewa adhabu zinazotweza au kudhalilisha.		
Ibara ya 26: Haki ya kutokuwa Mtumwa.	(1) Kila mtu ana haki ya kutotendewa au kutotumikishwa kama mtumwa, kutofanyishwa kazi za kulazimishwa	Ibara inapiga marufuku na kukomesha biashara haramu ya kusafirisha binadamu. Inakusudia	Ibara hii inazuia ajira za kutweza na za mateso ambazo zipo katika sekta mbali mbali za ajira ndani na nje ya nchi. Pia

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au kutweza, na kwa msingi huo, ni marufuku kwa mtu: (a) kufanywa au kutendewa kama mtumwa; (b) kulazimishwa kufanya kazi bila hiyari yake; au (c) kusafirishwa kwa nia ya kufanyiwa biashara au faida ya mtu mwingine. (2) Biashara haramu ya kusafirisha na kuuza binadamu ni marufuku katika Jamhuri ya Muungano.	kutukuza na kulinda utu wa kila mtu na kuhakikisha kuwa sheria zinasimamia haki ya mtu kutotiwa katika utumwa.	inazuia utumwa mambo leo ambao umekuwa ukiripotiwa katika vyombo vya habari na katika taarifa za taasisi zinazosimamia haki za binadamu. Ibara hii pia inazuia watu kuchukuliwa na kutiwa katika biashara haramu ya binadamu ndani au nje ya nchi.
Ibara ya 27: Uhuru wa Mtu binafsi.	(1) Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi akiwa mtu huru. (2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi	Kuweka msingi kwa Serikali na vyombo vyake kuheshimu uhuru wa mtu binafsi na mtu ambaye haki yake imechukuliwa kinyume	Pamoja na kuwepo na sheria na taratibu zinazoongoza Serikali na vyombo vyake kujali matakwa ya demokrasia na mipaka inayokubalika katika jamii na

Final Version
www.nlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu katika - (a) hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria; au (b) kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au kutiwa hatiani kwa kosa la jinai.	na utaratibu kuweza kudai fidia**.** Pia kuzuia maamuzi ya Serikali na vyombo vyake kuingilia au kuchukua uhuru wa mtu kinyume cha masharti ya Katiba.	kimataifa kuingilia uhuru wa mtu binafsi, lakini bado tatizo la kukamatwa watu nje ya utaratibu limekuwa likijitokeza. Sababu nyingine ni kuzuia vitendo vya kuhamishwa wananchi kwa sababu mbali mbali na hata kukamatwa, kushtakiwa kwa mashtaka bandia kunakotokea sehemu mbali mbali za nchi yetu**.**
Ibara ya 28: Haki ya Faragha na Usalama wa Mtu.	(1) Kila mtu anastahili kuheshimiwa na kupata hifadhi kwa nafsi yake, maisha yake binafsi na familia yake na nyumbani kwake,	Ibara inalinda na kuheshimu faragha, usalama na mawasiliano ya mtu.	Ibara hii imeingizwa katika Katiba ili kuheshimu faragha na mawasiliano binafsi ya mtu kwa mujibu wa mikataba ya kimataifa. Ibara inamwezesha

Final version www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutoteswa au kudhalilishwa, na pia heshima na hifadhi ya maskani yake na mawasiliano yake binafsi.		mwananchi kulindwa dhidi ya vyombo vya dola na taasisi nyingine kuingilia mawasiliano yake kwa kutumia vyombo vya kisasa vya kiteknolojia na kutumia taarifa hizo dhidi yake bila ya utaratibu wa sheria.
	(2) Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kuhusu hali, namna na kiasi ambacho haki ya mtu ya faragha na ya usalama wa nafsi yake, mali na maskani yake, yanaweza kuingiliwa bila ya kuathiri masharti ya Ibara hii.		
Ibara ya 29: Uhuru wa Mtu kwenda anakotaka.	(1) Kila raia anayo haki ya kwenda kokote katika Jamhuri ya Muungano na kuishi katika sehemu yoyote, kutoka nje ya nchi na kuingia, na pia haki ya kutoshurutishwa, kuhama au kufukuzwa kutoka katika Jamhuri ya Muungano.	Ni kutambua na kuweka masharti na haki ambayo inamuwezesha kutekeleza haki nyingine kama ya kazi, kuabudu na kujumuika. Lengo pia ni kujenga utaifa na utangamano ili kila raia awe na haki ya kuishi popote ndani ya	Hii ni katika kuendelea kudumisha kikatiba uhuru wa raia katika maeneo mbali mbali na kuwawezesha kwenda watakapo.

Trial Version
www.kiuliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Kitendo chochote halali au sheria yoyote yenye madhumuni ya -	Jamhuri ya Muungano.	
	(a) kupunguza uhuru wa mtu kwenda anakotaka na kumweka chini ya ulinzi au kifungoni; au		
	(b) kuweka mipaka kwa matumizi ya uhuru wa mtu kwenda anakotaka ili-		
	(i) kutekeleza hukumu au amri ya mahakama;		
	(ii) kumlazimisha kutimiza kwanza wajibu wowote anaotakiwa na sheria nyingine		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuutimiza; au		
	(iii) kulinda maslahi ya umma kwa jumla au kuhifadhi maslahi mahsusi au maslahi ya sehemu fulani ya umma,		
	hakitahesabiwa au sheria hiyo haitahesabiwa kuwa ni kinyume cha masharti ya Ibara hii.		
Ibara ya 30: Uhuru wa Maoni.	(1) Kila mtu:	Kutambua umuhimu wa uhuru wa maoni kama suala la amani, demokrasia na maendeleo. Pia ni kutambua uhalali wa kutoa maoni na kupata taarifa. Aidha, lengo jingine ni kujenga tabia ya watu kujiona huru, kujieleza, kusikilizwa na kuchangia katika mijadala ya	Moja ya sababu ya Ibara hii ni kuhamasisha watu kujieleza kwa uhuru, uwazi na ukweli bila ya wasiwasi wa kuchukuliwa hatua za kisheria kinyume cha misingi ya haki za binadamu. Pia inawezesha watu kushiriki katika majadiliano yanayojenga utashi wa kisiasa, maridhiano na mwafaka wa
	(a) ana haki na uhuru wa -		
	(i) kuwa na maoni na kueleza fikra zake;		
	(ii) kufanya mawasiliano na kutoingiliwa katika		

Trial Version www.iliana.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mawasiliano yake;	kuchochea maendeleo.	kitaifa juu ya masuala mbalimbali.
	(iii) kufanya ugunduzi, ubunifu na utafiti wa sanaa, sayansi na mapokeo ya asili;		
	(b) anayo haki ya kupewa taarifa wakati wowote kuhusu:		
	(i) matukio mbalimbali muhimu kwa maisha na shughuli za wananchi;		
	(ii) utekelezaji wa mamlaka ya nchi kuhusu sera za kitaifa na shughuli		

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya maendeleo ya jamii; na		
	(iii) masuala mengine muhimu kwa jamii.		
	(2) Utekelezaji wa haki zilizoainishwa katika ibara ndogo ya (1), utajumuisha wajibu muhimu kwa mwananchi na wajibu huo unaweza kupunguza haki hizo kutokana na -		
	(a) vita au machafuko ya kisiasa; au		
	(b) propaganda kuhusu vita, ushawishi wa chuki kwa misingi ya rangi, ukabila, jinsi, itikadi, dini au masuala yoyote		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yanayoweza kuleta madhara kwa Taifa.		
Ibara ya 31: Uhuru wa Habari na Vyombo vya Habari.	(1) Kila mtu ana haki na uhuru wa -	Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kulinda uhuru wa habari na vyombo vya habari. Pia ina lengo la kubainisha uhuru na wajibu wa vyombo vya habari kwa jamii. Lengo jingine la Ibara hii ni kuhamasisha ukuaji wa vyombo vya habari na kuweka mazingira bora ya uanzishaji na uendeshaji wa vyombo vya habari vilivyo huru na vyenye uwajibikaji kwa wananchi na taifa.	Kuimarisha uhuru wa habari ambao ni muhimu kwa ustawi wa mtu binafsi, jamii na taifa. Kujenga mazingira na utamaduni wa serikali na taasisi zake kutoa taarifa kwa umma na hivyo kuwezesha wananchi kushiriki na kujua kinachoendelea katika serikali yao. Pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa na kukidhi viwango na vigezo vya kimataifa vinavyohusu uhuru wa habari na vyombo vya habari. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imeweka haki ya mtu kupewa taarifa wakati wowote kuhusu matukio mbalimbali muhimu ya maisha na shughuli za wananchi na masuala muhimu kwa jamii. Rasimu hii
	(a) kutafuta, kupata, kutumia na kusambaza habari na taarifa; na (b) kuanzisha vyombo vya habari na njia nyingine za upashanaji wa habari bila kujali mipaka ya nchi.		
	(2) Vyombo vya habari vitakuwa huru na vitakuwa na -		
	(a) haki ya kupata, kutumia na kusambaza habari na taarifa wanazozipata;		
	(b) wajibu wa:		

TigiVision
www.tigi.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i) kusambaza habari na taarifa kwa wananchi; na		inakwenda mbali zaidi kwa kuweka uhuru kwa vyombo vya habari na wajibu wake kwa wanachi na jamii na pia kujali utu, heshima na staha ya mtu.
	(ii) kuheshimu na kulinda utu, heshima, uhuru na staha ya wananchi dhidi ya habari na taarifa wanazozitumia, wanazozitayarisha na kuzisambaza.		
	(3) Serikali na taasisi zake, asasi za kiraia na watu binafsi watakuwa na wajibu wa kutoa habari kwa umma juu ya shughuli na utekelezaji wa shughuli zao. (4) Bunge litatunga sheria kwa ajili ya kulinda:		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) haki na uhuru wa vyombo vya habari; na		
	(b) habari na taarifa kwa madhumuni ya usalama wa Taifa, amani, maadili ya umma, haki, staha na uhuru wa watu wengine.		
Ibara ya 32: Uhuru wa Imani ya Dini.	(1) Kila mtu anao uhuru wa mawazo, imani na uchaguzi katika mambo ya imani ya dini na anao uhuru pia wa kubadilisha dini, imani yake au kutokuwa na imani na dini.	Lengo la Ibara hii ni kulinda uhuru na hiari ya mtu kuwa au kutokuwa na imani ya dini na uhuru wa ibada maana suala hili ni la binafsi na siyo la dola wala shuruti yoyote ile. Pia lengo jingine ni kuweka mazingira yatakayowezesha dini zote kutumia uhuru kwa Amani, heshima, uvumilivu na staha kwa dini nyingine ili kulinda umoja na	Katika miaka ya karibuni kumekuwa na matukio, migogoro na mivutano ya kidini kati ya dini moja na dini nyingine au madhehebu kwa madhehebu ndani ya dini moja au makundi ndani ya madhehebu moja. Jambo hili lilizungumzwa na wananchi wengi. Pia wananchi hao walizungumzia sana juu ya kuachia hali itakayopelekea kuingia katika migogoro na mivutano ya kidini kama inavyoonekana katika nchi
	(2) Kazi ya kutangaza dini, kufanya ibada na kueneza dini itakuwa ni huru na jambo la hiari kwa mtu binafsi ilimradi hakiuki sheria za nchi.		

Trial Version www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Shughuli ya uendeshaji wa jumuiya za dini itakuwa nje ya shughuli za mamlaka ya Serikali.	mshikamano katika jamii na taifa.	nyingine. Kwa hivyo Ibara hii inazuia utumiaji wa uhuru wa kutangaza na kueneza dini kufanywa ndiyo sababu na chanzo cha mtafaruku wa kidini. Sababu nyingine ni kuepuka matumizi ya dini kupata manufaa na kutimiza malengo ya kisiasa. Katazo hili ndilo suala jipya katika uhuru wa imani ya dini katika Rasimu hii ikilinganishwa na katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977
	(4) Hifadhi ya haki zilizotajwa katika Ibara hii itakuwa chini ya taratibu zilizowekwa na sheria ambazo ni muhimu katika jamii ya kidemokrasia kwa ajili ya usalama, amani, maadili na umoja wa jamii na wa kitaifa na vitasimamiwa kwa utaratibu ulioainishwa kwenye sheria za nchi.		
	(5) Ni marufuku kwa mtu, kikundi au taasisi ya dini kutumia uhuru wa kutangaza dini kwa namna ambayo italeta uvunjifu wa amani, kujenga chuki au kuchochea vurugu na ghasia kwa madai ya		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutetea imani au dini hiyo. (6) Dini na imani ya dini haitatumika kwa namna yoyote itakayowagawa wananchi, kuleta uhasama au kuharibu amani miongoni mwa wananchi. (7) Neno "dini" kama lilivyotumika katika Ibara hii litatafsiriwa kwamba maana yake ni pamoja na madhehebu ya dini, na maneno mengine yanayofanana au kuambatana na neno hilo nayo yatatafsiriwa kwa maana hiyo.		
Ibara ya 33: Uhuru wa Mtu kujumuika na kushirikiana na Wengine.	Kila mtu anastahili kuwa huru, bila ya kuathiri sheria za nchi, kukutana na watu wengine kwa hiari yake na kwa amani, kujumuika na kushirikiana na watu wengine, kutoa mawazo hadharani, na hasa zaidi kuanzisha au	Kuendeleza uhuru wa raia kujumuika na kushirikiana na wengine katika mambo ya kisiasa, kijamii na kiuchumi. Uhuru huu unamwezesha mtu kutekeleza uhuru wake wa maoni na wajibu	Kuweka msingi wa kikatiba wa wananchi kuanzisha na kuendesha vyama vya siasa, vyama vya ushirika, vyama vya kijamii na makundi yenye malengo yanayofanana. Pia sababu ya kuwa na Ibara hii ni kuweka mazingira ya amani

Trial Version www.iance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kujiunga na vyama au mashirika yaliyoanzishwa kwa madhumuni ya kuhifadhi au kuendeleza imani au maslahi yake au maslahi mengineyo.	wake wa kushiriki katika kuchangia mawazo ya kuleta maendeleo na ustawi wa jamii. Pia, kuweza kufuatilia kupitia makundi hayo maamuzi mbalimbali ya serikali.	na utulivu ili kuwawezesha wananchi kutumia haki hii bila kuingiliwa kinyume cha Katiba na misingi ya kidemokrasia. Ibara hii ni mwendelezo wa Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
Ibara ya 34: Uhuru wa kushiriki shughuli za Umma.	(1) Kila raia wa Jamhuri ya Muungano ana haki ya kushiriki katika shughuli za utawala wa nchi kwa hiari yake, ama moja kwa moja au kupitia wawakilishi waliochaguliwa na wananchi, kwa kuzingatia utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi. (2) Kila raia ana haki na uhuru wa kushiriki kwa ukamilifu katika kufikia uamuzi juu ya mambo yanayomhusu yeye, maisha yake	Lengo la Ibara hii ni kuwawezesha raia kutekeleza na kutumia mamlaka yao juu ya serikali na mambo yote yanayohusu maisha yao.	Haki hii inamhakikishia mtu kujiona anahusika na kujisikia ni sehemu ya jamii kwa kuwa na uhuru wa kushiriki katika maamuzi ikiwa ni pamoja na kuchagua na kuchaguliwa kuwa kiongozi. Pia ni kutoa fursa ya kutoa maoni yao juu ya uendeshaji wa serikali na mikakati ya kuleta maendeleo.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au yanayolihusu Taifa.		
Ibara ya 35: Haki ya kufanya kazi.	(1) Kila mtu ana haki ya kufanya kazi ya kuajiriwa au kujiajiri mwenyewe. (2) Kila mtu ana haki na fursa sawa kushika nafasi yoyote ya kazi, uongozi au shughuli yoyote iliyo chini ya mamlaka ya nchi.	Lengo la Ibara hii ni kumwezesha raia kupata kipato halali kwa kufanya kazi ili kuweza kujikimu yeye pamoja na familia yake. Pia ni kutoa fursa sawa na kuepusha ubaguzi katika upatikanaji wa ajira kwa mujibu wa sifa ya kazi inayohusika. Kutambua kuwa kazi ndiyo inayompa mtu heshima na utu wake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kusisitiza umuhimu wa kuchukua hatua za makusudi kujenga mazingira na kutoa fursa ya kupatikana kwa ajira kwa kuajiriwa au kujiajiri. Mapendekezo haya pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa ikiwemo ile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO). Haki ya kufanya kazi ipo katika Ibara ya 22 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.
Ibara ya 36: Haki za Wafanyakazi na Waajiri.	(1) Kila mfanyakazi ana haki zifuatazo: (a) kufanya kazi bila ubaguzi wa aina yoyote; (b) kupata ujira na malipo	Lengo la Ibara hii ni kutambua na kulinda haki za wafanyakazi na waajiri na kujenga mazingira ya kuondoa mifarakano na kujenga	Kuweka misingi ya wafanyakazi na waajiri katika kujenga uchumi wa nchi. Aidha, sababu nyingine ni kuondoa uonevu, udhalilishaji na unyonyaji

Trial Version
www.nance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	halali kulingana na kiasi na sifa za kazi anayofanya; (c) kuunda au kujiunga na chama cha wafanyakazi mahali pa kazi; na	maelewano kati ya wafanyakazi na waajiri. Hii itasaidia sana kuondoa migogoro ya wafanyakazi.	kazini. Pia ni kutekeleza mikataba ya kimataifa ikiwemo ile ya Shirika la Kazi Duniani (ILO)
	(d) kushiriki katika shughuli za chama cha wafanyakazi.		
	(2) Kila chama cha waajiri na wafanyakazi kitakuwa na haki ya:		
	(a) kuamua kuhusu uongozi, programu na shughuli zake; na		
	(b) kuanzisha, kujiunga na kusimamia shirikisho lao.		
	(3) Kila chama cha wafanyakazi kitakuwa na haki ya kufanya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	majadiliano ya pamoja na mwajiri na kuingia mikataba ya hali bora ya kazi.		
	(4) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu haki za wafanyakazi na utaratibu utakaowezesha wafanyakazi kutumia haki zao.		
Ibara ya 37: Haki ya Kumiliki Mali.	(1) Kila mtu anayo haki ya kumiliki mali na hifadhi ya mali yake aliyonayo kwa mujibu wa sheria za nchi.	Lengo la Ibara hii ni kuweka haki ya kumiliki mali halali na kulipwa fidia stahiki na kwa wakati inapochukuliwa kwa madhumuni yoyote.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha mali za watu hazitaifishwi bila fidia na hivyo kujenga mazingira ya uhakika wa kuchuma na kumiliki mali kihalali. hii itatoa motisha wa kushiriki katika kujenga uchumi wa nchi. Ibara hii inapendekezwa ili kujenga mazingira ya kujenga imani na kuhamasisha uwekezaji wa ndani na nje nchini.
	(2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kuchukuliwa mali yake kwa madhumuni ya kuitaifisha au madhumuni mengine bila ya malipo yanayolingana na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	thamani halisi ya mali hiyo na yatakayotolewa mapema.		
	(3) Kwa madhumuni ya masharti ya Ibara hii, haki ya umiliki na hifadhi ya mali haitahusu mali iliyothibitishwa kwamba haikupatikana kwa njia halali.		
Ibara ya 38: Haki ya Uraia.	Kila raia ana haki ya kutambuliwa uraia wake na kwa madhumuni haya, mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha wananchi kupata hati ya kuzaliwa, kitambulisho cha uraia wake bila ya upendeleo na ubaguzi wa aina yoyote, na pale inapohitajika, nyaraka za kumwezesha kusafiri.	Lengo la Ibara hii ni kuifanya kuwa haki kwa raia kupewa hati ya kuwatambulisha uraia wao kwa madhumuni ya kufaidi haki za kiraia.	Sababu ya mapendekezo ya Ibara hii ni kutoa haki hii muhimu kwa raia. Kwa kuwa ibara ya 29 ya Rasimu hii inapendekeza haki ya raia kwenda anakotaka, ibara hii imewekwa kwaajili ya kuwezesha uhuru huo kutimizwa. Pia ni kuipa serikali wajibu wa kutambua na kulinda raia wake. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 56, 57, 58 na 59 za Rasimu ya Katiba.
Ibara ya 39: Haki ya	(1) Mtu aliyekamatwa au aliyewekwa	Lengo la Ibara hii ni kutambua	Sababu ya mapendekezo haya ni

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mtuhumiwa na Mfungwa.	kizuizini anayo haki ya:	utu, heshima na haki ya mtuhumiwa na mfungwa. Pia ni kuipa wajibu Serikali kuzingatia utu wa watuhumiwa na wafungwa juu ya ubinadamu wao na kuwatendea haki za kibinadamu.	kutekeleza mikataba ya kimataifa juu ya haki za watuhumiwa na wafungwa kwa kuzingatia ubinadamu wao ambao hauondosheki. Haki hii imewekwa kwa mara ya kwanza katika Rasimu hii ya Katiba.
	(a) kuelezwa kwa lugha anayoifahamu au lugha ya alama -		
	(a) sababu ya kukamatwa;		
	(b) haki ya kutokutoa maelezo yoyote; na		
	(c) matokeo ya kutoa maelezo;		
	(b) kutoa maelezo;		
	(c) kuwasiliana na wakili au mtu mwingine ambaye msaada wake ni muhimu kwa mtuhumiwa;		
	(d) kutolazimishwa kutoa		

Final Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	maelezo ya kukiri kosa ambayo yatatumika kama ushahidi dhidi yake; na		
	(e) kupelekwa mahakamani mapema iwezekanavyo.		
	(2) Mamlaka za nchi zitaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha:		
	(a) mtuhumiwa kupata nakala ya mashtaka yanayomkabili na kumbukumbu ya mwenendo wa mashtaka;		
	(b) mtuhumiwa au mfungwa kupata nakala ya mwenendo wa mashtaka na hukumu baada ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	shauri kukamilika mahakamani; na		
	(c) mtuhumiwa au mfungwa kufikishwa mahakamani ili kuthibitisha uwepo wake.		
Ibara ya 40: Haki ya Watu walio chini ya Ulinzi.	(1) Mtu aliye katika kizuizi au ulinzi ataendelea kuwa na haki zote za msingi zilizoainishwa katika Katiba hii kwa kiwango anachostahiki katika mazingira ya kuwekwa kizuizini au katika ulinzi.	Madhumuni ya Ibara hii ni kutunza usalama wa taifa bila ya kuathiri haki za msingi, heshima na utu wa mtu aliyewekwa kizuizini au chini ya ulinzi. Lengo jingine ni kumlinda raia wa Tanzania asipelekwe nje kwa mashitaka kwa shinikizo la mataifa mengine nje ya matakwa ya mikataba ya kimataifa ambayo Tanzania imeridhia.	Sababu ya mapendekezo haya inaiwezesha Serikali kulinda usalama wa nchi na jamii katika misingi inayoheshimu haki za binadamu. Pia kulinda raia wake wasichukuliwe na kupelekwa kushitakiwa nje ya nchi isipokuwa inapokuwa ni kutekeleza matakwa ya sheria za kimataifa. Haki hii imewekwa kwa mara ya kwanza katika Rasimu hii.
	(2) Mtu aliye katika kizuizi au ulinzi ana haki ya kuiomba mahakama ili mamlaka ya nchi inayomuhifadhi kueleza sababu za yeye kuwekwa au kuendelea kuwa katika kizuizi au ulinzi.		

Tanzlii.or.tz
www.tanzlii.or.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Raia wa Jamhuri ya Muungano hatapelekwa katika nchi ya nje yoyote kujibu mashtaka au kufanyiwa mahojiano ya aina yoyote kinyume cha ridhaa yake, isipokuwa kwa mujibu wa sheria za nchi na mikataba ya kimataifa na wajibu wa nchi katika uhusiano wa kimataifa.		
Ibara ya 41: Uhuru na Haki ya Mazingira safi na Salama.	(1) Kila mtu anayeishi katika Jamhuri ya Muungano ana haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya.	Ibara hii inalenga kukuza kiwango bora cha afya na ustawi wa kila raia na kuhakikisha kuwa mazingira yanahifadhiwa na kutumika kwa njia ambazo zitadumisha usafi, usalama na afya njema za jamii. Aidha, inalenga pia kuhamasisha utunzwaji wa mazingira kwa faida ya kizazi cha sasa na vya	Haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya afya haikuwekwa bayana katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Hata hivyo mahakama Kuu katika maamuzi yake ilitafsiri kwamba haki ya kuishi maana yake ni pia kuishi katika mazingira safi, salama na ya afya. Aidha, sheria ya usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191, imeweka
	(2) Haki ya kuishi katika mazingira safi, salama na ya kiafya inahusisha haki kwa kila mtu kutumia maeneo ya umma au sehemu mbalimbali za mazingira yaliyotengwa kwa madhumuni ya		

Final Version www.ilac.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	burudani, elimu, afya, ibada, utamaduni na shughuli za kiuchumi.	baadaye.	kifungu kinachotambua haki hii. Kwahiyo ibara hii inatekeleza maamuzi hayo ya Mahakama na kuipa nguvu Sheria ya Mazingira, Sura 191. Pia, umuhimu wa kuwa na nguvu za kikatiba umekuja kwa sababu ya matukio ya kidunia kama vile mabadiliko ya tabia nchi kunakopelekea mvua zisizo na mpango na kiangazi cha muda mrefu kinachosababisha majangwa. Hali kadhalika kumekuwa na athari za kimazingira kutokana na maendeleo kupitia viwanda na makazi na kuchafua mazingira na baionuai na mara nyingine kushindwa kurejesha mazingira katika hali ya asili. Vile vile kumekuwa na mtindo ulioenea wa katiba nyingi kuweka angalau viwango vya msingi vya kimazingira kwa mujibu wa matakwa ya mikataba ya
	(3) Mtu yeyote anayeishi Tanzania anao wajibu wa kutunza na kuendeleza mazingira na kutoa taarifa kwa mamlaka za nchi kuhusu shughuli au jambo lolote ambalo ni la hatari au lina uwezekano mkubwa wa kuharibu au kuathiri mazingira.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kimataifa. Kwa mfano katiba zenye vifungu vya kulinda na kuhimiza utunzanji wa mazingira ni pamoja na Afrika Kusini, Kenya, Namibia na Uganda.
Ibara ya 42: Haki ya Elimu na Kujifunza.	(1) Kila mtu ana haki ya: (a) kupata fursa ya kupata elimu bora bila ya vikwazo; (b) kupata elimu bora ya msingi bila ya malipo na inayomtayarisha kikamilifu mwanafunzi ama kuendelea na elimu ya ngazi inayofuatia au kuweka msingi wa kuanza kujitegemea; (c) kupata elimu bora	Ibara inakusudia kutambua umuhimu wa elimu bora na fursa sawa kwa gharama zilizo nafuu. Utoaji huo wa elimu kwa mapana yake na unafuu pia kusaidie kujenga jamii iliyoelimika na iliyo makini katika maamuzi na utekelezaji wa shughuli zake katika dunia hii ya utandawazi, teknolojia na ubunifu.	Moja ya sababu ya kuwekwa kwa haki ya elimu na kujifunza ni kutambua kuwa elimu haina mwisho na ni wajibu wa Serikali kuweka mazingira na kutoa fursa kwa raia wake kupata elimu na kujifunza kwa gharama nafuu. Watoa maoni wengi walilalamikia kuongezeka kwa tofauti baina ya walio nacho na wasio nacho na kunavyoathiri fursa na uwezo wa watu wa kipato cha chini kupata elimu. Kumekuwa na tofauti kubwa ya ubora wa elimu kwa shule za vijijini na zile za mijini, na tofauti kubwa zaidi baina ya shule za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	inayotolewa nje ya utaratibu wa umma kwa gharama nafuu; na		Serikali na shule za binafsi. Wananchi pia, walizungumzia kuwa watoto wa viongozi na wenye uwezo wanapata fursa na elimu bora zaidi kuliko watoto wa wakulima na wafanyakazi. Kumekuwa na malalamiko pia kuwa mabadiliko ya mitaala ya mara kwa mara yameleta hasara badala ya faida katika jamii. Tume imetambua hali mbaya ya elimu katika nchi yetu katika nyanja zake zote kama vile walimu, mitaala, vifaa, majengo na kadhalika na ndiyo sababu ya kuweka kipengele hiki. Hii ni mara ya kwanza haki ya elimu na kujifunza kutambulika katika Katiba.
	(d) kupata fursa sawa ya kupata elimu ya juu ilimradi ana sifa stahiki kupata elimu hiyo, bila ya ubaguzi wa aina yoyote.		
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), kila mtu ana haki ya kuchagua taaluma na ajira anayoitaka kwa mujibu wa elimu yake na ujuzi alionao.		
Ibara ya 43: Haki ya Mtoto.	(1) Kila mtoto ana haki ya -	Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kuainisha haki za msingi za mtoto na kuweka utaratibu wa	Ibara hii inatekeleza mkataba wa kimataifa na mkataba wa Afrika juu ya haki ya mtoto na sheria na sera za
	(a) kupewa jina na uraia;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) kutoa mawazo, kusikilizwa na kulindwa dhidi ya uonevu, ukatili na udhalilishaji; (c) kucheza na kupata elimu bora; (d) kuhifadhiwa katika mazingira mazuri, kwa walio katika ukinzani na sheria; (e) kupata lishe bora, huduma ya afya, makaazi na mazingira yanayomjenga kimaadili; (f) kushiriki katika shughuli zinazolingana na umri alionao; na	kisheria utakaowezesha utekelezaji na usimamizi wa haki hizo. Ibara kinaweka wajibu wa moja kwa moja wa wazazi, walezi, jamii na mamlaka za nchi kuona haki hizo kwa ujumla wake zinalindwa na zinatekelezwa kikamilifu. Kuweka mazingira ya kuelekeza kuwepo kwa kizazi chema zaidi kimaadili na kinachoweza kujua wajibu wake ili kukabili mabadiliko ya ndani na nje na kuweza kuchukua nafasi zao katika uchumi na ustawi wa taifa lao.	kitaifa. Kumekuwa na kiwango kikubwa cha unyanyasaji wa watoto nchini, matendo ambayo wakati mwingine yakinasibishwa na Imani za kichawi na kuchangiwa pia na ukosefu wa uwelewa katika jamii. Hivyo kumeonekana umuhimu wa kuweka Ibara hii kwa mara ya kwanza katika Katiba ili wazazi, walezi na jamii kwa ujumla wajue wajibu wao na kujenga hamasa ya kujenga kizazi kinachoepukana na makovu ya manyanyaso.

Trial Version
www.huanic.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(g) kupata malezi na ulinzi kutoka kwa wazazi, walezi au mamlaka za nchi, bila ya ubaguzi wa rangi, utaifa, lugha, mtazamo wa kisiasa, jamii anayotokea, kipato, uzazi, kabila, dini, jinsi au aina nyingine za hadhi.		
	(2) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha utekelezaji na usimamizi wa haki za mtoto kwa kufuata msingi wa kutoa kipaumbele kwa maslahi na manufaa ya mtoto.		
	(3) Itakuwa ni wajibu wa kila mzazi, mlezi, jamii na mamlaka za nchi kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika maadili stahiki		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa umri wao.		
Ibara ya 44: Haki ya Wajibu wa Vijana.	Kila kijana ana haki na wajibu wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo ya Jamhuri ya Muungano pamoja na jamii kwa ujumla, na kwa mantiki hiyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali za Nchi Washirika na jamii zitahakikisha kuwa vijana wanawekewa mazingira mazuri ya kuwa raia wema na kupatiwa fursa za kushiriki kikamilifu katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.	Madhumuni na lengo kuu la Ibara hii ni kutambua nafasi na umuhimu wa vijana kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa lao. Pia ni kuwatayarisha kuwa viongozi na raia wema, kushika uchumi wa nchi yao, kuwa wazazi bora na wana jamii bora kwa ujumla.	Kwa mujibu wa Sensa ya Tanzania iliyofanyika 2012 imeonesha kuwa vijana ndiyo kundi kubwa zaidi la Watanzania kwa asilimia 60 lakini hapajakuwa na kifungu cha katiba kinachotambua nguvu kazi hii. Kwa hivyo Tume imeona haja na umuhimu wa kuweka Ibara hiyo kwa mara ya kwanza ili taifa lijielekeze katika kuhakikisha kwamba nguvu kazi hiyo inatumika kwa njia chanya kwa faida yao na ile ya taifa kwa vijana hao kujua wajibu wao, na kuona na kutumia fursa zilizopo. Pia ulazima wa kuwepo Ibara hii ni kujaribu kama taifa kuwaelekeza vijana katika fikra za kisasa za kiuchumi na kimaendeleo ambazo zinaendana na

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia ili wasiachwe nyuma kuweza kujiajiri au kufanya kazi na kuweza kujiepusha na vitendo vya ukosefu wa maadili na kupoteza utamaduni, silka na mila za Kitanzania. Haki hii inawekwa ndani ya Katiba kwa mara ya kwanza.
Ibara ya 45: Haki za Watu wenye Ulemavu.	(1) Mtu mwenye ulemavu anastahiki: (a) kuheshimiwa, kutambuliwa na kutendewa kwa namna ambayo haishushi utu wake; (b) kupata elimu kwa kutumia vifaa maalum na kushiriki katika shughuli za kijamii;	Lengo la Ibara hii ni kutambua kundi hili ambalo ni asilimia 10 ya wananchi wa Tanzania na kujali upekee wa hali zao. Pia ni kutambua kuwa ni kundi linaloweza kutoa mchango mkubwa katika Taifa na hivyo kuhakikisha serikali inatoa mahitaji maalum na miundo mbinu stahiki ya kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli	Sababu ya kupendekeza haki hii ambayo ni mpya katika Katiba ni kutekeleza mikataba na maazimio ya kimataifa pamoja na sheria na sera za nchi zinazotambua na kulinda haki watu wenye ulemavu. Kwa kiasi kikubwa kundi hili halijapewa umuhimu na jicho linalostahiki na hivyo kuonekana haliwezi kutoa mchango wowote katika jamii. Mapendekezo ya

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) kuwekewa miundombinu na mazingira yatakayowezesha kwenda anapotaka, kutumia vyombo vya usafiri na kupata habari;	zote za jamii kwa mfano elimu, usafiri, uzalishaji, burudani na kadhalika	Rasimu hii ni kuweka nguvu za kikatiba ili hali hiyo irekebishwe. Imeonekana wazi kuwa pale kundi hili linapowezeshwa linaweza kutoa mchango mkubwa katika nyanja mbalimbali. Pia, ni kujenga mazingira ya kundi hili kujiamini na kuona kuwa jamii na taifa linawathamini na hivyo kujitokeza kuchukua fursa ambazo zinaweza kupatikana kwa kutengeneza ustawi wao, familia zao na kutoa mchango maridhawa kwa taifa.
	(d) kutumia lugha za alama, maandishi ya nukta nundu, maandishi yaliyokuzwa au njia nyingine zinazofaa;		
	(e) kusoma, kujifunza na kuchanganyika na watu wengine; na		
	(f) kupata ajira na kugombea nafasi za uongozi katika nyadhifa mbalimbali kwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	usawa.		
	(2) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha watu wenye ulemavu kushiriki katika nafasi za uwakilishi.		
Ibara ya 46: Haki za Makundi Madogo katika Jamii.	(1) Mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha makundi madogo katika jamii:	Ibara hii ni mpya na inalenga kuitambulisha jamii ya Kitanzania, hasa jamii ambazo zinazunguka makundi hayo, ili kujua namna ya kuishi na makundi hayo na kutambua haki zao. Lengo la kuwa na Ibara hii ni kutambua kuwepo kwa makundi hayo na haja ya kuhifadhi maisha na mazingira yao kwa ajili ya maendeleo yao. Ibara pia inataka kudumisha utambulisho wao lakini bila ya kuyaacha makundi hayo	Maoni mbalimbali yalielezea juu ya makundi madogo madogo kuachwa nyuma katika kasi ya maendeleo na mengi yakibakia kuishi katika mazingira ya asili na kuonekana kutengwa. Ibara inataka kubadilisha mtazamo wa Watanzania juu ya makundi hayo kuwafanya watambue kwamba yanaweza kuishi yakiwa na utambulisho wao lakini pia wakajumuishwa katika maisha, mazingira na utamaduni mpana wa Mtanzania. Sababu nyingine ni kukubali ukweli wa upana wa jamii ya
	(a) kushiriki katika uongozi wa mamlaka za nchi;		
	(b) kupewa fursa maalum za elimu na fursa za kujiendeleza kiuchumi na fursa za ajira; na		
	(c) kutengewa maeneo ya ardhi ambayo kwa desturi		

Ticlvic.on
www.nlanc.on

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	makundi hayo huitumia kama eneo la kuishi na kupata riziki ya chakula.	nyuma kimandeleo.	Kitanzania na aina za maisha za makundi mbalimbali.
	(2) Serikali na mamlaka za nchi zitachukua hatua za makusudi za kukuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kuweka miundombinu ya makazi, elimu na afya kwa ajili ya kizazi cha sasa na vijavyo vya jamii ya watu walio katika makundi madogo.		
	(3) Kwa madhumuni ya Ibara hii, "makundi madogo" maana yake ni jamii za watu wanaoishi kwa kutegemea uoto wa asili na mazingira yanayowazunguka kwa ajili ya chakula, malazi na mahitaji mengine ya maisha.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 47: Haki za Wanawake.	(1) Kila mwanamke ana haki ya:	Madhumuni na lengo ni kutambua na kurekebisha mtazamo hasi dhidi ya wanawake juu ya mchango wao na nafasi yao katika jamii. Kuizindua jamii kuwa katika ajira na elimu raia wote wana haki sawa bila kujali jinsi zao, na kwamba kwa kuwa kila mtu hulipwa kwa jasho lake basi mwanamke alipwe sawa na mwanamme kwenye ajira yenye sifa sawa. Aidha, Ibara inalenga kuwalinda wanawake dhidi ya ubaguzi na uonevu na mila zenye madhara. Muhimu zaidi ni kuweka msingi wa Kikatiba kuhakikisha kuwa wanawake wanalindwa katika	Wanawawake ni kundi muhimu katika jamii na lina mahitaji maalum ambayo upatikanaji wake ndiyo uhai wa taifa. Kwa kiasi kikubwa wamekuwa hawana sauti katika vikao vya maamuzi na hali hiyo inapaswa kurekebishwa kwa kutoa fursa ya wanawake kugombea na kushika nafasi kama hizo. Kwa kuwa jamii ya Tanzania bado haina usawa, Ibara hii imewekwa ili kuondoa ubaguzi, ukatili na unyonyaji dhidi ya wanawake. Pia mapendezo haya yanakuja kutekeleza mikataba ya kikanda na kimataifa juu ya haki mbalimbali za wanawake, kwa mfano Convention on Elimination of Discrimination Against
	(a) kuheshimiwa utu wake;		
	(b) kuwa salama dhidi ya unyonyaji na ukatili;		
	(c) kushiriki bila ya ubaguzi katika uchaguzi na ngazi zote za maamuzi;		
	(d) kupata fursa na ujira sawa na mwanaume katika kazi zenye sifa zinazofanana;		

Trial Version www.ntanet.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		jukumu lao la uzazi na kuwekewa msingi wa kikatiba wa upatikanaji wa huduma bora ya afya kwa ustawi wao na wa watoto.	Women (CEDAW) na Protocol to the African Charter on Human and Peoples Rights on the Right of Women in Africa, ambayo Tanzania imeridhia. Haki hizo ni pamoja na kuwa na kiwango cha asilimia 50-50 katika ngazi za uwakilishi na maamuzi. Ibara hii pia inazipa nguvu ya kikatiba haki za wanawake ambazo zimetambuliwa katika sheria na sera mbalimbali za nchi. Nchi ambazo zina vifungu vya kulinda haki za wanawake ni nyingi na kwa kweli Tanzania ilikuwa inaonekana iko nyuma kwa mujibu wa namna ambavyo demokrasia yake imekuwa na kupanuka.
	(e) kulindwa dhidi ya ubaguzi, uonevu na mila zenye madhara; (f) kulindwa ajira yake wakati wa ujauzito na pale anapojifungua; na		
	(g) kupata huduma bora ya afya.		
	(2) Mamlaka za nchi zitaweka utaratibu wa kisheria utakaosimamia masuala yanayohusu utekelezaji wa		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	masharti ya Ibara hii ikiwa ni pamoja na kukuza utu, heshima, usalama na fursa za wanawake wakiwemo wajane.		
Ibara ya 48: Haki za Wazee	Mamlaka za nchi zitaweka utaratibu utakaowezesha wazee kupata fursa ya: (a) kushiriki katika shughuli za kijamii; (b) kuendeleza maisha yao; (c) kutambuliwa utu wao na kuheshimiwa pasipo kudharauliwa; na (d) kupata mahitaji ya msingi kutoka kwenye familia zao, jamii na mamlaka ya	Kuwatambua wazee kuwa ni kundi ambalo lina mahitaji maalum lakini pia wakiwa na uzoefu na ujuzi ambao wanaweza kuutumia kwa faida ya jamii na taifa. Lengo pia ni kuwawezesha wazee kushiriki katika shughuli wanazoweza kufanya, kuheshimiwa na kupatiwa haki zao kama raia.	Kumekuwa na hali ya kuwatenga na kuwadharau wazee, hasa wanawake, katika jamii ya Kitanzania na hata kufikia kuuawa. Wazee wameonekana ni kundi ambalo halina msaada na ni tegemezi. Hivyo Ibara hii inataka kurekebisha muonekano na mtazamo huo. Maoni mengi ya wananchi yalilalamikia kuwa hali ya wazee hasa vijijini ni ya kutisha na inayohitaji hatua za makusudi katika maeneo ya afya, lishe na malazi kwa vile kunakosekana hifadhi ya kinga ya jamii katika ngazi ya taifa. Ibara hii pia inakidhi mahitaji ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nchi.		mikataba ya kimataifa kama vile African Charter of Human and People's Rights ya kuwatunza na kuwalinda wazee na kwa hivyo jukumu lianze kwa mtoto na jamii inayomzunguka.
SEHEMU YA PILI - WAJIBU WA RAIA NA MAMLAKA ZA NCHI NA MIPAKA YA HAKI ZA BINADAMU			
(a) Wajibu wa Raia kwa Taifa			
Ibara ya 49: Wajibu wa Raia.	(1) Kila raia ana wajibu wa: (a) kulinda na kutetea Katiba na sheria za nchi; (b) kulinda na kuheshimu Tunu za Taifa na vitu muhimu vya utambulisho na urithi wa Taifa; (c) kulipa kodi;	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu wajibu wa raia kwa taifa, jamii, watu wengine na mazingira. Aidha, ni kujenga utamaduni wa wananchi kuwajibika na kuchangia katika shughuli zinazohusu maendeleo ya nchi; na kusimamia, kuheshimu na kulinda haki za watu wengine**.**	Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ina Ibara inayohusu wajibu wa raia lakini Rasimu ya katiba imeongeza wajibu wa kulipa kodi, kulinda na kutunza mazingira. Ibara hii ni kutekeleza masharti ya Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu (African Charter of Human and Peoples' Rights) pamoja na maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya

Trial Version www.intans.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(d) kuheshimu haki, uhuru na maslahi ya watu wengine; (e) kuilinda Tanzania na kushiriki katika ulinzi wa Taifa; (f) kulinda na kuheshimu utamaduni na maadili ya Taifa; na (g) kulinda na kutunza mazingira. (2) Bunge linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuwawezesha raia kutekeleza masharti ya Ibara hii.		Tanzania (DPP v. Daudi Pete, Criminal Appeal No. 28 of 1990) ambayo inataka kila raia ajue wajibu wake katika suala la haki za binadamu na watu ambazo msimamizi wake mkuu ni dola**.**
Ibara ya 50: Wajibu wa Kushiriki Kazi.	(1) Kila raia ana wajibu wa: (a) kushiriki kwa kujituma na kwa uaminifu katika kazi	Madhumuni na lengo ni kuhakikisha kuwa kila mwenye uwezo wa kufanya kazi anafanya	Ibara hii inalenga kuwafanya watu waone kuwa kufanya kazi ndio chimbuko pekee la kipato na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	halali ya uzalishaji mali; na (b) kuwa na nidhamu ya kazi na kujitahidi kufikia malengo ya uzalishaji mali yake binafsi na malengo ya pamoja yanayotakiwa au yaliyowekwa na sheria. (2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), kazi yoyote ya shuruti ni marufuku katika Jamhuri ya Muungano. (3) Kwa madhumuni ya Katiba hii, kazi yoyote haitahesabiwa kuwa ni kazi ya shuruti au kazi ya kikatili au ya kutweza endapo kazi hiyo, kwa mujibu wa sheria za nchi ni - (a) kazi ambayo haina budi	kazi na kutumia nguvu kazi yake kwa faida yake na taifa. Aidha Ibara inalenga kupiga marufuku kazi za shuruti, ukatili na kutweza bila ya kuathiri kazi za dharura na zile za lazima kwa mujibu wa sheria na maslahi ya nchi.	kujitegemea, na ni msingi wa utu wa binadamu. Aidha, ni kujenga mazingira ya wananchi kushiriki katika kazi za kujitolea katika suala la ujenzi wa taifa, kazi za dharura wakati wa hali ya hatari au kuokoa maisha ya watu yanapotokea maafa. Maudhui ya Ibara hii yanalingana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya 25 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Live Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ifanywe kutokana na hukumu au amri ya mahakama;		
	(b) kazi ambayo haina budi kufanywa na askari wa jeshi lolote katika kutekeleza majukumu yao;		
	(c) kazi ambayo haina budi kufanywa kutokana na kuwapo hali ya hatari, baa au janga lolote linalotishia uhai na ustawi wa jamii; na		
	(a) kazi au huduma yoyote ambayo ni sehemu ya-		
	(i) majukumu ya kawaida ya		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuhakikisha ustawi wa jamii; (ii) ujenzi wa Taifa wa lazima kwa mujibu wa sheria za nchi; au (iii) jitihada za Taifa za kutumia uwezo wa kila mtu kufanya kazi kwa ajili ya kuimarisha ustawi wa jamii na uchumi wa Taifa na kuhakikisha maendeleo na tija ya kitaifa.		
Ibara ya 51: Ulinzi wa Mali ya Umma.	(1) Kila raia anao wajibu wa kulinda maliasili ya Taifa, mali ya mamlaka ya nchi na mali yoyote inayomilikiwa kwa pamoja na	Ibara hii ina madhumuni na lengo la kuweka masharti kuwa mali ya asili ya mamlaka ya nchi na	Ibara hii imewekwa ili kuhimiza tabia ya kuheshumu na kujali mali na rasilimali zinazomilikiwa kwa pamoja na umma zikiwemo ardhi na maliasili ambayo

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wananchi, na pia kuiheshimu mali ya mtu mwingine. (2) Kila mtu ana wajibu wa kulinda, kuhifadhi na kudumisha rasilimali za nchi na maliasili za Taifa. (3) Kila mtu anao wajibu wa kutunza vizuri mali ya mamlaka ya nchi na mali inayomilikiwa kwa pamoja, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu, na kuendesha uchumi wa Taifa kwa makini kwa kuzingatia mipango endelevu na haki ya vizazi vijavyo.	rasilmali zinalindwa na kuheshimiwa. Aidha, inalenga kujenga moyo wa Watanzania kukataa na kupiga vita uharibu na ubadhirifu.	ndiyo rasilimali kuu ya taifa. Sababu nyingine ni kumfanya kila mtu kujiona kuwa yeye ni mdhamini wa ardhi na maliasili kwa faida ya kizazi cha sasa na vizazi vijavyo. Mabadiliko ya kiuchumi duniani na nchini yamesababisha kujengeka katika mamlaka za nchi na jamii tabia ya ubinafsi, uroho, uvamizi na uchotaji wa rasilmali. Hivyo, Ibara hii itasimamia eneo hilo ipasavyo kwa kujenga uelewa na uzalendo zaidi ili kudhibiti madhara hayo. Ibara hii ya Rasimu ni mwendelezo wa maudhui ya Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.
Ibara ya 52: Haki ya Wajibu Muhimu.	(1) Kila raia wa Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kufaidi haki za msingi za binadamu, na matokeo ya kila mtu kutekeleza wajibu wake kwa jamii, kama	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kuhakikisha haki na wajibu sawa kwa wote. Lengo jingine ni kuziba njia ambapo mtu anapata kazi au cheo kwa misingi	Utekelezaji wa haki za binadamu ulilalamikiwa sana na wananchi na walisema kuwa katika hali halisi kumekuwa na upendeleo na matabaka

Trial Version www.nlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	zilivyofafanuliwa katika Katiba hii. (2) Kila raia katika Jamhuri ya Muungano anayo haki ya kupata hifadhi sawa chini ya sheria za Jamhuri ya Muungano. (3) Mtu yeyote katika Jamhuri ya Muungano hatakuwa na haki, hadhi au cheo maalum kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi wake. (4) Ni marufuku kwa sheria yoyote kutoa haki, hadhi au cheo maalum kwa mtu yeyote wa Jamhuri ya Muungano kwa misingi ya nasaba, jadi au urithi. (5) Ili watu wote wafaidi haki na	ya nasaba, jadi au urithi wake. Pia kunawekwa wajibu wa mtu mmoja mmoja kuheshimu uhuru na haki za watu wengine.	katika suala la utoaji wa haki. Kwahiyo, moja ya sababu ya kuwepo Ibara hii ni kujenga uelewa katika jamii kwamba dhana ya kuheshimu haki za binadamu ni pana na hivyo sio tu wajibu wa Serikali, bali unamhusu kila mtu. Dhana hii pana inawezesha kuwa na jamii ambayo inajali ustawi, haki na maisha ya raia wake. Sababu nyingine ni kuhamasisha na kujenga utamaduni wa raia wa kuchukua hatua pindi katiba inavunjwa na kuendeleza utamaduni huo kwa vizazi vijavyo. Ibara hii inafanana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya 29 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uhuru uliotajwa katika Katiba hii, kila mtu anao wajibu wa kutenda na kuendesha shughuli zake kwa namna ambayo haitaingilia haki na uhuru wa watu wengine au maslahi ya umma.		
	(b) Wajibu wa Mamlaka za Nchi		
Ibara ya 53: Hifadhi ya Haki za Binadamu.	(1) Serikali na mamlaka zote za nchi zinao wajibu wa kuzingatia na kuhifadhi haki za binadamu ikiwa ni msingi wa uhuru kama ilivyoainishwa katika Katiba hii. (2) Haki na uhuru wa kila mtu kama zilivyoainishwa katika Katiba hii zitaheshimiwa, kuhifadhiwa na kudumishwa na mamlaka za nchi, mamlaka binafsi na kila mwananchi. (3) Haki na uhuru ambao umeainishwa katika mikataba ya kikanda na ya kimataifa kuhusu	Lengo ni kuhakikisha kuwa serikali na mamlaka zake zinahifadhi na kulinda haki za binadamu kwa upana wake. Pia ni kujenga tabia ya wananchi kutambua, kudai na kutetea haki zao, za wenzao na za jamii kwa ujumla.	Wananchi wengi walizungumzia juu ya kushuka kiwango cha utekelezaji wa haki za binadamu na kujionyesha sana watendaji wa serikali katika ngazi mbalimbali hasa ngazi za chini kwa kuwa na kiburi katika kutumia nafasi zao. Sababu moja wapo ni kutekeleza masharti ya mikataba ya kimataifa inayotoa wajibu kwa mamlaka ya dola kulinda, kuheshimu na kuendeleza haki za binadamu. Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri

Tirion
www.tirion.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	haki za binadamu ambazo Jamhuri ya Muungano imeridhia, isipokuwa masharti ambayo Jamhuri ya Muungano imeeleza wazi kutojifunga nayo, zitakuwa Sehemu ya Haki za Binadamu zilizoainishwa katika Sura hii.		ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.
Ibara ya 54: Usimamizi wa Haki za Binadamu.	(1) Katika kutafsiri masharti ya Sura hii ya Haki za Binadamu, Mahakama au chombo kingine chochote cha kufanya uamuzi kitazingatia mambo yafuata (a) haki ya usawa, utu na uhuru wa mtu binafsi; (b) sheria za kimataifa na haki za binadamu; na (c) haki za jamii na maslahi ya jamii kwa ujumla. (2) Mtu anayeamini kuwa masharti yaliyomo katika Sura hii yamekiukwa au yanaelekea kukiukwa na mamlaka, chombo	Madhumuni na lengo ni kutoa nguvu za kisheria kwa mtu binafsi, muakilishi wake au kundi kuweza kufungua shauri la haki za binadamu mahakamani. Kuipa wajibu mahakama wa kusimamia na kulinda katiba na kuwa mlinzi na msimamizi mkuu wa haki za binadamu. Mahakama pia inapewa uwezo wa kikatiba wa kubatilisha sheria yoyote iwapo imekwenda kinyume na Katiba.	Mapendekezo haya yanatokana na hukumu mbalimbali za Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani ya Tanzania zilizotafsiri kwa upana na kukazia mashauri mbalimbali ya haki za binadamu. Moja ya hukumu hizo za Mahakama Kuu ni ile ya *W. K. Butambala v. Attorney General (Mwalusanya J)*. Hata hivyo, hukumu hizo na mapendekezo yake hazikuzingatiwa katika mabadiliko ya Katiba ya awali. Sababu ya mapendekezo haya ni

www.tuvision.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	cha uamuzi, sheria au sera yoyote dhidi yake, anaweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa hati maalumu ya maombi kwa mujibu wa sheria za nchi ili kupata nafuu inayohitajika. (3) Mahakama inaweza, kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1) kutoa maelekezo itakayoona yanafaa, kuweka zuio, katazo au kuamuru jambo lifanyike ambalo lilikuwa limenyimwa. (4) Shauri katika Mahakama ya kudai haki za kikatiba kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii yanaweza kufunguliwa na: (a) mtu anayejiwakilisha mwenyewe au taasisi		kuwepo mkanganyiko kuhusu uwezo wa kufungua mashauri mahakamani kudai haki za binadamu kati ya sheria mbali mbali za uendeshaji wa mashauri na katiba. Sababu nyengine ni kuendana na mabadiliko yanayotokea duniani juu ya namna ya kusimamia mashauri ya haki za binadamu ili wananchi wafaidi haki mbali mbali kwa uhakika, uwazi na uhuru. Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	inayowawakilisha wanachama wake;		
	(b) mtu anayemwakilisha mtu ambaye hawezi kujiwakilisha mwenyewe kwa mujibu wa sheria za nchi; au		
	(c) mtu anayewakilisha kundi la watu wenye malengo yanayofanana au jamii ya watu fulani wenye kuvunjiwa haki husika.		
(d)Mipaka ya Haki za Binadamu			
Ibara ya 55: Mipaka ya Haki za Binadamu.	(1) Haki zote zilizoainishwa katika Sura hii ya Katiba endapo zitahitajika kuwekewa mipaka ni	Lengo mojawapo ni kuainisha kikatiba na kuiwekea masharti mipaka ya haki za binadamu	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maamuzi ya mahakama juu ya haja ya katiba kuweka mipaka

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	lazima mipaka hiyo kutumika kwa uwazi na kidemokrasia kwa kuzingatia utu, usawa, uhuru na vigezo muhimu, ikijumuisha:	itakayokuwa ya wazi na kidemokrasia. Hii ina maana kuwa amri ya zuio au masharti yoyote ya kuzuia haki za binadamu pia yawe na mipaka yake.	kuhusu masuala ya haki za binadamu. Kwa maana kuwa kila hatua ya kuzuia uhuru lazima itoe sababu na kueleza mipaka ya uzuiaji huo**.** Moja ya hukumu hizo za Mahakama ya Rufani ya Tanzania ni katika shauri la *Kukutia ole Pumbun & Another v. Attorney General and Another* [1993] TLR. 159. Pamoja na shauri la *Attorney General v. Lohay Akonaay and Joseph Lohay, Court of Appeal of Tanzania, Civil Appeal No. 31 of 1994,* (**Nyalali C.J., Makame and Kisanga JJA**.). Ibara hii inaendeleza maudhui yaliyomo katika Ibara ya 30 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.
	(a) aina ya haki;		
	(b) umuhimu na sababu za kuweka mipaka;		
	(c) asili na ukubwa wa mpaka husika;		
	(d) uhusiano baina ya mpaka husika na sababu yake;		
	(e) njia nyepesi ya kufikia madhumuni ya matumizi ya mpaka husika; na		
	(f) umuhimu wa kulinda		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	usalama wa nchi.		
	(2) Bunge litatunga sheria, ambayo pamoja na mambo mengine, itasimamia matumizi na utekelezaji wa masharti ya Ibara hii.		
SURA YA TANO **URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO**			
Ibara ya 56: Uraia wa Jamhuri ya Muungano.	(1) Mtu ambaye, kabla ya Katiba hii kuanza kutumika, ni raia wa Jamhuri ya Muungano ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.	Lengo la Ibara hii ni kuweka uraia wa Jamhuri ya Muungano kuwa ni mmoja na kutoruhusu raia wa Tanzania awe wa kuzaliwa au wakuandikishwa kuwa raia wa nchi nyingine. Aidha madhumuni ya Ibara hii ni kumpa raia haki ya kutambuliwa, kulindwa, na kupata	Moja ya sababu za mapendekezo haya ni kwamba mamlaka makuu ya kidola (*Sovereign functions*) ni uraia ambalo limewekwa kuwa suala la Muungano. Uraia ni msingi wa utambulisho (*identity*) unaompa hadhi aliyenao kulindwa na nchi yake ikiwa ni pamoja na haki zake za binadamu za asili na
	(2) Uraia wa Jamhuri ya Muungano ni wa aina mbili na utapatikana kwa		

Trial Version www.nlaw.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	njia ya kuzaliwa au kujiandikisha.	huduma mbalimbali anazostahili kupata raia. Lengo jingine ni kuepusha kuwa na uraia wa nchi mbili katika Jamhuri ya Muungano.	zisizoondosheka (*inherent and inalienable rights*) kama zilivyotambuliwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba ya kimataifa. Msingi wa kuweka uraia wa nchi moja ni kuepuka kuwabagua au kuwatenga raia wa Tanzania katika matabaka na madaraja yanayotokana na utofauti wa hali na fursa zao. Ibara hii imezingatia maoni ya wananchi wengi na hasa wa maeneo ya mipakani waliokataa uraia wa nchi mbili kwa sababu za kiusalama, kiuchumi, kimaadili na matumizi mabaya ya rasilimali ya ardhi na uharibifu wa mazingira. Ibara hii ni mpya katika katiba ingawa ipo sheria ya uraia yenye maudhui

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			yanayofanana kwa kiasi kikubwa na Ibara ya Rasimu hii.
Ibara ya 57: Uraia wa Kuzaliwa.	(1) Kila mtu anayezaliwa Tanganyika au Zanzibar atakuwa raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano iwapo, wakati wa kuzaliwa, mama au baba yake ni, au alikuwa raia wa Jamhuri ya Muungano. (2) Kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, mtu aliyezaliwa nje ya Tanzania atakuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa kuzaliwa kuanzia tarehe ya kuzaliwa kwake ikiwa mama au baba yake ni raia wa Jamhuri ya Muungano. (3) Endapo mmoja kati ya wazazi	Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua na kuthamini uraia wa kuzaliwa na haki zake na pia kuupa wajibu na dhamana kubwa.	Uraia wa kuzaliwa umejengwa katika msingi wa uzalendo usiotiliwa shaka (*patriotism*) unaompa raia wajibu wa kuitetea, kuilinda na kuifia nchi yake bila ya tashwishi au shaka. Kwa hiyo uraia ndiyo kigezo na sifa ya kupewa dhamana ya uongozi wa taifa na kuwa katika vyombo na mifumno ya ulinzi na usalama. Madhumuni mengine ni kukiri uwepo wa Watanzania walio nje ya nchi na kuzaa, kuzaliwa na kutambua uzao wa raia wa Tanzania walio nje kuwa ni raia wa kuzaliwa na sio wa kurithi ingawa wamezaliwa nje ya nchi.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	alifariki kabla ya mtu huyo kuzaliwa, uraia wa mzazi huyo wakati wa kifo chake unatumika, kwa madhumuni ya kutambua uraia wa mtu huyo aliyezaliwa baada ya mzazi aliyefariki kama kwamba mzazi huyo alikuwa anaishi hadi kuzaliwa kwa mtu huyo.		
	(4) Mtoto mwenye umri chini ya miaka saba akikutwa ndani ya eneo la Jamhuri ya Muungano katika mazingira ambayo wazazi wake hawajulikani, atachukuliwa kuwa ni raia wa Jamhuri ya Muungano wa kuzaliwa.		
	(5) Endapo uraia wa wazazi wa mtoto aliyepewa uraia chini ya masharti ya ibara ndogo ya (4) utabainika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuwa si uraia wa Jamhuri ya Muungano, uraia wa mtoto huyo utasita.		
Ibara ya 58: Uraia wa Kuandikishwa	(1) Mara baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, mtu ambaye amekuwa mkaazi wa Jamhuri ya Muungano na ambaye ametimiza masharti yote ya sheria za nchi anaweza kuomba kuandikishwa kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.	Lengo la Ibara hii ni kuwatambua watu ambao wamekuwa wakaazi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wana sifa za kisheria za kuomba uraia wa kuandikishwa	Sababu ya mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa raia wa nchi nyingine ambao wapo tayari kuukana uraia wa nchi zao na kuchukua uraia wa Tanzania baada ya kuwa wameishi Tanzania kwa muda maalum uliowekwa na Katiba au sheria, wameoa au kuolewa na raia wa Tanzania na watoto walioasiliwa na raia wa Tanzania kuweza kuomba uraia wa kuandikishwa.
	(2) Mtu aliyefunga ndoa na raia wa Jamhuri ya Muungano na ambaye - (a) amedumu katika ndoa hiyo kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo; na		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) ametimiza masharti yaliyoainishwa katika sheria kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), anaweza kuomba uraia wa kuandikishwa kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.		
	(3) Endapo ndoa iliyotajwa katika ibara ndogo ya (2) itavunjika, kama mtu huyo hakuukana uraia wake wa Tanzania, ataendelea kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano.		
	(4) Mtoto aliyezaliwa katika ndoa iliyorejewa katika ibara ndogo ya (2), atakuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa kuzaliwa.		
	(5) Mtoto aliye na umri wa chini ya		

Final version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	miaka kumi na nane ambaye wazazi wake si raia wa Tanzania, akiasiliwa na raia wa Jamhuri ya Muungano, kwa kuasiliwa kwake huko, kutawezesha mtoto huyo kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano wa kuandikishwa. (6) Bunge litatunga sheria, pamoja na mambo mengine, kusimamia masuala yanayohusu uraia wa Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 59: Hadhi ya Watu wenye Asili au Nasaba na Tanzania.	Bila ya kuathiri masharti yaliyomo kwenye Sura hii, mtu yeyote mwenye asili au nasaba ya Tanzania na ambaye ameacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano kwa kupata uraia wa nchi nyingine, atakapokuwa katika Jamhuri ya Muungano, atakuwa na hadhi kama itakavyoainishwa	Lengo la Ibara hii ni kuwapa hadhi maalum watu walioacha kuwa raia wa Jamhuri ya Muungano tofauti na raia wa nchi nyingine ambao hawana asili au nasaba ya Tanzania.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuwawezesha watu waliokuwa raia wa Tanzania waliopoteza uraia kwa namna yoyote ile kuwa na hadhi maalum wanapokuwa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hadhi hiyo itawaondolea usumbufu wanaporejea Tanzania na kuwapa fursa mbalimbali za

Final Version
www.finance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika sheria za nchi.		kushiriki katika maendeleo ya nchi, jamii na familia zao zilizobaki Tanzania. Mapendekezo haya yalizingatia kuwa nchi itakapotambua uraia wa nchi mbili haitakuwa na msingi wa kikatiba na kisheria wa kuwazuia raia wa nchi nyingine kubaki na uraia wao wanapokuwa raia wa kuandikishwa wa Tanzania kwa kuzingatia kuwa Jamhuri ya Muungano inapakana na nchi nane na italeta changamoto ya usalama na ulinzi. Uzoefu wa nchi ya India na Ethiopia ambazo hazina na zimesita kutoa uraia wa nchi mbili kwa sababu za kiulinzi na usalama lakini zimetoa hadhi maalum kwa watu wenye asili na nasaba ya nchi hizo ambao wameacha kuwa raia wa nchi hizo. Katika Katiba ya India watu hao wanaitwa "Persons of Indian Origin"

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			na wana hadhi maalum. Kwa mujibu wa sheria za India, mtu mwenye asili au nasaba ya India hadi kizazi cha nne atapata hadhi ya "*Person of Indian Origin (PIO)"* isipokuwa kwa raia wa nchi za Afghanistan, Bangladesh, Bhutan, China, Iran, Nepal, Pakistan na Sri-Lanka. Watu hao wenye hadhi ya PIO wanaweza kupata fursa zifuatazo; i. Kupata kadi ya kitambulisho cha PIO. ii. Hahitaji viza ya kuingia na kutoka India. iii. Anaweza kukaa miezi sita nchini India mfululizo bila kulazimika kujiandikisha uhamiaji. iv. Wana haki sawa ya kupata huduma za kiuchumi, kifedha na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			elimu kama ilivyo kwa raia. v. Wana haki ya kununua, kumiliki, kuhamisha, kuuza mali isiyohamishika isipokuwa kwa mashamba makubwa ya kilimo. vi. Watoto wao wanahaki ya kudahiliwa katika vyuo vya elimu ya juu nchini India. vii. Wana haki ya kupata makazi katika utaratibu unaosimamiwa na Serikali au wakala wake. Hata hivyo hawana haki zifuatazo; i. Hawaruhusiwi kupiga kura. ii. Hawaruhusiwi kugombea nafasi yoyote ya kisiasa wala kushika madaraka ya utawala.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA SITA **MUUNDO WA JAMHURI YA MUUNGANO**			
Ibara ya 60: Muundo wa Muungano.	(1) Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakuwa na muundo wa shirikisho lenye serikali tatu ambazo ni: (a) Serikali ya Jamhuri ya Muungano; (b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na (c) Serikali ya Tanganyika. (2) Shughuli za Jamhuri ya Muungano zitatekelezwa na kusimamiwa na: (a) Serikali ya Jamhuri ya Muungano; (b) Bunge la Jamhuri ya Muungano; na (c) Mahakama ya Jamhuri ya Muungano.	Madhumuni na lengo la Ibara hii ni kutambua mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ni Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano, Mamlaka yasio ya Muungano ya Tanganyika na mamlaka yasio ya Muungano ya Zanzibar. Pili kuipa kila mamlaka kuwa na Serikali yake kusimamia maeneo yake yaliotajwa katika Katiba hii ikiwa ni pamoja na vyombo vyake vya utekelezaji na kwa hivyo kutenganisha mamlaka hizo au kuziweka bayana.	Kwa kawaida panapokuwa na muungano wa hiari wa nchi mbili huru na yakaainishwa mamlaka ya mambo ya muungano na mamlaka ya mambo yasio ya muungano, na yakatenganishwa mamlaka ya Mambo ya Muungano na mamlaka mambo yasiyo ya Muungano, muundo huo unapaswa kuwa ni muundo wa shirikisho la Serikali Tatu. Katiba ya Muungano inatambua kuwepo kwa mamlaka hizo tatu katika Ibara za **4, 34 na 64** za Katiba ya Jamhuri ya Muungano, 1977 na kwa upande wa Zanzibar Ibara ambazo zinahusu kukiri kuwepo kwa mamlaka hizo tatu ni za **5A na 99.** Ukweli huu umeelezwa na Mwalimu Nyerere katika kitabu chake cha Uongozi wetu na Hatima ya Tanzania ukurasa wa

Tanzlii www.tanzlii.org

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		Hali kadhalika madhumuni na lengo ya Ibara hii kuweka masharti ya Kikatiba ya kutambua kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano. Vilevile lengo jengine ni kuimarisha na kudumisha Muungano wa hiari wa pande mbili zinazohusika. Pia kuwawezesha Washirika wa Muungano kubaki na utambulisho wao wa kihistoria na kiutamaduni na kuondoa hisia za Zanzibar kumemwa na Tanganyika katika Muungano au utambulisho wa Tanganyika kutoweka kwa kuvaa hadhi ya Muungano.	15, "Nchi mbili zinapoungana na kuwa Nchi Moja mifumo ya kawaida mifumo ya miundo ya Katiba ni miwili: Kwa mfumo wa kwanza kila nchi itafuta serikali yake, na Nchi mpya inayozaliwa itakuwa ni nchi moja yenye serikali moja. Katika mfumo wa pili kila nchi itajivua madaraka Fulani ambayo yatashikwa na serikali ya shirikisho, na itakuwa na serikali ambayo itakuwa na mamlaka juu ya mambo yaliobaki. Mambo yatakayoshikwa na serikali ya shirikisho ni yale ambayo yakibaki katika mamlaka ya nchi zilizoungana, basi kwa kweli nchi hizo zitakuwa hazikuungana kuwa nchi moja, bali zinaendelea kuwa nchi mbili zenye ushirikiano mkubwa katika mambo fulani fulani...Shirikisho halisi la nchi mbili litakuwa ni nchi moja yenye serikali tatu, Serikali ya shirikisho na serikali mbili za zile nchi mbili za awali zilizoungana kuzaa nchi mpya moja." Pia Mwalimu alifafanua zaidi kuhusu
	(3) Muundo, madaraka na mambo mengine ya kiutendaji yahusuyo Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, yataainishwa katika Katiba za Nchi Washirika.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			jitihada za kuundwa kwa Shirikisho la Afrika Mashariki alisema, " kama jambo hilo lingetokea, nina hakika kabisa kwamba mfumo wa nchi mpya ambayo ingezaliwa ungekuwa ni wa Shirikisho; ama shirikisho la Nchi Tatu zenye serikali nne, au Shirikisho la Nchi Nne lenye Serikali Tano. Kwa kweli hata kesho nchi za Afrika Mashariki zikiamua kuungana na Tanzania ikawa ni mshiriki, naamini kuwa ni rahisi zaidi kushirikisha Tanzania yenye Serikali Mbili- ya Zanzibar na Tanganyika- kuliko Tanzania yenye Serikali Mbili, ya Tanzania na ya Zanzibar." Hata hivyo, mamlaka ya Mambo ya Muungano na mambo ya Tanganyika yasiyo ya Muungano yaliwekwa katika Katiba moja na Serikali moja yaani, Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Mamlaka ya mambo ya Zanzibar yasiyo ya Muungano yaliwekwa katika Katiba ya Zanzibar na yanasimamiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muundo wa Muungano unaelezewa katika Ibara ya 60 ya Rasimu ya Katiba, unazingatia matakwa ya kifungu cha 9(2) (a) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba yaliyoielekeza Tume pamoja na mambo mengine kuzingatia kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kudumisha Muungano. Tume imependekeza muundo wa Serikali tatu baada ya kufanya uchambuzi wa takwimu na kuchanganua sababu zilizotolewa na makundi mbalimbali inapendekeza muundo wa Seikali tatu ili: kuitambua Serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano, kuendelea kuitambua Serikali ya Zanzibar, kuondoa kero za muda mrefu zinazotokana na muundo uliopo wa Serikali mbili na kuthamini mapendekezo yaliyotolewa na Tume na Kamati mbalimbali zilizoundwa hapo awali kuhusu mfumo wa Serikali. Muundo huo uliochanganya Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Tanganyika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano kimantiki umeshindwa kueleweka kwa wananchi. Aidha muundo huo ndio chimbuko kuu la ubishi, migogoro mivutano (zinazojulikana kama kero) kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Kiuhalisia, katika utekelezaji wa Mambo ya Muungano, Serikali zote ama kwa kukubaliana au kujiamulia zenyewe zimebadili taswira ya muundo wa Muungano katika utendaji wake ambao umekiuka Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Utata na mkanganyiko unaouzonga Muungano unatokana na kuwepo kwa malalamiko kutoka kila upande wa Muungano. Kwa upande wa Zanzibar baadhi ya malalamiko yao kuhusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano ni: 1. Serikali ya Tanganyika imevaa taswira/koti la Serikali ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muungano ambalo linaisaidia Tanganyika zaidi kuliko Zanzibar. Taswira hiyo imeifanya Tanganyika kuwa ndiyo Tanzania na Watanganyika ndiyo wamekuwa Watanzania; na Wazanzibari wamebaki kuwa Wazanzibari. 2. Mambo ya Muungano yamekuwa yakizidi kuongezeka na hivyo kuathiri uhuru wa Zanzibar (Autonomy) na kufifisha hadhi ya Zanzibar (Identity). 3. Kuvunjwa kwa makubaliano ya Hati ya Muungano kwa kuificha sura ya Tanganyika katika Muundo wa Serikali ya Muungano. 4. Kumuondoa Rais wa Zanzibar kuwa Makamu wa Rais wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. 5. Kutokuwepo kwa uwazi wa mapato na matumizi ya fedha za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Serikali ya Muungano. 6. Kutokuanzishwa kwa Akaunti ya Fedha ya Pamoja. 7. Kuwepo kwa mkanganyiko wa ugawaji wa mapato na jinsi ya kuchangia gharama za uendeshaji wa shughuli za Muungano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Zanzibar. 8. Kuwepo kwa chumi mbili tofauti zinazoshindana katika nchi moja. 9. Zanzibar kutoshirikishwa kikamilifu na Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika masuala ya kupata misaada na mikopo kutoka nje ya nchi. 10. Malalamiko kuwa viongozi wakuu wa Zanzibar wanachaguliwa Dodoma na sio Zanzibar kwenyewe. 11. Zanzibar inalalamika kuwa kuna baadhi ya mambo yamefanywa kuwa ya Muungano kupitia

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kutungwa kwa sheria na Bunge la Jamhuri ya Muungano kwa mambo yasio ya Muungano na baada ya hapo mambo hayo kupata hadhi ya Muungano. 12. Mifano Malalamiko haya ya Zanzibar kwa kiwango kikubwa yanatokana na muundo wenyewe wa Muungano. Kuyaweka mambo ya Tanganyika chini ya Serikali ya Muungano, kumesababisha Serikali ya Muungano kujishughulisha zaidi na mambo ya Tanganyika, hasa mambo ya maendeleo. Serikali ya Jamhuri ya Muungano inashughulikia sana mambo ya kilimo, viwanda na biashara, ujenzi, uchukuzi, mawasiliano, nishati na madini, maji, elimu, huduma za afya na maliasili na utalii ambayo siyo Mambo ya Muungano. Ingawa Bunge ni la Mungano na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kinadharia kutarajiwa kushughulikia mambo ya Muungnao kwa kiasi kikubwa lakini linashughulikia mambo yaliotajwa hapo juu ambayo ni ya Tanganyika kwa uzito mkubwa. Kwa hali hiyo inavyotokea ni kuwa Wabunge kutoka Zanzibar kwenye Bunge la Muungano huwa hawashiriki katika mijadala kwa mambo ya Tanganyika lakini pia huonekana ni kuwapotezea muda Wabunge hao kutoka Zanzibar katika Bunge ambalo linajadili mambo yanayowahusu kwa uchache sana. Wakati wa kikao cha bajeti mambo yanayohusu Tanganyika ndiyo mambo yanayotengewa siku mbili au tatu za majadiliano; wakati Mambo ya Muungano kama vile: ulinzi, mambo ya ndani na mambo ya nje yanatengewa siku moja au nusu siku. Aidha, hata ziara za Kamati za Bunge la Jamhuri ya Muungano kukagua shughuli za maendeleo zinafanywa Tanzania Bara

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			tu. Mambo haya bungeni yanasimamiwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye, kihalisia hana mamlaka wala madaraka yoyote kuhusu Zanzibar. Muundo uliopo sasa wa Serikali mbili pia umesababisha kuwepo kwa wizara au taasisi zenye sura au zinazotekeleza mambo ya Muungano pekee; mambo ya Tanzania Bara na mambo ya mchanganyiko; kwa maana ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano hali ambayo inapelekea ugumu wa kutofautisha gharama za muungano na zisizo za muungano katika wizara au taasisi hizo. Hakuna njia ya kubadili hali hii kwa sababu Serikali ya Muungano haina mamlaka juu ya mambo ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar. Mawaziri katika Serikali ya Muungano wamelazimika kufanya mipango na kutafuta rasilimali kwa ajili ya Tanganyika tu. Zanzibar inalazimika kufanya mipango yake wenyewe na ili

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kupata rasilimali kama vile misaada na mikopo ni lazima ipitie Serikali ya Muungano, jambo ambalo utekelezaji wake una matatizo mengi. Njia pekee ambayo ingefanya mambo ya maendeleo kwa upande wa Zanzibar yapewe uzito sawa na Serikali ya Muungano ingekuwa ni kuyaweka mambo hayo chini ya Serikali ya Muungano, yaani hiyo ingekuwa Serikali Moja badala ya mbili; lakini hilo lingefanyika, Zanzibar ingekuwa imemezwa na Tanganyika. Kwa upande wa Tanzania Bara, baadhi ya malalamiko kuhusu utekelezaji wa Mambo ya Muungano ni haya yafuatayo: 1. Zanzibar imekuwa nchi huru, ina bendera yake, ina wimbo wake wa Taifa, ina Serikali yake na imebadili Katiba yake ili kujitambua kuwa ni nchi. 2. Zanzibar imebadili masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ambayo inasema Sheria za Muungano zinazotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano zitumike sehemu zote za Muungano, badala yake Katiba ya Zanzibar inaelekeza kuwa ili Sheria itumike Zanzibar ni sharti ipelekwe mbele ya Baraza la Wawakilishi. Maana yake ni kuwa, Katiba ya Zanzibar ipo juu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano. 3. Zanzibar imetunga sheria kuhusu fedha ambalo ni suala lililo kwenye madaraka ya Muungano. 4. Zanzibar imetunga Katiba ambayo imechukua madaraka ya Rais yaliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano yanayoeleza kwamba Rais wa Jamhuri ya Muungano ana madaraka ya kugawa nchi katika maeneo ya kiutawala. Marekebisho ya kumi ya Katiba

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ya Zanzibar ya mwaka 1984 yameitambua Zanzibar kuwa ni nchi na yanampa mamlaka Rais wa Zanzibar kuigawa nchi katika maeneo ya kiutawala. 5. Katiba ya Zanzibar inasema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni wa nchi mbili lakini Katiba ya Jamhuri ya Muungano inaeleza kwamba, Tanzania ni nchi moja. 6. Masharti ya Kikatiba yaliyowekwa na Katiba ya Zanzibar kuhusu mchango wa Zanzibar katika uendeshaji wa Mambo ya Muungano yanapingana na masharti ya Katiba ya Muungano. Mifano kwenye Katiba ya Zanzibar 7. Muundo wa Muungano uliopo umepoteza utambulisho wa kihistoria wa Tanganyika na fursa ya watu wa Tanganyika kutetea maslahi yao ndani ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muungano. 8. Wananchi wa Tanzania Bara kutokuwa na haki ya kumiliki ardhi Zanzibar wakati wenzao wa upande wa Zanzibar wana haki hiyo Tanzania Bara. 9. Pia Wabunge wa Tanganyika kulalamika kuwa Wabunge wa Zanzibar huchangia mijadala kwa mambo yasio ya Muungano na ambayo kwa uhakika wake ni mambo ya Tanganyika na kwamba Wabunge wa Tanganyika hawana nafasi ya kuchangia katika Baraza la Wawakilishi kwa mambo yasio ya Muungano na yanayohusu Zanzibar. 10. Kwa mujibu wa Sheria ya Mzanzibari, 1985 Watanzania ambao ni wa Watanganyika hutakiwa kutimiza sifa maalum ili kuweza kupata haki za kiraia huko Zanzibar ilhali Mzanzibari

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			huweza kupata haki ya kiraia wakati wowote na popote katika ardhi ya Tanganyika. Haki hizo za kiraia ni pamoja na kugombea uongozi na kupiga kura. Tangu mwanzo wa Muungano ilikubalika kwamba, Zanzibar ibaki na hadhi yake (identity) na iwe na uhuru wa maamuzi kuhusu mambo yasiyo ya Muungano (autonomy). Katika utekelezaji, Zanzibar imechukua hatua za kuimarisha hadhi yake: kwa maana ya kuwa na Bendera, Wimbo wa Taifa, Nembo na Ukuu wa nchi kamili. Pili kwa makubaliano na Serikali ya Muungano, baadhi ya Mambo ya Muungano yamebadilishwa kwa kiwango kikubwa ili kuipa Zanzibar uhuru wa kuamua (Autonomy). Hivi sasa mambo mengi ya Muungano hayatekelezwi kikamilifu kimuungano. Mambo hayo ni pamoja na kodi, bandari, leseni za viwanda, usafiri na usafirishaji wa anga, utafiti, takwimu, posta na simu, gesi na Mahakama ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Rufani.. Baadhi ya mabadiliko yaliyofanywa yameleta mgongano kati ya Katiba ya Muungano na Katiba ya Zanzibar, hasa kwenye vipengele vinavyohusu kodi, Madaraka ya Bunge kutunga Sheria, Madaraka ya Rais kuigawa Nchi, tafsiri ya nchi na uraia. Mambo haya yamebadilishwa bila kubadili Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977 na kwa maana hiyo mabadiliko hayo yamevunja Katiba. Kuna njia mbili za kurekebisha mambo hayo. Njia ya kwanza ni kuyarudisha chini ya Muungano mambo yote yaliyobadilishwa. Kiuhalisia jambo hili haliwezekani. Serikali zote mbili zilifikia makubaliano kuondoa mgongano wa Katiba kwa mambo fulani, kama vile Madaraka ya Bunge, Uraia na kodi, lakini utekelezaji wake ulishindikana kupitia "Taarifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu jitihada za kuondoa mambo ambayo ni vikwazo katika kutekeleza shughuli za Muungano

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			(Taarifa ya Kamati ya Shelukindo.” Hata hivyo miaka kadhaa baadae Ripoti ya Shelukindo imeshindwa kutekelezwa kwa ukamilifu wake na kubakisha hali ya mivutano na mizozano ndani ya Muungano, kama ambavyo imekuwa kwa Tume nyengine nyingi ambapo inaonekana zaidi mtizamo wa Tume hizo ni kuiridhisha zaidi Zanzibar ibakie ndani ya Muungano kuliko kutafuta suluhu ya kudumu ya kero za Muungano na kuwa na maslahi kwa pande zote mbili za Muungano. Hali inakuwa ngumu zaidi kwa sababu baadhi ya mabadiliko yatahitaji kura ya maoni kwa upande wa Zanzibar. Na hata kama ingewezekana kuyarudisha kwenye Mamlaka ya Muungano, matatizo na kero za Muungano zisingemalizika bali zingeongezeka. Njia ya pili ni kuyakubali mabadiliko yaliyofanywa na kuongeza mengine ambayo yataipa Zanzibar uhuru wa kuamua (Autonomy) mambo yake ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			uchumi. Hili linawezekana lakini likitokea ni lazima Tanganyika nayo ipate uhuru wa kuamua (Autonomy). Kwa maana hiyo kutakuwa na Serikali tatu na Serikali ya Muungano itabaki na mambo ambayo itakuwa na madaraka nayo kamili. Kutokana na malalamiko yanayotolewa na wananchi wa pande zote mbili ambayo Serikali zote mbili zimeshindwa kuyapatia ufumbuzi wa kudumu kwa muda mrefu, baadhi ya wananchi wa Zanzibar wanauona Muungano kuwa ni kero na baadhi ya wananchi wa Tanzania Bara wanauona Muungano kuwa ni mzigo. Aidha, wananchi wa Tanzania kwa kutumia Tume mbalimbali zilizoundwa kwa mfano Tume ya Nyalali na Kamati ya Kisanga walipendekeza Muungano wa Serikali tatu. Maoni hayo ya wananchi yamependekezwa tena mbele ya Tume ya Mabadiliko ya Katiba. Pamoja na maoni hayo, Tume pia,

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ilipitia taarifa mbalimbali za utafiti na uzoefu wa nchi nyingine zenye changamoto za muungano. Katika kutoa mapendekezo hayo yenye lengo madhubuti la kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tume ilizingatia ya wananchi yanayoakisi matakwa na matarajio yao ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Tume nayo ilifanya utafiti na kuandaa ripoti juu ya Muungano inayopatikana katika ripoti za utafiti kuhusu Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tatizo la msingi kabisa kwa Muungano wa Tanzania ni la muundo wenyewe wa Muungano wa Serikali mbili badala ya tatu ambao umetoholewa kutoka mifano ya miungano ambayo imeundwa kutokana na chimbuko la ukoloni kama ilivyokuwa kwa United Kindgodom of Great Britain na Northern Ireland pengine kwa sababu Mwanasheria Mkuu wa Tanganyika wakati huo alikuwa ni

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Rolland Brown ambaye ni Muingereza. Hali kadhalika Muungano kama huo ulilazimishwa kuunda Shirikisho la Malaysia, Sarwak na Borneo ambao ulidumu kwa muda mfupi. Takwimu za Tume zimeonyesha kwamba kwa upande wa Tanzania Bara, 13% walipendelea Serikali moja, 24% walipendekeza Serikali mbili na 61% walipendekeza Serikali tatu. Kwa upande wa Zanzibar, 34% walipendekeza Serikali mbili na 60% walipendekeza Muungano wa mkataba na 0.1% (watu 25) walipendekeza Serikali moja. Aidha, taasisi nyingi kama vyama vya siasa kwa mfano Chadema, CUF, NCCR Mageuzi;asasi za kiraia kwa mfano Legal and Human Rights Centre; - jumuiya za kidini kama Baraza la Maaskofu Tanzania, BAKWATA, Pentecost Council of Tanzania, Christian Professionals of Tanzania, Shuraa ya Maimamu, Baraza la Maimamu Zanzibar; , jumuia za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			wanasheria kama Zanzibar Law Society na Tanganyika Law Society, Law Academics; jumuia za wasomi; jumuia za wafanyakazi Zanzibar Trade Union ZATU, na Tanzania Union TUCTA, zilipendekeza muundo wa Serikali tatu. Baadhi ya taasisi za kiserikali ama moja kwa moja au kwa tafsiri ya mapendekezo yao, pia zilipendekeza serikali tatu. Kwa mfano, Baraza la Wawakilishi Zanzibar lilipendekeza kuwepo kwa mamlaka huru ya Zanzibar, Mamlaka huru ya Tanganyika na Mamlaka ya Muungano na iwekwe wazi maeneo, uwezo, nguvu, utendaji na mipaka ya kila mamlaka; kwa upande wa Makatibu Wakuu wa Zanzibar hali kadhalika kwa tafsiri ya mapendekezo hayo pia yalijitokeza kama vile lilivyoona Baraza la Wawakilishi. Aidha ya Makamo Rais, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii zimependekeza mfumo wa Serikali

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			tatu ili kuondoa kero za Muungano. Aidha, mamlaka ya Mapato Tanzania imependekeza kuwepo kwa Serikali tatu ili kutoa majibu ya kero zilizopo na kuleta utulivu zaidi ilimradi upangiliwe vizuri. Hivyo, muundo unaopendekezwa umezingatia kwamba: unaeleweka kwa urahisi katika ugawanyaji wa madaraka kati ya Mamlaka tatu ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa kila Mamlaka kuwa na Serikali yake; unawezesha nchi Washirika kubaki na utambulisho wao wa kihistoria na kiutamaduni, na hivyo, kuondoa hisia ya Zanzibar kumezwa na Tanganyika ndani ya Muungano na Tanganyika kupoteza utambulisho na uwepo wake; unasaidia kila upande wa Muungano kuendesha mambo yake yasiyo ya Muungano kwa kadri inavyoona inafaa kwa maslahi ya maendeleo na ustawi wa watu katika eneo lake na hivyo kuondoa visingizio dhidi ya muungano; unaleta uwajibikaji

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kwa kila Serikali ya Nchi Mshirika na kuchochea kasi ya maendeleo na kukuza maslahi ya watu katika eneo husika na unapanua zaidi demokrasia kwa kupeleka madaraka kwa wananchi kujiamulia mambo yao. Rasimu hii inaweka vyombo na mfumo wa utatuzi wa mambo ya muungano na pia kuwepo na utaratibu wa kikatiba wa ushirikiano wa mambo yasio ya Muungano. Pia Rasimu inaweka dhahiri dhamana na majukumu na kujua nani mwenye dhamana gani na mamlaka gani na kwa mipaka gani. Hivyo maamuzi yoyote yanaweza kuwa ya kutabirika na sio ya kushtukiza kama ilivyo hivi sasa na kuongeza tija na ufanisi jambo ambalo litaimarisha Muungano. Kwa mujibu wa maoni wananchi wengi waliopendekeza Muungano wa Serikali moja, walisema isipowezekana basi iwe ni Serikali tatu.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 61: Vyombo vya Utendaji vya Jamhuri ya Muungano.	(1) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa ndiyo chombo chenye mamlaka ya utendaji, Bunge litakuwa na mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo ya Muungano na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama itakuwa ni chombo cha utoaji haki. (2) Kila chombo kilichotajwa katika ibara hii kitaundwa na kutekeleza majukumu yake kwa kufuata masharti ya Katiba hii.	Kutambua kikatiba kuwepo kwa mihimili mitatu ya dola na mamlaka zao za kiutendaji ndani ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, madhumuni mengine ni kutenganisha majukumu na mamlaka ya kila mhimili ili kuimarisha misingi ya udhibiti na urari wa madaraka (*checks and balances).* Lengo lingine ni kuviweka vyombo hivi chini ya Katiba kwa kufuata masharti yaliyomo ndani yake.	Dhana ya mgawanyo wa madaraka ni moja ya misingi muhimu ya kikatiba na ukatiba wa nchi inayoheshimu misingi ya demokrasia, utawala wa sheria na uwajibikaji wa serikali kwa raia. Hivyo, Ibara hii inaimarisha dhana hiyo ili kujenga taifa linaloongozwa kwa misingi ya uwajibikaji kwa wananchi na kuheshimu haki za binadamu. Vile vile kuifanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa imara kisiasa na yenye mfumo wa utawala unaoeleweka na kutabirika. Dhana hii imekuwepo katika katiba za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ingawa wakati wa kipindi cha utawala wa chama kimoja (1965-1992) mihimili yote hii iliwekwa chini ya mamlaka ya chama tawala na kutekeleza maamuzi ya chama hata kama yalikuwa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			hayaendani na matakwa ya Katiba. Na baina ya mihimili mitatu hiyo ya dola, mhimili wa utendaji ulipewa mamlaka makubwa zaidi kuliko mihimili mengine miwili iliyobakia.
Ibara ya 62: Mamlaka ya Serikali ya Muungano.	(1) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na mamlaka ya utekelezaji kwa mambo yote yaliyoorodheshwa kuwa Mambo ya Muungano, na wakati inapotekeleza majukumu yake, itazingatia mamlaka yake iliyopewa chini ya Katiba hii. (2) Utekelezaji wa majukumu ya Serikali utafanywa kwa namna na kwa misingi iliyowekwa na Katiba hii au sheria za nchi. (3) Bila ya kuathiri au kukiuka	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya Kikatiba kwa Serikali ya Muungano katika kutekeleza Mambo ya Muungano. Pia kuweka fursa ya kikatiba kwa Nchi Washirika kuweza kukasimu mamlaka yake kutekelezwa na Serikali ya Muungano kwenye mambo yasiyo ya Muungano. Kuiwezesha Serikali ya Shirikisho kutekeleza majukumu yake kiufanisi katika Mambo ya Muungano. Vile vile ni kuweka msingi wa Serikali kutii Katiba	Ibara hii imezingatia kuwa katika miundo ya muungano inayotenganisha mambo ya muungano na mambo yasiyo ya muungano, huyaweka mamlaka yote ya mambo ya muungano kwenye serikali ya muungano. Katika usimamizi na utekelezaji wake mamlaka hayo hayaruhusiwi kukasimiwa au kuingiliwa na mshirika yoyote wa muungano. Huo ndio ukuu wa katiba ya Jamhuri ya Muungano na Serikali yake katika mamlaka ya Muungano. Sababu nyingine ni kuweka msingi kwa Jamhuri ya Muungano kusimamia

www.ilac.or.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	masharti ya Ibara hii, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kwa makubaliano na masharti maalum baina yake na Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Tanganyika, inaweza kutekeleza jambo lolote lililo chini ya mamlaka ya Serikali ya Zanzibar au Serikali ya Tanganyika kwa mujibu wa masharti ya makubaliano hayo.	katika utendaji na shughuli zake.	kikamilifu wajibu wake katika Muungano. Kwa mara ya kwanza Rasimu hii inajenga msingi wa ushirikiano (*cooperation*), mshikamano (*solidarity*) na kufikia kina cha ufanisi (*subsidiarity*) kwa kuweka kipengele cha Nchi Mshirika kuwa na fursa ya kuiomba Serikali ya Muungano kutekeleza mamlaka yaliyo chini yake kuweza kufikia malengo na matakwa yake kwa manufaa na ustawi wa wananchi. Dhana hii inasaidia zaidi kujenga muungano kwa vile inaweka mkazo kwa Serikali Jamhuri ya Muungano kutafuta kila njia kufanya kazi na Serikali za Nchi Washirika, na pia Serikali za Nchi Washirika kuwa karibu zaidi na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia kujenga na kudumisha utamaduni wa Nchi

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Washirika kuweza kushirikiana baina yao. Kwa hiyo, kwa mujibu wa Rasimu ya Katiba mamlaka ya Serikali ya Tanganyika au Serikali ya Zanzibar ni kwa mambo yasiyo ya Muungano tu na siyo vinginevyo.
Ibara ya 63: Mambo ya Muungano.	Kwa ajili ya utekelezaji bora wa shughuli za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na kwa ajili ya mgawanyo wa madaraka juu ya shughuli hizo baina ya vyombo vilivyotajwa katika Ibara ya 61, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na mamlaka juu ya mambo ya Muungano kama yalivyoorodheshwa katika Nyongeza ya Katiba hii.	Lengo la Ibara hii ni kuainisha na kutofautisha Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano ili kuleta ufanisi wa utekelezaji. Kwa kupunguza mambo ya Muungano kunaondoa kero zilizotokana na kuongezeka kwa Mambo mengi ya Muungano. Kurudi kwenye mambo ya msingi ya muungano yenye sifa ya kutambulisha mamlaka ya dola	Kwa mujibu wa Ibara hii ya Rasimu ya Katiba, Mambo ya Muungano yaliyopendekezwa ni saba badala ya 22 yaliyoorodheshwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Mambo mengine yaliyozingatiwa katika Rasimu hii ni kuhakikisha mambo makuu ya kidola (*Sovereign Functions*) yanabaki chini ya Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano. Mambo hayo ndiyo yanayoitambulisha nchi katika medani za sheria na

Final Version
www.katiba.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		(*sovereign functions*) na kwenye dhana ya asili ya Waasisi wa Muungano kama yalivyoainishwa kwenye Hati ya Muungano ya 1964. Muhimu zaidi ni kuweka mipaka ya kikatiba kwa mamlaka	mahusiano ya kimataifa na ndani ya nchi hayana budi yawe ya Muungano. Rasimu hii imezingatia mambo 11 ya awali yaliyokuwemo katika Hati ya Makubaliano ya Muungano na Katiba ya awali ya Jamhuri ya Muungano. Hata hivyo, masuala ya Bandari na Usafiri wa Anga ambayo ni Mambo ya awali ya Muungano yameachwa katika orodha mpya ya Mambo ya Muungano kwa sababu hayajawahi kutekelezwa kimuungano kwa makubaliano ya Serikali mbili. Mambo mengine ya Muungano yaliyoachwa ni yale 11 yaliyoongezwa baadaye ambayo ndio yamekuwa chanzo cha malalamiko na kero za Muungano. Kigezo kilichotumika katika kuamua Mambo ya Muungano katika Rasimu hii ni pamoja na kuhalalisha makubaliano

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au kwa hatua zilizochukuliwa na upande mmoja wa Muungano kutekeleza au kutokutekeleza Mambo ya Muungano bila ya kubadilisha Katiba. Mapendekezo haya yanakidhi haja ya wananchi walio wengi waliotoa maoni yao ya kutaka kuondoa kero za Muungano ambazo kwa kiasi kikubwa zimetokana na muundo wa Serikali mbili kwa kukosekana kwa mipaka iliyo wazi baina ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya muungano. Jumla ya maoni 2,452 yalitolewa katika pande zote mbili za Muungano juu ya Orodha ya Mambo ya Muungano. Maoni 6 katika kila 10 (61.9 asilimia) yalitaka mambo ya Muungano yapunguzwe hasa kutoka Tanzania Zanzibar. Waliotaka

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mambo yapunguzwe kutoka Tanzania Zanzibar ni asilimia 79.3 na kutoka Tanzania Bara ni asilimia 44. Rasimu inapendekeza katika hali mpya ya kuwa na mambo machache ya Muungano ambayo yataweka mipaka baina ya Serikali zote tatu
Ibara ya 64: Nchi Washirika.	(1) Kwa mujibu wa Katiba hii, Nchi Washirika ni Tanganyika na Zanzibar. (2) Serikali ya Tanganyika itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano yanayohusu Tanganyika. (3) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano	Madhumuni ya Ibara ni kutambua kuwepo kwa Nchi Washirika zinazounda na kuipa uhalali wa Jamhuri ya Muungano. Lengo la Ibara hii pia ni kuainisha hadhi na haki ya kila Nchi Mshirika ndani ya Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia usawa na ukweli kwamba Muungano huu ni wa hiari. Hadhi na haki inayotajwa hapa siyo ya usawa wa mahitaji	Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inatambua Nchi Washirika katika Ibara ya 4, 34, 64, 102. Aidha Ibara ya 151 inatamka kuwa Tanzania Bara maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa eneo la Jamhuri ya Tanganyika na Tanzania Zanzibar maana yake ni eneo lote la Jamhuri ya Muungano ambalo zamani lilikuwa ni eneo la Jamhuri ya Watu wa Zanzibar. Hivyo

Final Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yanayohusu Zanzibar. (4) Nchi Washirika zitatekeleza majukumu yao kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii na Katiba zao. (5) Nchi Washirika zitakuwa na hadhi na haki sawa ndani ya Jamhuri ya Muungano na zitatekeleza majukumu yao kwa mambo yote yasiyo ya Muungano katika mamlaka ya Nchi Washirika kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na Katiba za Nchi Washirika.	na kuchangia bali ya usawa na uhuru kwa maana kuwa kila moja ilikuwa nchi kamili ilipojiunga na Muungano.	moja ya sababu ya Ibara hii ni kuendeleza dhana hii ya kihistoria. Sababu nyingine ni kuweka wajibu wa msingi wa kuleta maendeleo na usatwi wa watu wa kila upande wa Muungano chini ya mamlaka ya Nchi Mshirika husika. Aidha, sababu ya Ibara hii pia ni kuitikia madai ya wananchi kutaka utambulisho rasmi na wa wazi kwa kila Nchi Mshirika katika Muungano. Takwimu za maoni ya wananchi kuhusu suala hili zimo katika Ripoti ya Tume, "Takwimu za Ukusanyaji wa Maoni ya Wananchi Kuhusu Mabadiliko ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania", Sura ya Nne, Eneo la Muungano, hoja 4.2.2, Hadhi za Washirika wa Muungano kwa Sehemu Mbili za Muungano.
Ibara ya 65: Mamlaka ya	1. Kila Nchi Mshirika wa Muungano	Madhumuni ya Ibara hii ni	Katiba hii inabainisha kuwa Nchi

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Nchi Washirika.	itakuwa na mamlaka na haki zote juu ya mambo yote yasiyo ya Muungano, na katika utekelezaji wa mamlaka hayo, kila Nchi Mshirika wa Muungano itazingatia misingi ya ushirikiano na mshirika mwingine kwa kuzingatia haki na usawa kwa ajili ya ustawi ulio bora kwa wananchi wa pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano. 2. Bila ya kuathiri mipaka iliyowekwa na Katiba hii, kila Nchi Mshirika wa Muungano itakuwa na uwezo na uhuru wa kuanzisha mahusiano au ushirikiano na jumuiya au taasisi yoyote ya kikanda au kimataifa kwa mambo yaliyo chini ya mamlaka yake kwa mujibu wa Katiba ya Nchi Mshirika wa	kuainisha mamlaka na haki ya kila Nchi Mshirika wa Muungano ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano; kuziwezesha Nchi Washirika kusimamia na kutekeleza mambo yasiyo ya Muungano katika maeneo yao; pia kuziwezesha kikatiba Nchi Washirika wa Muungano kutekeleza masuala ya ushirikiano wa kimataifa katika maeneo yasiyo ya Muungano na kuepusha migongano inayoweza kutokea kati ya Nchi Washirika na Jamhuri ya Muungano au Washirika wa Muungano wenyewe kwa wenyewe.	Washirika wa Muungano zitakuwa na mamlaka juu ya mambo yote yasiyo ya muungano yanayohusu Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa juu ya mambo yote yasiyo ya muungano yanayohusu Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, Nchi Washirika wa Muungano zitakuwa na mamlaka kamili ya kutekeleza mambo yote yasiyo ya Muungano ikiwa ni pamoja na kuanzisha ushirikiano na jumuiya au taasisi yoyote ya kikanda au kimataifa kuhusiana na mambo hayo kwa mujibu wa Katiba. Aidha, Rasimu inapendekeza Nchi Washirika kuruhusiwa kuomba ushirikiano kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kufanikisha suala hili. Jukumu la Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika suala hili ni

Tanzlaw.com
www.tanzlaw.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano.		kufanikisha utekelezaji wake. Mapendekezo haya yamezingatia kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni taifa moja lenye dola moja. Aidha, yanatambua hadhi na haki sawa za Nchi Washirika wa Muungano na kuweka utaratibu utakaorahisisha na kuharakisha juhudi za kuleta maendeleo na ustawi wa wananchi katika Jamhuri ya Muungano. Mapendekezo haya pia yanaweka msingi wa mshikamano (*Solidarity Principle*) baina ya Nchi Washirika. Moja ya sababu za mapendekezo haya ni hoja kwamba Zanzibar inastahili kuwa na mamlaka ya kujihusisha na masuala ya kimataifa ili kukuza maslahi yake. Inadaiwa kuwa hali ya sasa ambapo masuala yote ya mambo ya nje na ushirikiano wa kimataifa ni masuala ya
	3. Nchi Mshirika wa Muungano inaweza, wakati wa kutekeleza majukumu yake chini ya ibara ndogo ya (2), kuomba mashirikiano kutoka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kufanikisha mahusiano na jumuiya au taasisi ya kimataifa au kikanda, na Serikali ya Jamhuri Muungano inaweza kutoa ushirikiano kwa Nchi Mshirika wa Muungano kwa namna itakavyohitajika.		
	4. Bunge litatunga sheria itakayoainisha, pamoja na mambo mengine, utaratibu wa namna ya utekelezaji bora wa masharti ya Ibara hii.		

Final Version
www.iliuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muungano, Zanzibar inapungukiwa na fursa za kujistawisha kimaendeleo. Hivyo, imeonekana haja ya kutenganisha masuala ya mambo ya nje (*International Relations*) nay ale ya ushirikiano wa kimataifa (*International Co operation*) ili kutoa fursa pana kwa Nchi Washirika kushughulikia ustawi wa kimaendeleo wa maeneo yao. Sababu nyingine ni kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haitakuwa ya kwanza duniani kuruhusu washirika wake kuwa na mashirikiano ya kimataifa. Nchi za Marekani, Ujerumani, Canada, Austria na Uswisi zimeruhusu washirika wao wa Muungano kujihusisha na masuala ya ushirikiano wa kimataifa kwa njia mbalimbali kama vile kwenye masuala ya mikataba, kufanya ziara, kutafuta na kutoa misaada na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kuwasiliana na wadau mbalimbali wa kimataifa. Washirika wa Muungano wamekuwa wakiendesha shughuli za uhusiano wa kimataifa moja kwa moja kwa hadhi zao kama Washirika wa Muungano kwa mambo yaliyopo kwenye mamlaka zao na siyo shughuli za asili za nchi huru kama vile ulinzi na usalama (*strategic and security matters*). Mara nyingi masuala hayo yamekuwa yakihusiana na masuala yanayo wakabili katika maeneo yao ya utawala kama vile utamaduni, mazingira, biashara na masuala ya maendeleo kwa jumla. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 66 na 67.
Ibara ya 66: Mahusiano	(1) Kila Nchi Mshirika inaweza, katika kutekeleza majukumu yake katika	Ibara hii inalenga kuweka utaratibu wa kikatiba	Katika nchi yenye mfumo wa shirikisho au Muungano, Nchi Washirika na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kati ya Nchi Washirika.	maeneo mbalimbali, kutekeleza majukumu hayo kwa misingi ya kushirikiana na kushauriana na Nchi Mshirika nyingine au baina ya Nchi Mshirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa lengo la kukuza na kulinda maslahi ya Taifa na maendeleo ya wananchi.	utakaowezesha usimamizi na ushirikiano baina ya Nchi Washirika wenyewe, na kati yao na Jamhuri ya Muungano. Lengo jingine ni kukuza umoja na mtangamano wa kitaifa kwa kuzingatia maslahi ya taifa na ustawi wa wananchi. Kuwezesha Nchi Washirika kutambua na kuhamasisha wananchi wao kutumia fursa zilizopo katika pande zote mbili za Muungano na shughuli hizo zikifanywa na wananchi wenyewe.	Serikali ya Muungano zinawajibika kushirikiana na kushauriana ili kuweka misingi ya kuwahudumia wananchi wote kwa usawa, haki, ulinganifu na uwiano katika masuala ya ustawi wa jamii na maendeleo. Kwa mujibu wa Rasimu hii, vyombo vya kushughulikia suala hili ni pamoja na Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali na Mawaziri Wakaazi. Sababu ya mapendekezo haya ni kuepusha migongano katika uendeshaji wa shughuli za dola na serikali kwa kuwa na vyombo na taasisi vinavyosimamia na kuratibu uhusiano na ushirikiano wa pande husika. Sababu nyingine ni kukuza na kulinda maslahi na ustawi wa wananchi wa Jamhuri ya Muungano kwa ujumla wao lakini bila ya serikali za Nchi Washirika
	(2) Nchi Washirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano zinaweza kushauriana na kushirikiana katika mambo ya uongozi, utawala, vyombo vya uwakilishi na mahakama.		
	(3) Utendaji wa Serikali za Nchi Washirika au wa chombo chochote kati ya vyombo vya serikali hizo na uendeshaji wa shughuli, utatekelezwa kwa kuzingatia		

Final Version www.mwanance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	umoja wa Jamhuri ya Muungano, nia, umuhimu na azma ya kukuza umoja wa kitaifa na kudumisha heshima ya Taifa.		kuingiliana.
Ibara ya 67: Mawaziri Wakaazi.	(1) Kila Nchi Mshirika itateua Waziri Mkaazi atakayeratibu na kusimamia mahusiano baina ya Serikali za Nchi Washirika na kati ya Serikali ya Nchi Mshirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. (2) Mawaziri Wakaazi watakuwa na ofisi zao na watafanya kazi wakiwa Makao Makuu ya Serikali ya Muungano. (3) Pamoja na majukumu mengine watakayopangiwa na Serikali za Nchi Washirika, Mawaziri Wakaazi watakuwa na majukumu	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka chombo cha kikatiba chenye dhamana ya kushughulikia mambo yote yasiyo ya Muungano ili kuunganisha, kuratibu na kusimamia shughuli za kila siku. Ibara pia inalenga kujenga utamaduni wa kiutawala utakaoleta ukaribu na ushirikiano katika Jamhuri ya Muungano na hivyo kujenga imani juu ya maamuzi yanayofanywa katika ngazi hiyo.	Moja ya sababu za mapendekezo haya ni kurahisisha uratibu na ufuatiliaji wa shughuli za Nchi Washirika katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Vilevile ni kufuata uzoefu wa baadhi ya nchi zenye muundo wa shirikisho wa kuwa na Mawaziri Wakaazi au Ofisi za Uwakilishi wa kila Nchi Mshirika wanaoratibu na kusimamia mambo ya shirikisho na maslahi ya Nchi Washirika ndani ya Muungano. Mfano wa nchi hizo ni Ujerumani na Canada. Jumuia ya Umoja wa Ulaya nayo pia ina utaratibu kama huo. Aidha, sababu nyingine ni kuendeleza utaratibu ulioanzishwa na

Final Version www.iliac.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yafuatayo: (a) kushughulikia mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu ushirikiano au mahusiano ya kimataifa; na (b) kuwa kiungo baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Serikali za Nchi Washirika.		Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wa kuwa na Ofisi Jijini Dar-es-Salaam ambayo ni Makao Makuu ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano
Ibara ya 68: Mamlaka ya Wananchi.	(1) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itapata mamlaka yake kutoka kwa wananchi kupitia uchaguzi wa kidemokrasia utakaoendeshwa na kusimamiwa na chombo kitakachopewa mamlaka na Katiba	Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua ukuu wa wananchi kikatiba na kuziwajibisha mamlaka zote kwa wananchi.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kuwa mamlaka kuu ya dola na nchi ni wananchi na sio watawala au vyombo vya serikali na vyote hivyo viko chini ya wananchi kwa mujibu wa

Final Version
www.nance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hii, na vilevile, Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zitapata mamlaka kupitia uchaguzi wa kidemokrasia utakaoendeshwa na kusimamiwa na vyombo vitakavyopewa mamlaka chini ya Katiba zao. (2) Serikali za Nchi Washirika, katika kutekeleza mamlaka zao, zitawajibika kustawisha mamlaka ya wananchi kwa kugatua madaraka kwa serikali za mitaa zitakazoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Tanganyika au Katiba ya Zanzibar, kama itakavyokuwa.		katiba. Katika historia ya nchi nyingi za Kiafrika dhana ya ukuu wa wananchi ilififishwa na badala yake ikakuzwa dhana ya ukuu wa utawala na vyombo vya serikali. Mapendekezo haya ni kurudisha dhana ya ukuu wa wananchi katika uendeshaji wa nchi. Ili kuweza kutekeleza dhana ya Mamlaka ya wananchi ni vyema Katiba ikaanisha vyombo vya kikatiba kama uwepo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ambavyo ndivyo vyenye uwakilishi wa wananchi moja kwa moja na ndivyo vyenye wajibu wa kutoa huduma moja kwa moja kwa wananchi. Sababu ya mapendekezo ni kuendeleza maudhui ya Ibara ya 8 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Ibara ya 9 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 zinazotambua

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mamlaka ya wananchi ingawa katika utekelezaji bado mwelekeo umekuwa zaidi kwenye mamlaka ya watawala na vyombo vya serikali. Muhimu zaidi mapendekezo haya ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka Katiba ionyeshe wazi kuwa Mamlaka ya nchi yanatokana na wananchi wenyewe na kwamba, vyombo vya Serikali vimewekwa na wananchi kwa lengo la kuwatumikia.
Ibara ya 69: Wajibu wa Kulinda Muungano.	(1) Bila ya kuathiri wajibu wa kila raia kwa mujibu wa Katiba hii, viongozi wakuu wenye mamlaka ya utendaji katika Jamhuri ya Muungano waliotajwa katika ibara ndogo ya (3) watawajibika, kila mmoja wao katika kutekeleza madaraka waliyopewa kwa mujibu	Madhumuni ya Ibara hii ni kutambulisha kuwepo kwa Muungano katika maisha ya taifa letu na kujenga uzalendo na mshikamano; na hivyo, kuuthamini, kuulinda na kuutetea Muungano huo wa hiari baina ya raia wa Jamhuri ya Muungano	Sababu za kuwepo kwa Ibara hii ni kusisitiza wajibu wa viongozi wenye dhamana ya juu ya uongozi wa nchi kuuheshimu na kuusimamia Muungano kwa kila hali ili kuuendeleza, kuuhuisha na kuudumisha. Vilevile ni kutambua kuwa Muungano

Kiswahili Version www.tlae.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wa Katiba hii au Katiba za Nchi Washirika kuhakikisha kuwa analinda, kuimarisha na kudumisha Muungano.	kwa kuzingatia umoja wao, udugu, urafiki na mahusiano yao ambayo yana uhusiano ya muda mrefu.	huu wa hiari ni wa wananchi wenyewe na viongozi wao lazima wautii na wauheshimu. Uzoefu umeonyesha kuwepo kwa uvunjaji wa Katiba kwa viongozi kukubaliana masuala kadhaa bila ya kuwashirikisha wananchi kwa makusudi au vinginevyo.
	(2) Kwa madhumuni ya masharti ya ibara ndogo ya (1), kila mmojawapo wa viongozi wakuu waliotajwa katika ibara ndogo ya (3), kabla ya kushika madaraka yake ataapa kuutetea na kuudumisha Muungano kwa mujibu wa Katiba hii.		
	(3) Viongozi Wakuu wanaohusika na masharti ya Ibara hii ni:		
	(a) Rais wa Jamhuri ya Muungano;		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano;		
	(c) Rais wa Tanganyika; na		
	(d) Rais wa Zanzibar.		
SURA YA SABA			
SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO			
SEHEMU YA KWANZA - SERIKALI, RAIS, MAKAMU WA RAIS NA BARAZA LA MAWAZIRI			
***(a)*Serikali**			
Ibara ya 70: Serikali ya Jamhuri ya Muungano	(1) Kutakuwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambayo itaundwa na Rais, Makamu wa Rais na Mawaziri wa Jamhuri ya Muungano.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka mhimili wa utendaji (*The executive*) katika mfumo wa dola. Pia kutambua mamlaka ya Mkuu wa Serikali katika kutekeleza	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza msingi wa kikatiba wa mgawanyo wa madaraka kwa kutambua na kuanzisha ndani ya katiba mhimili wa utekelezaji wa shughuli za dola, na

Trial Version
www.nlace.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatahusu utekelezaji na hifadhi ya Katiba hii na pia mambo mengine ambayo yameainishwa katika sheria za nchi.	mambo ya utendaji yeye mwenyewe au kwa kukasimu madaraka yake. Ibara hii pia inatambua mamlaka ya mihimili mingine ya dola yaani Bunge na Mahakama katika uwezo wao wa kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria kwa watu au mamlaka nyingine yoyote ambayo si Rais.	kuweka wazi kwamba mhimili huu unaundwa na Rais, Baraza la Mawaziri na Utumishi wa Serikali. Vile vile ni kutambua mipaka ya kila mhimili wa dola katika kutekeleza majukumu yake. Rasimu hii ya Katiba kwa mara ya kwanza inauweka Utumishi wa Umma kuwa ni sehemu muhimu ya mhimili wa dola na siyo kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kuwa mhimili wa utendaji ni Rais na Baraza la Mawaziri. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuendelea kuwepo kwa mfumo wa Jamhuri inayoongozwa na Rais Mtendaji ambaye ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Amiri Jeshi Mkuu. Pia, ni kuzingatia matakwa ya kifungu cha
	(3) Madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatatekelezwa na Rais mwenyewe, au kwa kukasimu madaraka hayo kwa Makamu wa Rais au watu wenye madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.		
	(4) Ifahamike kwamba masharti yaliyomo katika Ibara hii hayatahesabiwa kwamba:		
	(a) yanahamishia kwa Rais madaraka yoyote ya kisheria yaliyowekwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria mikononi mwa mtu au mamlaka yoyote ambayo si Rais;		9(2)(b) cha Sheria ya Mabadiliko ya Katiba, Sura ya 83 yaliyoitaka Tume ya Mabadiliko ya Katiba kuzingatia kuwepo kwa Serikali.
	(b) yanalizuia Bunge kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria mikononi mwa mtu au watu au mamlaka nyingine yoyote ambayo si Rais; au		
	(c) yanazuia Mahakama kukabidhi madaraka yoyote ya kisheria kwa mtu au watu wenye madaraka katika Mahakama za Jamhuri ya Muungano.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b)Rais		
Ibara ya 71: Rais wa Jamhuri ya Muungano	(1) Kutakuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano. (2) Rais wa Jamhuri ya Muungano atakuwa Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu na: (a) atakuwa alama na taswira ya Jamhuri ya Muungano na watu wake; (b) atakuwa alama ya umoja, uhuru wa nchi na mamlaka yake; na (c) atakuwa na dhamana ya kukuza na kuhifadhi umoja wa kitaifa.	Lengo la Ibara hii ni kuainisha kikatiba kuwepo kwa Rais mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ni Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia, ni kubainisha na kuyaweka wazi mamlaka yake akiwa Mkuu wa Nchi, mamlaka yake akiwa ni Amiri Jeshi Mkuu na mamlaka yake akiwa ni Mkuu wa Serikali. Madhumuni mengine ni kutofautisha mamlaka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mamlaka ya Wakuu wa Nchi Washirika.	Mfumo wa nchi yetu ni wa Jamhuri na siyo wa Kifalme au vinginevyo na kwa hivyo ni lazima uongozwe na Rais wa kuchaguliwa. Aidha, Sheria ya Mabadiliko ya Katiba inataja mfumo wa kiutawala wa kijamhuri kuwa ni moja ya misingi muhimu ya kuzingatiwa na kuboreshwa katika Katiba Mpya. Sababu ya kupendekeza kuendelea mfumo huo wa kuwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwenye mamlaka kamili yasiyogawika kwa mwingine ambayo ni ya Mkuu wa Nchi, Amiri Jeshi Mkuu na pia Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Rais wa Jamhuri ya Muungano ndiye mwenye Mamlaka kamili kwa mambo yote yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya

Trial Version
www.iliveinc.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Muungano, wakati marais wa Nchi Washirika watakuwa wakuu wenye mamlaka kamili kwa Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar kwa mambo yasiyo ya Muungano. Mfumo huu wa Rais kuwa Mkuu wa Serikali unafuatwa na nchi kadhaa duniani ikiwemo Brazil, Marekani, Mexico, Nigeria, Ujerumani na Venezuela. Sababu nyingine ni kufafanua utekelezaji wa madaraka ya Rais akiwa katika nafasi zake tatu za Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali na Amiri Jeshi Mkuu.
Ibara ya 72: Madaraka na majukumu ya Rais	(1) Rais, katika nafasi ya madaraka ya Mkuu wa Nchi, atakuwa na madaraka na majukumu yafuatayo: (a) kuisimamia na kuilinda	*Lengo la Ibara hii ni kuweka wazi na kuainisha kwa kina mipaka ya madaraka na majukumu ya Rais katika nafasi zake tatu tofauti katika utekelezaji wa kazi zake.*	*Sababu moja ya mapendekezo haya ni kuendana na Katiba nyingine duniani ambazo zinatambua nafasi hizo tatu tofauti za mamlaka ya kiongozi wa nchi na zinatenganisha shughuli hizo kwa*

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Katiba ya Jamhuri ya Muungano; (b) kulinda utaifa wa Jamhuri ya Muungano; (c) kuhutubia na kufungua rasmi Bunge Jipya na kulivunja Bunge baada ya kumaliza muda wake; (d) kuhutubia na kufungua rasmi Kalenda ya Mwaka ya Mahakama;	*Lengo jingine ni kuweka masharti yanayomzuia Rais wa Jamhuri ya Muungano kujinasibisha na chama chochote cha siasa au kundi lolote kwa namna ambayo itaathiri umoja wa wananchi.*	*kufanywa na watu mbali mbali au kuwekwa chini ya mtu mmoja lakini kila nafasi ikiwa na mipaka inayoeleweka.* *Kwa hali hiyo, Mkuu wa Nchi dhamana yake ni alama ya umoja wa taifa na wananchi wake; Amiri Jeshi Mkuu dhamana yake ni ulinzi na usalama wa nchi, watu na mali zao; na Kiongozi wa Serikali dhamana yake ni usimamizi na uendeshaji wa kila siku wa shughuli za Serikali.* *Aidha, Ibara hii ni kuzingatia na maoni ya wananchi ambao walitaka kutenganishwa kwa shughuli za Serikali na zile za chama, Rais kutotumia rasilimali za Serikali kwa shughuli za chama na pia kuondoa uwezekano wa Rais kuegemea upande wa chama chake katika kufanya maamuzi na hivyo*
	(e) kuidhinisha uwasilishaji Bungeni wa makisio ya mapato na matumizi ya Serikali, Bunge na Mahakama katika mwaka wa fedha;		
	(f) kuweka saini katika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muswada wa Sheria uliyopitishwa na Bunge;		*kuwagawa wananchi katika makundi.*
	(g) kutunuku nishani za heshima kwa niaba ya Watu wa Jamhuri ya Muungano kwa ujumla;		
	(h) kuteua mabalozi, watu watakaoiwakilisha Tanzania nje ya nchi na wawakilishi wa nchi katika taasisi mbalimbali za kimataifa;		
	(i) kupokea hati za utambulisho za Mabalozi wa nchi za nje nchini;		
	(j) kutoa msamaha kwa mtu yeyote anayetumikia		

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	adhabu iliyotolewa na Mahakama kwa mujibu wa sheria za nchi; na		
	(k) kuidhinisha utekelezaji wa adhabu ya kifo iliyotolewa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
	(2) Rais, katika nafasi ya madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu, atakuwa na madaraka na majukumu yafuatayo:		
	(a) kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa;		
	(b) kuamuru Majeshi ya Ulinzi kwenda vitani au kusitisha vita;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) kutia saini makubaliano ya amani au kusitisha vita;		
	(d) kutangaza hali ya hatari au hali ya kuzingirwa eneo fulani la Jamhuri ya Muungano;		
	(e) kuteua Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama; na		
	(f) kuwapandisha vyeo maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama katika ngazi mbalimbali na kutoa kamisheni kwa maofisa wa Jeshi la Wananchi.		
	(3) Rais, katika nafasi ya madaraka ya Kiongozi wa Serikali, atakuwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	madaraka na majukumu yafuatayo:		
	(a) kuongoza vikao vya Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano;		
	(b) kupanga, kuelekeza, kusimamia na kuratibu majukumu ya wizara na taasisi za serikali;		
	(c) kuwateua Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;		
	(d) kumteua Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;		
	(e) kumteua Mwanasheria		

Trial Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mkuu wa Serikali; na		
	(f) kuwateua Wenyeviti, Makamu Wenyeviti, Wajumbe na Makamishna wa Tume mbalimbali zilizoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
	(4) Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Ibara hii, Rais ataepuka kujinasibisha, kwa namna yoyote ile, na chama chochote cha siasa au kundi lolote kwa namna ambayo inaathiri umoja wa wananchi.		
	(5) Rais atakuwa na mamlaka ya kutekeleza majukumu mengine ambayo kwa asili yake yanatekelezwa na Mkuu wa Nchi,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Amiri Jeshi Mkuu au Kiongozi wa Serikali, ambayo hayakuainishwa katika Ibara hii na ambayo hayakiuki Katiba hii na sheria za nchi.		
Ibara ya 73: Utekelezaji wa madaraka ya Rais.	(1) Katika utekelezaji wa madaraka ya Rais kwa mujibu wa Sura hii na kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (3), Rais ana mamlaka ya kuanzisha au kufuta nafasi za madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.	Sababu moja ya mapendekezo haya ni kuendana na Katiba nyingine duniani ambazo zinatambua nafasi hizo tatu tofauti za mamlaka ya kiongozi wa nchi na zinatenganisha shughuli hizo kwa kufanywa na watu mbali mbali au kuwekwa chini ya mtu mmoja lakini kila nafasi ikiwa na mipaka inayoeleweka. Kwa hali hiyo, Mkuu wa Nchi dhamana yake ni alama ya umoja wa taifa na wananchi wake; Amiri	Sababu za mapendekezo haya ni kuruhusu kikatiba kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano ni Mkuu wa Nchi, Kiongozi wa Serikali Amiri Jeshi Mkuu aendelee kuwa na madaraka ya uteuzi wa viongozi wa ngazi za juu Serikalini lakini ashauriwe na taasisi na vyombo vyengine mahsusi vya umma na baadhi ya viongozi anaowateua wathibitishwe na Bunge kabla ya kushika madaraka. Sababu nyingine ni kuondoa changamoto mbalimbali zinazotokana na mfumo wa sasa ambapo Rais ana mamlaka yasiyo na udhibiti ya kuteua
	(2) Rais atakuwa na madaraka ya kuteua watu wa kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika kuweka sera za idara na taasisi za Serikali, na watendaji wakuu wanaowajibika kusimamia utekelezaji wa sera za		

Final Version www.ilani.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	idara na taasisi hizo katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano. (3) Katika utekelezaji wa madaraka kama ilivyoainishwa katika ibara ndogo ya (1) na (2), Rais atazingatia masharti kuhusu uthibitisho wa Bunge katika nafasi za madaraka na vile vile ushauri wa mamlaka za Serikali, Bunge au Mahakama zilizopewa madaraka ya kumshauri katika kufanya uteuzi, kuanzisha au kufuta nafasi za madaraka katika utumishi wa Serikali. (4) Mamlaka ya kuwateua watu wengine wote wasiokuwa viongozi wala watendaji wakuu kushika nafasi za madaraka	Jeshi Mkuu dhamana yake ni ulinzi na usalama wa nchi, watu na mali zao; na Kiongozi wa Serikali dhamana yake ni usimamizi na uendeshaji wa kila siku wa shughuli za Serikali. Aidha, Ibara hii ni kuzingatia na maoni ya wananchi ambao walitaka kutenganishwa kwa shughuli za Serikali na zile za chama, Rais kutotumia rasilimali za Serikali kwa shughuli za chama na pia kuondoa uwezekano wa Rais kuegemea upande wa chama chake katika kufanya maamuzi na hivyo kuwagawa wananchi katika makundi.	Viongozi mbalimbali katika Utumishi wa Umma. Changamoto za mfumo huu ni pamoja na: 1. Uwezekano wa uteuzi kufanyika kwa upendeleo na rushwa bila kuzingatia uwezo na sifa stahili. Kwa mfano, kwa sababu ya mfumo huu, Rais wa zamani wa Marekani, James A. Garfield, aliuawa mwaka 1881 na mtu ambaye alitegemea kuteuliwa lakini akanyimwa nafasi kinyume cha matarajio yake kutokana na upendeleo na rushwa. Baada ya tukio hilo sheria ilitungwa ili kumpunguzia Rais madaraka ya uteuzi na kumbakishia nafasi chache kwa ajili ya viongozi wa ngazi za juu

Tiaki.com
www.tiaki.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na mamlaka ya kuwapandisha vyeo watu hao, kuwaondoa katika madaraka, kuwafukuza kazi, kuwasimamisha kazi na mamlaka ya kudhibiti nidhamu ya watu waliokabidhiwa madaraka, yatakuwa mikononi mwa Tume za Utumishi na mamlaka za nchi zilizotajwa na kupewa mamlaka hayo na sheria za nchi.		tu. 2. Uwezekano kwa Rais kufanya uteuzi kwa kupotoshwa na washauri wake hasa kukiwa na idadi kubwa ya wateule. 3. Uwezekano wa Rais kutumia muda mwingi kwenye uteuzi badala ya kufanya kazi nyingine muhimu. 4. Uwezekano wa wateuliwa kutowajibika kwa kujinasibisha kuwa wote ni wateule wa Rais.
	(5) Masharti ya ibara ndogo ya (2) na ya (3) hayazuii Rais kuchukua hatua za kudhibiti nidhamu ya watumishi na utumishi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano.		5. Uwezekano wa kushusha ufanisi katika utendaji wa kazi kwa kuwa Rais hayupo karibu na wateule wake wengi kuweza kuwasimamia kinidhamu na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kuwawajibisha. Mapendekezo haya pia yamezingatia maoni ya wananchi yaliyotaka Rais awekewe udhibiti katika utekelezaji wa madaraka yake ya uteuzi. Kwa mujibu wa Katiba ya Ufaransa, Rais amepewa madaraka ya uteuzi wa mabalozi, viongozi wa juu wa majeshi, wakurugenzi mbalimbali wa idara za serikali, wakuu wa taasisi za elimu, wakaguzi wa mahesabu ya serikali na wakuu wa mikoa. Uteuzi huo lazima uthibitishwe na Bunge. Vilevile, mamlaka ya uteuzi ya Rais yanafanyika kwa kushauriana na kamati husika za Bunge. Rais hatafanya uteuzi ikiwa theluthi mbili ya kura za kamati za Bunge zinazohusika zitakataa. Katika Katiba ya Finland, Rais anamteua

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Waziri Mkuu, na uteuzi huo huthibitishwa na Bunge. Rais pia anateua Mawaziri wengine kwa ushauri wa Waziri Mkuu. Rais anateua Makatibu Wakuu wa wizara, Mabalozi na viongozi wengine ambao Katiba na sheria zinaona kuwa zinahitaji kuteuliwa na mamlaka ya kipekee ya Rais kama Mkuu na Amiri Jeshi. Rais pia anateua Maofisa wa vyombo vya ulinzi na usalama. Viongozi na watendaji wa dola wengine wanateuliwa na Serikali kupitia mamlaka mbalimbali za nchi.
Ibara ya 74: Rais kuzingatia ushauri.	(1) Mbali na kuzingatia masharti yaliyomo katika Katiba hii, na sheria za nchi, Rais atakuwa na wajibu wa kufuata na kuzingatia ushauri atakaopewa na mamlaka	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya Kikatiba yatakayomlazimisha Rais kufuata ushauri usiokiuka Katiba au Sheria	Sababu ya kuweka Ibara ni kumtaka Rais kufuata na kuzingatia ushauri utakaotolewa na mamlaka husika kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi. Ibara hii pia imezingatia mapendekezo

Trial Version
www.iance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	za nchi, na endapo hakubaliani na ushauri aliopewa, sharti atoe sababu katika Baraza la Mawaziri kuhusu sababu ya kutokubaliana na ushauri aliopewa. (2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), Rais hatalazimika kufuata ushauri aliopewa ambao unakwenda kinyume au kukiuka masharti ya Katiba hii au sheria za nchi.	za Nchi. Lengo pia ni kujenga mfumo wa kitaasisi ambao una wajibu wa kutoa ushauri na ushauri huo kuheshimika na Rais. Hii pia inakusudia kujenga mfumo wa kutabirika (*certainity and continuity*) katika maamuzi na utekelezaji wa shughuli za Serikali.	ya wananchi ambao walitaka maamuzi ya Rais yasitegemee hekima na busara za mtu mmoja pekee. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika maamuzi ya kuendesha nchi.
Ibara ya 75: Rais kushindwa kumudu majukumu yake.	(1) Endapo Baraza la Mawaziri litaridhika kuwa Rais hawezi kumudu kazi zake kwa sababu ya maradhi, linaweza kuwasilisha kwa Jaji Mkuu azimio la kumwomba Jaji Mkuu athibitishe kwamba Rais, kwa sababu ya maradhi, hawezi kumudu kazi zake.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuainisha utaratibu wa kikatiba wa kuthibitisha kwamba Rais ameshindwa kumudu madaraka yake kutokana na maradhi. Lengo pia ni kuweka masharti ya kikatiba ya kujaza nafasi hii muhimu ili kuondoa uwezekano	Sababu kuu ni kutambua kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano amechaguliwa kwa kura na kwa hivyo mchakato wowote wa kumuondoa uwe wa wazi na haki kwa Rais mwenyewe na wananchi waliomchagua na kumpa dhamana ya kuwaongoza. Sababu ya mapendekezo haya ni

TUKO Vision
www.vision.co.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Baada ya kupokea azimio lililowasilishwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), Jaji Mkuu atateua bodi ya utabibu ambayo itachunguza suala hilo na kumshauri Jaji Mkuu ipasavyo. (3) Jaji Mkuu anaweza, baada ya kutafakari ushauri na ushahidi wa kitabibu, kuwasilisha kwa Spika hati ya kuthibitisha kwamba kutokana na maradhi, Rais ameshindwa kumudu kazi zake, na iwapo Jaji Mkuu hatabatilisha hati hiyo ndani ya siku saba kutokana na Rais kupata nafuu na kurejea kazini, basi itahesabiwa kwamba nafasi ya madaraka ya Rais iko wazi, na masharti yaliyomo katika Ibara ya 76	wa Rais kuendelea kukaa madarakani hata kama hana uwezo wa kumudu majukumu yake. Vilevile ni kuzuia Baraza la Mawaziri peke yao kufanya maamuzi ya kumuondoa Rais mpaka ithibitishwe na bodi ya utabibu ili kuhakikisha kuwa mfumo wa kuondolewa kwake ni wa haki kwa Rais mwenyewe na wananchi waliomchagua.	kuondoa utata unaoweza kujitokeza kuhusu utaratibu utakaotumika kutangaza nafasi ya Rais ipo wazi endapo itatokea Rais aliyepo madarakani kushindwa kumudu majukumu yake kutokana na sababu za maradhi. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 76 ya Rasimu ya Katiba.

Tribalchief
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yatatumika. (4) Bodi ya utabibu itakayoteuliwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) itajumuisha watu wasiopungua watatu watakaoteuliwa kutoka miongoni mwa madaktari bingwa wanaotambuliwa na sheria za nchi.		
Ibara ya 76: Utaratibu wa kujaza nafasi ya Rais kabla ya kumaliza muda wake.	(1) Endapo nafasi ya madaraka ya Rais itakuwa wazi kutokana na: (a) Rais kufariki dunia; (b) Rais kujiuzulu; (c) Rais kupoteza sifa za uchaguzi katika nafasi ya madaraka ya Rais; (d) Rais kutomudu kazi zake kutokana na maradhi;	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba utakaopaswa kuzingatiwa wakati wa kujaza nafasi ya Rais itakapokuwa wazi kwa sababu yoyote iliyoainishwa katika Katiba. Utaratibu huu utasaidia kuondoa mgongano na kuweka uhakika wa kujaza nafasi ya Rais pale inapotokea kuwa wazi.	Sababu moja ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa nafasi ya Rais, aliye taswira ya dola, ina mtu anayeishikilia wakati wote. Pia ni kumfanya Makamu wa Rais kujaza nafasi ya Rais kwa sababu yeye amechaguliwa kuwa mgombea mwenza na Rais kwa tiketi moja. Sababu nyingine ni muendelezo mfumo kwa makamu wa Rais kuweza kushika

Trial Version
www.mtaa.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) Rais kushtakiwa Bungeni na kuondolewa katika madaraka kwa mujibu wa Katiba hii, basi Makamu wa Rais ataapishwa na kushika madaraka ya Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano na kwa masharti yaliyoainishwa katika Ibara ya 80.	Hilo pia ni kwa nafasi ya Makamu wa Rais.	nafasi ya Urais wakati inapotokea dharura kwa Rais kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara ya 80.
	(2) Mara tu baada ya Rais kuapishwa na kushika madaraka kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), au kwa vyovyote vile ndani ya kipindi kisichozidi siku kumi na nne tangu alipoapishwa:		
	(a) kwa Rais aliyepatikana kwa kupendekezwa na chama cha siasa, baada ya kushauriana na chama cha		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	siasa anachotoka; au (b) kwa Rais aliyepatikana kwa utaratibu wa mgombea huru, baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zaidi ya asilimia hamsini ya Wabunge wote.		
Ibara ya 77: Utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo.	(1) Ikitokea kwamba nafasi ya madaraka ya Rais iko wazi kutokana na: (a) masharti yaliyomo katika Ibara ya 75;	Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kukaimu utekelezaji wa majukumu ya Rais akiwa hayupo. Utaratibu huu utasaidia ili kuondoa utata wa utekelezaji wa	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kwamba, majukumu na kazi za Rais zinaendelea kutekelezwa iwapo Rais mwenyewe hayupo. Pia kumzuia anayekaimu madaraka ya Rais

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) masharti yaliyomo katika Ibara ya 88; (c) kutokuwepo katika Jamhuri ya Muungano, kazi na shughuli za Rais zitatekelezwa na mmoja wapo wa wafuatao, kwa kufuata orodha kama ilivyopangwa - (i) Makamu wa Rais au kama nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, basi; (ii) Waziri Mwandamizi; au (iii) kama Waziri Mwandamizi nafasi yake iko wazi au kama naye hayupo au ni mgonjwa, basi Waziri mwingine yeyote atakayeteuliwa na Baraza	majukumu ya Rais pale inapotokea Rais hayupo. Pia kuweka mipaka inayozuia mamlaka ya msingi ya Rais kukasimiwa kwa mtu mwingine yeyote na hivyo Rais kulazimika kutokuwa nje ya nchi kwa muda mwingi zaidi.	kuyatumia vibaya. Sababu nyingine ni kuepusha mgogoro au mvutano unaoweza kukwamisha utendaji wa Serikali na kutaja wazi mpangilio wa viongozi wanaoweza kukaimu madaraka ya Rais. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 75 na 88 ya Rasimu.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	la Mawaziri.		
	(2) Endapo mtu yeyote aliyetajwa katika ibara ndogo ya (1) atatekeleza kazi na shughuli za Rais kutokana na sababu kwamba mtu mwingine anayemtangulia katika orodha hiyo hayupo, basi mtu huyo ataacha kutekeleza kazi na shughuli hizo mara tu mtu huyo mwingine anayemtangulia atakaporejea na mtu huyo ataanza kutekeleza kazi na shughuli za Rais.		
	(3) Mtu yeyote atakayekaimu nafasi ya madaraka ya Rais, kwa namna yoyote ile, hatakuwa na madaraka katika mambo yafuatayo:		
	(a) kuteua au kumuondoa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	madarakani kiongozi yeyote yule aliyeteuliwa na Rais kwa mujibu wa Katiba hii; au		
	(b) jambo jingine lolote kama litakavyoainishwa na Rais katika hati ya kukasimu madaraka yake.		
	(4) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (2) na (3), Rais atakasimu madaraka yake kwa hati maalum aliyotia saini yake.		
	(c) Uchaguzi wa Rais		
Ibara ya 78: Uchaguzi wa Rais.	(1) Rais atachaguliwa na wananchi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na kwa mujibu wa sheria za nchi.	Madhumuni ni kuweka mamlaka ya wananchi ya kumchagua Rais na kumpa dhamana ya uongozi wa nchi na kumfanya awajibike	Kuweka utaratibu wa kidemokrasia wa wananchi kubadili uongozi kwa vipindi vilivyowekwa na kwa njia ya uchaguzi ili kudhihirisha mamlaka yao ya kumuweka

Final Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Nafasi ya madaraka ya Rais itakuwa wazi na uchaguzi wa Rais utafanyika baada ya Rais kumaliza muda wake wa kuwa madarakani kwa mujibu wa Katiba hii.	kwao. Pia ni njia ya kutimiza matakwa ya demokrasia ya kubadili uongozi kwa vipindi maalum na kwa njia ya uchaguzi.	na kumuondoa Mkuu wa nchi. Mapendekezo haya pia yanaendeleza utaratibu wa uchaguzi wa Rais kwa vipindi vilivyoainishwa kikatiba. Ibara hii isomwe pamoja na Ibara za 79 na 80.
Ibara ya 79: Sifa za Rais.	(1) Mtu atakuwa na sifa ya kuchaguliwa kushika nafasi ya madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano ikiwa: (a) ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa Katiba hii na sheria za nchi; (b) ni mwenye akili timamu; (c) wazazi wake wote wawili ni raia wa kuzaliwa wa	Lengo ni kuweka vigezo vitakavyowezesha nchi kupata Rais atakayekidhi matakwa ya wananchi kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Pia, ni kuweka vigezo vya kumuondolea sifa mtu anaetaka kugombea Urais.	Kuhakikisha kuwa Urais, ambao ni wadhifa mkubwa katika nchi na ni alama na taswira ya nchi, unashikwa na mtu ambaye ni muadilifu na anayeamika, mzoefu wa uongozi, aliyekomaa kifikra na kiutendaji. Sababu ya kuweka umri wa miaka 40 ni kwamba mgombea atakuwa amekomaa kifikra na kimatendo na kuweza kubeba jukumu la kuwa kiongozi mkuu. Aidha tafiti zimeonesha kuwa umri wa miaka 40 au zaidi ni sifa iliyo katika katiba za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Jamhuri ya Muungano; (d) wakati wa kugombea, ana umri usiopungua miaka arobaini; (e) anayo shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi; (f) ni mwanachama wa mgombea aliyependekezwa na chama cha siasa au mgombea huru; (g) sera zake au sera za chama chake si za mrengo wa kuligawa Taifa kwa misingi ya ukabila,		nchi nyingine duniani.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	dini, rangi au jinsi; na		
	(h) ni mwadilifu, anayeheshimu haki za binadamu, asiyedharau wala kubagua watu kwa misingi ya kabila, dini, jinsi, maumbile au hali zao katika jamii na anafuata maadili ya viongozi na mwenendo wake hautiliwi shaka na jamii. (2) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea nafasi ya Urais ikiwa -		
	(a) mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalum		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa mujibu wa sheria za nchi, na iwapo amekiuka miiko hiyo;		
	(b) kwa mujibu wa sheria ya nchi inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote, mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura au kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu; au (c) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi amewahi kutiwa hatiani katika mahakama kwa kosa la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali au makosa yanayohusu kukosa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uaminifu.		
Ibara ya 80: Utaratibu wa uchaguzi wa Rais.	(1) Katika Uchaguzi wa Rais, kila chama cha siasa kinachopenda kushiriki katika uchaguzi wa Rais kitawasilisha kwa Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano, kwa mujibu wa sheria za nchi, jina la mwanachama mmoja anayependekezwa kwa nafasi ya madaraka ya Rais. (2) Endapo ni Mgombea huru, kwa kuzingatia sifa zilizoainishwa katika Katiba hii, atawasilisha jina lake kwenye Tume Huru ya Uchaguzi. (3) Mapendekezo ya majina ya wagombea katika uchaguzi wa Rais yatawasilishwa kwa Tume	Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kumpata Rais mwenye uhalali wa kuongoza kwa kupigiwa kura na kuchaguliwa kwa idadi kubwa ya wananchi. Pia inaruhusu mgombea huru wa nafasi hiyo ili kunapanua wigo wa demokrasia.	Sababu za mapendekezo haya ni kurudisha utaratibu uliokuwepo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 wa mgombea Urais kutakiwa kupata kura kwa zaidi ya asilimia 50, utaratibu ambao uliondolewa kupitia Mabadiliko ya 13 ya Katiba ya mwaka 2000. Pia yamezingatia maoni ya wananchi waliotaka Rais anayechaguliwa apate kura zaidi ya asilimia hamsini ili kuonyesha kukubalika kwake na wananchi walio wengi. Uzoefu wa baadhi ya nchi nyingi ni kuwa ili mtu atangazwe kuwa Rais katika uchaguzi anatakiwa apate zaidi ya nusu ya kura halali zilizopigwa na

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Huru ya Uchaguzi katika siku na kwa utaratibu uliyoainishwa katika sheria za nchi. (4) Endapo itafika siku na saa iliyotajwa		wananchi. Kwa kuwa kupiga kura na kupigiwa kura ni haki ya kila raia wa Tanzania na hivyo si vyema kumlazimisha raia anayetaka kugombea uongozi kuwa mwanachama wa chama cha siasa. Mapendekezo ya kuwa na mgombea huru yamezingatia msingi wa demokrasia kuwa kupiga kura na kupigiwa kura ni haki ya kila raia. Vilevile ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa mgombea huru katika kiti cha Urais. Pia ni kuridhia maamuzi ya Mahakama ya Rufani ya Tanzania yaliyoelekeza Bunge kubadili Katiba ili kuweka haki ya mgombea huru. Aidha, Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu kupitia kesi ya Rev. Christopher Mtikila v. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwamba iwe

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ndani ya kipindi cha mwaka mmoja iwe imechukua hatu za kuweka mgombea huru katika Katiba.
	(5) Endapo itafika siku na saa iliyotajwa kwa ajili ya kuwasilisha mapendekezo ya majina ya wagombea, ni mgombea mmoja tu ambaye anapendekezwa kuwa halali, Tume Huru ya Uchaguzi itawasilisha jina lake kwa wananchi, nao watapiga kura ya kumkubali au kumkataa kwa mujibu wa masharti yaliyoainishwa katika Katiba hii na sheria za nchi.		
	(6) Uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano utafanyika siku itakayoteuliwa na Tume Huru ya Uchaguzi kwa mujibu wa sheria za		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nchi.		
	(7) Mgombea wa nafasi ya madaraka ya Rais atatangazwa kuwa amechaguliwa kuwa Rais iwapo atapata kura zinazozidi asilimia hamsini ya kura zote halali kwa nafasi ya madaraka ya Rais.		
	(8) Endapo katika Uchaguzi wa Rais hakuna mgombea aliyekidhi masharti ya ibara ndogo ya (6), basi uchaguzi utarudiwa ndani ya siku sitini kwa wagombea walioshika nafasi ya kwanza na ya pili.		
Ibara ya 81: Malalamiko kuhusu uhalali wa uchaguzi wa Rais.	(1) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (2), endapo mtu yeyote aliyeshiriki kama mgombea katika nafasi ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka msingi wa kikatiba wa kuhakikisha kuwa nchi inakuwa na Rais aliyechaguliwa kihalali.	Mapendekezo haya yamezingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka matokeo ya uchaguzi wa Rais yaweze kuhojiwa Mahakamani.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	madaraka ya Rais katika Uchaguzi wa Rais hakuridhika na matokeo ya uchaguzi huo, anaweza kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Juu kupinga matokeo ya Uchaguzi wa Rais yaliyotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi.	Hii itasaidia kuondoa malalamiko kuhusiana na uhalali wa ushindi wa Rais aliyechaguliwa. Ibara pia inawapa fursa watu wasioridhika na matokeo ya aliyechaguliwa kuwa Rais kuweza uhoji Mahakamani. Madhumuni mengine ni kujenga utamaduni wa kuendesha chaguzi huru, wa wazi na kuondosha vitendo vya rushwa na udanganyifu kwenye chaguzi.	Aidha, hii ni fursa inayotoa haki kwa wagombea wanaodhani kuwa aliyetangazwa kuwa mshindi wa nafasi ya Urais hakuwa mshindi halali. Utaratibu huu utasaidia kuimarisha demokrasia katika mfumo mzima wa uchaguzi wa Rais kwa kuwa unaruhusu chombo kingine yaani Mahakama ya Juu ambacho ni huru kutathmini na kutolewa uamuzi juu ya suala hilo la uhalali wa mtu aliyeshinda nafasi ya Urais na kutoa kauli ya mwisho ili nchi iendelee katika shughuli zake za kawaida.
	(2) Malalamiko ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa Rais yatawasilishwa Mahakama ya Juu ndani ya muda uliowekwa na sheria ya nchi baada ya siku ya kutangazwa kwa matokeo ya Uchaguzi wa Rais.		
	(3) Mahakama ya Juu itasikiliza na kutoa uamuzi wa shauri la kupinga matokeo ya uchaguzi wa Rais ndani ya muda		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utakaoainishwa na sheria ya nchi tangu kupokea malalamiko yaliyowasilishwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) na uamuzi huo utakuwa wa mwisho.		
	(4) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (3), Mahakama ya Juu inaweza kutoa uamuzi bila kutoa sababu za uamuzi na sababu hizo zikatolewa ndani ya kipindi kisichozidi siku thelathini tangu siku ya kutoa uamuzi.		
	(5) Iwapo Mahakama ya Juu itaamua kuwa matokeo ya Uchaguzi wa Rais si halali, Uchaguzi wa Rais utarudiwa ndani ya siku sitini baada ya uamuzi kutolewa.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 82: Kiapo cha Rais na muda wa kushika Madaraka.	(1) Rais Mteule ataapishwa na Jaji Mkuu na atashika nafasi ya madaraka ya Rais mapema iwezekanavyo baada ya kutangazwa kwamba amechaguliwa kuwa Rais, lakini kwa hali yoyote, hatashika madaraka kabla ya kupita siku thelathini kutoka siku matokeo ya Uchaguzi wa Rais yalipotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi au siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu. (2) Isipokuwa kama ataacha kushika nafasi ya madaraka ya Rais mapema zaidi, Rais atashika nafasi ya madaraka ya Rais kwa muda wa miaka mitano tangu siku alipoapishwa kuwa Rais.	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu kiapo cha Rais cha kulinda na kutetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano; na kufuata utawala wa sheria unaoheshimu haki za binadamu. Aidha, ni kuweka ukomo wa Rais kuwa madarakani na kuwapa fursa wananchi kubadilisha viongozi wao kila baada ya kipindi maalum. Hii ni pamoja na kuwapa wananchi fursa na haki ya kuomba ridhaa ya uongozi kwa kuchaguliwa. Lengo jingine ni kuimarisha msingi wa kuwa uongozi ni dhamana na hivyo kuepuka watu kuhodhi au kurithisha uongozi kwa ndugu na marafiki zao. Aidha, Ibara hii	Sababu za mapendekezo haya ni kuwekwa utaratibu wa kikatiba wa kumuapisha Rais mteule hataapishwa kabla ya kupita siku thelathini tokea siku ya matokeo yalipotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi au siku ya kuthibitishwa na Mahakama ya Juu. Sababu ya kupendekeza utaratibu huu ni kutoa muda wa kutosha wa kukabidhiana madaraka kati ya Rais anayemaliza muda wake na Rais anayeingia madarakani. Sababu nyingine za mapendekezo haya ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliosema kuwa kipindi cha siku thelathini kitatoa fursa kwa wagombea wa uchaguzi wa Rais wasioridhika na matokea waweze kupata haki ya kulalamika

Final Version www.klaw.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Rais atashika nafasi ya madaraka ya Rais hadi -	inajenga utamaduni wa kufuata utaratibu wa kikatiba na vyombo vya kikatiba katika kushughulikia malalamiko yao pale ambapo hawajaridhika na matokeo ya uchaguzi.	Mahakamani. Aidha sababu nyingine ni kumfanya Rais ailinde na kuitetea Katiba ya Jamhuri ya Muungano na kuutetea na kuulinda Muungano wa Tanzania. Uzoefu wa Katiba za nchi nyingine kama Kenya, Marekani ambazo Rais wake huapishwa baada ya kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu.
	(a) siku ambapo Rais mteule ataapa kushika nafasi ya madaraka ya Rais;		
	(b) siku ambapo atafariki dunia;		
	(c) siku atakapojiuzulu; au		
	(d) atakapoacha kushika nafasi ya madaraka ya Rais kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
Ibara ya 83: Haki ya kuchaguliwa tena.	(1) Mtu ambaye ni Rais anaweza kuchaguliwa tena kushika nafasi ya madaraka ya Rais kwa kipindi	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu ukomo wa kushika	Sababu ya kwanza ni kuendeleza utaratibu nzuri wa sasa uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kingine cha miaka mitano. (2) Mtu hatakuwa na sifa ya kugombea na kuchaguliwa zaidi ya vipindi viwili katika nafasi ya madaraka ya Rais. (3) Mtu aliyewahi kuwa Rais wa Tanganyika au Zanzibar hatapoteza sifa za kugombea na kuchaguliwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa sababu aliwahi kushika nafasi ya madaraka ya Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar. (4) Endapo Makamu wa Rais atashika nafasi ya madaraka ya Rais kwa mujibu wa masharti ya Ibara ya 76 kwa kipindi kisichozidi miaka mitatu,	madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano. Pia, ni kuweka msingi wa kung'atuka, kwamba si suala tu la kuondoka madarakani lakini pia ni dhana ya kupokezana madaraka kwa njia za kikatiba.	mwaka 1977 iliyoweka ukomo wa Urais na kuifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi Barani Afrika ambapo marais wamepokezana Urais bila ya mivutano wala misuguano kuanzia 1985. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa ukomo wa kushika nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, kujenga utamaduni wa kupokezana madaraka kwa njia ya amani, kutoa fursa kwa Watanzania wengine wenye uwezo na sifa kushika madaraka ya Rais, na kuepusha uwezekano wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kukaa madarakani bila ukomo.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ataruhusiwa kugombea nafasi ya Rais kwa vipindi viwili, lakini kama atashika nafasi ya madaraka ya Rais kwa muda wa miaka mitatu au zaidi ataruhusiwa kugombea nafasi ya madaraka ya Rais kwa kipindi kimoja tu.		
(d) Masharti Mahsusi kuhusu Mamlaka ya Rais			
Ibara ya 84: Madaraka ya kutangaza vita.	(1) Kwa kuzingatia masharti ya Ibara hii, Rais atakuwa na mamlaka ya kutangaza kuwepo kwa vita kati ya Jamhuri ya Muungano na nchi nyingine au kundi lolote lile baada ya kupata idhini ya Bunge.	Lengo ni kumpa Rais madaraka ya kutangaza vita, kulinda amani na usalama wa nchi kwa idhini ya Bunge na ushauri wa Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa. Lengo jingine ni kuweka utaratibu wa kumuwezesha Rais	Rais anapewa madaraka ya kutangaza vita kwa nafasi yake ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye mwenye madaraka ya kuamuru jeshi kuingia katika vita. Masharti ya kikatiba ya Rais kupata idhini ya Bunge kabla ya kutangaza vita yatawezesha kutoa nafasi kwa Bunge ambalo ni chombo
	(2) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), endapo Jamhuri ya		

Trial Version
www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano itakuwa imevamiwa au kundi lolote limeanzisha vita ndani ya Jamhuri ya Muungano basi, Rais anaweza, baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa, kutangaza kuwepo kwa vita katika Jamhuri ya Muungano. (3) Baada ya kutoa tangazo kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2), Rais atalitaarifu Bunge kwa kupeleka nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge ambaye, ndani ya siku kumi na nne kuanzia tarehe ya tangazo, ataitisha Mkutano wa Bunge ili kulijulisha Bunge kuhusu tangazo lililotolewa na Rais.	kusimamia hali ya ulinzi wakati wa dharura. Vilevile ni kuweka masharti ya kikatiba ya Rais kushirikisha Bunge na vyombo vingine katika kufikia uamuzi wa kutangaza vita.	cha uwakilishi kulitafakari jambo hilo kwa sababu suala la kuingiza nchi vitani ni kubwa na athari yake kwa taifa kijamii na kiuchumi ni makubwa. Rais kutangaza vita baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa inatoa fursa ya kwenda vitani katika hali ya dharura ambapo muda wa kuomba idhini ya Bunge haupo. Uzoefu wa nchi mbalimbali unaonesha kuwa Rais peke yake hana mamlaka ya kuingiza nchi vitani kabla ya kupata idhini ya mamlaka nyingine au inapolazimika kuingiza nchi vitani atapaswa kutoa taarifa kwenye mamlaka husika kwa mujibu masharti ya Katiba. Nchini Uganda, Rais analazimika kutoa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			tangazo la vita baada ya kupata kibali cha Bunge, na kama hali imelazimisha Rais kutangaza vita kabla ya Bunge kutoa kibali, Rais ataomba kibali baada ya hatua hiyo. Uzoefu uliotofauti na mfumo wa Tanzania ni ule wa Marekani ambapo Bunge ndiyo lenye mamlaka ya kutangaza vita na siyo Rais. Ingawa hiyo haimzuii Rais wa nchi hiyo kuchukua hatua za kivita kwa jambo linalohitaji uamuzi wa haraka katika kujilinda.
Ibara ya 85: Madaraka ya Raia kutangaza hali ya hatari.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii au sheria za nchi, Rais anaweza, baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, kutangaza hali ya hatari au hali ya kuzingirwa kwa eneo fulani la Jamhuri ya Muungano au katika	Madhumuni ya Ibara hii ni kuhakikisha kuwa hali ya amani na usalama katika nchi inaendelea. Aidha, ni kumwekea Rais mipaka ya kutumia madaraka ya kutangaza hali ya hatari au kuzingirwa kwa	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia sheria na mikataba ya kimataifa inayoorodhesha sababu mahsusi za kutangaza hali ya hatari kama vile: wakati kuna vita hasa pale nchi imevamiwa; panapokuwa na uasi au vitendo vingine vinavyolenga

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sehemu yake yoyote.	kutumia madaraka hayo, na kukabiliana na vitisho vya ndani na nje na kudhibiti athari mbalimbali yakiwemo majanga ya kimazingira.	kuiangusha Serikali iliyochaguliwa kihalali; panapokuwa na majanga makubwa ya kitaifa kwa mfano matetemeko ya ardhi, mafuriko, milipuko ya volkano au panapokuwa na matatizo makubwa ya kiuchumi kiasi cha kuhatarisha uhai wa Taifa. Sababu ya kumtaka Rais kushauriana na Baraza la Usalama la Taifa kabla ya kutangaza hali ya hatari ni kuweka utaratibu wa kushirikisha mamlaka nyingine halali ili madaraka hayo yasitumike vibaya au kutumiwa bila sababu ya msingi. Hii ni kwa sababu kutangaza hali ya hatari kunaambatana na athari kubwa kwa Taifa na haki za wananchi. Utangazaji wa hali ya hatari unaidhinisha dola kuchukua hatua zisizo za kawaida
	(2) Rais anaweza tu kutangaza kuwa kuna hali ya hatari iwapo -		
	(a) Jamhuri ya Muungano iko katika vita;		
	(b) kuna hatari ya dhahiri kwamba Jamhuri ya Muungano inakaribia kuvamiwa na kuingia katika hali ya vita;		
	(c) kuna hali halisi ya kuvurugika kwa amani katika jamii au kutoweka kwa usalama wa jamii katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yake yoyote kiasi kwamba		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ni lazima kuchukua hatua za pekee ili kurejesha amani na usalama; (d) kuna hatari dhahiri na kubwa, kiasi kwamba amani katika jamii itavurugika na usalama wa raia kutoweka katika Jamhuri ya Muungano au sehemu yake yoyote ambayo haiwezi kuepukika isipokuwa kwa kutumia mamlaka ya pekee; (e) karibu kutatokea tukio la hatari au tukio la balaa au janga la kimazingira ambalo linatishia jamii au sehemu ya jamii katika Jamhuri ya Muungano; au		ambazo zitaathiri haki za kiraia na za kibinadamu. Hivyo basi, madaraka hayo yanapaswa kudhibitiwa. Kwa mfano, uzoefu wa zaidi ya miaka 200 ya Marekani unaonyesha kuwa kuweka madaraka mengi kwa chombo kimoja kunaweza kuleta hatari kwa nchi. Hivyo, ni muhimu kuweka utaratibu wa kudhibiti utumiaji wa madaraka hayo.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(f) kuna aina nyingineyo ya hatari ambayo kwa dhahiri ni tishio kwa usalama wa nchi.		
	(3) Endapo inatangazwa kwamba kuna hali ya hatari katika Jamhuri ya Muungano au eneo lolote la Jamhuri ya Muungano, Rais atawasilisha nakala ya tangazo hilo kwa Spika wa Bunge ambaye, ndani ya siku zisizozidi kumi na nne tangu kutolewa kwa tangazo hilo, ataitisha mkutano wa Bunge ili kulijulisha juu ya taarifa ya hali ya hatari iliyotangazwa na Rais.		
	(4) Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti kuhusu nyakati na taratibu ambazo zitawawezesha baadhi ya watu		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wenye kusimamia utekelezaji wa mamlaka ya Serikali katika sehemu mahsusi za Jamhuri ya Muungano kumuomba Rais kutumia madaraka aliyopewa na Ibara hii kuhusiana na yoyote kati ya sehemu hizo endapo katika sehemu hizo, kunatokea lolote kati ya hali zilizotajwa katika aya ya (c), (d) na (e) za ibara ndogo ya (2) na hali hiyo haivuki mipaka ya sehemu hizo, na pia, kwa ajili ya kufafanua utekelezaji wa mamlaka ya Serikali wakati wa hali ya hatari.		
	(5) Tangazo la hali ya hatari lililotolewa na Rais kwa mujibu wa Ibara hii litakoma kutumika iwapo litafutwa na Rais.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(6) Kwa madhumuni ya kuondoa mashaka juu ya ufafanuzi au utekelezaji wa masharti ya Ibara hii, masharti ya utangazaji wa hali ya hatari kama ilivyotajwa katika Ibara hii, yatatumika tu katika sehemu ya Jamhuri ya Muungano ambapo hali hiyo ya hatari imetangazwa.		
Ibara ya 86: Mamlaka ya kutoa msamaha.	(1) Rais kwa mamlaka ya Mkuu wa Nchi, anaweza -	Madhumuni ni kumpa Rais, kwa nafasi yake ya Mkuu wa Nchi, mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa; na kutambua kuanzishwa chombo na utaratibu wa kumshauri Rais kuhusu kutoa msamaha.	1. Mamlaka ya kutoa msamaha kwa wafungwa ni muhimu katika nchi yoyote na kiongozi wa nchi ndiye anayestahili kuwa na mamlaka ya aina hii. Sababu za dhana hii ni pamoja na: kuwasamehe wafungwa kwa sababu za kibinadamu (mfano umri wao, afya mbaya au vigezo vingine
	(a) kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia kwa kosa lolote mbele ya Mahakama dhidi ya Jamhuri ya Muungano kwa masharti maalum kama yatakavyoainishwa katika		

Trial Version
www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria za nchi; au		vinavyofaa); Kumsamehe mfungwa aliyetiwa hatiani kimakosa; na Kuimarisha mashirikiano na mahusiano na mataifa mengine kwa kumsamehe raia wa nchi nyingine ambaye amefungwa katika Magereza ya Tanzania. Sababu ya kuanzishwa kwa Kamati ya Taifa ya Ushauri yenye wajibu wa kumshauri Rais kuhusu kutoa msamaha ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka uwepo utaratibu wa wazi wa kikatiba wa kutekeleza mamlaka hayo ya Rais ili kuondoa uwezekano wa matumizi yasiyo mazuri ya madaraka ya aina hii kwa kuwasamehe watu ambao jamii huona hawastahili kusamehewa.
	(b) kubadilisha adhabu ya kifo kuwa adhabu ya kifungo cha maisha.		
	(2) Masharti ya Ibara hii yatatumika kwa mtu aliyehukumiwa na kuadhibiwa akiwa Zanzibar na kwa adhabu zilizotolewa Zanzibar kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayotumika Zanzibar, hali kadhalika, masharti hayo yatatumika kwa mtu aliyehukumiwa na kuadhibiwa Tanganyika kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Bunge inayotumika Tanganyika.		
	(3) Kwa madhumuni ya Ibara hii, kutakuwa na Kamati ya Taifa ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Ushauri ambayo itakuwa na wajibu wa kumshauri Rais kuhusu kutoa msamaha kwa mtu yeyote aliyepatikana na hatia mahakamani na anatumikia adhabu.		
	(4) Utaratibu wa namna ya utekelezaji wa madaraka kwa mujibu wa Ibara hii, muundo, majukumu na utendaji kazi wa chombo kinachohusika na masuala ya msamaha wa wafungwa utaainishwa na sheria za nchi.		
Ibara ya 87: Kinga ya Mashtaka dhidi ya Rais.	(1) Wakati Rais akiwa madarakani, hatashitakiwa wala mtu yeyote hataendesha mashtaka ya aina yoyote dhidi yake mahakamani kwa ajili ya kosa lolote la jinai.	Madhumuni ya Ibara ni kulinda hadhi na heshima ya Rais akiwa Mkuu wa Nchi kwa kuwa yeye ni taswira na alama ya umoja wa kitaifa. Vilevile kumuondolea Rais hofu katika kutekeleza	Sheria za kimataifa na sheria za nchi zinawapa viongozi wa nchi kinga dhidi ya kushtakiwa kama ilivyo kwa wana diplomasia. Kwamantiki hiyo na pia kwa kuzingatia maoni ya wananchi ni muhimu kwa
	(2) Wakati Rais ameshika madaraka		

Final Version
www.finance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa mujibu wa Katiba hii, haitaruhusiwa kufungua mahakamani shauri la madai kuhusu jambo lolote alilolitenda au alilokosa kulitenda yeye binafsi kama raia ama kabla au baada ya kushika madaraka ya Rais, ila tu kama angalau siku thelathini kabla ya shauri kufunguliwa mahakamani, Rais atapewa au ametumiwa taarifa ya madai kwa maandishi kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi, na taarifa hiyo ikiwa inatoa maelezo kuhusu chanzo cha shauri hilo, kiini cha madai yenyewe, jina lake na anwani ya mahali anapoishi huyo mdai na jambo hasa analodai.	majukumu yake.	Rais akiwa Mkuu wa Nchi na Taswira ya Umoja wa Taifa abaki na kinga dhidi ya mashtaka akiwa madarakani na anapomaliza muda madaraka yake. Sababu ya mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa baadhi ya watu kuitumia fursa hiyo vibaya na hivyo kumfanya Rais asijiamini na kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Aidha, sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuimarisha utawala wa sheria na uwajibikaji kwa upande wa Mkuu wa Nchi na hivyo kumfanya Rais akiwa Kiongozi Mkuu kuwa mfano kwa wananchi wengine katika kufuata na kutii sheria.
	(3) Isipokuwa kama ataacha kushika madaraka ya Rais		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutokana na kuondolewa madarakani na Bunge, haitakuwa halali kwa mtu kumshtaki au kufungua mahakamani shauri lolote la jinai au la madai dhidi ya mtu aliyekuwa anashika madaraka ya Rais baada ya kuacha madaraka hayo kutokana na jambo alilofanya wakati alipokuwa bado anashika madaraka ya Rais.		
Ibara ya 88: Bunge Kumshtaki Rais.	(1) Bunge linaweza kupitisha azimio la kumuondoa Rais madarakani endapo itatolewa hoja ya kumshtaki Rais na ikapitishwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu utakaotumika kumuwajibisha Rais, kujenga tabia na utamaduni wa kutii Katiba na kulinda hadhi ya ofisi ya Rais na heshima ya nchi.	Kuweka utaratibu wa Bunge kumshtaki Rais ambao ni muhimu katika nchi ya kidemokrasia inayofuata utawala wa sheria kama Tanzania. Ni utaratibu unaomkumbusha kiongozi wa nchi kuwa anawajibika kufanya kazi yake ipasavyo, na kuheshimu Katiba na sheria za nchi. Aidha, ni
	(2) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Ibara hii, hoja		

Trial Version www.miarie.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yoyote ya kumshtaki Rais haitatolewa isipokuwa tu kama itadaiwa kwamba Rais ametenda mojawapo ya makosa yafuatayo: (a) ukiukwaji mkubwa wa masharti ya Katiba hii; (b) makosa makubwa ya jinai; (c) kuzuia kwa namna yoyote ile yeye kuchunguzwa kwa mujibu wa Ibara hii; (d) uhaini; (e) rushwa; (f) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha nafasi ya madaraka ya Rais wa		utaratibu unaomkumbusha kiongozi wa nchi kuwa mwenendo wake binafsi unafaa kuwa wenye maadili mema. Rais anatakiwa kuwa ni mfano kwa wananchi wote (*role model*). Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 imetoa mamlaka ya kumshtaki Rais kwa Bunge na siyo mhimili wa Mahakama ambao ndiyo wenye jukumu la kutoa haki, kutafsiri sheria na kuilinda Katiba ya nchi. Utaratibu huu umefuata mfumo wa Kiingereza na Kimarekani ambako mhimili wa Bunge ndiyo umepewa mamlaka ya kuwashtaki viongozi wa Serikali. Kihistoria, huko Uingereza Bunge lilihodhi madaraka hayo ili kuonyesha uwezo wake dhidi ya Serikali baada ya kumshinda

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Jamhuri ya Muungano; (g) kupuuza au kukataa kutekeleza uamuzi au amri halali ya Mahakama; au (h) amefanya kitendo ambacho kinakiuka kanuni za maadili au miiko ya uongozi. (3) Bunge halitapitisha hoja ya kumshtaki Rais isipokuwa tu kama- (a) hoja ya namna hiyo itatolewa baada ya miezi kumi na miwili tangu hoja kama hiyo ilipotolewa na ikakataliwa na Bunge; na (b) taarifa ya maandishi,		Mfalme. Lakini huko Marekani Bunge lilipewa mamlaka hayo kwa sababu tofauti. Suala la kumuondoa Rais wa nchi ni nyeti kwa hivyo ni muhimu kuweka utaratibu madhubuti ili kuepuka uwezekano wa kuvuruga amani na utulivu wa nchi. Mfano Katiba ya Marekani iliyotungwa mwaka 1787 na kuanza kutumika mwaka 1789 ililipa Bunge (Congress) mamlaka ya kumshtaki na kumuondoa madarakani Rais wa nchi hiyo. Kuwepo kwa utaratibu madhubuti wa kumuondoa Rais madarakani kutaepusha uwezekano wa kuvuruga amani na utulivu wa nchi.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	iliyotiwa saini na kuungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia ishirini na tano ya Wabunge wote itawasilishwa kwa Spika siku kumi na nne kabla ya kikao ambapo hoja hiyo inakusudiwa kutolewa Bungeni.		
	(4) Taarifa itakayowasilishwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (3)(b) itafafanua makosa aliyoyatenda Rais, na itapendekeza kuwa Tume ya Uchunguzi iundwe ili ichunguze tuhuma zilizotolewa dhidi ya Rais.		
	(5) Wakati wowote baada ya kupokea taarifa iliyotiwa saini na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Wabunge na kujiridhisha kuwa masharti ya Katiba kwa ajili ya kuwasilisha hoja yametimizwa, Spika atamruhusu mtoa hoja kuiwasilisha mbele ya Bunge na kisha Spika atalitaka Bunge, bila ya kufanya majadiliano, lipige kura juu ya hoja ya kuunda Kamati ya Uchunguzi.		
	(6) Endapo hoja ya kuunda Kamati ya Uchunguzi itaungwa mkono na Wabunge wasiopungua asilimia sabini na tano ya Wabunge wote, Spika atatangaza majina ya wajumbe wa Kamati ya Uchunguzi.		
	(7) Kamati ya Uchunguzi, kwa madhumuni ya Ibara hii, itakuwa na wajumbe wafuatao:		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Kamati;		
	(b) Jaji Mkuu wa Tanganyika;		
	(c) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na		
	(d) Wabunge sita kutoka Bunge la Jamhuri ya Muungano, watatu kutoka kila upande wa Nchi Washirika watakaoteuliwa na Spika.		
	(8) Endapo Bunge litapitisha hoja ya kuunda Kamati ya Uchunguzi, Rais atahesabiwa kuwa hayupo kazini na madaraka ya Rais yatatekelezwa na Makamu wa		

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Rais hadi Spika atakapomfahamisha Rais juu ya Azimio la Bunge kuhusiana na mashtaka yaliyotolewa dhidi yake.		
	(9) Ndani ya siku saba baada ya Kamati ya Uchunguzi kuundwa, itachunguza na kuchambua mashtaka dhidi ya Rais, pamoja na kumpatia Rais fursa ya kujieleza, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.		
	(10) Mapema iwezekanavyo, na kwa vyovyote vile katika muda usiozidi siku tisini, Kamati ya Uchunguzi itatoa taarifa yake kwa Spika.		
	(11) Baada ya Spika kupokea		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	taarifa ya Kamati ya Uchunguzi, taarifa hiyo itawasilishwa Bungeni kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Kudumu za Bunge.		
	(12) Baada ya taarifa ya Kamati ya Uchunguzi kuwasilishwa, Bunge litaijadili taarifa hiyo na kutoa fursa kwa Rais kujieleza, na kisha, kwa kura za Wabunge wasiopungua asilimia sabini na tano ya Wabunge wote, Bunge litapitisha azimio kuwa mashtaka dhidi ya Rais ama yamethibitika au hayakuthibitika.		
	(13) Endapo Bunge litapitisha azimio kuwa mashtaka dhidi ya Rais yamethibitika na kwamba hastahili kuendelea kushika nafasi ya madaraka ya Rais, Spika		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	atamfahamisha Rais juu ya Azimio la Bunge na Rais atakuwa ameondolewa madarakani na Makamu wa Rais ataapishwa mara moja kushika nafasi ya madaraka ya Rais.		
	(14) Endapo Rais ataacha kushika nafasi ya madaraka ya Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika hatakuwa na haki ya: (a) kushika nafasi ya madaraka ya Rais, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar; na (b) kupata malipo yoyote ya uzeeni, posho wala kupata haki au nafuu nyingine		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	anazopewa Rais au mtu aliyekuwa Rais kwa mujibu wa Katiba au sheria za nchi.		
Ibara ya 89: Maslahi ya Rais.	(1) Rais atalipwa mshahara na malipo mengineyo kama yatakavyoainishwa na Tume ya Utumishi wa Umma na atakapostaafu atapokea malipo ya uzeeni na stahili nyingine kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina.	Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupanga na kulinda maslahi ya Rais.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kikatiba mapato ya Rais ili kuziba mianya ya ubadhirifu, ufisadi na matumizi mabaya kwa ujumla. Vilevile ni kuimarisha dhana kuwa Rais ni mtumishi wa wananchi na kwa hivyo, kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina, atatunzwa kwa kazi yake ya kutumikia umma. Mapendekezo haya pia ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa chombo kitakachokuwa na jukumu la kupanga mishahara na maslahi ya Viongozi na Watumishi wa Umma ili kuweka uwiano wa malipo ya
	(2) Mshahara na malipo mengineyo yote ya Rais hayatapunguzwa wakati Rais atakapokuwa bado ameshika madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			mishahara na maslahi mengine katika Utumishi wa Umma.
(e) Makamu wa Rais			
Ibara ya 90: Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.	(1) Kutakuwa na Makamu wa Rais ambaye atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano kwa jumla na: (a) atafanya kazi zote atakazoagizwa na Rais; (b) atafanya kazi zote za Rais kama Rais hayupo kazini au yupo nje ya nchi; na (c) atakuwa Mwenyekiti wa Tume ya Mahusiano na Uratibu wa Serikali.	Madhumuni na lengo ni kuainisha kikatiba kuwepo kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ni Msaidizi Mkuu wa Rais pamoja na majukumu ya Makamu wa Rais aliyopewa na Katiba.	Mapendekezo haya ni kuendeleza masharti yaliyomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 kumtambua Makamu wa Rais kuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais Mtendaji. Aidha, kuwepo kwa nafasi ya Makamu wa Rais kutarahisisha utaratibu wa kukaimisha nafasi ya Rais pindi inapokuwa wazi. Sababu nyingine ni kwamba Makamu wa Rais atahusika pia na uratibu wa Ushirikiano wa Nchi Washirika wa Muungano katika mambo yasiyo ya Muungano na uhusiano wa Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika. Kwa sababu hiyo, Makamu
	(2) Katika utekelezaji wa madaraka		

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yake, Makamu wa Rais atatekeleza au atawezesha au kusimamia utekelezaji wa jambo lolote au mambo yoyote ambayo Rais ataagiza kwamba yatekelezwe. (3) Bila kuathiri masharti ya Katiba hii, Makamu wa Rais atawajibika kwa Rais kuhusu utekelezaji wa majukumu yake.		wa Rais ndiye Mwenyekiti wa Tume ya Uratibu na Ushirikiano ambayo Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar pia ni wajumbe. Aidha, inapendekezwa Tume ya Uratibu na Ushirikiano ipeleke taarifa zake Baraza la Ulinzi na Usalama ambalo Mwenyekiti wake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar ni wajumbe.
Ibara ya 91: Upatikanaji wa Makamu wa Rais.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 76, Makamu wa Rais atapatikana kwa kuchaguliwa katika uchaguzi pamoja na Rais, baada ya kupendekezwa na chama chake au mgombea huru wakati ule ule anapopendekezwa mgombea wa nafasi ya madaraka	Madhumuni ya Ibara hii ni kuainisha upatikanaji wa Makamu wa Rais kwa kupigiwa kura katika Uchaguzi Mkuu wa Rais kwa tiketi moja na Mgombea Urais.	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuendelea kuwepo kwa nafasi ya Makamu wa Rais. Pia ni kuonesha kuwepo kwa sura mbili za Nchi Washirika katika uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano.

Trial Version
www.tlace.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Rais na watapigiwa kura kwa pamoja.		Pia Ibara hii inaondoa uwezekano wa upande mmoja wa Muungano kutoa nafasi zote mbili za Rais na Makamu wa Rais
	(2) Endapo mgombea wa nafasi ya madaraka ya Rais atachaguliwa basi na Makamu wa Rais atakuwa amechaguliwa.		
	(3) Mtu atateuliwa kugombea nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais kwa kufuata kanuni kwamba endapo mgombea wa nafasi ya madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu wa Rais atakuwa ni mtu anayetoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 92: Sifa za	(1) Mtu hatateuliwa kugombea au kushika nafasi ya madaraka ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba sifa na vigezo	Sababu za kupendekeza sifa za Makamu wa Rais ziwe sawa na sifa za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Makamu wa Rais.	Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano isipokuwa tu kama anazo sifa za kuchaguliwa kuwa Rais.	vitakavyowezesha kumpata Makamu wa Rais. Pia ni kugawa nafasi za uongozi wa juu wa Jamhuri ya Muungano kati ya Nchi Washirika.	Rais ni kuwa yeye ndiye Msaidizi Mkuu wa Rais, na ndiye atayekaimu au kushika nafasi ya Rais ikiwa Rais atafariki dunia au ataondolewa madarakani kwa mujibu wa mashrti ya Katiba.
	(2) Chama cha siasa chochote au mtu yeyote anayekusudia kugombea nafasi ya madaraka ya Rais, akiwa mgombea huru, hatazuiwa kumpendekeza mtu yeyote kuwa mgombea nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais kwa sababu tu kwamba mtu huyo kwa wakati huo ameshika kiti cha Rais wa Zanzibar au Rais wa Tanganyika.		
	(3) Endapo mtu ambaye ni Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar anateuliwa au kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais ataacha nafasi ya madaraka ya Rais wa Tanganyika		

Unofficial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au ya Rais wa Zanzibar, kadri itakavyokuwa.		
Ibara ya 93: Kiapo cha Makamu wa Rais.	Makamu wa Rais, kabla ya kushika madaraka yake ataapishwa na Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano, kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.	Ibara hii inalenga kuweka utaratibu wa Makamu wa Rais kula kiapo cha kikatiba kabla ya kushika madaraka yake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba uliopo kwa Makamu wa Rais kula kiapo cha utii na uaminifu kabla ya kushika madaraka. Aidha, ni kuzingatia utaratibu wa kikatiba unaowataka Viongozi Wakuu kuapa kwa mujibu wa Katiba ili waweze kuwajibika na kutekeleza viapo vyao ikiwa ni pamoja na kulinda Muungano. Uzoefu wa Katiba za nchi nyingine kama Kenya na Marekani ambazo Rais wake huapishwa baada ya kipindi cha kati ya mwezi mmoja hadi miezi mitatu na huapishwa pamoja na Makamu wake.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 94: Wakati wa Makamu wa Rais kushika Madaraka.	(1) Makamu wa Rais atashika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais siku hiyo hiyo Rais anaposhika madaraka. (2) Makamu wa Rais atashika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais hadi - (a) muda wake utakapokwisha; (b) akifariki dunia akiwa katika madaraka; (c) atakapojiuzulu; (d) atakapoapishwa kuwa Rais baada ya nafasi ya madaraka ya Rais kuwa wazi; (e) atakapoapishwa Rais mwingine kushika nafasi ya	Lengo la Ibara hii ni kuonesha muda wa kuanza na ukomo wa Makamu wa Rais kushika madaraka kwa mujibu wa Katiba.	Sababu za mapendekezo ni kuendeleza utamaduni wa kuwepo kwa ukomo wa kushika madaraka kwa Viongozi Wakuu wa nchi kwa kutambua kuwa uongozi ni dhamana na siyo haki.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	madaraka ya Rais pamoja na Makamu wake;		
	(f) atakapoondolewa madarakani baada ya kushtakiwa Bungeni kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii; au		
	(g) atakapoacha kushika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais vinginevyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
Ibara ya 95: Bunge kumshtaki Makamu wa Rais.	(1) Bunge litakuwa na mamlaka ya kumshtaki na kumuondoa Makamu wa Rais madarakani kwa utaratibu unaotumika kumshtaki Rais kwa mujibu wa Katiba hii, isipokuwa kwamba, hoja yoyote ya kumshtaki	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kumuwajibisha Makamu wa Rais, kujenga tabia na utamaduni wa kutii Katiba, kulinda hadhi ya ofisi ya	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa Bunge kumshtaki Makamu wa Rais kwa mujibu wa Katiba, ambalo ni suala muhimu katika nchi ya kidemokrasia inayofuata

Trial Version
www.iLance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Makamu wa Rais itatolewa tu iwapo: (a) Rais amewasilisha hati kwa Spika inayoeleza kwamba Makamu wa Rais ameacha au ameshindwa kutekeleza kazi za madaraka ya Makamu wa Rais; (b) amekuwa na mwenendo unaodhalilisha nafasi ya madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au kiti cha Makamu wa Rais; au (c) anadaiwa kutenda kosa lolote kati ya makosa yanayoweza kusababisha Rais kushtakiwa na Bunge kwa mujibu wa Katiba hii,	Makamu wa Rais na heshima ya nchi. Lengo pia ni Kulipa Bunge mamlaka, ambacho ni chombo kinachowakilisha wananchi, kuchukua hatua kwa mujibu wa Katiba kumshtaki na kumuondoa madarakani Makamu wa Rais inapothibitika ametenda makosa yaliyoainishwa kwenye Rasimu ya Katiba.	utawala wa sheria.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	isipokuwa kwamba, haitatolewa hoja ya namna hiyo ndani ya miezi kumi na miwili tangu hoja kama hiyo ilipotolewa na ikakataliwa na Bunge.		
	(2) Masharti mengine kuhusu utaratibu wa kumshtaki Rais yatatumika wakati wa kumuondoa madarakani Makamu wa Rais.		
	(3) Masharti mengine yote ya Ibara ya 87 yatatumika pia kwa Makamu wa Rais isipokuwa tu kwamba Makamu wa Rais aliyeondolewa madarakani chini ya ibara ndogo ya (1), hatakuwa na sifa tena za kushika nafasi ya Rais, Makamu wa Rais, Rais wa Tanganyika au Rais wa Zanzibar.		
	(4) Endapo Makamu wa Rais ataacha kushika nafasi ya madaraka ya		

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Makamu wa Rais kutokana na mashtaka dhidi yake kuthibitika, hatakuwa na haki ya kupata malipo yoyote ya uzeeni, posho wala kupata haki au nafuu nyinginezo anazopewa Makamu wa Rais au mtu aliyekuwa Makamu wa Rais kwa mujibu wa Katiba hii au sheria za nchi.		
Ibara ya 96: Upatikanaji wa Makamu wa Rais wakati nafasi hiyo inapokuwa wazi	Endapo nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais iko wazi kutokana na masharti yaliyomo katika Ibara ya 94 na 95, basi mapema iwezekanavyo na kwa vyovyote vile ndani ya siku zisizozidi kumi na nne tokea kifo au baada ya kuachia madaraka, Rais atamteua mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura za Wabunge zaidi ya asilimia hamsini ya Wabunge wote.	Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa namna ya kujaza nafasi ya Makamu wa Rais itakapotokea kuwa wazi kabla ya kufika muda wake wa kuondoka madarakani kwa mujibu wa Katiba. Vile vile ni kulipa Bunge mamlaka ya kumthibitisha Makamu wa Rais, kwa niaba ya wananchi na kumpa kikatiba Makamu wa Rais uhalali wa	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kumpata Makamu wa Rais bila ya kusubiri uchaguzi mkuu na kuwezesha majukumu yake kuendelea kutekelezwa na hivyo kuzuia ombwe katika uongozi wa juu. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuendeleza maudhui mazuri ya ibara ya 50(4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Final Version
www.mlange.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		kisiasa.	
SEHEMU YA PILI - BARAZA LA MAWAZIRI LA SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO			
(a) Baraza la Mawaziri			
Ibara ya 97: Kuundwa kwa Baraza la Mawaziri.	(1) Kutakuwa na Baraza la Mawaziri la Jamhuri ya Muungano litakalokuwa na wajumbe wafuatao: (a) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; na (b) Waziri Mwandamizi na Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.	Lengo ni kuanzisha Baraza la Mawaziri na kutambua jukumu lake la msingi la kumshauri kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Pia, ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa Baraza la Mawaziri kufanya kazi yake ya ushauri kwa Rais bila ya hofu wala woga.	Sababu za mapendekezo haya ni kuanzisha chombo hiki na kutambua umuhimu wake katika kumshauri Rais kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Serikali. Aidha, ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977. Sababu nyingine ni kujenga mazingira ya chombo hicho kufanya kazi zake kwa uhuru bila kuingiliwa na mihimili mingine ya dola.
	(2) Rais ataongoza mikutano ya Baraza la Mawaziri, na endapo Rais hayupo, mikutano itaongozwa na Makamu wa Rais na kama wote wawili, Rais na Makamu wa Rais hawapo, Waziri Mwandamizi		

Trial Version
www.uandiko.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ataongoza Mikutano hiyo.		
	(3) Mwanasheria Mkuu wa Serikali atahudhuria vikao vya Baraza la Mawaziri lakini hatakuwa na haki ya kupiga kura.		
	(4) Baraza la Mawaziri ndicho chombo kikuu cha kumshauri Rais kuhusu mambo yanayohusu utekelezaji wa madaraka na matumizi ya mamlaka ya Rais.		
	(5) Bunge na Mahakama hazitakuwa na uwezo wa kisheria kuchunguza kama ushauri wowote au ushauri wa aina gani ulitolewa na Baraza la Mawaziri kwa Rais.		
Ibara ya 98: Uteuzi wa Mawaziri na Naibu	(1) Kutakuwa na Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya	Lengo la Ibara hii ni pamoja na kuweka ukomo wa idadi ya	Kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka Katiba itamke ukomo wa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mawaziri.	Muungano watakaoteuliwa na Rais kwa kushauriana na Makamu wa Rais na baadaye kuthibitishwa na Bunge. (2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), idadi ya Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano haitazidi kumi na tano. (3) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na Wizara kwa kuzingatia mamlaka ya Serikali kwa mujibu wa Katiba hii. (4) Uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano utazingatia uwakilishi wa Nchi Washirika. (5) Majukumu ya Waziri na Naibu Waziri yatakuwa kama yatakavyoainishwa na Rais kwenye	Mawaziri na Naibu Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Pia ni kulipa Bunge mamlaka ya kuwasaili na kuwathibitisha Mawaziri na Naibu Mawaziri kwa niaba ya wananchi ili kujenga uadilifu na kuthibitisha uweledi wa wateuliwa ili kukuza uwajibikaji katika uongozi wa taifa.	idadi ya Mawaziri ili kupunguza gharama za uendeshaji wa Serikali. Hii pia ni kutekeleza maoni ya wananchi waliotaka madaraka ya Rais ya uteuzi yasimamiwe kwa kulipa Bunge mamlaka ya kuwathibitisha. Aidha, kutokana na Mambo ya Muungano kupungua hadi kufikia saba na kupunguza ukubwa wa Serikali ya Shirikisho, Rasimu inapendekeza kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wasizidi kumi na tano.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Hati ya Uteuzi.		
Ibara ya 99: Waziri Mwandamizi.	(1) Kutakuwa na Waziri Mwandamizi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano atakayeteuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuweka nafasi ya Kikatiba ya Waziri Mwandamizi katika utendaji wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa na majukumu yaliyoainishwa katika Ibara ya 100 Rasimu.	Kwa kuzingatia ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za kila siku za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
	(2) Waziri Mwandamizi kabla ya kushika madaraka yake, ataapa mbele ya Rais kiapo cha uaminifu na kiapo kingine chochote kama itakavyoelezwa na sheria za nchi.		
	(3) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Waziri Mwandamizi endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 101.		
	(4) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Waziri Mwandamizi atashika madaraka ya Waziri Mwandamizi hadi:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) siku ambapo Rais mteule ataapa kushika madaraka ya Urais; au		
	(d) siku ambapo atafariki dunia akiwa katika madaraka; au		
	(e) siku atakapojiuzulu; au		
	(f) siku ambapo Rais atakapomteua mtu mwingine kushika madaraka ya Waziri Mwandamizi.		
Ibara ya 100: Kazi na Mamlaka ya Waziri Mwandamizi	(1) Waziri Mwandamizi atakuwa na madaraka ya udhibiti na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali za siku hadi siku. (2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba	Lengo ni kuweka Waziri Mwandamizi atakayemsaidia Rais kusimamia Wizara na Mawaziri katika utendaji wao wa shughuli za kila siku za Serikali.	Kusimamia na kutekeleza majukumu ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanatekelezwa na yanasimamiwa na Waziri Mkuu.

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hii, Waziri Mwandamizi atatekeleza majukumu yote atakayoelekezwa na Rais, na katika utekelezaji wa majukumu yake atawajibika kwa Rais.	Pia lengo la Ibara hii ni kumpa uwezo wa kikatiba Waziri Mwandamizi kukaimu nafasi ya Rais ikiwa Rais na Makamu wa Rais hawapo nchini.	Rasimu ya Katiba inapendekeza kuondoa nafasi ya Waziri Mkuu ambaye kiuhalisia alikuwa anasimamia mambo yasiyo ya Muungano ya Tanganyika kwasababu majukumu hayo sasa yatakuwa chini ya mamlaka ya Serikali ya Tanganyika.
Ibara ya 101: Sifa za Mawaziri na Naibu Mawaziri.	(1) Mtu atateuliwa kuwa Waziri au Naibu Waziri wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwa: (a) ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano. (b) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi; na	Lengo la Ibara hii ni kuleta ufanisi wa Serikali kwa kutaja sifa na vigezo mahsusi kwa mtu kuweza kuwa Waziri au Naibu Waziri. Aidha, Ibara hii inalenga kuweka mfumo wa kikatiba wa kutenganisha madaraka ya mihimili ya dola (*separation of powers*), kupunguza misuguano	Mfumo unaopendekezwa katika Rasimu hii kuwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wasitokane na Wabunge na wala wasihudhurie vikao vya Bunge isipokuwa kama watahitajika kutoa ufafanuzi kwenye vikao vya Kamati za Bunge au kwa Bunge zima kuhusu suala lolote lililopo katika madaraka yao ya utendaji ni kuzingatia maoni ya Wananchi waliotaka kutenganishwa kwa utendaji kazi wa Mihimili ya

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) ana uweledi na uzoefu.	kati ya Bunge na Mawaziri, na kuondoa uwezekano wa kuwepo mgongano wa kimasilahi unaotokana na majukumu ya Uwaziri na Ubunge au kazi nyingine.	Bunge na Serikali ili kuongeza uwajibikaji wa Bunge katika kuisimamia Serikali. Aidha, mapendekezo haya yataondoa manung'uniko ya wananchi kwamba majimbo yanayoongozwa na Wabunge ambao ni Mawaziri au Naibu Mawaziri yanapendelewa katika huduma za maendeleo. Sababu ya kupendekeza kuwa uteuzi wa Mawaziri na Naibu Mawaziri, uthibitishwe na Bunge pia ni kuzingatia maoni wananchi walio wengi walisema kuwa Bunge ndicho chombo chenye ridhaa ya wananchi wote, na hivyo kiwe na uhalali wa kudhibiti madaraka ya Rais katika uteuzi huo. Muhimu zaidi matarajio ni kuwa utaratibu huu utaongeza uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu
	(2) Watu wafuatao hawatakuwa na sifa ya kuteuliwa kuwa Mawaziri au Naibu Mawaziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano:		
	(a) Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Wabunge wa Bunge la Tanganyika, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar au madiwani katika Nchi Washirika;		
	(b) mtu aliyewahi kutiwa hatiani kwa makosa ya ubadhirifu wa mali za umma, ama katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika.		Mawaziri.
Ibara ya 102: Kiapo, Muda na Masharti ya Kazi ya Waziri na Naibu Mawaziri.	(1) Waziri au Naibu Waziri hatashika nafasi ya madaraka hadi awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha uaminifu na pia kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi yake kitakachowekwa na sheria za nchi. (2) Muda wa kushika nafasi ya madaraka ya Waziri au Naibu Waziri utaanza tarehe ambayo Waziri au Naibu Waziri anayehusika ataapishwa. (3) Kila Waziri anawajibika binafsi na kwa pamoja kwa Rais katika utekelezaji wa majukumu na katika kutumia nafasi ya madaraka ya Waziri. (4) Waziri au Naibu Waziri atashika	Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya kushika madaraka ya Waziri au Naibu Waziri katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Vile vile ni kuweka msingi wa uwajibikaji wa Waziri au Naibu Waziri, binafsi au kwa pamoja kwa Rais.	Sababu za mapendekezo haya ni kuwepo kwa masharti ya Kikatiba ya kiapo na ya kazi ya Waziri au Naibu Waziri ili kujenga imani kwa wananchi kuwa watatekeleza majukumu yao kwa uaminifu na uadilifu. Aidha, ni kuzingatia utaratibu unaopendekezwa wa Rais Mtendaji ambapo Mawaziri na Naibu Mawaziri watawajibika, binafsi au kwa pamoja kwa Mkuu wa Serikali aliyewateua. Utaratibu huu unaongeza nidhamu, ufanisi wa utendaji na uwajibikaji wa Mawaziri na Naibu Mawaziri.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nafasi ya madaraka kwa muda wote isipokuwa kama: (a) atajiuzulu au kufariki; (b) Rais atatengua uteuzi wake; au (c) zimebaki saa ishirini na nne kabla ya Rais mteule kushika madaraka ya Rais.		
Ibara ya 103: Utekelezaji wa shughuli za Serikali Bungeni.	(1) Mawaziri na Naibu Mawaziri hawatakuwa na haki ya kuhudhuria vikao vya Bunge isipokuwa tu: (a) endapo kutakuwa na hoja mahsusi ambayo Bunge linahitaji ufafanuzi kwa Waziri husika; au	Lengo la Ibara hii ni kubainisha kikatiba mgawanyo wa madaraka baina ya Mhimili wa Bunge na Mhimili wa Utendaji ambao ni Serikali. Aidha, lengo jingine ni kuweka utaratibu wa Mawaziri kuhudhuria vikao vya Kamati za	Sababu za mapendekezo ni kuweka utaratibu wa kuwawezesha Mawaziri ambao si Wabunge kuhudhuria vikao vya Bunge. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kutenganisha mamlaka ya Serikali na Bunge kwa kuweka wazi mipaka ya kiutawala ili kuondoa

Trial Version www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) endapo Serikali au Waziri ataomba na kuruhusiwa kuwasilisha au kuitolea ufafanuzi hoja yoyote Bungeni.	Bunge kwa kualikwa. Pia, ni kuweka msingi wa kuipa Serikali uwezo wa kufanya maamuzi juu ya masuala ya kisera kwa ujumla.	muingiliano wa majukumu ya mihimili ya dola katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku.
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), Waziri atakayeruhusiwa kuhudhuria kikao cha Bunge anaweza kulihutubia Bunge.		
	(3) Serikali ya Jamhuri ya Muungano, chini ya mamlaka ya Rais, ndiyo itakuwa na uwezo wa kufanya maamuzi juu ya sera za Serikali kwa jumla.		
	(4) Kila Waziri atahudhuria vikao vya Kamati za Bunge kila atakapohitajika na kutoa maelezo au ufafanuzi wa suala lolote linalohusu utendaji katika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nafasi ya madaraka yake.		
	(5) Kwa kuzingatia masharti mengine ya jumla ya Katiba hii, Mawaziri watatoa maelezo au taarifa ambazo zinahitajika kutolewa Bungeni kwa mujibu wa sheria za nchi.		
(b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali			
Ibara ya 104: Mwanasheria Mkuu wa Serikali.	(1) Kutakuwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ambaye katika Katiba hii ataitwa kwa kifupi kama "Mwanasheria Mkuu" ambaye atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge.	Lengo ni kuweka nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika kusimamia masuala ya kisheria ya Serikali, pia kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, utaratibu wa uteuzi wake na ukomo wake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Katiba wa kuanzisha na kuainisha nafasi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Majukumu yake. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali athibitishwe na Bunge kabla ya kuapishwa na Rais. Vile vile Mwanasheria Mkuu wa
	(2) Mtu anayestahili kuwa Mwanasheria Mkuu atakuwa na sifa zifuatazo:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano; (b) awe na shahada ya sheria ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi;		Serikali aendelee kushika madaraka hadi Rais atakapomteua Mwanasheria Mkuu mwingine ili nafasi hiyo isiwe wazi. Katiba ya mwaka 1977 iliweka masharti ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kukoma mara tu baada ya matokeo ya Urais kutangazwa.
	(c) awe ni mweledi na mwenye sifa ya uwakili wa Mahakama Kuu ya Zanzibar au Mahakama Kuu ya Tanganyika;		
	(d) awe ni mtumishi mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi Washirika;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) awe ni mtu ambaye amedumu na sifa hizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano; na		
	(f) ana tabia njema na mwenendo usiotiliwa shaka na jamii.		
	(3) Mwanasheria Mkuu atakuwa ndiye mshauri mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo ya sheria na, kwa ajili hiyo, atawajibika kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuhusu mambo yote ya kisheria, na◇ kutekeleza shughuli nyinginezo zozote zenye asili au kuhusiana na sheria zitakazopelekwa kwake au atakazoagizwa na Rais kuzitekeleza.		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(4) Mwanasheria Mkuu atatekeleza kazi au shughuli nyingine zilizokabidhiwa kwake na Katiba hii au sheria za nchi.		
	(5) Katika kutekeleza kazi yake, Mwanasheria Mkuu atakuwa na haki ya kuhudhuria na kusikilizwa na Mahakama katika Jamhuri ya Muungano na Mahakama Kuu za Nchi Washirika.		
	(6) Mwanasheria Mkuu hatashika nafasi ya madaraka ya Mwanasheria Mkuu hadi awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha utii na uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi yake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(7) Mwanasheria Mkuu, isipokuwa kama ataacha kushika nafasi ya madaraka yake mapema zaidi, ataendelea kushika madaraka hadi Rais atakapomteua Mwanasheria Mkuu mwingine.		
(c) ***Katibu Mkuu Kiongozi na Makatibu Wakuu***			
Ibara ya 105: Katibu Mkuu Kiongozi	(1) Kutakuwa na Katibu Mkuu Kiongozi atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi watatu katika utumishi wa umma watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kumtambua kikatiba Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Mkuu wa Utumishi wa Umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Lengo jingine ni kumpa Katibu Mkuu Kiongozi mamlaka ya kikatiba ya kutoa maelekezo kuhusiana na masuala ya utumishi wa umma.	Wadhifa wa Katibu Mkuu Kiongozi ni nafasi muhimu sana katika utendaji wa Serikali, hivyo ni vyema majukumu yake yakaainishwa katika Katiba. Katika utaratibu wa mgawanyo wa madaraka, Utumishi wa Umma ni chombo muhimu sana katika utekelezaji wa shughuli za serikali. Katibu Mkuu Kiongozi kwa nafasi yake ya Katibu wa Baraza la Mawaziri na Mkuu wa Utumishi wa Umma ni
	(2) Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Katibu wa Baraza la Mawaziri, Mwenyekiti wa Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu, Katibu wa Baraza la		

Final Version www.klarace.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Ulinzi na Usalama wa Taifa na Mkuu wa Utumishi wa Umma.	Aidha, kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Katibu Mkuu Kiongozi na utaratibu wa uteuzi wake kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi wa umma.	kiungo muhimu kati ya Baraza la Mawaziri na Watumishi wa Umma na hivyo ni vyema akawepo kikatiba.
	(3) Katika wadhifa wake wa Katibu wa Baraza la Mawaziri, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Mtendaji Mkuu katika Ofisi ya Baraza la Mawaziri, na atatekeleza shughuli zifuatazo kwa kufuata maagizo ya jumla au maalum atakayopewa na Rais, yaani:		
	(a) kuandaa ratiba ya mikutano na kutayarisha orodha ya shughuli za Baraza la Mawaziri;		
	(b) kuandika na kuweka kumbukumbu za mikutano;		
	(c) kutoa taarifa na maelezo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya uamuzi wa Baraza la Mawaziri kwa kila mtu au chombo cha umma kinachohusika na uamuzi uliotolewa; na		
	(d) kutekeleza kazi na shughuli nyingine zozote ambazo Rais ameagiza.		
	(4) Akiwa Mkuu wa Utumishi wa Umma, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa na mamlaka ya kutoa maelekezo ya mara kwa mara kuhusiana na masuala ya utumishi wa umma.		
	(5) Katika nafasi ya madaraka ya Katibu wa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa, Katibu Mkuu Kiongozi atakuwa Mkuu na Mratibu wa Sekretarieti ya Baraza la Ulinzi na		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Usalama wa Taifa. (6) Katibu Mkuu Kiongozi hatashika madaraka yake hadi awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha utii na uaminifu au kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi zake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
Ibara ya 106: Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu.	(1) Kutakuwa na Makatibu Wakuu watakaoteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi waandamizi katika utumishi wa umma kama watakavyopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma. (2) Kila Katibu Mkuu atakuwa kiongozi na Mtendaji Mkuu wa Wizara ya Serikali aliyopangiwa na Rais na atashika nafasi ya madaraka ya Katibu Mkuu na kutekeleza	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba masharti yanayobainisha sifa na wajibu wa Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu, na utaratibu wa uteuzi wao. Aidha, lengo jingine ni kuwapa hadhi ya kikatiba viongozi na watendaji wakuu wa Wizara na kuhakikisha kuwa nafasi hizi zinajazwa na watu wenye	Kutambua umuhimu wa Makatibu Wakuu ambao ndiyo Watendaji Wakuu wa Serikali na kuhakikisha kuwa wanapatikana kwa kuzingatia mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma. Katika mfumo wa Serikali ya Kidemokrasia inayoheshimu utawala wa sheria, katika nchi yenye mfumo wa siasa za vyama vingi ni vyema

Final Version www.ilanga.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	majukumu yake kama itakavyoainishwa katika sheria za nchi.	uweledi na uzoefu katika Utumishi wa Umma na ambao ni waadilifu.	Katiba ikalinda nafasi ya Katibu Mkuu.
	(3) Rais anaweza, kwa mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma, kumteua mtumishi mwandamizi katika Utumishi wa Umma kuwa Naibu Katibu Mkuu.		
	(4) Kila Katibu Mkuu atakuwa mshauri wa mwisho kwa Waziri kwa masuala yote ya utendaji na atatoa ushauri kwa Baraza la Mawaziri katika vikao na Kamati zitakazoitishwa na Katibu wa Baraza la Mawaziri.		
	(5) Katibu Mkuu au Naibu Katibu Mkuu hatashika madaraka yake hadi awe ameapa mbele ya Rais kiapo cha		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utii na uaminifu au kiapo kingine chochote kinachohusu utendaji wa kazi zake kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
(d) Utekelezaji wa Shughuli za Baraza la Mawaziri			
Ibara ya 107: Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu	Kutakuwa na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu itakayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi ambayo itakuwa na majukumu ya kuchambua na kulishauri Baraza la Mawaziri juu ya masuala mbalimbali kabla ya kuwasilishwa na kufanyiwa uamuzi na Baraza hilo na itatekeleza majukumu mengine kama itakavyopangiwa na Baraza la Mawaziri.	Kuweka kikatiba chombo cha ushauri cha Baraza la Mawaziri, na kutambua umuhimu wa kulinda kikatiba nafasi ya washauri wakuu wa Serikali. Aidha, lengo jingine ni kuweka msingi wa ushauri wao kuzingatiwa na kuheshimiwa na Viongozi wa kisiasa.	Ni vyema vyombo vyote vya utekelezaji wa majukumu ya nchi vikabainishwa kwenye Katiba ya nchi. Katika mfumo wa nchi unaozingatia utawala bora na wa sheria wenye lengo la kuongeza ufanisi wa utendaji wa Serikali ni muhimu kuwa na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (*Inter-Ministerial Technical Committee*). Utaratibu huu unaimarisha uelewa wa pamoja katika mwelekeo wa maamuzi ya Serikali .

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 108: Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri	(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ambayo itakuwa na jukumu la kuhudumia Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na kutekeleza majukumu mengine kama itakavyopangiwa na Katibu wa Baraza la Mawaziri. (2) Bunge linaweza kutunga sheria kuhusu utaratibu na utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.	Kutambua kikatiba Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kuwa ndio chombo cha ushauri na uratibu cha Baraza la Mawaziri katika utekekezaji wa majukumu ya Serikali. Lengo jingine ni kuhakikisha ulingano, mwendelezo na weledi katika maamuzi ya Baraza la Mawaziri na Serikali; na kuweka Kundi la Wataalam Waliobobea katika nyanja zao (*Think Tank*) la Serikali inayofanya utafiti na kutoa ushauri kwa Baraza la Mawaziri na Serikali. Kuimarisha uratibu wa ushauri wa kitaalam Serikalini.	Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ni chombo muhimu sana katika usimamizi wa shughuli za Serikali. Katika nchi nyingine za Afrika na hasa zile zilizotawaliwa na Wafaransa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ni chombo muhimu cha kikatiba na kinaongozwa na mtu mwenye hadhi ya Waziri wa Nchi. Chombo hiki ndicho "Think Tank" ya Baraza la Mawaziri na pia, kinachoratibu ushauri wa masuala yote ya Serikali kwa kushirikisha Wizara zote Serikalini. Hivyo, sababu ya mapendekezo haya ni kuanzisha kikatiba kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi yetu chombo hiki muhimu cha kuhudumia Baraza la Mawaziri na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA NANE **UHUSIANO NA URATIBU WA SERIKALI**			
Ibara ya 109: Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali.	(1) Kutakuwa na Tume ya kusimamia na kuratibu mahusiano baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na kusimamia na kuratibu uhusiano baina ya Serikali za Nchi Washirika, ambayo itajulikana kwa kifupi kama "Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali".	Kuanzisha kikatiba chombo kitakachosimamia uhusiano na uratibu baina ya Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; na baina ya Serikali za Nchi Washirika juu ya mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Kuweka utaratibu wa mawasiliano na mashauriano endelevu kati ya Serikali hizo tatu utakaotoa mwelekeo wa kuimarisha na kudumisha Muungano.	Kuhakikisha kuwepo kwa utaratibu wa kikatiba utakaowezesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kukutana kwa lengo la kujadiliana na kushauriana katika mambo ya msingi ya maendeleo ya wananchi ndani ya Jamhuri ya Muungano. Aidha, utaratibu huu utasaidia sana kuweka mahusiano mema na kuoanisha sera zote za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Kuwepo kwa Muungano wa zaidi ya Serikali moja katika Jamhuri ya Muungano kunahitaji mfumo madhubuti wa uratibu wa uhusiano na ushirikiano
	(2) Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali itakuwa na wajumbe wafuatao:		
	(a) Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa		

Trial Version www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mwenyekiti; (b) Rais wa Tanganyika; (c) Rais wa Zanzibar; (d) Mawaziri Wakaazi; (e) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya nje wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano.		baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za nchi Washirika na baina ya Serikali za nchi washirika zenyewe kwa zenyewe kwa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Moja ya udhaifu wa utaratibu unaotumika sasa ni kukosekana kwa nguvu ya kikatiba ya uratibu wa masuala ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni ya kiutawala na ya hiyari. Uzoefu wa nchi nyingine zenye mfumo wa Muungano au shirikisho na hata zile zenye Serikali za majimbo zina Tume za aina hii zinazoitwa kwa majina mbalimbali. Nchi nyingi zenye Tume hizi zinaitwa *Inter-Governmental Relations Commission*.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Nchi zenye tume hizi katika Katiba zao ni pamoja na India, Canada, Nigeria, Afrika ya Kusini na Kenya.
Ibara ya 110: Malengo ya Tume.	Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali itakuwa na malengo yafuatayo: (a) kuweka utaratibu bora na endelevu wa kushauriana na kushirikiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; (b) kukuza na kuwezesha uratibu na ushirikiano miongoni mwa Nchi Washirika kuhusu mambo yasiyo ya Muungano kwa lengo la kuwezesha	Kuimarisha kikatiba uratibu, uhusiano na ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Nchi Washirika zenyewe kuhusu mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano. Kujenga utamaduni wa kikatiba wa kutatua migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Nchi Washirika kwa njia ya majadiliano, mashauriano na maridhiano.	Kuweka utaratibu wa kikatiba utakaoweka mazingira mazuri ya kushauriana na kushirikiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na baina ya Nchi Washirika. Pia kuwezesha uratibu wa ushirikiano miongoni mwa nchi washirika katika mambo yasiyo ya muungano ili kuweka kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wao katika sura inayofanana. Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali pia itasaidia kuibua na kuyasimamia, kwa manufaa ya nchi, masuala mbalimbali ya Muungano na yasiyo ya Muungano yenye maslahi

Trial Version
www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kufanana kwa kiwango cha utoaji huduma kwa wananchi wote;		kwa Taifa kwa lengo la kuleta ustawi wa Taifa na jamii nzima ya Tanzania.
	(c) kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kujadili utekelezaji wa mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano kwa manufaa na ustawi wa wananchi wote; na		
	(d) kuweka mazingira mazuri ya utatuzi wa migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Nchi Washirika.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 111: Majukumu ya Tume.	(1) Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali itakuwa na jukumu maalum la kuwezesha uratibu na ushirikiano katika kutekeleza masharti ya Katiba hii, sera, sheria, mipango na mikakati baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Serikali za Nchi Washirika na pia itakuwa chombo maalum kwa ajili ya: (a) kushauriana na kushirikiana baina ya - (i) Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; na (ii) Serikali za Nchi Washirika zenyewe katika masuala yasiyo	Madhumuni ya ibara hii ni kuainisha kikatiba majukumu ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali ili kuipa nguvu kiutekelezaji. Kuimarisha Muungano kwa kuhakikisha kuna uwiano wa sera na sheria za Nchi Washirika katika mambo yasiyo ya Muungano. Madhumuni mengine ni kuwa na chombo cha kikatiba cha awali kwa ajili ya kuzuia, na inapotokea, kusuluhisha migogoro miongoni mwa Serikali ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika kabla ya migogoro hiyo kufikishwa kwenye Mahakama ya Juu kwa uamuzi wa mwisho.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kwamba kuna uwiano wa sera na sheria kwa Nchi Washirka katika mambo yasiyo ya muungano, pia kuweka utaratibu wa kusimamia na kukuza masuala yenye maslahi kwa Taifa, na kuweka utaratibu wa usuluhishi na utatuzi wa migogoro baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika na baina ya Serikali za Nchi Washirika. Aidha, kuwepo kwa zaidi ya Serikali moja ndani ya Jamhuri moja kunaweza kusababisha tofauti za kisera kwenye masuala ya msingi kama vile elimu, afya n.k baina ya Serikali za Nchi Washirika, hivyo ni muhimu kuwa na chombo maalum

Trial Version
www.nlaw.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Muungano; (b) kusimamia, kuratibu na kuhakikisha kwamba kuna kuwiana kwa sera na sheria za Nchi Washirika katika mambo yasiyo ya Muungano; (c) kushauriana na kushirikiana baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taasisi za kimataifa kwa niaba ya Nchi Washirika; (d) usimamizi na ukuzaji wa masuala yenye maslahi kwa Taifa; (e) usuluhishi na utatuzi wa		kwa ajili ya kusimamia na kuhakikisha kwamba, kunakuwa na ufanani (*harmonisation*) na ulinganifu (*approximation*) wa sera na sheria baina ya Serikali hizo katika mambo yasiyo ya Muungano.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	migogoro baina ya -		
	(i) Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; na		
	(ii) Serikali za Nchi Washirika katika mambo yasiyo ya Muungano.		
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1)(e), endapo upande wowote katika mgogoro hautaridhika na uamuzi wa Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali, unaweza kulipeleka suala hilo katika Mahakama ya Juu na uamuzi wa Mahakama hiyo utakuwa ni wa mwisho.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Bunge litatunga sheria kwa ajili ya -		
	(a) kusimamia uhusiano na uratibu baina ya Serikali za Nchi Washirika na kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika; na		
	(b) kuweka utaratibu wa utatuzi wa migogoro kwa mujibu wa Ibara hii.		
Ibara ya 112: Sekretarieti ya Tume.	(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Tume ya Uhusiano na Uratibu wa Serikali itakayoongozwa na Katibu akisaidiwa na Naibu Katibu ambao watateuliwa na Rais.	Kuanzisha kikatiba chombo cha kitaalam na kiutendaji cha Tume kitakachokuwa na wataalam wa fani mbalimbali watakaotoa ushauri wa kitaalam juu ya ulinganifu wa sera na sheria, na	Sababu za mapendekezo haya ni kuwa na chombo cha kutoa ushauri kwa Tume, kurahisisha na kusimamia utekelezaji wa majukumu na shughuli za kila siku za Tume. Uzoefu wa nchi nyingine kama vile
	(2) Mtu atateuliwa kuwa Katibu au		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Naibu Katibu ikiwa ana sifa zifuatazo:	pia juu ya uhusiano wa kimataifa.	Afrika ya Kusini, India, Kenya na Nigeria Sekretareti kama hizi zina idara za kisekta zenye kongane (*Clusters*) na Kamati za Ufundi (*Technical Committees*) ili kuimarisha usimamizi, uratibu na utendaji wa Tume na Serikali tatu katika Jamhuri ya Muungano. Kwa hiyo itafaa Sekretarieti inayopendekezwa kuwa na muundo kama huo.
	(a) ni mtumishi mwandamizi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi Washirika;		
	(b) ana shahada kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi; na		
	(c) ana mwenendo usiotiliwa shaka na jamii.		
	(3) Katibu na Naibu Katibu watawajibika kwa Tume na watafanya kazi na kutekeleza majukumu ya Sekretarieti.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(4) Uteuzi wa Katibu na Naibu Katibu wa Tume utafanywa kwa kuzingatia msingi kwamba endapo Katibu atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Naibu Katibu atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		
SURA YA TISA **BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO**			
SEHEMU YA KWANZA **KUUNDWA NA MADARAKA YA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO**			
Ibara ya 113: Kuundwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano.	(1) Kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano. (2) Wajumbe wa Bunge watakuwa wa aina zifuatazo:	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka mamlaka ya nchi itakayohusika na kutunga sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuweka aina na	Sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuanzisha chombo cha uwakilishi wa wananchi ambacho ni Bunge la Jamhuri ya Muungano litakalotunga sheria, kusimamia utekelezaji wa

Trial Version
www.hiari.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) Wabunge sabini wa kuchaguliwa kupitia majimbo ya uchaguzi yatakayotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi, hamsini kutoka Tanganyika na ishirini kutoka Zanzibar; na	utaratibu wa upatikanaji wa wawakilishi wa wananchi katika Bunge la Jamhuri ya Muungano.	shughuli za Serikali na kuwajibika kwa wananchi. Aidha, pamoja na sababu hiyo, ni kuweka utaratibu wa kuwapata Wabunge wa kuchaguliwa na Wabunge wa kuteuliwa na Rais kuwakilisha Watu Wenye Ulemavu. Sababu nyingine ya mapendekezo ni kuweka usawa wa kijinsi katika uwakilishi Bungeni, kuzingatia Mikataba ya kikanda na kimataifa na kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa Bunge dogo ili kupunguza gharama za uendeshaji na kuongeza ufanisi wa shughuli za Bunge.
	(b) Wabunge watano wenye ulemavu watakaoteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watu wenye sifa za kuchaguliwa kuwa wabunge kuwakilisha watu wenye ulemavu kwa kuzingatia uwakilishi wa Nchi Washirika na jinsi.		
	(3) Katika kila Jimbo la Uchaguzi kutakuwa na nafasi mbili za ubunge,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	moja kwa ajili ya mwanamke na moja kwa ajili ya mwanamme.		
	(4) Wabunge kutoka kila Jimbo la Uchaguzi watapatikana kwa kupigiwa kura na wananchi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na sheria inayoweka utaratibu kuhusu mambo ya uchaguzi.		
Ibara ya 114: Muda wa Bunge.	(1) Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Katiba hii, maisha ya kila Bunge yatakuwa ni muda wa miaka mitano.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka muda maalum wa kipindi cha Bunge ambao ni miaka mitano na kujenga utamaduni wa Bunge kutimiza malengo na majukumu yake katika muda uliopangwa.	Kuweka ukomo wa Wabunge ili kuwezesha uchaguzi mwingine kufanyika kila baada ya miaka mitano. Kutoa nafasi kwa wananchi wengine kushika madaraka ili kuleta mawazo mapya ya kifikra na kimaendeleo katika nchi.
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), maneno "maisha ya Bunge" maana yake ni muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge Jipya litaitishwa ili kukutana kwa mara ya kwanza baada ya uchaguzi wa wabunge na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuishia tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge kwa ajili ya kuwezesha uchaguzi mwingine kufanyika.		
Ibara ya 115: Madaraka ya Bunge.	(1) Bunge ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano——chenye madaraka, kwa niaba ya wananchi, kuisimamia Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii. (2) Katika kutekeleza majukumu yake, Bunge litakuwa na madaraka yafuatayo: (a) kutunga sheria pale ambapo utekelezaji unahitaji kutungiwa sheria; (b) kujadili na kutoa ushauri	Lengo la Ibara hii ni kuainisha majukumu ya Bunge kuwa ni chombo chenye madaraka ya kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali, kutunga sheria na kutoa ushauri kwa Serikali juu ya mambo yote yenye maslahi kwa Taifa.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua Bunge kuwa ni chombo kinachowakilisha wananchi katika kufanya maamuzi mbalimbali yanayohusiana na maslahi ya wananchi na Taifa. Sababu nyingine ni kuendeleza mfumo unaotumika katika nchi za kidemokrasia duniani ambapo kunakuwa na chombo cha aina hii ambacho kazi yake kubwa ni kutetea na kusimamia maslahi ya wananchi na kuimarisha msingi wa mgawanyo wa madaraka baina ya Bunge, Mahakama na Serikali.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika mambo yote yenye maslahi kwa taifa na umma wa Watanzania;		
	(c) kumuuliza Waziri yeyote suala lolote kuhusu mambo ya umma katika Jamhuri ya Muungano ambayo yako katika wajibu wake;		
	(d) kujadili mgawanyo na kuidhinisha matumizi ya fedha kwa Wizara, taasisi na mashirika ya Serikali;		
	(e) kujadili utekelezaji wa majukumu ya kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa bajeti;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(f) kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu, muda wa kati au muda mfupi unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali katika Jamhuri ya Muungano;		
	(g) kujadili na kuridhia mikataba ya kimataifa inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa; na		
	(h) kujadili na kuridhia mikataba yote inayohusisha rasilimali zinazosimamiwa na Serikali ya Jamhuri ya		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano.		
	(3) Bunge litaisimamia Serikali kwa kuangalia mwenendo wa utendaji wa Rais, Makamu wa Rais, Mawaziri na watendaji wakuu katika utumishi wa umma.		
Ibara ya 116: Mipaka ya Bunge katika kutumia madaraka yake.	(1) Katika kutekeleza madaraka ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba hii, wajibu wa Bunge utakuwa ni kuishauri Serikali na endapo Bunge halitaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika utekelezaji wa suala lililotolewa ushauri, basi Bunge litakuwa na haki ya kuiwajibisha Serikali kwa mujibu wa madaraka liliopewa katika Katiba hii.	Lengo la Ibara hii ni kuainisha masharti juu ya mipaka ya Bunge katika kuiwajibisha Serikali na kubainisha umuhimu wa mipaka ya mamlaka kati ya Mihimili Mikuu ya Dola.	Kuepusha muingiliano wa majukumu baina ya Bunge na mihimili mingine hasa wa utendaji na kuimarisha misingi ya udhibiti na urari wa madaraka (*Checks and balance*).
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo		

Trial Version
www.luanda.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya (1), Bunge halitachukua hatua yoyote ya kiutendaji ambayo, kwa desturi ni shughuli za Serikali, na halitatoa maagizo yoyote ya kiutendaji kwa Serikali na watumishi wa umma, isipokuwa kwamba, Bunge litashauri kuhusu suala lolote lililo katika dhamana ya Waziri anayehusika.		
Ibara ya 117: Madaraka ya Bunge Kutunga Sheria.	(1) Madaraka ya kutunga sheria kwa mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano yatakuwa chini ya Bunge la Jamhuri ya Muungano. (2) Madaraka ya kutunga sheria katika Tanganyika kwa mambo yote yasiyo ya Muungano yatakuwa chini ya Bunge la Tanganyika na madaraka ya kutunga sheria katika Zanzibar kwa mambo yote yasiyo ya Muungano yatakuwa chini ya Baraza	Kuainisha kikatiba kuwa Bunge la Jamhuri ya Muungano ndicho chombo chenye mamlaka ya kutunga sheria kwa mambo yote yanayohusu Jamhuri ya Muungano. Kuainisha kikatiba kuwa madaraka ya kutunga sheria ya Nchi Washirika kwa mambo yasiyo ya Muungano yamepewa Bunge la Tanganyika na Baraza la Wawakilishi	Sababu za mapendekezo ni kutofautisha majukumu ya kutunga sheria baina ya Bunge la Jamhuri ya Muungano na baina ya vyombo vya kutunga sheria vya Nchi Washirika. Pamoja na majukumu hayo, Ibara inaweka mipaka ya kila mamlaka katika kutunga sheria. Mipaka hiyo inalipa Bunge la Jamhuri ya Muungano litatunga sheria katika Mambo ya Muungano tu na vyombo vya kutunga

Tiri Version
www.tiri.or.tz

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	la Wawakilishi la Zanzibar.	Zanzibar. Ibara hii pia inalenga kubatilisha sheria yoyote itakayotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, Bunge la Tanganyika na Baraza la Wawakilishi Zanzibar kinyume na masharti ya Katiba hii.	sheria vya nchi Washirika vitatunga Sheria katika mambo yasiyo ya Muungano yanayohusu maeneo yao.
	(3) Endapo sheria iliyotungwa na Bunge inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge la Tanganyika au Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, sheria hiyo itakuwa batili na itatenguka.		
	(4) Endapo sheria iliyotungwa na Bunge la Tanganyika au Baraza la Wawakilishi la Zanzibar inahusu jambo lolote ambalo liko chini ya mamlaka ya Bunge la Jamhuri ya Muungano, sheria hiyo itakuwa batili na itatenguka.		
	(5) Bila ya kuathiri kutumika kwa Katiba ya Tanganyika na Katiba ya Zanzibar, Katiba hii itakuwa na nguvu ya sheria katika Jamhuri ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano kwa mambo yanayohusu Muungano na endapo sheria nyingine yoyote itakiuka masharti yaliyomo katika Katiba hii, basi sheria hiyo nyingine, kwa kiasi kinachokiuka Katiba hii, itakuwa batili.		
Ibara ya 118: Utaratibu wa Kubadilisha Katiba.	(1) Bunge linaweza kutunga Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii. (2) Muswada wa sheria wa kubadili Katiba utahesabiwa kuwa umepitishwa na Bunge iwapo utaungwa mkono kwa kura za Wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanganyika na wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Zanzibar. (3) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (1)	L Lengo ni kuweka utaratibu wa jinsi ya kufanya mapitio ya Katiba pindi itakapolazimu kurekebishwa na kuzuia marekebisho ya Katiba ya mara kwa mara.	Sababu za mapendekezo ni kufanya marekebisho ya Katiba yaridhiwe na pande zote mbili za Muungano ili kuimarisha hadhi sawa za Nchi Washirika. Sababu nyingine ni kulipa mamlaka Bunge kufanya mabadiliko ya masharti ya Katiba hii pale itakapoonekana inafaa.

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kubadilisha masharti ya Katiba hii maana yake ni pamoja na kurekebisha au kusahihisha masharti haya au kufuta na kuweka masharti mengine badala yake au kusisitiza au kubadilisha matumizi ya masharti hayo.		
Ibara ya 119: Utaratibu wa Kubadilisha Masharti mahsusi.	Bunge halitaweza kufanya mabadiliko ya Katiba kuhusu: (a) masharti yaliyomo katika Sura ya Kwanza, Sura ya Pili na Sura ya Nne; (b) masharti ya Ibara ya 60; (c) masharti ya Ibara ya 79; (d) kuongeza au kupunguza jambo lolote la Muungano;	Lengo ni kuliwekea Bunge mipaka katika kufanya mabadiliko ya masharti mahsusi ya Katiba. Aidha, kuhakikisha kuendelea kuwepo kwa Jamhuri ya Muungano na kwamba maeneo ya msingi ya masharti ya Katiba yanabadilishwa kwa ridhaa ya wananchi wenyewe.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuwapa nafasi wananchi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushiriki moja kwa moja katika kufanya maamuzi kuhusu maeneo muhimu ya Katiba kwa maslahi ya Taifa lao.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) uwepo wa Jamhuri ya Muungano; (f) masharti ya Ibara hii, hadi kwanza mabadiliko hayo yaungwe mkono na theluthi mbili ya wananchi wa Jamhuri ya Muungano kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano kwa Kura ya Maoni itakayoendeshwa na kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa sheria za nchi.		
Ibara ya 120: Utaratibu wa Kutunga Sheria.	(1) Bunge litatumia madaraka yake ya kutunga sheria kwa kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria ambao utawekwa saini na Rais. (2) Bila kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), Muswada wa Sheria	Lengo la Ibara ni kuainisha utaratibu utakaotumiwa na Bunge la Muungano katika kutekeleza wajibu wake wa kutunga sheria na Kanuni za Kudumu.	Sababu za mapendekezo hayo ni kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Bunge na kuhakikisha kunakuwa na ushirikishwaji wa wananchi katika utungaji wa sheria. Kutoa nafasi sawa kwa Wabunge wa pande zote mbili za

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	unaweza kuandikwa na Serikali, Kamati ya Bunge au kikundi cha Wabunge.		Muungano kushiriki katika kutunga Sheria na Kanuni. Aidha, ni kuhakikisha kuwa kunakuwa na utaratibu mmoja unaofuatwa katika kutunga sheria.
	(3) Wakati wa kuandaa Muswada wa Sheria kuhusu jambo lolote la Muungano, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itahakikisha kwamba inawashirikisha wananchi kwa ajili ya kupata maoni na mapendekezo juu ya muswada huo.		
	(4) Muswada wa sheria utahesabiwa kuwa umepitishwa na Bunge iwapo utaungwa mkono kwa kura za wabunge wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanganyika na wasiopungua theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Zanzibar.		
	(5) Bila kuathiri masharti ya ibara		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ndogo ya (4), Bunge litatunga Kanuni za Kudumu zitakazoweka utaratibu wa -		
	(a) kuwasilisha, kujadili na kupitisha Muswada wa Sheria; na		
	(b) utekelezaji bora wa masharti ya ibara ndogo ya (3).		
Ibara ya 121: Utaratibu wa Kutunga Sheria Kuhusu mambo ya Fedha.	(1) Bunge halitashughulikia jambo lolote kati ya mambo yanayohusika na Ibara hii isipokuwa kama Rais amependekeza kwamba jambo hilo lishughulikiwe na Bunge na pendekezo hilo la Rais liwe limewasilishwa kwenye Bunge na Waziri.	Lengo ni kuweka mipaka ya kikatiba kuhusu utaratibu wa kutunga sheria kuhusu mambo ya fedha. Mambo hayo ni pamoja na miswada ya Sheria kuhusu kodi, malipo au matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina au mfuko	Sababu ni kuondoa muingiliano wa madaraka kati ya Serikali na Bunge katika kutekeleza majukumu yao kuhusu masuala ya fedha.

Final Version www.kiuna.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Mambo yanayohusika na Ibara hii ni yafuatayo: (a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya jambo lolote kati ya mambo yafuatayo: (i) kutoza kodi au kubadilisha kodi kwa namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza; (ii) kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina au mfuko mwingine wowote wa Serikali au kubadilisha	mwingine wowote wa Serikali na kusamehe au kufuta deni lolote la Serikali. Lengo jingine ni kuweka mipaka kati ya madaraka ya Serikali na ya Bunge kuhusu masuala ya fedha.	

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kiwango hicho na namna nyingine yoyote isipokuwa kupunguza;		
	(b) kuagiza kwamba malipo au matumizi ya fedha yafanywe kutokana na Mfuko Mkuu wa Hazina au mfuko mwingine wowote wa Serikali wakati ikifahamika kwamba fedha iliyomo katika mifuko hiyo haikupangiwa itolewe kwa ajili ya malipo au matumizi hayo, au kuagiza kwamba malipo au matumizi yanayofanywa kutokana na mifuko hiyo yaongezwe;		
	(c) kufuta au kusamehe deni		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	lolote linalotakiwa lilipwe kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; au		
	(d) hoja au mabadiliko yoyote ya hoja kwa ajili ya lolote kati ya mambo yaliyoelezwa katika aya ya (a) ya Ibara hii ndogo.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 122: Madaraka ya Mkuu wa Nchi Kuhusu Muswada wa Sheria.	(1) Muswada wa Sheria uliopitishwa na Bunge sharti kupata saini ya Rais, ili kuthibitisha kukubaliwa kwake na Rais. (2) Muswada wa Sheria uliyowasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali utawekewa saini na Rais ndani ya siku zisizozidi thelathini kutoka siku ambayo Muswada huo uliwasilishwa na kupokelewa na	Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua nafasi ya Rais akiwa Mkuu wa Nchi katika utaratibu wa kuidhinisha Miswada ya Bunge kuwa Sheria. Sababu nyingine ni kuweka udhibiti kwa Bunge katika jukumu lake la kutunga sheria kwa kuhakikisha maslahi ya taifa na maslahi ya wananchi.	Chini ya mapendekezo ya Rasimu hii, Rais si sehemu ya Bunge, hata hivyo ni muhimu kwake kuidhinisha Miswada ya Serikali kama ilivyo katika nchi nyingine zenye utaratibu huu kwa mfano Marekani na Kenya. Sababu nyingine ni kujenga uhusiano bora na mzuri kati ya Bunge na Serikali na kuepuka uwezekano wa kukwamishana katika utekelezaji wa shughuli zao na kuepuka kuvunja Bunge kama ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Katibu wa Baraza la Mawaziri.		
	(3) Baada ya Muswada wa Sheria kuwasilishwa kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, Rais anaweza kukubali au kukataa Muswada huo, na iwapo Rais atakataa kuukubali Muswada huo basi ataurudisha Bungeni pamoja na maelezo ya sababu za kukataa Muswada huo.		
	(4) Baada ya Muswada wa Sheria kurudishwa Bungeni na Rais kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii, Muswada huo hautapelekwa tena kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake kabla ya kumalizika muda wa siku sitini tangu uliporudishwa Bungeni.		
	(5) Endapo katika kujadiliwa tena Bungeni kabla haujapelekwa tena kwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Rais, Muswada uliorudishwa Bungeni na Rais umeungwa mkono na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote, basi Muswada huo unaweza kuwasilishwa mapema zaidi kwa Rais.		
	(6) Iwapo Muswada uliorudishwa Bungeni na Rais na katika kuujadili ukaungwa mkono na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote na kupelekwa tena kwa Rais kwa ajili ya kupata kibali chake, basi Rais atatakiwa kuukubali Muswada husika kabla ya kumalizika muda wa siku sitini, na endapo siku sitini zitapita tangu Muswada huo ulipopelekwa tena kwa Rais pasipo Rais kuukubali, basi Katibu wa Bunge ataandika Hati kuthibitisha kuwa Muswada huo		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	umekuwa sheria.		
Ibara ya 123: Kupitishwa Kwa Hoja za Serikali.	(1) Endapo Bunge halitaridhishwa na mchanganuo au mgawanyo wa hoja ya Bajeti ya Serikali, Bunge linaweza kurudisha hoja ya Bajeti ya Serikali pamoja na mapendekezo mahsusi kuhusiana na upungufu uliobainika. (2) Serikali itawajibika kuyafanyia kazi mapendekezo ya Bunge kwa kadri itakavyowezekana na kisha kuwasilisha tena Bungeni hoja husika pamoja na maelezo ya utekelezaji wa maelekezo ya Bunge na endapo Bunge litakataa kwa mara ya pili hoja kuhusu Bajeti ya Serikali, basi hoja hiyo itahesabika kuwa imepitishwa na Bunge.	Lengo ni kuhakikisha kuwa bajeti ya serikali inapitishwa kwa kuzingatia mapendekezo ya Bunge. Lengo jingine ni kuepuka Bunge kukwamisha shughuli za utendaji za nchi na Serikali bila sababu za msingi lakini wakati huo huo kuzuia serikali kuliburuza Bunge.	Sababu ya mapendekezo haya ni kwamba Serikali ndio yenye jukumu la kukusanya kodi kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kwa ajili ya maendeleo ya Serikali. Sababu nyingine ni kwamba Bunge ndio chombo cha wananchi chenye mamlaka ya kuweka viwango na utozaji wa kodi kutokana na mapendekezo ya Serikali.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SEHEMU YA PILI - WABUNGE			
		(a) Uchaguzi wa Wabunge	
Ibara ya 124: Uchaguzi wa Wabunge.	(1) Kila baada ya Bunge kumaliza muda wake wa kipindi cha miaka mitano, kutakuwa na uchaguzi wa Wabunge katika Majimbo ya uchaguzi kama itakavyotangazwa na Tume Huru ya Uchaguzi utakaofanyika kwa mujibu wa sheria za nchi. (2) Kutakuwa na uchaguzi wa Mbunge katika jimbo la uchaguzi ikiwa kiti cha Mbunge aliyechaguliwa kuwakilisha jimbo la uchaguzi kwa utaratibu wa mgombea huru, kitakuwa wazi kwa sababu nyingine yoyote isiyohusika na Bunge kumaliza muda wake.	Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya kuwa na uchaguzi wa mara kwa mara katika vipindi maalum. Lengo jingine ni kuwapa wananchi mamlaka ya kutoa ridhaa kwa wawakilishi wao.	Bunge ndicho chombo cha uwakilishi cha wananchi chenye dhamana ya kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali. Kwa hiyo, ni vyema wabunge wakawa wanathibitishwa kila baada ya kipindi maalum ili waendelee kuwa na ridhaa ya wananchi. Aidha, sababu nyingine ya mapendekezo ya Ibara hii ni kuepusha gharama za chaguzi ndogo katika mfumo wa uchaguzi nchini.

Hiqu Vision
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Endapo tarehe ya Bunge kumaliza muda wake imetangazwa au inafahamika, hakutakuwa na uchaguzi mdogo wa mbunge kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2) ndani ya kipindi cha miezi kumi na minane kabla ya tarehe hiyo.		
	(4) Endapo Mbunge anayetokana na chama cha siasa atapoteza sifa za kuwa Mbunge kwa sababu yoyote isiyokuwa ya Bunge kumaliza muda wake, Tume Huru ya Uchaguzi, kwa mujibu wa masharti yatakayowekwa na sheria za nchi kwa ajili hiyo, itamteua na kumtangaza kuwa Mbunge mtu mwingine kutoka kwenye orodha ya majina ya wagombea iliyowasilishwa na chama hicho kwa mujibu wa ibara ndogo ya (		

Trial Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(4) Orodha ya majina ya wagombea kutoka kila chama cha siasa iliyowasilishwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi katika Uchaguzi Mkuu ndiyo itakayotumiwa na Tume Huru ya Uchaguzi baada ya kushauriana na chama cha siasa kinachohusika, kwa madhumuni ya kujaza nafasi ya Mbunge inapotokea kuwa wazi, wakati wowote wa Maisha ya Bunge.		
Ibara ya 125: Sifa za kuchaguliwa kuwa Mbunge.	(1) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika Ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge endapo: (a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano aliyetimiza umri wa miaka ishirini na moja wakati wa kugombea;	Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba ya sifa za mtu kuchaguliwa au kuteuliwa kuwa Mbunge. Vilevile kutambua kikatiba haki ya msingi ya uraia ya kupiga kura na kupigiwa kura bila kuhitaji kuwa mwanachama wa chama cha siasa. Pia	Kwa kuzingatia haki ya msingi ya uraia ya kupiga na kupigiwa kura, ni vyema Katiba ikatoa nafasi kwa wananchi kushiriki katika maamuzi yenye maslahi kwa Taifa lao. Aidha, kuondoa masharti ya Katiba ya sasa ya kuhitaji mgombea awe mwanachama wa Chama cha Siasa ili kuweza kugombea

Trial Version
www.iuace.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) anajua kusoma na kuandika lugha ya Kiswahili au Kiingereza na ana elimu isiyopungua kidato cha nne; (c) ni mwanachama aliyependekezwa na chama cha siasa au mgombea huru (d) ni mwadilifu na anayeheshimu haki za binadamu na asiyedharau wala kubagua watu kwa misingi ya kabila, dini, jinsi, maumbile au hali zao katika jamii; na (2) Mtu hatakuwa na sifa za kugombea kuchaguliwa kuwa	kuhakikisha mgombea atamudu kutekeleza majukumu ya nafasi ya ubunge kwa kiwango kikubwa na kuhakikisha anapatikana Mbunge mwenye uzalendo na maadili.	nafasi ya uongozi. Kuwepo kwa Mgombea Huru kunaimarisha haki ya uraia na kupanua wigo wa demokrasia, kwa kutoa fursa kwa wananchi ambao siyo wanachama wa Vyama vya Siasa kushiriki katika chaguzi mbalimbali. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi kwamba nafasi ya Mgombea Huru iwepo kwa sababu ni haki ya msingi kwa kila mwananchi kuchagua au kuchaguliwa. Suala la kuwepo kwa Mgombea Huru katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania limeshaagizwa na uamuzi uliotolewa na Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu iliyoipa Tanzania mwaka mmoja kuwa imetekeleza agizo hilo. Pia Mahakama ya Rufani ya Tanzania

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mbunge ikiwa -		imeshalishauri Bunge lirekebishe Katiba na kuruhusu kuwepo kwa Mgombea Huru. Maamuzi haya ya Mahakama yalitokana na shauri la kupinga Mabadiliko ya Kumi na Moja ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 yaliyoweka masharti ya mgombea nafasi ya uongozi kulazimika kuwa mwanachama wa Chama cha Siasa. Mabadilko haya ya Katiba yalifanywa na Bunge ili kufuta uamuzi wa Mahakama Kuu ya Tanzania ulioruhusu Mgombea Huru.
	(b) mtu huyo aliwahi kuwa Mbunge kwa vipindi vitatu vya miaka mitano; au		
	(c) imethibitishwa rasmi kwamba mtu huyo ana ugonjwa wa akili;		
	(d) mtu huyo amehukumiwa na Mahakama yoyote katika Jamhuri ya Muungano na kupewa adhabu ya kifo au ya kufungwa gerezani kwa muda unaozidi miezi sita kwa kosa lolote;		
	(e) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uchaguzi amepata kuhukumiwa na kupewa adhabu ya kifungo kwa kosa linaloambatana na kukosa uaminifu au kwa kuvunja sheria inayohusiana na Maadili ya Uongozi;		
	(f) mtu huyo ana maslahi yoyote katika mkataba wa Serikali wa aina yoyote aliyowekewa miiko maalum kwa mujibu wa sheria za nchi, na iwapo amekiuka miiko hiyo; au		
	(g) mtu huyo anashika madaraka ya ofisa mwandamizi katika utumishi wa Serikali ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Jamhuri ya Muungano au Nchi Washirika; (h) kwa mujibu wa sheria ya nchi inayoshughulikia makosa yanayohusika na uchaguzi wa aina yoyote, mtu huyo amezuiliwa kujiandikisha kama mpiga kura au kupiga kura katika uchaguzi wa Wabunge; au (i) katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya uchaguzi amewahi kutiwa hatiani katika mahakama kwa kosa la kukwepa kulipa kodi yoyote ya Serikali au makosa yanayohusu kukosa uaminifu.		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Bunge linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti yatakayomzuia mtu asichaguliwe kuwa Mbunge wa kuwakilisha Jimbo la Uchaguzi ikiwa mtu huyo ni mwenye madaraka yanayohusika na shughuli za kuongoza au kusimamia uchaguzi wa Wabunge au shughuli za uandikishaji wa wapiga kura kwa ajili ya uchaguzi wa Wabunge.		
	(4) Katika aya ya (e) ya ibara ndogo ya (2) ya Ibara hii "mkataba wa Serikali" maana yake ni mapatano yoyote ya mkataba ambayo mmojawapo wa walioshiriki ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali ya Mapinduzi Zanzibar au Serikali ya Tanganyika, Idara		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au Taasisi yoyote ya Serikali yoyote kati ya hizo au mtumishi yeyote wa Serikali aliyeshiriki katika majadiliano ya mkataba husika kwa niaba ya Serikali yoyote miongoni mwa hizo.		
	(5) Watu wenye nyadhifa zifuatazo katika Utumishi wa Umma hawatakuwa na sifa ya kuwa Wabunge:		
	(a) Rais na Makamu wa Rais;		
	(b) Rais wa Tanganyika na Rais wa Zanzibar na Makamu wao;		
	(c) Spika na Naibu Spika wa Bunge;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(d) Waziri na Naibu Waziri;		
	(e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali;		
	(f) Katibu Mkuu Kiongozi, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu;		
	(g) Viongozi na watumishi wa vyombo vya ulinzi na usalama;		
	(h) mtu ambaye ameajiriwa katika vyombo vya dola kama askari;		
	(i) Jaji Mkuu, Jaji au Hakimu wa Mahakama,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Wakili wa Serikali na Ofisa Sheria Katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Washirika;		
	(j) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;		
	(k) Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi; na		
	(l) mtu yeyote aliyeajiriwa, kuteuliwa au kuchaguliwa katika utumishi wa umma.		
	(6) Kwa madhumuni ya kutoa fursa ya kukata rufani kwa mtu yeyote:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) aliyethibitishwa rasmi kisheria kuwa ana ugonjwa wa akili;		
	(b) aliyehukumiwa na kupewa adhabu ya kifo au kifungo; au		
	(c) aliyepatikana na hatia ya kosa lolote lililotajwa katika sheria kwa mujibu wa ibara ndogo ya (2),		
	mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria kwa ajili ya kuweka masharti kwamba hukumu inayopingwa haitakuwa na nguvu kwa ajili ya utekelezaji wa masharti ya ibara ndogo ya (2) hadi upite muda uliotajwa katika sheria hiyo.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 126: Utaratibu wa Uchaguzi wa Bunge.	(1) Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi watachaguliwa na wananchi kwa kufuata masharti ya Katiba hii na sheria za nchi kwa mujibu wa Katiba hii, inayoweka masharti kuhusu uchaguzi wa Wabunge. (2) Wagombea uchaguzi katika majimbo ya Uchaguzi watatakiwa kuwasilisha majina yao kwa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na sheria za nchi.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka msingi wa hiyari wa mtu kugombea ubunge na kuainisha utaratibu wa uchaguzi unaowezesha kupatikana kwa Wabunge. Lengo jingine ni kuandaa mazingira ya uwazi katika kuwapata wawakilishi wa wananchi Bungeni.	Sababu ya mapendekezo haya ni kumfanya mtu anayetaka kugombea ubunge kuthibitisha dhamira na nia yake ya kugombea ubunge kwa hiyari ili awajibike kwa uamuzi wake iwapo atachaguliwa kuwa mwakilishi wa wananchi. Ubunge ni dhamana na ni vyema kabla ya mtu kuomba ridhaa ya wananchi kuwaongoza awe ametafakari kwa makini na kuthibitisha yeye mwenyewe kwa kuomba. Sababu nyingine ni kukuza uwazi katika mchakato wa kuwapata wawakilishi wa wananchi bungeni.
bara ya 127: Kiapo na Masharti ya Kazi ya	(1) Kila Mbunge ataapishwa kiapo cha uaminifu na Spika katika Bunge	Lengo ni kuweka msingi wa uwajibikaji wa Mbunge kwa	Sababu za mapendekezo ya masharti ya kula kiapo cha uaminifu na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Bunge.	kabla hajaanza kushiriki katika shughuli za Bunge, lakini Mbunge anaweza kushiriki katika uchaguzi wa Spika hata kabla hajaapishwa. (2) Mbunge atashika madaraka kwa mujibu wa Katiba hii, na atalipwa mshahara, posho na malipo mengine kama yatakavyopangwa na Tume ya Utumishi wa Umma kwa mujibu wa sheria za nchi. (3) Wakati wowote wa madaraka yake, Mbunge atawajibika moja kwa moja kwa wapiga kura wake.	wapiga kura wake. Pia kuwapa nguvu ya kikatiba wapiga kura kumuwajibisha Mbunge wao. Lengo jingine ni kuweka chombo huru nje ya Bunge kitakachopanga na kusimamia maslahi na posho za Mbunge. Aidha, kuweka utaratibu wa kuwabana Wabunge kuheshimu, kutii na kulinda Katiba na dhamana yao kwa wapiga kura wao na kuainisha kikatiba masharti ya kushika nafasi ya ubunge.	uwajibikaji kwa wananchi kunajenga msingi kuwa Mbunge kuwa na dhamana kwa wananchi waliomchagua. Katika baadhi ya nchi za Afrika baada ya uhuru nafasi ya ubunge iligeuzwa kuwa ni mahali pa kuchuma na kujinufaisha binafsi na siyo kuwatumikia wananchi kwa kujitolea. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuzingatia malalamiko ya wananchi wengi kuhusu tabia ya Wabunge kujiongezea posho mara kwa mara bila kujali hali ya maisha ya mwananchi wa kawaida. Ni muhimu kwa chombo cha wawakilishi wa wananchi kuwa na haiba, heshima na imani ya wananchi. Sababu nyingine ni kuashiria mwanzo wa utekelezaji wa madaraka ya Mbunge pamoja na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kujenga imani ya wananchi kuwa Mbunge atatekeleza majukumu yake kwa uaminifu, umakini, haki na usawa.
Ibara ya 128: Kupoteza Sifa za Ubunge.	(1) Mbunge atakoma kuwa Mbunge ikiwa litatokea lolote kati ya mambo yafuatayo: (a) tukio lolote ambalo, kama asingekuwa Mbunge lingemfanya asiwe au apoteze sifa za kuchaguliwa au kuteuliwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;	Kuhakikisha kwamba Mbunge anahudhuria vikao vyote na kutekeleza wajibu wake ipasavyo ili kuimarisha maadili na uadilifu kama yalivyoainishwa katika sheria za nchi. Lengo jingine ni kuweka msingi wa mbunge aliyependekezwa na chama kuwajibika kwa vyama vyao vya siasa na kuainisha kikatiba sababu za kupoteza sifa za kuwa Mbunge.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni wa wananchi walisistiza kuwa na Wabunge wanaowajibika kwa wapiga kura wao, wenye maadili na mwenendo mzuri usio na ubinafsi. Sababu nyingine ni kuweka vigezo vya nidhamu na staha ndani na nje ya Bunge.

Trial Version
www.nuane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) atakosa kuhudhuria Mikutano ya Bunge miwili mfululizo bila ya ruhusa ya Spika;		
	(c) itathibitishwa kwamba amevunja masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;		
	(d) atashindwa kufanya kazi za Mbunge kwa muda wa miezi sita mfululizo kutokana na maradhi au kizuizi ndani ya gereza;		
	(e) atashindwa kutoa tamko rasmi kuhusu sifa za kuwa Mbunge au taarifa rasmi kuhusu mali kwa mujibu wa masharti ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Katiba hii katika muda uliowekwa mahsusi na sheria za nchi;		
	(f) atajiuzulu ubunge;		
	(g) kwa ridhaa yake atajiondoa au kujivua uanachama wa chama chake cha siasa, atafukuzwa au kuvuliwa uanachama na chama chake cha siasa;		
	(h) ataondolewa madarakani kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii;		
	(i) kufariki dunia.		
	(2) Mbunge anaweza kukata rufani		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mahakamani kupinga hukumu ya kuthibitishwa kwake kuwa ana maradhi au kupinga adhabu ya kufungwa gerezani, au kupinga kupatikana kwake na hatia kwa kosa la aina iliyotajwa katika ibara ndogo ya (1).		
Ibara ya 129: Haki ya wapiga kura kumwajibisha Mbunge.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, wananchi watakuwa na haki ya kumuondoa Mbunge wao madarakani, endapo Mbunge atafanya moja wapo au zaidi ya mambo yafuatayo: (a) kuunga mkono sera ambazo zinaenda kinyume na maslahi ya wapiga kura au kinyume na maslahi ya Taifa; (b) kushindwa kuwasilisha au	Madhumuni ya mapendekezo ni kuwapa wapiga kura haki ya kumuondoa madarakani Mbunge wao kabla ya muda wake kwisha na kuweka vigezo na sababu ya wananchi kumuondoa Mbunge husika.	Sababu ya ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliodai haki yao ya kumuondoa Mbunge wao kabla ya kumaliza muda wake ikiwa hatekelezi wajibu wake ipasavyo. Wananchi walio wengi walilalamika kwamba Wabunge wengi baada ya kuchaguliwa hawakai katika majimbo yao hadi msimu mwingine wa uchaguzi. Uzoefu wa nchi nyingine zinazosimamia demokrasia shirikishi

Trial version www.iuanee.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutetea kwa dhati hoja zinazotokana na kero za wapiga kura wake; (c) kuacha kuishi au kuhamisha makaazi yake kutoka eneo la Jimbo la Uchaguzi kwa zaidi ya miezi sita bila sababu za msingi; au		zikiwemo Uganda, Kenya na Brazili zimetambua haki ya wapiga kura kuwaondoa Wabunge wao. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuwalazimisha Wabunge kutekeleza ahadi wanazozitoa wakati wa kampeni na hivyo kuwafanya Wabunge waingie mkataba na wapiga kura wao.
	(d) mambo mengine yatakayoainishwa kwenye sheria ya nchi.		
	(2) Bunge litatunga sheria kuweka masharti ya kuendesha uchunguzi kwa Mbunge atakayeshindwa kutekeleza majukumu yake kwa wapiga kura wake na utaratibu wa kumuondoa katika Ubunge.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 130: Uamuzi wa Suala kama Mtu ni Mbunge.	(1) Kila shauri kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala - (a) kama uchaguzi wa Mbunge ulikuwa halali au sivyo; au (b) kama Mbunge amekoma kuwa Mbunge na nafasi ya madaraka ya Ubunge iko wazi au hapana, litafunguliwa na kusikilizwa kwanza katika Mahakama Kuu. (2) Bunge linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti kuhusu mambo yafuatayo: (a) watu wanaoweza kufungua shauri katika Mahakama Kuu kwa ajili ya kupata uamuzi juu ya suala lolote	Madhumuni ya mapendekezo haya ni kutoa mamlaka kwa Mahakama Kuu ambacho ni chombo cha mhimili mwingine kuamua uhalali wa Ubunge. Lengo jingine ni kuwawezesha wananchi kwenda mahakamani kuhoji uhalali wa Mbunge wao.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 juu ya haki ya kufungua shauri Mahakama Kuu kuhoji matokeo ya Ubunge. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kuhalalisha au kubatilisha uchaguzi wa Mbunge pale ambapo imethibitika ulifanyika kinyume na utaratibu wa kisheria. Miongoni mwa haki ambazo wananchi wamezitumia kikamilifu ni ya kuhoji uhalali wa chaguzi wa Wabunge wao mahakamani. Hivyo mapendekezo haya ni kutekeleza maamuzi ya Mahakama Kuu juu ya haki ya wananchi kuhoji matokeo ya uchaguzi wa Mbunge.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii;		
	(b) sababu na nyakati za kufungua shauri la namna hiyo, utaratibu wa kufungua shauri na masharti yanayotakiwa yatimizwe kwa kila shauri kama hilo; na		
	(c) kutaja mamlaka ya Mahakama Kuu juu ya shauri kama hilo na kueleza utaratibu wa kusikiliza shauri lenyewe.		
Ibara ya 131: Tamko Rasmi la Wabunge kuhusu Maadili ya	(1) Kila Mbunge kabla ya kumalizika siku thelathini tangu aapishwe kushika nafasi ya madaraka ya Mbunge sharti awasilishe kwa	Kubainisha uadilifu wa Mbunge na jinsi anavyozingatia maadili.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 wa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Uongozi.	Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji nakala mbili za tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa za kuwa mbunge kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. (2) Tamko rasmi lililotajwa katika ibara ndogo ya (1), litatolewa katika fomu maalum itakayoandaliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		kuwataka Wabunge kutoa Tamko kuhusu maadili ya uongozi. Ibara hii inamtaka kiongozi awasilishe yeye mwenyewe Tamko kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji tofauti na ilivyo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania ya mwaka 1977 ambapo Mbunge anawasilisha Tamko hilo kwa Spika. Kwa ujumla sababu za mapendekezo haya ni kulinda maadili ya uongozi.
SEHEMU YA TATU - UONGOZI WA BUNGE			
(a) ***Spika na Naibu Spika***			
Ibara ya 132: Spika na Mamlaka ya Spika.	(1) Kutakuwa na Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na Wabunge na atakuwa ndiye Kiongozi wa Bunge na	Madhumuni ni kuhakikisha kuwa Spika anatenda na anaonekana kutenda haki na kutoa fursa sawia kwa Wabunge wote.	Sababu za mapendekezo ni kuzingatia maoni ya wananchi kuwa Spika anapotoka kwenye chama inajitokeza kama sehemu ya chama chake na

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	atawakilisha Bunge katika vyombo na vikao vingine vyote nje ya Bunge. (2) Waziri, Naibu Waziri, Mbunge au mtu mwenye madaraka ya aina nyingine yoyote yatakayotajwa na sheria za nchi kwa madhumuni ya Ibara hii, hataweza kuchaguliwa kuwa Spika. (3) Mtu yeyote atakayechaguliwa kuwa Spika atatakiwa, kabla ya kumaliza siku thelathini tangu kuchaguliwa kwake, kuwasilisha kwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji tamko rasmi kwamba hajapoteza sifa za uchaguzi kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, tamko hilo litatolewa katika fomu maalum	Kumfanya Spika kuwa huru na kumuondoshea Spika shinikizo la kichama katika kusimamia shughuli za Bunge ambacho ni chombo cha uwakilishi wa wananchi wote. Aidha, ni kuweka msingi wa Spika kuzingatia maadili.	kuwanyima Wabunge wanaotoka nje ya chama chake fursa mbalimbali. Aidha, hutumika kuwadhibiti Wabunge wa chama chake mwenyewe hasa kwa wale ambao wanaonekana wanakengeuka mwelekeo wa chama.

Final Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	itakayoandaliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
Ibara ya 133: Ukomo wa Spika.	(1) Spika atakoma kushika nafasi ya madaraka ya Spika litokeapo lolote kati ya mambo yafuatayo: (a) atachaguliwa kuwa Mbunge; (b) kutatokea jambo lolote ambalo, kama asingekuwa Spika, lingemfanya mtu huyo asiwe na sifa za uchaguzi au apoteze sifa za uchaguzi wa Spika; (c) ataondolewa kwenye madaraka ya Spika kwa Azimio la Bunge lililoungwa mkono na Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka ukomo wa Spika kwa mujibu wa masharti ya Katiba. Kuweka msingi wa kumuwajibisha Spika.	Sababu ya mapendekezo ni kujenga uwajibikaji Kwa kuwa Spika kwa kumuwekea masharti ya kikatiba yatakayomfanya aondolewe katika nafasi yake anapokosa sifa za msingi za kuwa Spika au kufanya vitendo vinavyokiuka maadili na uadilifu.

Trial version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Wabunge wote; (d) atashindwa kuwasilisha tamko rasmi kuhusiana na mali na madeni yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii; (e) atapatikana na hatia kwa kosa la kutoa habari za uongo, kwa kiapo kinyume cha sheria kuhusu tamko rasmi lolote lililotolewa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii; (f) atashindwa kuwasilisha taarifa ya mali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kabla ya kumalizika muda uliowekwa kwa ajili hiyo;		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(g) itathibitika kuwa amevunja masharti ya sheria inayohusu maadili ya uongozi wa umma; au (h) kufariki dunia.		
	(2) Isipokuwa shughuli ya kumchagua Spika, hakuna shughuli yoyote itakayotekelezwa katika Bunge wakati wowote ambao nafasi ya madaraka ya Spika itakuwa wazi.		
Ibara ya 134: Naibu Spika.	(1) Kutakuwa na Naibu Spika wa Bunge ambaye atachaguliwa na Wabunge.	Lengo la Ibara hii ni kuhakikisha kuwa Naibu Spika anatenda na anaonekana kutenda haki na kutoa fursa sawa kwa Wabunge wote. Lengo jingine ni kumfanya	Sababu za mapendekezo hayo ni kuwa Naibu Spika ndiye Msaidizi Mkuu wa Spika na ana dhamana inayofanana na Spika katika uongozi wa Bunge.
	(2) Waziri, Naibu Waziri, Mbunge au mtu mwenye madaraka ya aina		

Trial Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nyingine yoyote yatakayotajwa na sheria za nchi kwa madhumuni ya Ibara hii, hataweza kuchaguliwa kuwa Naibu Spika.	Naibu Spika kuwa huru na kumuondoshea shinikizo la kichama katika kusimamia shughuli za Bunge. Aidha, kuweka msingi wa Naibu Spika kuzingatia maadili.	
	(3) Wabunge watamchagua Naibu Spika nyakati zifuatazo:		
	(a) Bunge litakapokutana kwa mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu au mapema iwezekanavyo baada ya wakati huo; na		
	(b) katika kikao cha kwanza cha Bunge baada ya nafasi ya madaraka ya Naibu Spika, kuwa wazi kwa sababu yoyote isiyohusika na Bunge kuvunjwa au mapema iwezekanavyo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	baada ya kikao hicho.		
	(4) Naibu Spika atakoma kushika nafasi ya madaraka ya Naibu Spika litokeapo lolote kati ya mambo yaliyoainishwa katika Ibara ya 133(1).		
Ibara ya 135: Sifa za Mtu kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika.	(1) Mtu atastahili kuchaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika endapo atakuwa na sifa zifuatazo - (a) angalau awe na elimu ya shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi; (b) wakati wa kugombea, awe mwenye umri usiopungua miaka arobaini;	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka sifa muafaka za mtu kuwa Spika au Naibu Spika wa Bunge. Pia, ni pamoja na kutenganisha ya maslahi ya kichama na uongozi wa shughuli za Bunge.	Ababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka Spika na Naibu Spika wasitokane na uongozi wa kitaifa wa chama chochote cha siasa kuepusha uwezekano wa mgongano wa kimaslahi au kupendelea chama chake. Pia kujenga imani katika uongozi wa Bunge na kuweka taswira nzuri ndani na nje ya Bunge.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) bila ya kuathiri masharti ya aya ya (a) na (b), awe na sifa za kumuwezesha kuchaguliwa kuwa Mbunge; na (d) asiwe kiongozi au amewahi kuwa kiongozi wa juu wa chama cha siasa katika kipindi cha miaka mitano kabla ya tarehe ya kuomba kuchaguliwa kushika nafasi ya madaraka ya Spika au Naibu Spika.		
	(2) Kwa madhumuni ya aya ya (d), kiongozi wa juu wa chama cha siasa ni Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu au Mjumbe wa		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	chombo chochote cha kitaifa chenye mamlaka katika chama cha siasa.		
Ibara ya 136: Utaratibu wa Uchaguzi na Kiapo cha Spika na Naibu Spika.	(1) Kutakuwa na uchaguzi wa Spika katika kikao cha kwanza cha Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya, na katika kikao cha kwanza chochote mara baada ya kutokea nafasi ya madaraka ya Spika kuwa wazi. (2) Kutakuwa na uchaguzi wa Naibu Spika wakati wowote katika Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya na vile vile katika kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofuata mara baada ya kutokea nafasi ya madaraka ya Naibu Spika kuwa wazi.	Lengo la Ibara hii ni kuainisha utaratibu wa kumpata Spika na Naibu Spika. Pia, Ibara inaainisha masharti ya kiapo cha Spika na Naibu Spika.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Spika na Naibu Spika wanatii Katiba katika kutimiza wajibu wao na kujenga mazingira ya uaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Sababu ya kuweka nafasi ya Spika na Naibu Spika kutoka pande mbili tofauti za Muungano ni kuupa uongozi wa Bunge kuwa na sura ya Muungano.
	(3) Uchaguzi wa Spika na Naibu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Spika, utafanywa kwa kura ya siri, na utaendeshwa kwa kufuata utaratibu uliowekwa na Kanuni za Bunge.		
	(4) Spika na Naibu Spika watachaguliwa kwa misingi kwamba, endapo Spika atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, Naibu Spika atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		
	(5) Isipokuwa kama ataacha madaraka yake, Spika na Naibu Spika watakaa madarakani kwa vipindi visivyozidi viwili vya miaka mitano.		
	(6) Mtu yeyote atakayechaguliwa kuwa Spika au Naibu Spika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	atatakiwa, kabla ya kuanza kutekeleza madaraka yake, kuapishwa katika Bunge kiapo cha uaminifu.		
	(a) Ofisi ya Bunge		
Ibara ya 137: Katibu wa Bunge.	(1) Kutakuwa na Katibu wa Bunge ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina matatu ya watu wenye madaraka ya juu katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Spika na Naibu Spika wanatii Katiba katika kutimiza wajibu wao na kujenga mazingira ya uaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao. Sababu ya kuweka nafasi ya Spika na Naibu Spika kutoka pande mbili tofauti za Muungano ni kuupa uongozi wa Bunge kuwa na sura ya Muungano.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu utakaohakikisha kuwa nafasi ya Katibu wa Bunge inajazwa kwa kuzingatia sifa, weledi, uaminifu na uzoefu ndani ya Utumishi wa Umma.
	(2) Katibu wa Bunge atakuwa ndiye Mtendaji Mkuu wa Ofisi ya Bunge na atawajibika kwa utendaji bora wa shughuli za Bunge kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii		

Final Version www.ilac.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na sheria za nchi.		
Ibara ya 138: Sekretarieti ya Bunge.	(1) Kutakuwa na Sekretarieti ya Bunge itakayokuwa na watumishi kutoka pande zote za Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia ngazi za utumishi kwa mujibu wa mahitaji ya shughuli za Bunge kama itakavyoamuliwa na Tume ya Utumishi ya Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Sekretarieti ya Bunge. Aidha, ni kuweka kikatiba majukumu ya Sekretariati ya Bunge ili kuunda Sekretariati imara yenye kuendeshwa kwa misingi ya weledi na ufanisi.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka chombo cha utendaji kinachosaidia Bunge kutekeleza wajibu na shughuli zake kwa ukamilifu na ufanisi. Sababu nyingine ni kuweka bayana sura ya Muungano.
	(2) Sekretarieti ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, itatekeleza kazi na shughuli zote zilizowekwa au zitakazokuwa ni muhimu kwa ajili ya kuhakikisha utekelezaji bora wa shughuli za Bunge, Wabunge na madaraka ya Bunge.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SEHEMU YA NNE - UTARATIBU WA SHUGHULI ZA BUNGE			
Ibara ya 139: Kanuni za Kudumu za Bunge.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, Bunge linaweza kutunga Kanuni za Kudumu kwa ajili ya kuweka utaratibu wa kutekeleza shughuli zake. (2) Kanuni za Kudumu zilizotungwa kwa mujibu wa Ibara hii, zinaweza kuweka utaratibu wa Mawaziri kuiwakilisha Serikali ndani ya Bunge, kusimamia utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti ya Bunge, utekelezaji wa Shughuli za Bunge ndani ya Bunge, Kamati na Kamati Ndogo za Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kutunga Kanuni za Kudumu za Bunge kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bunge. Pia, kudhihirisha uhuru wa chombo hicho kutunga kanuni zao wenyewe katika kuimarisha uwezo na uwajibikiaji kwa kujiwekea utaratibu wake wa kuendesha shughuli zake. Lengo jingine ni kuweka uhakika na ulingano katika uendeshaji wa vikao vya Bunge na maamuzi yake.	Sababu za mapendekezo ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Mabunge yote duniani wa kuwepo kanuni za uendeshaji wa Bunge kwa kujitungia wenyewe kanuni zao.
Ibara ya 140: Rais	(1) Rais atalihutubia Bunge Jipya	Madhumuni ya ibara hii ni	Sababu za mapendekezo haya ni

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kulihutubia Bunge.	katika Mkutano wa Kwanza na kulifungua rasmi. (2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Rais anaweza wakati wowote kulihutubia Bunge au kupeleka kwenye Bunge taarifa ambayo itasomwa na Waziri Mwandamizi.	kumpa Rais wajibu wa kulihutubia na kulizindua rasmi Bunge.	kuendeleza utaratibu wa kibunge duniani kote kwa Mkuu wa Nchi kulihutubia na kulifungua Bunge katika kikao chake cha kwanza. Ni utaratibu wa Mabunge mengi duniani kwa Rais kulihutubia Bunge mara moja kwa mwaka ili kueleza sera, mipango, utekelezaji, mikakati na mwelekeo wa nchi. Utaratibu huu unajenga na kuimarisha mahusiano kati ya mihimili ya Serikali na Bunge katika kufikia malengo makuu ya taifa
Ibara ya 141: Mikutano ya Bunge.	(1) Bunge litafanya mikutano yake mahali ambapo ni desturi kufanya Mikutano hiyo au mahali pengine popote katika Jamhuri ya Muungano patakapotajwa na Spika kwa ajili hiyo. (2) Mkutano wa Kwanza wa Bunge Jipya katika Maisha ya Bunge	Madhumuni ya ibara hii ni kuweka utaratibu wa kuitishwa kwa mikutano ya Bunge na mahali pa kufanyiwa mikutano ya Bunge. Aidha, kumpa Rais mamlaka ya kikatiba ya kuitisha mikutano ya Bunge.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu na desturi ya Mabunge duniani kufanya mikutano ya Bunge na kumpa Mkuu wa Nchi nafasi ya kuliitisha Bunge inapohitajika kufanya hivyo. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa kikatiba

Trial Version
www.iLovePDF.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utaitishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano na utaanza siku ile ambayo Bunge limeagizwa kukutana, na kila Mkutano unaofuata utaanza siku yoyote itakayopangwa na Bunge au siku yoyote itakayopangwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge.		unaowezesha kikao cha Bunge kufanyika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano
	(3) Rais anaweza kuitisha Mkutano wa Bunge wakati wowote kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
Ibara ya 142: Uongozi na Vikao vya Bunge.	Kila kikao cha Bunge kitaongozwa na mmoja wapo wa watu wafuatao:	Madhumuni ni kuweka masharti ya uongozi, uendeshaji na usimamizi wa vikao vya Bunge Kikatiba.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu kwamba vikao vya Bunge vinaendeshwa kwa mujibu wa utaratibu wa kikatiba ili kuvifanya vikao hivyo kuwa halali. Vile vile ni kuweka uhakika wa kuwepo kwa viongozi na vikao vya Bunge wakati wowote.
	(a) Spika;		
	(b) ikiwa Spika hayupo, Naibu Spika; au		
	(c) ikiwa Spika na Naibu Spika wote hawapo, Mbunge yeyote aliyechaguliwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Bunge kwa ajili hiyo.		
Ibara ya 143: Akidi ya Vikao vya Bunge.	(1) Akidi ya kila kikao cha Bunge ni nusu ya Wabunge wote, isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo katika Katiba hii. (2) Kila suala litakalowasilishwa kwa ajili ya kupata uamuzi wa Bunge litaamuliwa kwa kufuata wingi wa kura za Wabunge waliohudhuria na kupiga kura, isipokuwa kwa masuala yaliyowekewa masharti mahsusi chini ya Katiba hii.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba akidi ya kila kikao cha Bunge ambacho ndicho kigezo cha maamuzi halali ya Bunge.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka akidi ya vikao vya Bunge ili kujenga imani ya kuwa maamuzi yanafikiwa kwa idadi ya kutosha ya Wabunge inayowakilisha mtazamo mpana wa wananchi wanaowawakilisha. Sababu nyingine ni kujenga uhalali wa vikao na kuhakikisha kwamba maamuzi ya vikao vya Bunge yanafikiwa kwa njia ya demokrasia. Sababu nyingine kuzuia kuwepo hali ya utoro na kuhakikisha kuwa Wabunge wanahudhuria vikao na wanatelekeza shughuli za Bunge ipasavyo.
Ibara ya 144: Kamati za Bunge.	(1) Bunge linaweza kuunda Kamati za Bunge za aina mbalimbali kadri litakavyoona inafaa kwa ajili ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kulipa Bunge mamlaka ya kuunda kamati zake kwa ajili ya	Sababu ya mapendekezo haya ni kuboresha na kupanua mijadala na maamuzi ya Bunge na kuhuisha

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utekelezaji bora wa madaraka yake. (2) Kanuni za Bunge zinaweza kufafanua muundo na shughuli za Kamati za Bunge zitakazoundwa kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii.	utekelezaji bora wa shughuli zake. Lengo jingine ni kuongeza ufanisi kwa kuhakikisha kuwa maeneo muhimu yote yanaundiwa Kamati ili kuweza kufuatiliwa kikamilifu.	utaratibu wa kibunge wa kuwa na Kamati za Bunge. Sababu nyingine ni kutimiza wajibu wa Bunge wa kuisimamia Serikali, na pale inapohitajika kuwaita na kuwahoji Mawaziri na watendaji wa Serikali kutoa ufafanuzi wa masuala yanayotakiwa na Kamati ya Bunge.
SEHEMU YA TANO - MADARAKA NA HAKI ZA BUNGE			
Ibara ya 145: Uhuru wa Majadiliano bungeni.	(1) Wabunge wakiwa Bungeni, watakuwa na uhuru wa kutoa mawazo, maoni na majadiliano na uhuru huo hautavunjwa wala kuhojiwa na chombo chochote katika Jamhuri ya Muungano, au katika Mahakama au mahali pengine nje ya Bunge. (2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu uhuru wa majadiliano Bungeni. Aidha, kuwapa kinga Wabunge na kuondoa hofu, kupanua wigo wa ukweli na uwazi katika mijadala ya Bunge.	Sababu za mapendekezo haya ni kutoa nafasi kwa Wabunge kujadili kwa uhuru, umakini, uwazi na haki hoja zote zinazowasilishwa Bungeni kwa maslahi ya Taifa. Sababu nyingine kupewa kinga Wabunge ili wasiwe na woga katika kuikosoa Serikali na kufichua maovu. Aidha, kupewa kinga na fursa kwa Wabunge ni katika nguzo

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hii au sheria nyingine yoyote, Bunge litakuwa na uhuru wa maoni na Mbunge yeyote akiwa Bungeni kwa vyovyote itakavyokuwa, hatatakiwa kutoa kauli za uongo, kuudhi au kumuumiza Mbunge au mtu mwingine yeyote katika jamii.		muhimu ya kuimarisha uhuru wa Wabunge katika majadiliano na maamuzi yao.
	(3) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2), Mbunge yeyote hatashtakiwa kwa kosa la jinai au kufunguliwa shauri la madai mahakamani kutokana na jambo lolote alilolisema ndani ya Bunge.		
	(4) Bunge linaweza kutunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuwezesha mahakama na sheria kuhifadhi na kutilia nguvu uhuru wa mawazo, majadiliano na utaratibu wa shughuli katika Bunge.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 146: Mipaka ya Majadiliano bungeni.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, ni marufuku kusema uongo Bungeni na kwa sababu hiyo, Mbunge anapozungumza ndani ya Bunge ana wajibu wa kuhakikisha kwamba anatoa kauli au maelezo kuhusu jambo au suala ambalo yeye mwenyewe anaamini kuwa ni la kweli na siyo jambo la kubuni au la kubahatisha.	Lengo la Ibara hii kuweka mipaka ya kikatiba juu ya uhuru wa Wabunge katika majadiliano Bungeni na kuimarisha tabia na utamaduni kwa Wabunge kuwa wakweli na makini katika kauli zao Bungeni.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka mipaka kwa uhuru wa Wabunge wanapotoa maoni na hoja zao Bungeni pamoja na kwamba wana kinga na fursa ya kutoshtakiwa. Sababu nyingine ni kuwa chombo hiki kina watu ambao wanapima na kutafakari wanayoyasema yawe ya kweli na wanayoyatenda yazingatie haki kwa watu wengine ambao hawana nafasi ya kujibu hoja hizo Bungeni.
	(2) Mbunge anapokuwa akizungumza Bungeni hatahesabika wala kutafsiriwa kuwa anasema uongo iwapo anafanya rejea ya habari kuhusu jambo lililotangazwa au lililoandikwa na vyombo vya habari au nyaraka nyingine yoyote ambayo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	chanzo chake kinafahamika au kitaelezwa na Mbunge huyo.		
SEHEMU YA SITA - TUME YA UTUMISHI WA BUNGE			
(a) Tume ya Utumishi wa Bunge			
Ibara ya 147: Tume ya Utumishi wa Umma.	(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Bunge ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao: (a) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Mwenyekiti; (b) Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti; (c) Wabunge wawili wa	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Tume ya Utumishi wa Bunge kikatiba.	Sababu ya mapendekezo ni kuwa na Tume inayosimamia uongozi wa Bunge kwa jumla katika mambo ya utumishi, ajira na nidhamu miongoni mwa watumishi wa Bunge.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Bunge la Jamhuri ya Muungano, mmoja kutoka kila upande wa Jamhuri ya Muungano;		
	(d) Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni; na		
	(e) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.		
	(2) Katibu wa Bunge atakuwa Katibu wa Tume ya Utumishi wa Bunge.		
	(3) Tume inaweza kumualika mtu mwingine yeyote mwenye utaalam mahsusi kushiriki kikao chochote cha Tume, isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.		
Ibara ya 148: Majukumu	(1) Tume ya Utumishi wa Bunge	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha	Sababu za mapendekezo haya ni

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
ya Tume ya Utumishi wa Umma.	itakuwa na wajibu wa kuendeleza, kuwezesha na kuhakikisha utekelezaji wa kazi na shughuli za Bunge, kwa ufanisi na uwazi. (2) Tume ya Utumishi wa Bunge itatekeleza majukumu yafuatayo: (a) kuajiri, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo na kusimamia nidhamu za watumishi wa Bunge na kupokea malalamiko dhidi yao kwa mujibu wa sheria za nchi; (b) kuandaa na kutekeleza mipango ya kujiendeleza kielimu kwa Watumishi wa Bunge; (c) kuandaa na	Tume ya Utumishi wa Bunge na kuainisha majukumu yake.	kutoa nafasi ya kusimamia mambo ya nidhamu miongoni mwa watumishi wa Bunge. Sababu nyingine ni kuyatambua kikatiba majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge pamoja na kusimamia majukumu hayo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika taasisi ya Bunge.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kupendekeza viwango vya mishahara, posho na marupurupu mengine kwa Wabunge na Watumishi wa Bunge kwa chombo chenye jukumu la kusimamia maslahi ya Watumishi wa Umma;		
	(d) kupendekeza Serikalini maboresho ya Taasisi ya Bunge ili kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kikatiba ya Bunge;		
	(e) kutekeleza majukumu yoyote yatakayowekwa kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyingine.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Tume ya Utumishi wa Bunge.		
(b) Mfuko wa Bunge			
Ibara ya 149: Mfuko wa Bunge.	(1) Kutakuwa na Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Mfuko wa Bunge ili kulipa Bunge uhakika na uhuru wa kifedha.	Sababu za mapendekezo ni kuwa na mfuko mahsusi kwa ajili ya muhimili wa Bunge ili kunaimarisha dhana ya mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili ya Bunge na Serikali. Aidha ni kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Bunge kwa kuondoa urasimu uhusiana masuala ya fedha. Kwa sasa upo Mfuko wa Bunge ambao umeanzishwa kwa sheria ya kawaida ya Bunge.
	(2) Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano utatumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za uendeshaji, pamoja na shughuli nyingine muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Bunge la Jamhuri ya Muungano.		

Final Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Serikali itahakikisha kwamba, katika kila bajeti ya mwaka wa fedha wa Serikali, inatenga kwa kiwango kinachotosha, fedha ambazo zitaingizwa katika Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.		
	(4) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.		
SURA YA KUMI **MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO**			
SEHEMU YA KWANZA - MISINGI YA UTOAJI HAKI NA UHURU WA MAHAKAMA			
Ibara ya 150: Kuanzishwa kwa Mahakama ya Jamhuri ya	(1) Kutakuwa na Mahakama ya Jamhuri ya Muungano.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na mfumo wake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Katiba za nchi nyingi duniani kuanzisha na
	(2) Mahakama ya Jamhuri ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Muungano.	Muungano kupitia Katiba hii, itakuwa na mamlaka kutoka kwa wananchi na itatekeleza mamlaka yake kupitia Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani. (3) Mahakama ya Jamhuri ya Muungano itakuwa ni chombo chenye mamlaka ya mwisho ya utoaji haki katika Jamhuri ya Muungano.		kutambua Mahakama kuwa ni moja ya mihimili ya dola yoyote. Kwa mara ya kwanza Rasimu hii inatamka bayana kuwa Mahakama inapata mamlaka na uhalali wake kutoka kwa wananchi
Ibara ya 151: Misingi ya Utoaji Haki.	Katika kutoa uamuzi wa mashauri ya madai na jinai kwa kuzingatia sheria, Mahakama ya Jamhuri ya Muungano itafuata kanuni zifuatazo, yaani: (a) kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii, kisiasa, kiutamaduni au	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya utoaji haki kikatiba.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya Wananchi wengi waliolalamika kuwa kwa sasa misingi ya utoaji haki haifuatwi na Mahakama, na kwamba uendeshaji na utoaji haki katika Mahakama umetawaliwa na tuhuma za rushwa, upendeleo na kupokea maelekezo kutoka kwa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kiuchumi; (b) kutocheleweshe haki bila sababu ya kimsingi; (c) kutoa fidia ipasayo kwa watu wanaoathirika kutokana na makosa ya watu wengine, na kwa mujibu wa sheria za nchi zilizotungwa mahususi kwa ajili hiyo; (d) kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro; na (e) kutenda haki bila kufungwa na masharti ya kiufundi.		baaadhi ya viongozi wa ngazi za juu au wanasiasa. Aidha, uwepo kwenye Katiba misingi ya utoaji haki kutaboresha utendaji kazi wa Mahakama. Pia wananchi walililalamikia juu ya Mahakama ya Rufani kutumia masharti ya kiufundi kufuta mashauri badala ya kutumia misingi ya utoaji haki inayozingatia maslahi ya wananchi na taifa. Aidha, kujenga taswira mpya ya Mahakama kama chombo cha kutoa haki na kuonekana kutenda haki.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 152: Uhuru wa Mahakama.	(1) Katika kutekeleza mamlaka ya utoaji haki, Mahakama ya Jamhuri ya Muungano itaongozwa na masharti ya Katiba hii na haitaingiliwa ama kwa kudhibitiwa, kushinikizwa au kupewa maelekezo na mtu au chombo chochote.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba uhuru wa Mahakama wa kutoingiliwa katika utekelezaji wa majukumu yake, kulinda haki, ajira na uhuru wa Majaji	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza uhuru wa Mahakama kama ni mmoja wa misingi mikuu ya demokrasia na utawala wa sheria. Aidha kuwapa Majaji uhuru ili kuwawezesha kutoa maamuzi yao bila ya woga wala upendeleo kwa kuzingatia misingi ya haki iliyoainishwa katika Katiba na sheria nyingine za nchi.
	(2) Nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu au Mahakama ya Rufani haitafutwa wakati wowote ule ikiwa kuna mtu ambaye kwa wakati huo anashikilia nafasi hiyo.		
	(3) Mishahara na malipo mengine ya Majaji wa Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani yatalipwa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina.		
	(4) Mshahara na malipo mengine yanayolipwa kwa Jaji wa Mahakama		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Juu au wa Mahakama ya Rufani hayatabadilishwa kwa maana ya kumuondolea faida Jaji husika.		
	(5) Malipo ya mafao ya kustaafu ya Jaji wa Mahakama ya Juu au Jaji wa Mahakama ya Rufani hayatabadilishwa kwa maana ya kumuondolea faida Jaji husika wakati wote wa uhai wake.		
	(6) Jaji wa Mahakama ya Juu au Jaji wa Mahakama ya Rufani hatoshtakiwa kwa jambo lolote alilolifanya au kutolifanya kwa nia njema katika utekelezaji wa shughuli ya utoaji haki kwa mujibu wa sheria za nchi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SEHEMU YA PILI - MUUNDO WA MAHAKAMA			
(a) Mahakama za Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 153: Muundo wa Mahakama.	(1) Bila ya kuathiri masharti yoyote yaliyotangulia katika Sehemu hii, kutakuwa na Muundo wa Mahakama katika Jamhuri ya Muungano utakaokuwa kama ifuatavyo: (a) Mahakama ya Juu; na (b) Mahakama ya Rufani. (2) Mahakama Kuu ya Tanganyika na Mahakama Kuu ya Zanzibar zitakuwa na mamlaka sawa ya kusikiliza katika ngazi ya awali, mashauri ya madai na jinai kuhusu Mambo ya Muungano katika maeneo ya utawala ya Nchi	Lengo la Ibara hii ni kuweka muundo mpya wa Mahakama katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania..	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi mbalimbali waliopendekeza mabadiliko ya muundo wa Mahakama kwa kuongeza Mahakama nyingine ya juu. Aidha, wananchi pia walisisitiza kuwa Mahakama Kuu ya Zanzibar na Mahakama Kuu ya Tanganyika kuendelea kuwa na mamlaka ya usikilizaji wa awali wa masuala ya madai na jinai kwenye maeneo yao. Sababu nyingine ni kuimarisha mfumo wa utoaji haki utakaoendana na muundo wa Muungano na Serikali

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika.		zake.
	(b) Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano		
Ibara ya 154: Mahakama ya Juu.	(1) Kutakuwa na Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano au kwa kifupi itaitwa "Mahakama ya Juu" ambayo itakuwa na: (a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Rais wa Mahakama ya Juu; (b) Naibu Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Makamu wa Rais wa Mahakama ya Juu; na	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano na kuweka vigezo vya uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.	Moja ya sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuzingatia maoni ya Wananchi ya kuwepo ngazi nyingine ya juu ya Mahakama ambayo itakuwa na mamlaka ya kusikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama ya Rufani. Kwa kuwa Rasimu hii imeruhusu matokeo ya uchaguzi wa Urais kuhojiwa ilionekana kuwa chombo kinachofaa kufanya kazi hiyo ni Mahakama ya Juu kama ilivyo kwa Kenya na Uganda. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu ambapo mashauri ya kikatiba baina ya

Final Version www.inuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) Majaji wengine wa Mahakama ya Juu wasiopungua saba.		Serikali ya Muungano na Nchi Washirika au baina ya Washirika wenyewe kusikilizwa na Mahakama hiyo ya juu,
	(2) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu utazingatia sifa zitakazoainishwa katika Katiba hii na uwakilishi wa sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 155: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Juu.	(1) Akidi ya kikao cha Mahakama ya Juu itakuwa ni Majaji wa Mahakama ya Juu watano. (2) Akidi ya Majaji katika vikao vya Mahakama ya Juu kwa madhumuni ya kusikiliza shauri linalohusu masuala yaliyoainishwa katika Ibara ya 156(1) (a), (b), (c) na (e) itazingatia uwakilishi wa sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano.	Lengo la kuweka kikatiba akidi ya Majaji inayotakiwa kwenye vikao vya Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kusikiliza kesi na kutoa maamuzi.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kawaida katika uendeshaji wa Mahakama ya Juu na akidi ya Majaji wanaosikiliza shauri kwa pamoja. Msingi wake ni kuongeza uhalali na uhakika wa kutoa haki katika kusikiliza na kuamua rufaa kwa kuwashirikisha Majaji wengi kwa sababu hatua hiyo ni ya mwisho kwa raia

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Kila shauri na rufani inayohitaji uamuzi wa Mahakama ya Juu itaamuliwa kwa kufuata kauli ya walio wengi kati ya Majaji wa Mahakama ya Juu waliosikiliza shauri au rufani hiyo.		
Ibara ya 156: Mamlaka ya Mahakama ya Juu.	(1) Mahakama ya Juu itakuwa ni ngazi ya mwisho ya rufani katika Jamhuri ya Muungano na itakuwa na madaraka ya: (a) pekee na ya awali ya kusikiliza na kuamua mashauri yanayohusu matokeo ya uchaguzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano; (b) kusikiliza na kuamua mashauri yatakayowasilishwa na	Lengo la Ibara hii ni kuainisha mamlaka na madaraka ya Mahakama ya Juu ya Jamhuri ya Muungano ambayo ndiyo yenye maamuzi ya mwisho.	Sababu ya Ibara hii ni kuzingatia na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa chombo cha juu zaidi cha kutoa haki. Kutokana na mapendekezo ya Rasimu ya Katiba kuwa matokeo ya Rais yahojiwe Mahakamani ilionekana ni vyema kufuata uzoefu wa nchi nyengine kama Kenya na Uganda ambapo mashauri kama hayo husikilizwa na Mahakama ya Juu pekee. Kwa kuwa Rasimu inakusudia mizozo

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wananchi, Serikali au Serikali za Nchi Washirika kuhusu tafsiri au utekelezaji wa Katiba hii;		ya Muungnao itatuliwe kwa njia za kimahakama kuliko kisiasa kama ilivyo sasa, ndipo Rasimu ikapendekeza Mahakama ya Juu kuwa na mamlaka ya kusikiliza mashauri ya tofauti za kikatiba katika kutekeleza mambo ya Muungano baina ya Washirika wenyewe au Washirika na Muungano na Jamhuri ya Muungano.
	(c) kusikiliza na kuamua migogoro baina ya Nchi Washirika au baina ya Nchi Mshirika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano;		
	(d) kusikiliza na kuamua rufani kutoka Mahakama ya Rufani;		
	(e) kutoa ushauri kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi Washirika, pale itakapoombwa; na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(f) kusikiliza na kuamua shauri lolote litakalowasilishwa mbele yake kwa mujibu wa Katiba hii au sheria nyingine yoyote itakayoipa Mahakama hiyo mamlaka.		
	(2) Mahakama ya Rufani pamoja na mahakama za Nchi Washirika, isipokuwa Mahakama ya Juu, zitalazimika kufuata maamuzi ya Mahakama ya Juu.		
	(3) Mahakama ya Juu itaandaa Kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka yake.		
	(4) Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti zaidi kuhusu uendeshaji wa Mahakama ya Juu.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 157: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Juu.	(1) Jaji wa Mahakama ya Juu atakuwa na madaraka ya kusikiliza na kuamua shauri lolote katika Mahakama ya Juu. (2) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), iwapo Jaji wa Mahakama ya Juu, kabla ya kuteuliwa kwake alikuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu ya Nchi Washirika, Jaji huyo anaweza kuendelea kufanya kazi zake katika Mahakama aliyotoka hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu. (3) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (2), itakuwa ni halali kwa Jaji wa Mahakama ya Juu kutoa	Ni kuweka kikatiba madaraka na wajibu wa Majaji Mahakama ya Juu.	Ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwa Jaji anayeteuliwa kwenda Mahakama ya Juu. Hii itamuwezesha kusikiliza na kuamua mashauri aliyokuwa anayasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu ili kuwe na mwendelezo wa kusikiliza mashauri na kupunguza au kuondoa mlundikano wa kesi zinazoachwa na Majaji waliopandishwa vyeo.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hukumu au uamuzi mwingine wowote unaohusika kwa kutumia na kutaja nafasi ya madaraka aliyokuwa akishika kabla ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu na endapo hukumu hiyo au uamuzi huo utapingwa kwa njia ya rufani itakayofikishwa mbele ya Mahakama ya Juu, Jaji huyo hatakuwa na madaraka ya kusikiliza rufani hiyo.		
(c) Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu			
Ibara ya 158: Uteuzi wa Jaji Mkuu.	(1) Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka orodha ya majina ya watu watatu yaliyopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na kabla ya kuapishwa jina lake litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge.	Lengo la Ibara ni kuweka sifa na utaratibu wa kupatikana kwa Jaji Mkuu.	Sababu za mapendekezo ni kuhuisha utaratibu wa kuweka na vigezo vya uteuzi wa Jaji Mkuu ambaye ndiye kiongozi wa mhimili wa Mahakama. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo na uwazi na kutoa fursa sawa kwa watu

Final Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Jaji Mkuu ndiye atakuwa Mkuu wa Mhimili wa Mahakama katika Jamhuri ya Muungano.		wenye uwezo, uadilifu na uaminifu katika kutoa haki kupata nafasi. Aidha walitaka kuwepo kwa vyombo vingine vya kikatiba vya kumshauri na kumsaidia Rais kufanya teuzi mbalimbali za Viongozi na Watendaji Wakuu wa Serikali na teuzi hizo kuthibitishwa na Bunge.
	(3) Mtu ataweza kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu endapo atakuwa amefikisha umri wa miaka arobaini na tano au zaidi na mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema, uaminifu na:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;		
	(b) awe na shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Jamhuri ya Muungano; na		
	(c) awe:		
	(i) amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au		
	(ii) amefanya kazi ya utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano au uanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka ishirini.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 159: Uteuzi wa Naibu Jaji.	(1) Naibu Jaji Mkuu atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina ya watu watatu yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na kabla ya kuapishwa jina lake litawasilishwa Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge. (2) Mtu atateuliwa kuwa Naibu Jaji Mkuu endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 158 na kwa kufuata msingi kwamba endapo Jaji Mkuu atatoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Naibu Jaji Mkuu atatoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. (3) Naibu Jaji Mkuu atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Jaji Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kwa mara ya kwanza nafasi ya Naibu Jaji Mkuu na kuweka sifa na utaratibu wa kikatiba wa kupatikana kwake.	Kuzingatia maoni ya wananchi juu ya umuhimu wa Naibu Jaji Mkuu ambae pia atakaimu nafasi ya Jaji Mkuu anapokuwa hayupo au ameshindwa kazi. Aidha, nafasi ya Naibu Jaji Mkuu itaweka sura ya Jamhuri ya Muungano katika uongozi wa Mahakama ya Juu.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 160: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Juu.	(1) Majaji wa Mahakama ya Juu watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.	Kuanzisha Jaji wa Mahakama ya Juu na kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Naibu Jaji Mkuu.	Ni kukubaliana na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa uwazi na kutoa fursa sawa kwa watu wenye uwezo, uadilifu na uaminifu katika kutoa haki, kupata nafasi ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Makahama ya Juu. Pia ni kuweka vyombo vyengine vya kikatiba vya kumshauri na kumsaidia Rais kufanya teuzi mbalimbali za Majaji wa Mahakama ya Juu.
	(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Juu endapo atakuwa na sifa zifuatazo:		
	(b) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano mwenye tabia njema, uadilifu na uaminifu;		
	(c) awe na shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano; na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i) awe amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au (ii) awe wakili, mtumishi wa umma au mwanataaluma akiwa na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.		
Ibara ya 161: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Juu.	Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu atashika madaraka yake mara tu atakapokuwa ameapishwa na Rais kiapo cha uaminifu na kiapo kingine chochote	Kuweka utaratibu wa kikatiba wa kiapo cha Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu. Kujenga imani kwa wananchi kuwa Jaji	Kuwataka Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu kutii na kuilinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutekeleza wajibu wao kwa haki, uaminifu na

Final Version
www.iance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kinachohusika na utendaji wa kazi kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.	Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu watatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kiapo.	uadilifu.
Ibara ya 162: Muda wa kuwa madarakani kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama Kuu.	(1) Jaji Mkuu atashika nafasi ya madaraka ya Jaji Mkuu hadi atakapofikisha umri wa miaka sabini, isipokuwa tu kama: (a) atajiuzulu; (b) atashindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na maradhi; (c) kufariki dunia; au (d) atavuliwa madaraka ya Jaji Mkuu kwa mujibu wa	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Majaji wa Mahakama ya Juu kushika madaraka. Pia ni kuweka masharti ya wazi ya kikatiba kuhusu muda na ukomo wa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama ya Juu.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kawaida wa kustaafu Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Majaji wa Mahakama. Aidha, ni muhimu katiba ikatamka bayana sababu nyengine ambazo zinaweza kumfanya Jaji aondolewe katika nafasi yake na sababu hizo zaweza kuwa za kiafya, kiutendaji na kimaadili. Kutanabahisha Jaji, Naibu Jaji au Jaji wa Mahakama ya Juu kuhusu unapokaribia muda wake wa kustaafu kumaliza mashauri yaliyo mbele yake

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Katiba hii. (2) Masharti ya ibara ndogo ya (1) yatatumika pia kwa Naibu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahakama ya Juu.		kuelekea muda wa kustaafu.
	(3) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2), Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahakama ya Juu aliyetimiza umri wa kustaafu atalazimika kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri wa kustaafu.		
	(4) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (3), Jaji Mkuu au Naibu Jaji Mkuu aliyetimiza umri wa kustaafu, ataachia nafasi ya madaraka yake,		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	isipokuwa ataendelea kutekeleza shughuli ambazo hajazikamilisha akiwa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu hadi atakapokamilisha shughuli hizo.		
Ibara ya 163: Utaratibu wa Kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu.	**(**1) Iwapo itatokea kwamba - (a) nafasi ya madaraka ya Jaji Mkuu itakuwa wazi; (b) Jaji Mkuu hayupo katika Jamhuri ya Muungano; au (c) Jaji Mkuu atashindwa kumudu kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote iliyoainishwa katika Katiba hii, Naibu Jaji Mkuu atatekeleza kazi za Jaji Mkuu hadi atakapoteuliwa Jaji	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba masharti ya kukaimu nafasi ya Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu inapokuwa wazi.	Sababu za mapendekezo ni kuhakikisha kuwa wakati wote kuna mtu anaeshika nafasi ya a Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu inapotokea kuwa wazi. Sababu nyingine ni kuepusha kuwepo kwa ombwe la uongozi na usikilizaji wa mashauri na hivyo kuwanyima au kucheleweshe wananchi haki yao.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mkuu mwingine au hadi Jaji Mkuu ambaye alikuwa hayupo au alikuwa hamudu kazi zake atakaporejea kazini.		
	(2) Ikitokea kwamba nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu itakuwa wazi au endapo Jaji wa Mahakama ya Juu yeyote ameteuliwa kutekeleza kazi za Naibu Jaji Mkuu au kama Jaji wa Mahakama ya Juu atashindwa kutekeleza kazi zake kwa sababu yoyote, au Jaji Mkuu atamshauri Rais kuwa kazi za Mahakama ya Juu zilivyo kwa wakati huo zinahitaji ateuliwe Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu, basi Rais anaweza kumteua Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu kutoka miongoni mwa watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Juu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	watakaopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.		
	(3) Mtu atakayeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu atafanya kazi kama Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu kwa muda wote utakaotajwa kwenye hati ya kuteuliwa kwake.		
	(4) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (2), mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu ataendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi amalize shughuli nyingine yoyote inayohusika na rufani au mashauri mengine ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla ya muda wake wa uteuzi haujamalizika au uteuzi wake haujafutwa.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Kwa madhumuni ya masharti ya Ibara hii, Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu atakuwa na mamlaka kamili ya Jaji wa Mahakama ya Juu na atatekeleza kazi zote za Jaji wa Mahakama ya Juu na kwamba idadi ya Majaji wa Mahakama ya Juu iliyotajwa katika Ibara ya 155 haitaathirika kwa sababu tu mmoja au zaidi ya Majaji wa Mahakama ya Juu katika kikao chochote ni Kaimu Jaji wa Mahakama ya Juu.		
Ibara ya 164: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu.	(1) Jaji wa Mahakama ya Juu ataondolewa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu kwa sababu ya kushindwa kutekeleza madaraka yake ama kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya	Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba utakaofuatwa katika hatua zote za kushughulikia nidhamu za Majaji wa Mahakama ya Juu. Lengo lingine ni kuweka mfumo bora utakaosimamia na kushughulikia	Sababu ya mapendekezo haya ni kulinda Mahakama na kuhakikisha kuwa hatua za kinidhamu zinazochukuliwa zinatenda haki kwa Mahakama na kwa Jaji anayehusika. Utaratibu huu unaondoa hofu ya Jaji kuondolewa kwa mizengwe au hila

Trial Version www.nlane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	tabia mbaya inayoathiri maadili ya kazi ya Jaji au sheria inayohusu maadili ya uongozi wa umma, na hataondolewa madarakani isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2).	masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Juu na kujenga nidhamu na uadilifu katika Mahakama ya Juu.	pindi akitoa uamuzi dhidi ya dola. Sababu nyingine ni kuendeleza utaratibu wa kinidhamu wa Majaji ndani ya Jumuiya ya Madola.
	(2) Endapo Rais anaona kuwa suala la kumuondoa Jaji madarakani linahitaji kuchunguzwa, basi katika hali hiyo utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:		
	(a) Rais anaweza, baada ya kushauriana na Jaji Mkuu, kumsimamisha kazi Jaji huyo;		
	(b) Rais atateua Tume ambayo itakuwa na Mwenyekiti na Wajumbe wengine wasiopungua		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wawili na angalau nusu ya wajumbe hao wawe ni Majaji wa Mahakama ya Juu au Mahakama ya Rufani kutoka nchi yoyote iliyomo kwenye Jumuiya ya Madola; na		
	(c) Tume hiyo itachunguza shauri lote kisha itatoa taarifa kwa Rais kuhusu maelezo ya shauri hilo na itamshauri Rais kama Jaji huyo anayehusika aondolewe madarakani kwa mujibu wa masharti ya Ibara hii kwa sababu ya kushindwa kufanyakazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mbaya.		
	(3) Jaji aliyesimamishwa kazi kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2), ataendelea kulipwa mshahara na maslahi yake mengine hadi Jaji huyo atakapoondolewa kazini na Rais chini ya masharti ya ibara ndogo ya (4).		
	(4) Endapo Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) itamshauri Rais kwamba Jaji ambaye mwenendo wake umechunguzwa na Tume hiyo aondolewe kazini kwa sababu ya kushindwa kufanya kazi kutokana na maradhi au sababu nyingine yoyote au kwa sababu ya tabia mbaya, Rais atamuondoa kazini Jaji huyo na utumishi wake utakuwa umekoma.		

Draft Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Endapo Tume iliyoteuliwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (2) itamshauri Rais kwamba Jaji ambaye mwenendo wake umechunguzwa na Tume hiyo asiondolewe, Rais atafuta uamuzi wa kumsimamisha kazi na utumishi wa Jaji huyo utaendelea.		
	(6) Masharti ya Ibara hii hayatawahusu watu walioteuliwa kukaimu nafasi ya Ujaji.		
(d) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 165: Mahakama ya Rufani.	(1) Kutakuwa na Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano, itakayojulikana kwa kifupi kama "Mahakama ya Rufani" na ambayo itakuwa na:	Lengo ni kuanzisha Mahakama ya Rufani na muundo wake.	Sababu za mapendekezo ni kuendelea na utaratibu wa kuwa na Mahakama moja ya Rufani katika Jamhuri ya Muungano ili kutoa nafasi kwa mtu ambaye hajaridhika na maamuzi ya

Trial Version www.muine.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani; (b) Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani; na (c) Majaji wengine wasiopungua kumi na saba. (2) Majaji wa Mahakama ya Rufani watateuliwa kwa kuzingatia sifa zitakazoainishwa katika Katiba hii na uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano. (3) Sheria zitakazotungwa kwa mujibu wa Katiba za Nchi Washirika zitaweka masharti kuhusu utaratibu wa kuwasilisha rufani mbele ya Mahakama ya Rufani.		Mahakama Kuu za Nchi Washirika kukata rufani mbele zaidi. Sababu nyingine ni kuwepo kwa Mahakama moja ya Rufani itakayokuwa na Mamlaka na madaraka ya kusikiliza rufani itakayowasilishwa kutoka Mahakama Kuu za Nchi Washirika.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 166: Akidi ya Vikao vya Mahakama ya Rufani.	(1) Akidi ya kila kikao cha Mahakama ya Rufani itakuwa ni Majaji wa Mahakama ya Rufani watatu. (2) Kila shauri na rufani inayohitaji uamuzi wa Mahakama ya Rufani itaamuliwa kwa kufuata kauli ya walio wengi kati ya Majaji wa Mahakama ya Rufani waliosikiliza shauri au rufani husika.	Lengo ni kuweka kikatiba akidi ya Majaji inayotakiwa kwenye Mahakama ya Rufani kwa ajili ya kusikiliza na kutoa maamuzi.	Sababu ya mapendekezo haya ni kurahisisha utendaji kazi wa Mahakama ya Juu na kutoa uhalali wa maamuzi yatakayofikiwa na Mahakama hiyo.
Ibara ya 167: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.	(1) Mahakama ya Rufani itakuwa na mamlaka ya - (a) kusikiliza na kuamua juu ya kila rufani inayowasilishwa mbele ya Mahakama ya Rufani kutokana na hukumu au uamuzi wowote wa Mahakama Kuu za Nchi	Lengo ni kuweka masharti ya kikatiba juu ya mamlaka na madaraka ya Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na kuipa uwezo wa kusikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi mbalimbali ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika	Sababu ya mapendekezo ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa Mahakama moja ya Rufani katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania itakayosikiliza rufaa na kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika.

Trial Version
www.pdfelement.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika au Mahakama yoyote ya chini iliyopewa mamlaka maalum ya kusikiliza mashauri ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu;		
	(b) kufanya mapitio ya maamuzi ya Mahakama Kuu za Nchi Washirika au mahakama yoyote ya chini iliyopewa mamlaka maalum ya kusikiliza mashauri ambayo kwa kawaida husikilizwa na Mahakama Kuu; na		
	(c) kufanya jambo jingine kama itakavyoainishwa kwenye sheria za nchi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Mahakama ya Rufani itaandaa kanuni kwa ajili ya utekelezaji wa mamlaka yake. (3) Bunge linaweza kutunga sheria itakayoweka masharti zaidi kuhusu uendeshaji wa Mahakama ya Rufani.		
Ibara ya 168: Madaraka ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.	(1) Jaji wa Mahakama ya Rufani atakuwa na madaraka ya kusikiliza na kuamua shauri lolote katika Mahakama ya Rufani. (2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), iwapo Jaji wa Mahakama ya Rufani kabla ya kuteuliwa kwake alikuwa Jaji wa Mahakama Kuu ya Nchi Washirika, Jaji huyo anaweza kuendelea kufanya kazi	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya madaraka na wajibu wa Majaji wa Mahakama ya Rufani katika kutekeleza wajibu wao.	Kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwa Jaji anayeteuliwa kwenda Mahakama ya Rufani amalize kusikiliza mashauri aliyokuwa anayasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani ili kuwa na mwendelezo wa kusikiliza mashauri na kupunguza au kuondoa mlundikano wa kesi zinazoachwa na Majaji waliopandishwa vyeo.

Final Version
www.kuanza.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika mahakama aliyotoka hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajateuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.		
	(3) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (2), itakuwa ni halali kwa Jaji wa Mahakama ya Rufani kutoa hukumu au uamuzi mwingine wowote unaohusika kwa kutumia na kutaja nafasi ya madaraka aliyokuwa akishika kabla ya kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani na endapo hukumu hiyo au uamuzi huo utapingwa kwa njia ya rufani itakayowasilishwa mbele ya Mahakama ya Rufani, Jaji huyo hatakuwa na mamlaka ya kusikiliza		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	rufani hiyo.		
(e)Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani			
Ibara ya 169: Uteuzi wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani.	(1) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atateuliwa na Rais kutoka orodha ya majina ya watu watatu yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama. (2) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atakuwa ndiye Mkuu wa Mahakama ya Rufani na msaidizi wa Jaji Mkuu katika utendaji wa kazi katika Mahakama ya Rufani, na katika madaraka hayo, Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atatekeleza kazi na shughuli atakazopangiwa mara kwa mara na Jaji Mkuu.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atakayetekeleza kazi na shughuli zake kwa maelekezo au kama atakavyopangiwa na Jaji Mkuu.	Sababu za mapendekezo haya ni kuwa na utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atakayekuwa Kiongozi wa Mahakama ya Rufani badala ya utaratibu uliyomo katika katiba ya Jamhuri ya Mwaka 1977 ambapo Jaji Mkuu ndiye Kiongozi wa Mahakama ya Rufani.
	(3) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani		

Draft Version 1.0
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	endapo atakuwa na sifa zifuatazo:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano mwenye tabia njema, uadilifu na uaminifu;		
	(b) awe na shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano; na		
	(i) awe amefanya kazi ya ujaji katika Mahakama Kuu za Nchi Washirika; au (iii) awe wakili, mtumishi wa umma au mwanataaluma akiwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na sifa ya kusajiliwa kuwa wakili na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi na tano.		
Ibara ya 170: Uteuzi wa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani.	(1) Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atateuliwa na Rais kutoka katika orodha ya majina ya watu watatu yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama na atakuwa ndiye Msaidizi Mkuu wa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani. (2) Mtu atateuliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani	Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kupatikana Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani.	Sababu kuu mbili za mapendekezo haya ni kuondoa uwezekano wa kuwepo kwa ombwe iwapo Mwenyekiti hatakuwepo na kuupa uongozi wa Mahakama ya Rufani sura ya Muungano.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 169(3).		
	(3) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani utafanywa kwa msingi kwamba, endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 171: Uteuzi wa Majaji wa Mahakama ya Rufani.	(1) Majaji wa Mahakama ya Rufani watateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa majina yatakayopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba na sifa za mtu anayeweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa watu wanaoteuliwa kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani wanakuwa na sifa na uwezo stahiki, na wamepatikana kwa utaratibu wa wazi na wa ushindani
	(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Jaji wa Mahakama ya Rufani endapo atakuwa na sifa zilizoainishwa katika Ibara ya 169(3).		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 172: Kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani.	Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Makamu Mwenyekiti na Jaji wa Mahakama ya Rufani atashika madaraka yake mara tu atakapoapishwa na Rais kiapo cha uaminifu na kiapo kingine chochote kinachohusika na utendaji wa kazi kitakachowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi.	Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kiapo cha Majaji wa Mahakama ya Rufani.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuwataka Majaji wa mahakama ya Rufani kutii na kulinda Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kutoa haki kwa uadilifu bila upendeleo au huba.
Ibara ya 173: Muda wa kuwa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani.	**173.**-(1) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani atashika nafasi ya madaraka ya Ofisi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani hadi atakapofikisha umri wa miaka sabini, isipokuwa kama: (a) atajiuzulu; (b) atashindwa kumudu kazi	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba umri wa kustaafu na muda wa kushika madaraka kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Majaji wa Mahakama ya Rufani.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba wa kutamka wa umri wa kustaafu kwa Majaji. Aidha, mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliotaka Majaji wanaostaafu kabla ya kumaliza mashauri waliyoanza kusikiliza wamalize kazi zao ili

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutokana na maradhi; (c) ataondolewa katika nafasi ya madaraka ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba hii; au (d) atafariki dunia. (2) Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani au Jaji wa Mahakama ya Rufani atashika madaraka hadi atakapotimiza umri wa miaka sabini, isipokuwa kama: (a) atajiuzulu; (b) atashindwa kumudu kazi kutokana na maradhi; (c) ataondolewa katika nafasi ya madaraka ya Makamu		kuharakisha utoaji wa haki na kuwapunguzia usumbufu wananchi.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba hii; au (d) atafariki dunia.		
	(3) Jaji aliyetimiza umri wa kustaafu atalazimika kuendelea kufanya kazi baada ya kutimiza umri huo hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi akamilishe shughuli nyingine yoyote inayohusika na mashauri ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla hajatimiza umri wa kustaafu.		
	(4) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (3), Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani aliyetimiza umri wa kustaafu, ataachia nafasi ya madaraka ya Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, isipokuwa ataendelea		

Final Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutekeleza shughuli ambazo hajazikamilisha akiwa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Rufani hadi atakapokamilisha shughuli hizo.		
Ibara ya 174: Utaratibu wa Kukaimu nafasi ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani.	(1) Iwapo itatokea kwamba -	Madhumuni ni kuweka utaratibu wa kikatiba unaopaswa kufuatwa katika kujaza nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Jaji wa Mahakama ya Rufani ikiwa wazi.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa kila wakati kuna mtu anayeshika nafasi ya Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Jaji wa Mahakama ya Rufani kuwa wazi kwa sababu yoyote iliyoainishwa kwenye Katiba.
	(a) nafasi ya madaraka ya Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani ipo wazi;		
	(b) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani hayupo katika Jamhuri ya Muungano;		
	(c) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani ameshindwa kutekeleza kazi kwa mujibu wa Katiba hii,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Makamu Mwenyekiti atatekeleza kazi za Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani hadi atakapoteuliwa Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani mwingine au hadi Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani ambaye alikuwa hayupo nchini au alikuwa hawezi kumudu kazi zake kutokana na maradhi atakaporejea kazini.		
	(2) Endapo ufanisi wa kazi za Mahakama ya Rufani utahitaji ateuliwe Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani, Jaji Mkuu atamshauri Rais kumteua Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani.		
	(3) Endapo Rais ataridhika na ushauri wa Jaji Mkuu, atamteua Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani kutoka miongoni mwa watu wanaoweza kuteuliwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuwa Majaji wa Mahakama ya Rufani.		
	(4) Mtu atakayeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani atafanya kazi kama Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani kwa muda wote utakaotajwa wakati wa kuteuliwa kwake, au kama muda haukutajwa, basi hadi uteuzi utakapofutwa na Rais.		
	(5) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (4), mtu aliyeteuliwa kuwa Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani ataendelea kufanya kazi kama Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani hadi amalize kutayarisha na kutoa hukumu au hadi amalize shughuli nyingine yoyote inayohusika na rufani au mashauri mengine ambayo alikwishaanza kuyasikiliza kabla ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	muda wake wa kazi haujamalizika au uteuzi wake haujafutwa. (6) Kwa madhumuni ya Ibara hii, Kaimu Jaji wa Mahakama ya Rufani atakuwa na mamlaka kamili ya Jaji wa Mahakama ya Rufani na atatekeleza kazi zote za Jaji wa Mahakama ya Rufani.		
Ibara ya 175: Utaratibu wa kushughulikia nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.	(1) Jaji wa Mahakama ya Rufani anaweza kuondolewa katika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Rufani kwa sababu ya kushindwa kutekeleza kazi yake kutokana na: (a) maradhi; (b) kukiuka kanuni za maadili ya Majaji wa Mahakama ya Rufani; (c) kutokuwa na uwezo wa	Lengo ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa mfumo bora utakaosimamia na kushughulikia masuala ya nidhamu ya Majaji wa Mahakama ya Rufani.	Sababu ya mapendekezo haya ni kulinda uhuru wa Majaji na hadhi ya Mahakama kwa kuweka utaratibu utakaotenda haki kwa Mahakama na Jaji anayehusika kuchunguzwa.

Trial Version
www.luanda.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kumudu kazi za Jaji; au (d) tabia mbaya au mwenendo unaokiuka maadili ya uongozi wa umma.		
	(2) Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani au Jaji wa Mahakama ya Rufani anaweza kuondolewa katika nafasi ya madaraka ya Jaji kwa kufuata utaratibu unaofanana na ule uliowekwa kwa ajili ya kumuondoa kazini Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu au Jaji wa Mahakama ya Juu kama ilivyoelezwa.		
(f)Usimamizi wa Shughuli za Mahakama			
Ibara ya 176: Msajili	(1) Kutakuwa na Msajili Mkuu wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Msajili Mkuu	Sababu za mapendekezo ni kuimarisha utendaji kazi wa shughuli za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mkuu wa Mahakama.	atakayeitwa "Msajili Mkuu wa Mahakama", atakayeteuliwa na Rais kufuatia mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Mahakama.	wa Mahakama na upatikanaji wake.	kimahakama katika utoaji wa haki. Aidha, ni kuendeleza utaratibu uliopo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 ambao una mfumo wa Mahakama kuwa na Msajili wa Mahakama kwa ajili ya kuratibu uendeshaji wa shughuli za kimahakama. Sababu nyingine ni kutambua kuwa Msajili Mkuu wa Mahakama ndiye kiungo kati ya Majaji na watumishi wengine wa katika kutekeleza majukumu ya kimahakama.
	(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Msajili Mkuu wa Mahakama endapo atakuwa na sifa zifuatazo:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano mwenye sifa ya uadilifu, tabia njema na uaminifu;		
	(b) awe na shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na mamlaka inayoshughulikia elimu ya juu katika Jamhuri ya Muungano; na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i)awe amefanya kazi ya uhakimu katika Mahakama za Nchi Washirika; au		
	(ii) amekuwa mtumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano, —na amekuwa na sifa hizo mfululizo kwa muda usiopungua miaka kumi.		
Ibara ya 177: Majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama.	(1) Msajili Mkuu wa Mahakama atakuwa na majukumu yafuatayo:	Lengo la Ibara hii ni kuweka kwenye Katiba masharti yanayohusu majukumu ya Msajili Mkuu wa Mahakama.	Sababu za mapendekezo haya ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama. Sababu nyingine ni kumpa Msajili wa Mahakama dhamana na wajibu wa kusimamia shughuli za kimahakama na kuhakisha zinafanyika
	(a) kusimamia utekelezaji wa shughuli za kimahakama;		
	(b) kuratibu masuala ya		

Trial Version
www.iLance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kimahakama; na		kwa ufanisi na kwa utaratibu uliowekwa.
	(c) majukumu mengine atakayopangiwa na Jaji Mkuu.		
	(2) Katika kutekeleza majukumu yake, Msajili Mkuu wa Mahakama atawajibika kwa Jaji Mkuu.		
Ibara ya 178: Mtendaji Mkuu wa Mahakama.	(1) Kutakuwa na Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakayeteuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi wa umma kufuatia mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma na kuidhinishwa na Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama mwenye dhamana ya kusimamia utawala, fedha na mipango ya maendeleo ya Mahakama.	Sababu za mapendekezo haya ni kuimarisha utendaji wa Mahakama kwa kuwa na mtaalamu wa utawala, fedha na mipango tofauti na ilivyokuwa kabla kwa nafasi hii kushikiliwa na Msajili Mkuu wa Mahakama. Sababu nyingine ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama.
	(2) Mtu hatateuliwa kushika nafasi ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama isipokuwa tu kama ni:		

Katiba Version
www.katiba.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) mtumishi mwandamizi wa umma;		Halikadhalika ni kuzingatia na maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa vyombo vya Kikatiba vya kumshauri Rais kuhusu uteuzi wa nafasi mbalimbali za Watendaji Wakuu wa Serikali na teuzi hizo kuidhinishwa na Bunge.
	(b) mwenye uweledi na uzoefu katika masuala ya utawala na mambo ya fedha; na		
	(c) mwadilifu na mwenye tabia na mwenendo usiotiliwa shaka na jamii.		
Ibara ya 179: Majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.	(1) Mtendaji Mkuu wa Mahakama atakuwa na majukumu yafuatayo:	Lengo ni kuweka kwenye Katiba masharti yanayohusu majukumu ya Mtendaji Mkuu wa Mahakama.	Sababu za mapendekezo ni kuboresha utendaji kazi wa mhimili wa Mahakama kwa kumuweka mtendaji mahsusi katika mfumo wa Mahakama anayesimamia masuala ya fedha na utawala. Uzoefu wa nchi nyingine kama Jamhuri ya Ireland yenye Mtendaji Mkuu wa Mahakama
	(a) Katibu wa Tume ya Utumishi wa Mahakama;		
	(b) Ofisa Masuuli wa Mahakama;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) msimamizi mkuu wa Mfuko wa Mahakama;		umeonyesha ufanisi mkubwa katika utendaji wa kila siku wa shughuli za Mahakama.
	(d) msimamizi wa masuala ya utawala ya Mahakama; na		
	(e) kutekeleza kazi nyingine atakazopangiwa na Jaji Mkuu.		
	(2) Katika kutekeleza majukumu yake, Mtendaji Mkuu wa Mahakama atawajibika kwa Jaji Mkuu.		
SEHEMU YA TATU - TUME YA UTUMISHI WA MAHAKAMA NA MFUKO WA MAHAKAMA			
(a) Tume ya Utumishi wa Mahakama			
Ibara ya 180: Tume ya Utumishi wa Mahakama.	(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Mahakama ambayo itakuwa na wajumbe nane watakaoteuliwa na	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Utumishi wa Mahakama na kuainisha kazi na	Sababu za mapendekezo ya Ibara hii ni kuendeleza utaratibu uliopo Tanzania na katika nchi mbalimbali

Trial Version
www.mlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Rais kama ifuatavyo: (a) Jaji Mkuu ambaye atakuwa Mwenyekiti; (b) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; (c) Jaji mmoja wa Mahakama ya Juu; (d) Jaji mmoja wa Mahakama ya Rufani; (e) Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria Tanganyika; (f) Mwakilishi wa Chama cha Wanasheria Zanzibar;	majukumu ya Tume hiyo.	duniani wa kuwepo Tume ya Utumishi wa Mahakama. Aidha kuwepo kwa utaratibu huo kunaweka bayana utengano wa mihimili ya dola katika kutekeleza majukumu yao. Pia, Ibara inaipa Mahakama, chombo ambacho kinaimarisha uhuru na mamlaka ya Mahakama kwa kushughulikia ajira, nidhamu na maslahi ya watendaji wa Mahakama. Sababu nyingine ni kuwa, chombo hiki kitahakikisha kuwepo kwa uwiano wa wajumbe wa Tume wa Mahakama kutoka pande mbili za Muungano.
	(g) Wawakilishi wawili wa vitivo vya sheria kutoka vyuo vikuu, mmoja kutoka Tanganyika na mmoja		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutoka Zanzibar watakaopendekezwa na vyuo vya elimu ya juu husika; na Mtendaji Mkuu wa Mahakama ambaye atakuwa Katibu.		
	(2) Tume inaweza kumualika mtu mwingine yeyote mwenye utaalamu mahsusi kushiriki katika kikao chochote cha Tume, isipokuwa mtu huyo hatakuwa na haki ya kupiga kura.		
	(3) Tume itaweka utaratibu wa kuendesha vikao vyake.		
Ibara ya 181: Majukumu ya Tume ya Utumishi wa	(1) Tume ya Utumishi wa Mahakama itakuwa na wajibu wa kuendeleza na kuwezesha uhuru na	Lengo ni kuweka kikatiba majukumu ya Tume ya Utumishi	Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua kuwa Tume ya Utumishi wa Mahakama ikiwa ni moja ya vyombo

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Umma.	uwajibikaji wa Mahakama na utoaji haki wenye ufanisi, mafanikio na uwazi. (2) Tume ya Utumishi wa Mahakama itakuwa na wajibu wa: (a) kupendekeza kwa Rais majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Majaji wa Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani;	wa Mahakama.	vinavyoimairisha ufanisi na utendaji wa mahakama kwa kusimamia maendeleo ya Mahakama na watumishi wake. Aidha chombo hiki kitasimamia nidhamu ya watumishi wa Mahakama ambao si Majaji ili kuimarisha uhuru wa Mahakama.
	(b) kupitia na kupendekeza masharti ya utumishi wa Majaji na watumishi wengine wa mahakama		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ikiwemo masuala yanayohusu nidhamu na maslahi yao;		
	(c) kuteua wasajili na kuajiri watumishi wengine wa Mahakama, kupokea malalamiko dhidi yao na kuwachukulia hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria za nchi;		
	(d) kuandaa na kutekeleza mipango ya kujiendeleza kielimu kwa Majaji na watumishi wengine wa Mahakama;		
	(e) kupendekeza Serikalini hatua za kuimarisha Mahakama ili kuongeza		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ufanisi katika utoaji haki;		
	(f) kutoa fursa ya majadiliano kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na hivyo kumsaidia Jaji Mkuu katika kutekeleza majukumu yake kwa malengo ya kuleta ufanisi na mafanikio katika utoaji haki; na		
	(g) kutekeleza majukumu yoyote itakayopewa kwa mujibu wa Katiba hii au sheria za nchi.		
	(3) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume itazingatia: (a) uwazi katika mchakato wa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uteuzi wa Majaji na ajira ya watumishi wengine wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano;		
	(b) uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano; na		
	(c) uwakilishi wa kijinsia.		
	(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Tume inaweza kukasimu madaraka yake kwa kamati mbalimbali zitakazoundwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
	(5) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (2)(b), mapendekezo ya maslahi kwa Majaji na watumishi wengine wa Mahakama		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yatawasilishwa kwenye chombo chenye jukumu la kusimamia maslahi ya watumishi wa umma.		
	(6) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti ya utekelezaji wa majukumu ya Tume.		
Ibara ya 182: Uanachama katika Vyama vya Siasa.	Itakuwa ni marufuku kwa Jaji wa Mahakama ya Juu, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Msajili Mkuu wa Mahakama, Msajili wa ngazi yoyote na Mtendaji Mkuu wa Mahakama kuwa mwanachama wa chama chochote cha siasa, isipokuwa atakuwa na haki ya kupiga kura kuchagua viongozi katika vyombo vya uwakilishi.	Lengo la Ibara hii ni kuwazuia Majaji na viongozi wengine wa Mahakama kuwa wanachama wa Vyama vya Siasa.	Sababu za Mapendekezo haya ni kutambua kuwa Mahakama ni chombo cha utoaji haki ambacho viongozi na watumishi wake wa juu ni lazima waonekane wanatenda kwa haki bila ya tashwishi. Sababu nyingine ni kuondoa uwezekano wa watumishi wa Mahakama kufanya maamuzi ya mashauri kwa huba au ushawishi wa kisiasa. Rasimu imependekeza Ibara hii ili wananchi wawe na imani kuwa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Mahakama itatenda haki kwa watu wote bila kujali itikadi za Vyama vya Siasa.
(b) Mfuko wa Mahakama			
Ibara ya 183: Mfuko wa Mahakama.	(1) Kutakuwa na Mfuko wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano ambao utakuwa chini ya usimamizi wa Mtendaji Mkuu wa Mahakama.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Mfuko wa Mahakama na kuainisha majukumu yake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu ulioanzishwa wa kila mhimili kuwa na Mfuko wake wa kusimamia gharama za utekelezaji wa majukumu yake.
	(2) Mfuko wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano utatumika kwa ajili ya kugharamia shughuli za utawala na uendeshaji wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano na shughuli nyingine muhimu katika utekelezaji wa majukumu ya Mahakama.		
	(3) Serikali itahakikisha kwamba		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika kila bajeti ya mwaka wa fedha wa Serikali, inatenga kwa kiwango kinachotosha fedha ambazo zitaingizwa katika Mfuko wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano.		
	(4) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu uendeshaji wa Mfuko wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano.		
SURA YA KUMI NA MOJA **UTUMISHI WA UMMA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO**			
Ibara ya 184: Misingi Mikuu ya Utumishi wa Umma.	(1) Kutakuwa na utumishi wa umma katika Jamhuri ya Muungano utakaozingatia misingi na kanuni zifuatazo:	Lengo ni kutambua kikatiba Utumishi wa Umma wa Jamhuri ya Muungano na kuainisha misingi mikuu na kanuni za	Sababu za mapendekezo haya ni kujua kuwa Utumishi wa Umma ni nguzo muhimu ya mhimili wa Serikali na hivyo kutakiwa kutambuliwa,

Final Version
www.mlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) kwamba utumishi wa umma ni dhamana kutoka kwa wananchi na hivyo mtumishi anatakiwa kutumikia wananchi kwa uadilifu, uaminifu na unyenyekevu;	Utumishi wa Umma.	kukuzwa, kuimarishwa na kusimamiwa kikatiba. Kujenga mazingira ya kuwa na Utumishi wa Umma uliotukuka. Kujenga misingi mikuu ya Utumishi wa Umma itakayotumiwa na mtendaji wa umma katika kutoa huduma kwa jamii bila ya ubaguzi wa aina yoyote wa kijinsi, rangi, kabila, dini au mahali anapotoka mtu anayehitaji huduma hiyo.
	(b) umuhimu wa kudumisha na kukuza viwango vya juu vya maadili ya kitaaluma;		
	(c) umuhimu wa kuzingatia matumizi bora na yenye tija ya rasilimali;		
	(d) kutoa huduma kwa umma kwa njia ya haki, usawa na bila upendeleo;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) kuhamasisha wananchi kushiriki katika maandalizi ya sera mbalimbali za nchi;		
	(f) kuitikia matakwa na mahitaji ya watu kwa haraka na kwa wakati unaofaa;		
	(g) kujitolea katika utekelezaji wa sera na mipango ya kitaifa;		
	(h) uwajibikaji wa viongozi kwa makosa yanayofanyika chini yao;		
	(i) kuhamasisha na kutekeleza sera ya uwazi katika kutoa habari za		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kweli kwa umma na kwa wakati unaofaa; na		
	(j) kuhakikisha kwamba uteuzi na uajiri katika nafasi mbalimbali kwa kuzingatia uwezo wa kitaaluma, weledi, maarifa, ujuzi na uzoefu wao katika eneo husika.		
	(2) Misingi na Kanuni za Utumishi wa Umma zilizoainishwa katika Ibara hii zitazingatiwa na kutumika katika uteuzi wa kushika nafasi za madaraka ya uongozi katika:		
	(a) mamlaka katika mihimili ya dola;		
	(b) taasisi na idara zote za		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Serikali; na (c) mashirika, makampuni na wakala wa Serikali. (3) Bunge litatunga sheria kuweka masharti ya utekelezaji wa misingi ya utumishi iliyoainishwa katika ibara ndogo ya (1).		
Ibara ya 185: Ajira na Uteuzi wa Viongo wa Taasisi katika Serikali.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba hii, ajira katika utumishi wa umma na uteuzi katika nafasi za madaraka ya uongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano na taasisi zake, itatolewa na kufanyika kwa kuzingatia: (a) taaluma na uweledi; na (b) uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu ajira katika Utumishi wa Umma na uteuzi wa viongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Taasisi zake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuwa na sifa na taratibu za kuzingatiwa katika ajira ndani ya Utumishi wa Umma katika Serikaili ya Jamhuri ya Muungano na Taasisi zake. Aidha, kuweka msingi wa kuzingatia uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano. Mapendezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi waliodai kuwa Zanzibar haishirikishwi kikamilifu katika ajira za

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), uteuzi wa viongozi katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano utafanyika kwa kuzingatia ushiriki wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.		Muungano na kuwa kero za muda mrefu.
Ibara ya 186: Tume ya Utumishi wa Umma.	(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Umma itakayokuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine sita watakaoteuliwa na Rais na kuidhinishwa na Bunge.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Utumishi wa Umma na uongozi wake.	Sababu za mapendekezo haya kuipa hadhi na madaraka ya kikatiba Tume ya Utumishi wa Umma katika kutekeleza majukumu yake na kutoa uhuru unaostahiki. Aidha, ni kutambua jukumu kubwa liliopewa Tume hii kumshauri Rais kuhusu teuzi mbalimbali.
	(2) Katika kuteua wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma, Rais atazingatia Kanuni za Utumishi wa Umma zilizoainishwa katika Katiba hii.		
	(3) Sifa za Mwenyekiti na Mjumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	zitakuwa kama ifuatavyo:		
	(a) awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi;		
	(c) awe na uzoefu wa utumishi wa umma, upeo mkubwa katika mambo ya utumishi, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka kumi; na		
	(d) awe na heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wenye kutiliwa shaka na jamii.		
Ibara ya 187: Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma.	(1) Kutakuwa na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma ambaye atateuliwa na Rais kutoka miongoni mwa watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano au Serikali za Nchi Washirika baada ya kuidhinishwa na Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia utaratibu uliozoeleka wa tume za aina hii kuwa na Katibu ambaye ndiye Mtendaji Mkuu na msimamizi wa shughuli za Tume.
	(2) Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma atakuwa ndiye Mkuu wa Sekretarieti ya Utumishi wa Umma, Mtendaji Mkuu na mtekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Tume.		
Ibara ya 188: Mamlaka na Majukumu ya Tume ya	(1) Tume ya Utumishi wa Umma itakuwa ni chombo cha juu katika utumishi wa umma chenye	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba mamlaka na majukumu ya Tume ya Utumishi	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kuwa Tume ya Utumishi wa Umma ina wajibu na dhamana kubwa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Utumishi wa Umma.	mamlaka ya kusimamia na kuratibu mambo yote kuhusu utumishi wa umma. (2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), majukumu ya Tume ya Utumishi wa Umma yatakuwa ni: (a) kumshauri Rais juu ya uteuzi wa viongozi katika nafasi mbalimbali kwa mujibu wa Katiba hii; (b) kutoa miongozo mbalimbali na kusimamia mchakato wa ajira katika utumishi wa umma kwa kuzingatia vigezo stahiki; (c) kuteua watu kuhudumu au kushikilia ofisi kwa muda katika utumishi wa umma,	wa Umma.	kwa Serikali na taifa wa kuhakikisha kuwa watumishi wa umma wana weledi, uzoefu, uadilifu, na uaminifu katika utumishi wao. Chombo hiki ndicho kinachohakikisha kuwa viongozi wanaoteuliwa na Rais ni wale wenye sifa zilizoainishwa katika sheria na kanuni mbalimbali za Utumishi wa Umma. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuongeza uwajibikaji wa Tume ya Utumishi wa Umma kwa kusimamia misingi mikuu ya Utumishi wa Umma.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuidhinisha uteuzi na kudhibiti nidhamu na kuwaondoa watumishi wanaohudumu au kushikilia ofisi hizo;		
	(d) kusimamia na kuhamasisha utekelezaji wa misingi na kanuni za utumishi katika sekta zote za utumishi wa umma;		
	(e) kushughulikia rufani zinazowasilishwa na watumishi wa umma dhidi ya uamuzi wa mamlaka mbalimbali za nidhamu katika utumishi wa umma;		
	(f) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yatakavyoainishwa katika sheria za nchi juu ya masuala ya utumishi wa umma na sheria nyingine za nchi;		
	(g) kuunda na kupanga ngazi za mishahara na marupurupu ya watumishi wa umma, ikiwemo, viongozi wa kisiasa, watumishi katika Utumishi wa Serikali, Utumishi wa Bunge na Utumishi wa Mahakama; na		
	(h) kudurusu na kusawazisha mishahara na marupurupu ya watumishi wa umma ikiwemo viongozi wa kisiasa, watumishi katika		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Utumishi wa Serikali, Utumishi wa Bunge na Utumishi wa Mahakama.		
SURA YA KUMI NA MBILI **UCHAGUZI KATIKA VYOMBO VYA UWAKILISHI NA VYAMA VYA SIASA**			
SEHEMU YA KWANZA - UWAKILISHI WA WANANCHI			
Ibara ya 189: Ushiriki katika Uchaguzi na Kura ya Maoni.	(1) Kila raia wa Jamhuri ya Muungano mwenye umri wa miaka kumi na nane au zaidi mwenye akili timamu ana haki ya kupiga kura na haki ya kuandikishwa na kushiriki kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni.	Madhumuni ni kuweka haki ya kuandikishwa na kupiga kura au kura ya maoni.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutambua na kulinda haki ya msingi ya kila raia ya kupiga kura ambayo ni lazima itambuliwe na kulindwa na Katiba. Aidha, ni muhimu kwa Katiba kuweka mfumo wa wazi wa utaratibu wa ushiriki wa wananchi katika uchaguzi na kura ya maoni na kutoa nafasi kwa watu wenye ulemavu na mahitaji maalum kupata nafasi za uwakilishi katika vyombo vya kutunga
	(2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), mamlaka ya kusimamia uchaguzi itazingatia misingi		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwamba:		sheria.
	(a) wananchi wanatumia haki ya kisiasa kwa mujibu wa Katiba hii;		
	(b) watu wenye ulemavu wanapewa fursa za uwakilishi;		
	(c) kunakuwa na haki ya kila raia kupiga kura moja kufuatana na utashi wa uwakilishi na kura sawa; na		
	(d) uchaguzi unakuwa huru na wa haki ambao -		
	(i) ni wa kura ya siri;		
	(ii) hauna matumizi ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nguvu, vitisho, vishawishi wala rushwa;		
	(iii) hauna matamshi au vitendo vinavyoashiria ukabila, ukanda, udini, dharau na kashfa kwa jinsi au unyanyapaa kwa walemavu au makundi madogo katika jamii;		
	(iv) unaendeshwa na kusimamiwa na chombo huru; na		
	(v) unaendeshwa bila upendeleo au		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuegemea upande wowote, ulio makini na unaoonyesha uwajibikaji wa watendaji.		
	(3) Katika kutekeleza masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2), mamlaka ya nchi itaweka utaratibu wa sheria utakaowezesha:		
	(a) mamlaka zinazosimamia uchaguzi kutangaza majimbo kwa madhumuni ya uchaguzi wa wabunge;		
	(b) uteuzi wa wagombea;		
	(c) uandikishaji wa wapiga		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kura;		
	(d) kuendesha na kusimamia uchaguzi na kura ya maoni;		
	(e) kuweka utaratibu wa kuandikisha raia wa Jamhuri ya Muungano wanaoishi nje kuweza kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni; na		
	(f) utaratibu wa kufanya uchaguzi kuwa mwepesi, wazi na unaozingatia mahitaji ya watu wenye mahitaji maalum.		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(4) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (2) na kwa kuzingatia masharti kuhusu kupinga matokeo ya uchaguzi wa Rais, kila mpiga kura ana haki ya kufungua shauri Mahakamani kupinga matokeo ya uchaguzi, anayoamini yamekiuka masharti ya Katiba hii au sheria za nchi.		
SEHEMU YA PILI - TUME HURU YA UCHAGUZI			
(a) Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi			
Ibara ya 190: Kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi.	(1) Kutakuwa na Tume Huru ya Uchaguzi ◇ ya Jamhuri ya Muungano itakayoitwa "Tume Huru ya Uchaguzi". (2) Tume Huru ya Uchaguzi itakuwa na Mwenyekiti, Makamu	Lengo ni kuanzisha kikatiba Tume Huru ya Uchaguzi na kuainisha sifa za wajumbe wake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ambao wamekuwa wanadai kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi. Tume Huru ya Uchaguzi ni chombo muhimu katika mfumo wa utawala wa kidemokrasia.

Trial Version
www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mwenyekiti na wajumbe wengine saba watakaoteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati ya Uteuzi.		Aidha uchaguzi huru na wa haki ndiyo njia ya kuwapata viongozi wa taifa wenye ridhaa ya wananchi. Sababu nyingine ya mapendekezo haya yamezingatia misingi inayokubalika duniani ya vyombo huru vya usimamizi wa uchaguzi ambayo ni: uhuru, uadilifu, uwajibikaji na uwazi.
	(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi watashika madaraka mara baada ya kuthibitishwa na Bunge.		
	(4) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi utafanywa kwa misingi kwamba, endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi watakuwa na sifa zifuatazo:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) awe ni mtu aliyewahi kushika nafasi ya madaraka ya Jaji wa Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu na ameshika nafasi ya madaraka hayo kwa kipindi kisichopungua miaka		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mitano;		
	(c) awe ni mwaminifu, mwadilifu na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;		
	(d) awe ni mtu ambaye, hajawahi kushika nafasi ya madaraka katika chama cha siasa; na		
	(e) awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusiana na uaminifu.		
	(6) Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi atakuwa na sifa zifuatazo:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;		
	(c) awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha siasa;		
	(d) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na		
	(e) awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu.		
	(7) Kwa madhumuni ya Ibara hii, watu wafuatao hawatakuwa na sifa ya kuwa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi:		
	(a) Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Mbunge wa Bunge la Tanganyika, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Diwani katika Serikali ya Tanganyika au Zanzibar; au		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) mtu ambaye ni mtumishi wa umma.		
	(8) Uteuzi wa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi utazingatia uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano.		
Ibara ya 191: Kamati ya Uteuzi.	(1) Kutakuwa na Kamati ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi itakayokuwa na wajumbe wafuatao:	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na kuainisha majukumu yake.	Sababu za mapendekezo zimezingatia maoni ya wananchi waliotaka kuwepo kwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi wateuliwe kwa mfumo wa wazi na unaotoa fursa kwa watu wengi kuomba au kupendekezwa kuwa wajumbe. Sababu nyingine ni kuondoa dhana ya chombo hiki muhimu kutumiwa na mamlaka iliyokiteua na hivyo kutoaminika na pia kuweka utaratibu wa uwazi katika upatikanaji wa
	(a) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;		
	(b) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Makamu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Mwenyekiti;		wajumbe wa Tume na kujenga ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume.
	(c) Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;		
	(d) Spika wa Bunge la Tanganyika;		
	(e) Jaji Mkuu wa Tanganyika;		
	(f) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na		
	(g) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.		
	(2) Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi atakuwa Katibu wa Kamati ya Uteuzi.		
	(3) Kamati ya Uteuzi itakuwa na jukumu la kupokea na kuchambua		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	majina ya watu walioomba na waliopendekezwa kuwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mujibu wa utaratibu utakaoainishwa na sheria za nchi.		
	(4) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (3), Kamati ya Uteuzi mara baada ya kuchambua majina ya watu walioomba na waliopendekezwa kuwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi, itapendekeza kwa Rais majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi.		
	(5) Rais atateua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kutoka miongoni mwa majina		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yaliyowasilishwa na Kamati ya Uteuzi na atawasilisha majina hayo Bungeni kwa ajili ya kuthibitishwa na Bunge.		
	(6) Kwa madhumuni ya Ibara hii, asasi za kiraia na zisizo za kiserikali zinaweza kupendekeza majina ya watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi.		
	(7) Bunge litatunga Sheria ambayo pamoja na mambo mengine itaweka masharti kuhusu kiapo cha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wa Tume Huru ya Uchaguzi.		
Ibara ya 192: Ukomo wa	(1) Mjumbe wa Tume atashika nafasi	Lengo la Ibara hii ni kuweka	Sababu za mapendekezo haya ni

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kushika nafasi ya Madaraka ya Tume Huru ya Uchaguzi.	ya madaraka kwa kipindi cha miaka mitano na anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja cha miaka mitano. (2) Mtu atakoma kuwa mjumbe wa Tume endapo litatokea tukio lolote kati ya matukio yafuatayo: (a) kujiuzulu; (b) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya maradhi; (c) kuondolewa kwa makosa ya kukiuka Kanuni za Maadili ya Uongozi wa Umma;	masharti ya Katiba kuhusu ukomo wa kushika madaraka ama kwa kumaliza muda wake wa ujumbe au kuondolewa kwa kukiuka kanuni za maadili.	kuondoa dhana kuwa nafasi ya ujumbe ni ya kudumu ili kutoa fursa kwa wananchi wengine. Pia, utaratibu wa kubadilisha Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kutasaidia kuleta mawazo mapya na mabadiliko ya kifikra na kimaendeleo katika nchi. Aidha, kuwepo kwa Kamati ya Uteuzi kutawezesha kupatikana kwa wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa mchakato wa wazi kupitia utaratibu wa kupendekezwa au kuomba nafasi na kuchujwa.

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(d) kutiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifungo gerezani kwa muda unaozidi siku saba;		
	(e) kupoteza sifa ya kuteuliwa kuwa mjumbe; au		
	(f) kufariki dunia.		
	(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa majukumu ya Tume, kutakuwa na kanuni za maadili kama zitakavyoainishwa na sheria za nchi.		
	(4) Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye atakiuka masharti ya kanuni za maadili atapoteza sifa za kuendelea kuwa mjumbe.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Endapo suala la kumuondoa Mjumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi kwa kukiuka kanuni za maadili litajitokeza, Rais atateua Kamati itakayoundwa na:		
	(a) Jaji wa Mahakama ya (b) Rufani ambaye atakuwa Mwenyekiti;		
	(c) Kamishna wa Tume ya Haki za Binadamu;		
	(d) Mjumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji; na		
	(e) Mawakili, mmoja kutoka Tanganyika na mmoja kutoka Zanzibar watakaopendekezwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Chama cha Wanasheria Tanganyika na Chama cha Wanasheria Zanzibar,		
	na Kamati hiyo itafanya uchunguzi wa suala hilo na kisha kutoa mapendekezo kwa Rais.		
	(6) Endapo, baada ya uchunguzi, Kamati itapendekeza kuwa mjumbe huyo aondolewe madarakani, Rais atamuondoa mjumbe huyo madarakani na endapo Kamati itapendekeza kuwa mjumbe huyo asiondolewe, suala la kumuondoa mjumbe huyo litakoma.		
	(7) Kamati itaweka utaratibu wa kufanya uchunguzi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 193: Wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi.	(1) Tume Huru ya Uchaguzi itakuwa na wajibu wa: (a) kusimamia na kuendesha shughuli zote za uchaguzi wa Wabunge na Rais katika Jamhuri ya Muungano; (b) kusimamia na kuendesha kura ya maoni; (c) kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura katika Jamhuri ya Muungano; na (d) kugawa na kutangaza majimbo ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti kuhusu wajibu wa Tume Huru ya Uchaguzi na utekelezaji wa majukumu yake.	Sababu ya mapendekezo ni kuongeza uadilifu katika usimamizi wa masuala ya uchaguzi na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake bila woga wala upendeleo. Pia kuiwezesha Tume Huru ya Uchaguzi kuwa na uwezo wa kusimamia na kuendesha shughuli zote za uchaguzi na kura ya maoni kwa uhuru, uadilifu, uwajibikaji na uwazi.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Tume Huru ya Uchaguzi itakuwa pia na wajibu wa kutoa elimu ya mpiga kura wakati wa uchaguzi au kura ya maoni na kuratibu utoaji wa elimu ya uraia kuhusu uchaguzi na kusimamia asasi za kiraia, taasisi, jumuiya au makundi ya watu yatakaotoa elimu hiyo.		
	(3) Tume Huru ya Uchaguzi pia ina wajibu wa kuhakikisha kuwepo kwa:		
	(a) uhuru wa wananchi katika kutumia haki ya uchaguzi na◇ kuchaguliwa kupitia vyama vya siasa au mgombea huru;		
	(b) uwakilishi unaozingatia		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	jinsi;		
	(c) uwakilishi wa watu wenye ulemavu au mahitaji maalum katika jamii;		
	(d) uzingatiaji wa misingi ya upigaji kura wa mtu mmoja kura moja kwa kuzingatia uwakilishi wenye usawa; na		
	(e) uchaguzi huru na wa haki.		
	(4) Tume Huru ya Uchaguzi inaweza kutekeleza shughuli zake bila kujali kwamba kuna nafasi ya madaraka ya mjumbe iliyo wazi miongoni mwa wajumbe au kwamba Mjumbe yeyote hayupo, lakini kila uamuzi wa Tume Huru		

Live Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Uchaguzi ni lazima uungwe mkono na wajumbe walio wengi kati ya idadi ya Wajumbe wote wa Tume Huru ya Uchaguzi.		
	(5) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, Tume Huru ya Uchaguzi haitalazimika kufuata amri, maagizo au maoni ya mtu yeyote, mamlaka yoyote ya Serikali, chama cha siasa, taasisi au asasi yoyote.		
	(6) Katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba hii, Tume Huru ya Uchaguzi itashauriana mara kwa mara na Tume ya Uchaguzi ya Tanganyika na Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(7) Itakuwa ni marufuku kwa watu wanaohusika na uchaguzi kujiunga na chama chochote cha siasa, isipokuwa tu kwamba kila mmoja wao atakuwa na haki ya kupiga kura katika uchaguzi au kura ya maoni.		
	(8) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (7), watu wanaohusika na uchaguzi au kura ya maoni ni-		
	(a) Mwenyekiti wa Tume;		
	(b) Makamu Mwenyekiti wa Tume;		
	(c) Wajumbe wote wa Tume;		
	(d) Mkurugenzi wa Uchaguzi pamoja na watumishi wote		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wa Tume; na		
	(e) wasimamizi wote wa uchaguzi.		
Ibara ya 194: Malalamiko kuhusu Uchaguzi.	(1) Tume Huru ya Uchaguzi itasimamia na kutatua mapema iwezekanavyo malalamiko yanayohusu kuteuliwa kwa mgombea katika uchaguzi.	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya kufungua kesi za malalamiko kuhusu uchaguzi.	Sababu za mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa wananchi kuwasilisha malalamiko yao kuhusu uchaguzi na kutafutiwa ufumbuzi kwenye Tume au Mahakama ili haki ipatikane. Utaratibu huu pia unaupa uchaguzi uhalali kwa kuiwezesha Mahakama, pindi pakiwa na shaka, kuthibitisha matokeo ya uchaguzi baada ya kuridhika kuwa uchaguzi huo ulikuwa ni huru na haki.
	(2) Kesi za malalamiko kuhusu uchaguzi wa Wabunge zitafunguliwa Mahakama Kuu mapema iwezekanavyo baada ya Tume Huru ya Uchaguzi kutangaza matokeo na kwa vyovyote vile si zaidi ya muda ulioainishwa katika sheria za nchi.		
(b) Mkurugenzi wa Uchaguzi			

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 195: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Uchaguzi.	(1) Kutakuwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mkurugenzi wa Uchaguzi na sifa za kuteuliwa kwake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo wa Tume za Uchaguzi kuwa na Mkurugenzi ambaye ndiye Mtendaji Mkuu anayesimamia shughuli za kila siku.
	(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa na sifa zifuatazo:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa na angalau mmoja kati ya wazazi wake ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu, na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii;		
	(c) awe ni mtu ambaye		

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha kisiasa; (d) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi; na (e) awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu.		
Ibara ya 196: Majukumu ya Mkurugenzi wa Uchaguzi.	(1) Mkurugenzi wa Uchaguzi atakuwa ndiye msimamizi na mtekelezaji mkuu wa majukumu ya kila siku ya Tume Huru ya Uchaguzi kuhusiana na masuala ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya majukumu ya Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba wa kuanisha majukumu ya Mkurugenzi wa Tume Huru ya Uchaguzi ambaye ndiye

Final Version
www.iance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	uchaguzi, uandikishaji wa wapiga kura na uendeshaji wa kura ya maoni.	ndiye Mtendaji Mkuu wa Tume.	Mtendaji Mkuu wake.
	(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kufuata utaratibu ulioainishwa na sheria za nchi kuhusu masuala ya uchaguzi na kura ya maoni.		
	(3) Mkurugenzi wa Uchaguzi atatekeleza majukumu yake kwa kusaidiwa na watendaji ambao ni watumishi wa umma kwa kadri ya idadi inayohitajika.		
	(4) Katika kutekeleza majukumu yake, Mkurugenzi wa Uchaguzi atawajibika kwa Tume Huru ya Uchaguzi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SEHEMU YA TATU: USAJILI NA USIMAMIZI WA VYAMA VYA SIASA			
(a) Vyama vya Siasa			
Ibara ya 197: Usajili wa Vyama vya Siasa.	(1) Chama cha siasa kinaweza kufanya shughuli za siasa endapo kitasajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba masharti na makatazo kuhusu usajili wa vyama vya siasa.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua jukumu kubwa la vyama vya siasa na kujenga utashi wa kisiasa katika kutwaa uongozi wa nchi. Hivyo basi, ni muhimu visajiliwe kikatiba na kuhakikisha vina muelekeo na muonekano wa kitaifa vikisimamia na kulinda misingi ya kidemokrasia ya utawala wa nchi. Aidha, Ibara hii inampa Msajili wa Vyama vya Siasa nguvu za kikatiba kuweza kuendelea kufuatilia iwapo chama kinafuata makatazo yaliyotajwa katika sehemu hii ya Katiba.
	(2) Haitakuwa halali kwa chama chochote cha siasa kusajiliwa ambacho kutokana na Katiba au sera yake -		
	(a) kinakusudia kukuza au kupigania maslahi ya -		
	(i) imani au kundi lolote la dini;		
	(ii) kundi lolote la kikabila,		

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	pahala watu watokeapo, rangi au jinsi;		
	(iii) eneo fulani tu katika sehemu yoyote ya Jamhuri ya Muungano;		
	(b) kinapigania kuvunjwa kwa Jamhuri ya Muungano;		
	(c) kinakubali au kupigania matumizi ya nguvu au mapambano kama njia za kufikia malengo yake ya kisiasa;		
	(d) kinapigania au kinakusudia kuendesha shughuli zake za kisiasa katika sehemu moja tu ya Jamhuri ya		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano; au		
	(e) hakiruhusu uongozi wake kuchaguliwa kwa vipindi na kwa njia za kidemokrasia.		
	(3) Bila ya kuathiri sheria za nchi zinazohusika ni marufuku kwa mtu yeyote kulazimishwa kujiunga na chama chochote au kwa chama cha siasa kukataliwa kusajiliwa kwa sababu tu ya itikadi au falsafa.		
	(4) Bunge linaweza kutunga sheria inayoweka masharti yatakayohakikisha kuwa vyama vya siasa vinazingatia mipaka na vigezo vilivyowekwa na masharti ya ibara ndogo ya (2) kuhusu uhuru na haki ya watu		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kushirikiana na kujumuika.		
	(5) Mambo yote yanayohusu uandikishaji na uendeshaji wa vyama vya siasa nchini yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
	(b) Msajili wa Vyama vya Siasa		
Ibara ya 198: Uteuzi wa Msajili wa Vyama vya Siasa.	(1) Kutakuwa na Msajili wa Vyama vya Siasa atakayeteuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma na kuthibitishwa na Bunge.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa na kuweka utaratibu wa upatikanaji wake.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua nafasi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ambaye ni mlezi na msimamizi wa vyama vya siasa mwenye jukumu la kuhakikisha kuwa vyama hivyo vinatii Katiba na kufuata misingi ya kidemokrasia katika uongozi wake na uhusiano wake kwa umma.
	(2) Msajili wa Vyama vya Siasa atakuwa na sifa zifuatazo: (a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) awe ni mtu mwaminifu, mwadilifu na mwenye mwenendo usiotiliwa shaka na jamii; (c) awe ni mtu ambaye hajawahi kushika nafasi ya madaraka yoyote katika chama cha siasa; na (d) awe na shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa kwa mujibu wa sheria za nchi.		
Ibara ya 199: Wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa.	(1) Msajili wa Vyama vya Siasa atakuwa na wajibu wa: (a) kusimamia na kuratibu uandikishaji na shughuli za vyama vya siasa kwa	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba wajibu wa Msajili wa Vyama vya Siasa.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kuwa Vyama vya siasa ni taasisi za wananchi wenye malengo yanayofanana. Hivyo basi ni lazima shughuli zake, ikiwa ni pamoja na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mujibu wa masharti ya Katiba na sheria za nchi;		matumizi ya fedha ambazo zinatokana na ruzuku ya Serikali, michango ya wanachama wao na wahisani na hivyo kupaswa kusimamiwa na Msajili wa Vyama vya Siasa na umma kufahamishwa.
	(b) kutayarisha na kuchapisha taarifa za kila mwaka kuhusu ripoti za ukaguzi wa fedha kwa kila chama cha siasa; na		
	(c) kusimamia fedha za vyama vya siasa.		
	(2) Msajili wa Vyama vya Siasa atatekeleza majukumu yake kwa kufuata utaratibu ulioainishwa na sheria za nchi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA KUMI NA TATU **TAASISI ZA UWAJIBIKAJI**			
SEHEMU YA KWANZA: TUME YA MAADILI YA UONGOZI NA UWAJIBIKAJI			
Ibara ya 200: Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.	(1) Kutakuwa na Tume ambayo itaitwa "Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji" itakuwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiozidi saba.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji kuwa chombo cha kusimamia maadili ya uongozi na uwajibikaji wao.	Sababu za mapendekezo hayo ni kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka kuwepo kwa chombo cha kikatiba kitakachokuwa na nguvu ya kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma. Hii ni kwa sababu walidai maadili ya viongozi wa umma yameshuka kwa kiwango kikubwa na hatua za uwajibishwaji hazichukuliwi inavyostahili kwa viongozi wanaovunja miiko na maadili.Sababu nyingine ni kuwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi iliyopo haina uwezo na mamlaka ya kuchukua hatua zinazostahili kwa viongozi wanaovunja na kukiuka maadili. Uzoefu unaonyesha kwamba
	(2) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi.		
	(3) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume utafanywa kwa kuzingatia msingi kwamba endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande mmoja wa Jamhuri		

Final Draft
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano. (4) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watashika madaraka baada ya kuthibitishwa na Bunge. (5) Sifa za Mwenyekiti wa Tume zitakuwa kama ifuatavyo: (a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano; (b) mtu mwenye shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi; (c) mtu mwenye uzoefu katika utumishi wa umma kwa		utaratibu wa kuwa na Tume kama hii kikatiba upo katika nchi mbalimbali duniani. Kwa mfano, Katiba ya Ufilipino ya Mwaka 1987 iliweka misingi ya maadili ya viongozi wa umma kama njia ya kuzuia rushwa na matumizi mabaya ya madaraka yaliyokuwa yamekithiri kwa takriban miongo miwili ya utawala wa Ferdinand Marcos ili kuwafanya viongozi waliokuwepo kufanya kazi kwa maslahi ya wananchi. Katiba ya Afrika Kusini ya mwaka 1994, iliweka misingi ya maadili na miiko ya viongozi iliyowafanya viongozi wa umma kuwajibika katika kuwatumikia wananchi waliokuwa na matumaini makubwa kwa Serikali kusaidia kuboresha maisha yao baada ya miongo kadhaa chini ya Serikali ya kibaguzi.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kipindi kisichopungua miaka kumi na tano;		
	(d) mtu mwenye heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii; na		
	(e) awe ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu.		
	(6) Sifa za Makamu Mwenyekiti zitakuwa kama zilivyoainishwa katika ibara ndogo ya (5).		
Ibara ya 201: Uteuzi na	(1) Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba utaratibu na sifa za	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimu wa kuwa na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Sifa za Wajumbe.	watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati Maalum ya Uteuzi.	uteuzi wa mjumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.	Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji wenye heshima na wanaoaminiwa na wananchi kutokana na dhamana kubwa waliyonayo ya kuwasimamia miiko na maadili ya viongozi wa umma.
	(2) Sifa za Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji, zitakuwa kama ifuatavyo:		
	(b) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		
	(c) mtu mwenye shahada ya chuo cha elimu ya juu kinachotambulika kwa mujibu wa sheria za nchi;		
	(d) mtu mwenye uzoefu kwenye uongozi kwa kipindi kisichopungua miaka kumi;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) mtu mwenye heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii.		
Ibara ya 202: Kamati Maalum ya Uteuzi.	Kutakuwa na Kamati Maalum ya Uteuzi ambayo itakuwa na Wajumbe wafuatao:	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kuweka vyombo vya kikatiba vyenye mamlaka ya kufanya uteuzi wa Wajumbe wa Tume mbalimbali zitakazoshughulikia masuala ya maadili ya Viongozi na watumishi wa Umma na uwajibikaji wao. Utaratibu huu utajenga imani kwa wananchi kwamba uwepo wa vyombo hivi kutaimarisha utendaji na uwajibika.
	(a) Jaji Mkuu wa Mahakama ya Jamhuri ya Muungano;		
	(b) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;		
	(c) Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanganyika;		
	(d) Jaji wa Mahakama Kuu ya Zanzibar;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(e) Spika wa Bunge la Tanganyika;		
	(f) Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar; na		
	(g) Mwanasheria Mkuu wa Serikali.		
Ibara ya 203: Majukumu ya Jumla ya Tume.	(1) Majukumu ya jumla ya Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji yatakuwa ni kufuatilia na kuchunguza tabia na mwenendo wa viongozi wa umma na watumishi wa umma kwa madhumuni ya kusimamia na kuhakikisha kuwa Maadili na Miiko ya Uongozi wa Umma inazingatiwa, inalindwa na kuheshimiwa katika utumishi wa Serikali, Bunge, Mahakama, taasisi	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu ya jumla ya Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ambao walipendekeza kuundwa kwa chombo cha kikatiba chenye mamlaka na uwezo wa kusimamia na kuwawajibisha watumishi na viongozi wanaokiuka maadili na kuvunja miiko ya uongozi. Sababu nyingine ni kuzingatia malalamiko ya wananchi kwamba maadili ya viongozi yameporomoka na

Final Version
www.mlanet.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na idara nyingine zote za umma.		uwajibikaji wao umeshuka. Hivyo wananchi wengi walipendekeza kurejeshwa kwa miiko ya uongozi iliyokuwemo katika Azimio la Arusha. Pia, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi iliyopo sasa haina uwezo na mamlaka ya kuchukua hatua zinazostahili kwa Viongozi wanaovunja na kukiuka maadili.
	(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya ibara ndogo ya (1), majukumu mahsusi ya Tume yatakuwa ni:		
	(a) kusimamia maadili na uwajibikaji katika utumishi wa umma;		
	(b) kufanya upekuzi kwa kushirikiana na taasisi nyingine;		
	(c) kuchunguza tabia na mwenendo wa mtumishi au kiongozi wa umma na kuchukua hatua pale inapostahili, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha katika vyombo vya sheria		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	watumishi watakaobainika kukiuka maadili na miiko ya uongozi;		
	(d) kusimamia sheria za nchi kuhusu maadili na uwajibikaji wa viongozi wa umma na watumishi wa umma;		
	(e) kutoa ushauri juu ya masuala ya ubadhirifu wa fedha kwa mamlaka husika;		
	(f) kufanya upekuzi kwa kiongozi wa umma anayependekwa kabla ya kuingia madarakani;		
	(g) kutoa elimu kwa umma		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuhusu maadili na miiko ya viongozi wa umma;		
	(h) kufanya uchunguzi kwa maamuzi yake yenyewe, au baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa mtu yeyote, kutokana na kutenda au kutokutenda kwa kiongozi wa umma au mtumishi yeyote wa umma, au wakala wa serikali, ikiwa kitendo kilichotendwa au kutokutendwa ni kinyume cha maadili ya umma;		
	(i) kumwelekeza, baada ya kupata malalamiko au itakapoona inafaa, kiongozi wa umma au mtumishi wa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	umma, taasisi au wakala wa serikali au chombo chochote cha umma kufanya jambo lolote linalotakiwa na sheria, kuacha, kuzuia au kusahihisha utendaji mbaya au usio sahihi wa majukumu yake;		
	(j) kutoa ushauri kuhusu kuchukuliwa hatua kiongozi wa umma au mtumishi wa umma;		
	(k) kumwelekeza kiongozi wa umma au mtumishi wa umma, kwa mujibu wa sheria za nchi, kutoa nyaraka zinazohusiana na matumizi ya ofisi, matumizi		

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya fedha au mali za umma, au kutoa taarifa ya matumizi mabaya kwa Tume, kwa hatua stahiki;		
	(l) kuomba msaada au taarifa muhimu kutoka kwa mamlaka yoyote ya serikali au binafsi katika kutekeleza wajibu wake, na kukagua kumbukumbu muhimu na nyaraka husika;		
	(m) kwa kuzingatia sheria, kutangaza kwa umma, mambo yote yanayohusiana na uchunguzi uliofanywa na Tume, iwapo mazingira yanaruhusu;		

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(n) kuchunguza jambo au mazingira yoyote yanayokiuka au kusababisha ukiukaji wa maadili; na		
	(o) kuandaa kanuni za taratibu na matumizi ya mamlaka au utekelezaji wa kazi na majukumu ya Tume kama itakavyoelekezwa na sheria za nchi.		
Ibara ya 204: Muda wa kukaa madarakani kwa Mjumbe wa Tume.	(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wengine wote kila mmoja atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu au kipindi kingine cha chini ya miaka mitatu kama itakavyoainishwa katika barua ya uteuzi, ikizingatiwa kwamba uteuzi wa	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa kukaa katika madaraka kwa Wajumbe wa Tume na masharti ya utendaji wa kazi zao.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji wanabadilishwa bila kuathiri utendaji wa Tume na kuwa na mwendelezo wa uhakika wa maamuzi na kuwapa uzoefu Wajumbe wapya.

Draft Version
www.kuze.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Wajumbe wa Tume utafanywa kwa namna ambayo Wajumbe wa Tume hawataanza au kumaliza muda wao kwa wakati mmoja. (2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara ndogo ya (1), Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa.		
	(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume wakati watakapokuwa madarakani hawataruhusiwa kuteuliwa, kuchaguliwa au kushika nafasi ya madaraka nyingine yoyote.		
Ibara ya 205: Kuondolewa Madarakani	(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anaweza	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba	Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kumuondoa

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kwa Mjumbe wa Tume.	kuondolewa madarakani kwa: (a) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya maradhi; (b) kukiuka kanuni za maadili ya uongozi wa umma; (c) kukiuka Miiko ya Uongozi wa Umma; (d) kukosa uweledi; au (e) utovu wa nidhamu. (2) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma au malalamiko ya mtu yeyote kwa Tume ya	wa kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume anapokosa sifa za kuendelea kushika nafasi hiyo.	Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Mjumbe wa Tume ambaye ameshindwa kutekeleza majukumu yake au amekosa sifa ili kulinda heshima ya Tume na imani ya wananchi. Hata hivyo, ni vyema kuwepo kwa Tume ya Uchunguzi ili kulinda haki za msingi za kusikilizwa kwa Wajumbe na Tume ya Uchunguzi na kuonyesha haki imetendeka na kuwalinda Wajumbe wasiondolewe kwa sababu za hila

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Utumishi wa Umma, kwa masharti kwamba:		
	(a) mapendekezo au malalamiko yawe kwa maandishi; na		
	(b) yaainishe masuala yanayopendekezwa au yanayolalamikiwa.		
	(3) Baada ya kupokea mapendekezo au malalamiko, Rais ataunda Kamati Maalum itakayofanya uchunguzi kuhusu malalamiko hayo.		
	(4) Baada ya kukamilisha uchunguzi, Kamati Maalum itapeleka mapendekezo kwa Rais kwa uamuzi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Masuala yanayohusu idadi na sifa za wajumbe, muda na utaratibu wa kufanya kazi wa Kamati Maalum yatakuwa kama itakavyoamuliwa na Rais.		
Ibara ya 206: Uhuru wa Tume.	(1) Tume itakuwa huru na kwa mantiki hiyo haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote katika utekelezaji wa majukumu yake.	Madhumuni ya Ibara hii ni kutambua uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wananchi ya kutaka Tume ifanye kazi zake kwa uhuru, uaminifu, uadilifu na bila woga au upendeleo. Sababu nyingine ni kujenga imani kwa wananchi kuwa maamuzi yatakayofaywa na Tume hayatokani na maelekezo, shinikizo au matakwa ya mtu, kikundi cha watu au chombo chochote.
	(2) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu:		
	(a) utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Tume;		
	(b) utayarishaji na utoaji wa taarifa za Tume;		
	(c) utaratibu wa utoaji wa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mapendekezo na maamuzi ya Tume; (d) watumishi wa Tume; na (e) masuala mengine muhimu yanayoihusu Tume.		
Ibara ya 207: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali.	Serikali itahakikisha kuwa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji inapatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu ya kutosha kadri hali itakavyoruhusu ili kutekeleza kazi na wajibu wake kwa ufanisi.	Lengo la Ibara hii ni kuweka wajibu wa kikatiba kwa Serikali kuhakikisha Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji inapatiwa nyenzo na rasilmali za kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikishia Tume ya Maadili upatikanaji wa fedha, nyenzo na rasilmali watu wa kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Hii pia itaepusha uwezekano wa Tume hii kunyimwa fedha, nyenzo na rasilmali watu inazozihitaji kwa lengo la kudhoofisha na kukwamisha shughuli zake ambazo ni pamoja na kuwachunguza na kuwachukulia hatua viongozi na watumishi wa umma.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SEHEMU YA PILI: TUME YA HAKI ZA BINADAMU			
Ibara ya 208: Tume ya Haki za Binadamu.	(1) Kutakuwa na Tume itakayoitwa "Tume ya Haki za Binadamu" itakayokuwa na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wasiozidi saba. (2) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu watateuliwa na Rais baada ya kupendekezwa na Kamati ya Uteuzi. (3) Uteuzi wa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu utafanywa kwa kuzingatia msingi kwamba endapo Mwenyekiti atateuliwa kutoka	Lengo ni kuanzisha kikatiba Tume ya Haki za Binadamu yenye dhamana ya kusimamia masuala ya haki za binadamu. Pia kujenga tabia na mazoea ya wananchi kutambua na kutetea haki zao.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliomo katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inayoanzisha Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora. Sababu nyingine ni kuzingatia maoni ya wananchi walio wengi waliotaka kuwepo kwa utaratibu utakaokuza, kuhifadhi na kulinda haki za binadamu. Aidha, mapendekezo ya Ibara hii ni kutilia nguvu utekelezaji wa mikataba au makubaliano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo.

Kiolezo cha www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano, basi Makamu Mwenyekiti atateuliwa kutoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano.		
	(4) Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti watashika madaraka baada ya kuthibitishwa na Bunge.		
	(5) Sifa za Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Tume zitakuwa kama ifuatavyo:		
	(a) awe ni raia wa kuzaliwa wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) mtu mwenye shahada ya sheria kutoka chuo cha elimu ya juu kinachotambuliwa na		

Trial Version
www.vuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria za nchi;		
	(c) mtu mwenye kuheshimu haki za binadamu;		
	(d) mtu mwenye uzoefu wa utumishi wa umma, upeo mkubwa katika mambo ya haki za binadamu, utawala na mambo ya jamii kwa kipindi kisichopungua miaka kumi; na		
	(e) mtu mwenye heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii.		
	(6) Sifa za Makamishna wa Tume zitakuwa kama ifuatavyo:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) awe ni raia wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) mtu mwenye kuheshimu haki za binadamu;		
	(c) mtu mwenye uzoefu usiopungua miaka kumi ikiwa angalau ana sifa ya masuala ya sheria, haki za binadamu, utawala, siasa na mambo ya jamii;		
	(d) mtu mwenye heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na tabia au mwenendo wenye kutiliwa shaka na jamii;		
	(e) mtu mwenye shahada ya chuo cha elimu ya juu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kinachotambuliwa na sheria za nchi.		
Ibara ya 209: Kamati ya Uteuzi.	(1) Kutakuwa na Kamati ya Uteuzi wa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu itakayokuwa na wajumbe wafuatao:	Kuweka kikatiba Kamati ya Uteuzi wa Wajumbe wa Tume ya Haki za Binadamu.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutekeleza utaratibu na matakwa ya mikataba ya kimataifa kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu wapendekezwe na Kamati Maalum ya Uteuzi. Utaratibu huu ndio uliomo katika Sheria ya Tume ya Haki za Binaadamu na Utawala Bora.
	(d) Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa ni Mwenyekiti;		
	(e) Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;		
	(f) Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(g) Spika wa Bunge la Tanganyika;		
	(h) Jaji Mkuu wa Tanganyika;		
	(i) Jaji Mkuu wa Zanzibar; na		
	(j) Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji.		
	(2) Katibu wa Tume ya Haki za Binadamu atakuwa Katibu wa Kamati ya Uteuzi.		
	(3) Kamati ya Uteuzi itakuwa na jukumu la kupokea na kuchambua majina ya watu walioomba na waliopendekezwa kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu kwa mujibu wa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utaratibu utakaoainishwa na sheria za nchi.		
	(4) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (3), Kamati ya Uteuzi mara baada ya kuchambua majina ya watu walioomba na waliopendekezwa kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, itapendekeza kwa Rais majina ya watu wanaofaa kuteuliwa kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu.		
	(5) Rais atateua Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu kutoka miongoni mwa majina yaliyowasilishwa na Kamati ya Uteuzi na atawasilisha majina hayo Bungeni kwa ajili ya		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuthibitishwa na Bunge.		
	(6) Kwa madhumuni ya Ibara hii, asasi za kiraia na zisizo za kiserikali zinaweza kupendekeza majina ya watu wanaoweza kuteuliwa kuwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu.		
	(7) Kutakuwa na Sekretarieti ya Tume ya Haki za Binadamu itakayoongozwa na Katibu atakayeteuliwa na Rais kutokana na orodha ya majina ya watu watatu waliopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma.		
	(8) Bunge litatunga sheria ambayo pamoja na mambo mengine		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	itaweka masharti kuhusu kiapo cha Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu.		
Ibara ya 210: Kazi na Majukumu ya Tume.	(1) Kazi na majukumu ya Tume ya Haki za Binadamu yatakuwa kama ifuatavyo: (a) kuhamasisha hifadhi ya haki za binadamu na wajibu kwa jamii kwa mujibu wa katiba na sheria za nchi; (b) kupokea malalamiko juu ya uvunjaji wa haki za binadamu kwa ujumla; (c) kuchunguza uvunjaji wa haki za binadamu na ukiukwaji wa misingi ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu na mamlaka maalum ya Tume ya Haki za Binadamu.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza majukumu ya Tume za Haki za Binadamu yaliyomo katika mikataba ya kimataifa, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria ya Haki za Binadamu na Utawala Bora ya mwaka 2001. Sababu nyingine ni kuhakikisha kwamba haki za binadamu zinapewa kipaumbele katika shughuli zote za serikali, vyombo vya umma na sekta binafsi.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utawala bora;		
	(d) kufanya utafiti na kutoa elimu kwa umma kuhusu haki za binadamu na utawala bora;		
	(e) kufungua mashauri Mahakamani ili kuzuia vitendo vya uvunjaji wa haki za binadamu au kurekebisha haki inayotokana na uvunjwaji huo wa haki za binadamu au ukiukwaji wa misingi ya utawala bora;		
	(f) kuchunguza mwenendo wa mtu yeyote anayehusika au taasisi yoyote inayohusika na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	masharti ya Ibara hii katika utekelezaji wa kawaida wa madaraka ya kazi au majukumu yake au utekelezaji unaokiuka madaraka hayo;		
	(g) kutoa ushauri kwa Serikali na vyombo vingine vya umma na vya sekta binafsi kuhusu haki za binadamu na utawala bora;		
	(h) kuchukua hatua zinazostahiki kwa ajili ya kukuza na kuendeleza usuluhishi miongoni mwa watu na taasisi mbalimbali wanaofika au kufikishwa mbele ya Tume;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i) kutembelea magereza, vituo vya polisi au mahali pengine popote ambapo mtu au watu wanazuiliwa kwa madhumuni ya kutathmini na kukagua hali za watu wanaozuiliwa katika sehemu hizo na kutoa mapendekezo yatakayowezesha kurekebisha kasoro zilizopo;		
	(j) kutoa mapendekezo yanayohusiana na sheria iliyokwishatungwa au inayokusudiwa kutungwa, kanuni, au mambo ya kiutawala ili kuhakikisha zinakidhi viwango vya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kimataifa na kikanda vya haki za binadamu;		
	(k) kuwasilisha taarifa na maoni huru kwenye vyombo na taasisi za kimataifa na za kikanda kuhusu hali ya haki za binadamu nchini pale inapobidi;		
	(l) kuihamasisha Serikali kutia saini na kuridhia mikataba au makubaliano ya kimataifa yanayohusu haki za binadamu, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa haki za binadamu zilizomo kwa mujibu wa Katiba hii, Katiba za Nchi Washirika,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria za nchi na mikataba au makubaliano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano inawajibika nayo; na		
	(m) kwa kupitia Serikalini, kushirikiana na wawakilishi wa Umoja wa Mataifa, Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Umoja wa Nchi za Afrika, Jumuiya ya Madola na taasisi nyingine zenye mahusiano baina yao, miongoni mwao au ya kikanda na taasisi za nchi nyingine katika maeneo ya hifadhi na ukuzaji wa haki za binadamu.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Tume ya Haki za Binadamu itakuwa na mamlaka maalum kama ifuatavyo:		
	(a) kumuita mtu yeyote mbele ya Tume na kumtaka awasilishe mbele yake nyaraka zozote, kumbukumbu au kitu chochote kilicho katika mamlaka yake kinachohusiana na jambo linalochunguzwa na Tume;		
	(b) kumtaka mtu yeyote kutoa taarifa anayoifahamu kwa Tume juu ya jambo linalochunguzwa na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Tume; (c) kusababisha mtu yeyote anayekiuka maagizo au taratibu za Tume kufunguliwa mashtaka ya jinai mahakamani.		
Ibara ya 211: Muda wa kukaa madarakani kwa Kamishna wa Tume.	(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume kila mmoja atashika madaraka yake kwa kipindi cha miaka mitatu au kipindi kingine cha chini ya miaka mitatu kama itakavyoainishwa katika barua ya uteuzi, ikizingatiwa kwamba uteuzi wa Makamishna wa Tume utafanywa kwa namna ambayo hawataanza au kumaliza muda wao kwa wakati mmoja. (2) Bila ya kuathiri masharti ya ibara	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba muda wa kukaa madarakani kwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume na masharti ya utendaji wa kazi zao.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu wanapatikana wapya bila ya kuathiri utendaji na ufanisi wa Tume kwa kuwa na muendelezo wa uzoefu ndani ya Tume.

Final Version
www.nuane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ndogo ya (1), Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anaweza kuteuliwa tena kwa kipindi kingine kimoja tu cha miaka mitatu au vinginevyo vyovyote itakavyokuwa.		
	(3) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Kamishna wa Tume wakati watakapokuwa madarakani hawataruhusiwa kuteuliwa, kuchaguliwa au kushika nafasi ya madaraka nyingine.		
Ibara ya 212: Kuondolewa Madarakani kwa Kamishna wa Tume.	(1) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kwa:	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kumuondoa madarakani Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anapokosa sifa za	Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka misingi madhubuti ya kikatiba ambayo kwa utekelezaji wake itawahakikishia Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume kufanya kazi zao kwa uaminifu,
	(a) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza		

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) majukumu yake kwa sababu ya maradhi;	kuendelea kushika nafasi hiyo.	uadilifu, bila upendeleo na kufanya maamuzi sahihi bila woga wa kuondolewa kwenye Tume kwa hila. Aidha, utaratibu huu unaweka mashart ya kuwaondoa kwa misingi ya haki wanaposhindwa kufanya kazi au kukiuka kanuni za maadili na miiko ya uongozi. Hatua hii italinda heshima ya Tume na Makamishna wake.
	(c) kukiuka kanuni za maadili ya uongozi wa umma;		
	(d) kukiuka Miiko ya Uongozi wa Umma;		
	(e) kukosa uweledi; au		
	(f) utovu wa nidhamu.		
	(2) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti au Kamishna wa Tume anaweza kuondolewa madarakani kutokana na mapendekezo ya Tume ya Utumishi wa Umma au kutokana na malalamiko ya mtu yeyote kwa Tume ya Utumishi wa Umma, kwa masharti kwamba:		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(a) mapendekezo au malalamiko hayo yawe kwa maandishi; na		
	(b) yaainishe masuala yanayopendekezwa au yanayolalamikiwa.		
	(3) Baada ya kupokea mapendekezo au malalamiko, Tume ya Utumishi wa Umma itaunda Kamati Maalum kufanya uchunguzi kuhusu mapendekezo au malalamiko hayo.		
	(4) Baada ya kupokea ripoti ya Kamati Maalum, Tume ya Utumishi wa Umma itapeleka mapendekezo ya Kamati Maalum kwa Rais kwa uamuzi.		

Trial version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Rais atachukua hatua kama atakavyoshauriwa na Kamati Maalum.		
	(6) Masuala yanayohusu idadi na sifa za wajumbe, muda na utaratibu wa kufanya kazi wa Kamati Maalum yatakuwa kama itakavyoamuliwa na Tume ya Utumishi wa Umma.		
Ibara ya 213: Uhuru wa Tume.	(1) Tume itakuwa huru na haitaingiliwa na mtu au mamlaka yoyote katika utekelezaji wa majukumu yake.	Madhumuni ya Ibara hii ni kubainisha kikatiba uwepo wa uhuru wa Tume katika utekelezaji wa majukumu yake.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuifanya Tume ifanye kazi zake kwa uhuru na kuwawezesha Makamishna watekeleze majukumu yao kwa uaminifu, uadilifu na bila ya woga wa upendeleo. Aidha, mapendekezo haya yanajenga imani kwa wananchi kuwa maamuzi yatakayofaywa na Tume hayatokani
	(2) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu:		
	(a) utaratibu wa utekelezaji wa majukumu ya Tume;		

Final Version
www.inuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) utayarishaji na utoaji wa taarifa za Tume;		na maelekezo, shinikizo au matakwa ya mtu, kikundi cha watu au chombo chochote. Pia, kuwepo kwa uhuru wa Tume, kutaiwezesha Tume kufanya kazi zake kwa ufanisi na matokeo yake masuala ya Haki za Binadamu yataimarika.
	(c) utaratibu wa utoaji wa mapendekezo na maamuzi ya Tume;		
	(d) watumishi wa Tume; na		
	(e) masuala mengine muhimu yanayoihusu Tume.		
Ibara ya 214: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali.	Serikali itahakikisha kuwa Tume ya Haki za Binadamu inapatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu ya kutosha kadri hali itakavyoruhusu ili kutekeleza kazi na wajibu wake kwa ufanisi.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba wajibu wa Serikali wa kuhakikisha kuwa Tume ya Haki za Binadamu inapatiwa fedha, nyenzo na rasilmali watu ya kutosha ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi.	Sababu za mapendekezo haya ni kuifanya Tume kuwa na uhakika wa kupata fedha, nyenzo na rasilmali watu ya kutosha kutimiza wajibu wake kwa ufanisi mkubwa. Hii pia kutaifanya Tume kutokwamishwa kwa makusudi katika shughuli zake ambazo ni pamoja na kuwachunguza viongozi na watumishi wa umma

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ambao wamekiuka au kuvunja haki za binadamu katika utekelezaji wa kazi na majukumu yao. Sababu nyingine ni kuhakikisha kwamba shughuli za Tume zinapewa kipaumbele stahiki katika bajeti ya Serikali.
SEHEMU YA TATU: MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI			
Ibara ya 215: Uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	(1) Kutakuwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye atateuliwa na Rais na kuthibitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano. (2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atashika nafasi ya madaraka yake baada ya kuapishwa na Rais.	Lengo ni kuanzisha nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuweka kikatiba utaratibu wa uteuzi wake.	Sababu za mapendekezo haya ni kumlinda Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kikatiba na kuendeleza utaratibu unaotumika nchi nyingi duniani ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kama ilivyo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Sababu nyingine ni kuhakikisha kuwa hesabu na matumizi ya Serikali yanasimamiwa na kudhibitiwa na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			chombo ambacho kimepewa dhamana kikatiba.
Ibara ya 216: Sifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atateuliwa kutoka katika orodha ya majina matatu ya watumishi wa umma yaliyopendekezwa na Tume ya Utumishi wa Umma.	Lengo ni kuweka kikatiba sifa na utaratibu wa uteuzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakisha kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni mtu mwenye sifa za kitaaluma, weledi, uzoefu wa kutosha na pia mwenye maadili. Ofisi hii ni muhimu sana katika usimamizi wa matumizi ya Serikali na ina wajibu wa kuzuia na kuchukua hatua dhidi ya ubadhirifu, ufujaji na wizi wa fedha na rasilmali za Serikali.
	(2) Mtu anaweza kuteuliwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikiwa ana sifa zifuatazo:		
	(a) ni raia wa Jamhuri ya Muungano;		
	(b) amefuzu mafunzo ya juu ya uhasibu na kusajiliwa na mamlaka husika;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) ana uzoefu usiopungua miaka kumi na tano katika masuala yanayohusu ukaguzi wa hesabu za Serikali; (d) ni mtu ambaye hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa lolote la jinai linalohusu kukosa uaminifu; na (e) ni mtu mwenye heshima, uweledi, uaminifu, uadilifu na asiye na mwenendo unaotiliwa shaka na jamii.		
Ibara ya 217: Kazi na Majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	(1) Kazi na majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yatakuwa ni: (a) kuhakikisha kwamba fedha	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba kazi, majukumu na uhuru wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kikatiba wadhifa wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo ni nafasi muhimu

Final Version
www.mlance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	zozote zinazokusudiwa kutolewa kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina matumizi yake yameidhinishwa na kwamba zitatolewa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, na iwapo atatosheka kwamba masharti hayo yatatekelezwa ipasavyo, basi ataidhinisha fedha hizo zitolewe; (b) kuhaki kisha kwamba fedha zote ambazo matumizi yake yameidhinishwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina au fedha ambazo matumizi yake yameidhinishwa na		sana katika utendaji wa Serikali. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kumlinda Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kumpa uhuru ili atekeleze majukumu yake bila hofu wala woga wa kuchukuliwa hatua na watu, taasisi anazozikagua na kuzichukulia hatua. Kujenga nidhamu ya kifedha katika matumizi ya Serikali.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria za nchi, na kwamba zimetumika kwa ajili ya shughuli zilizohusika na matumizi ya fedha hizo na matumizi hayo yamefanywa kwa kufuata idhini iliyotolewa kuhusu matumizi hayo;		
	(c) angalau mara moja kila mwaka, kufanya ukaguzi na kutoa taarifa kuhusu -		
	(i) hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano;		
	(ii) hesabu zinazosimamiwa na taasisi na wakala wa Serikali ya Jamhuri ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano;		
	(iii) hesabu za Mahakama ya Jamhuri ya Muungaano; na		
	(iv) hesabu za Bunge la Jamhuri ya Muungano.		
	(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa huru katika utekelezaji wa kazi na majukumu yake na hataingiliwa na mtu au mamlaka yoyote katika utekelezaji wa kazi zake.		
	(3) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au mtu yeyote aliyeruhusiwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa na haki ya		

Final version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuchunguza vitabu, kumbukumbu, hati nyinginezo zote zinazohusika na hesabu za aina yoyote iliyotajwa katika ibara ndogo ya (1).		
	(4) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayotoa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
	(5) Baada ya kupokea taarifa hiyo, Rais atawaagiza watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Bunge kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku saba tangu siku ile ulipoanza Mkutano huo, na iwapo Rais hatachukua		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwa Spika, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika, ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Bunge.		
	(6) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa pia na jukumu la kutekeleza kazi na shughuli nyingine, na atakuwa na madaraka mengine ya namna mbalimbali, kama itakavyoelezwa na sheria kuhusu hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, hesabu za vyombo vya umma au hesabu za mashirika.		
	(7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1), (3), (4) na (5) ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Ibara hii, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwingine yeyote au idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo hayo ya ibara hii ndogo hayataizuia Mahakama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au sivyo.		
	(8) Bunge linaweza kutunga sheria itakayosimamia, pamoja na mambo mengine, matumizi ya mamlaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.		
Ibara ya 218: Muda wa	(1) Muda wa kukaa madarakani kwa	Madhumuni ya Ibara hii ni	Sababu za mapendekezo haya ni

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kukaa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali utakuwa ni kipindi kimoja cha miaka saba mfululizo. (2) Bila ya kujali masharti ya ibara ndogo ya (1), Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kujiuzulu nafasi ya madaraka yake kwa kutoa taarifa ya siku thelathini kwa Rais.	kuweka kikatiba muda wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukaa madarakani ambao ni kipindi kimoja cha miaka saba mfululizo.	kumlinda kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili afanye kazi yake kwa uhuru akiwa na uhakika wa ajira yake. Utaratibu huu ndio unaotumika katika nchi nyingi duniani wa kumpa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kipindi kimoja cha muda maalum ili kuepuka athari za kuzoea na kuzoeleka na anaowakagua.
Ibara ya 219: Kuondolewa madarakani kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.	(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaweza kuondolewa madarakani kwa: (a) kutokuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu yake kwa sababu ya maradhi; (b) kukiuka kanuni za maadili	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba na sababu za kumuondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kabla ya kumaliza muda wake.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimu wa nafasi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na hivyo kutakiwa alindwe na asiondolewe madarakani isipokuwa kwa utaratibu maalum wa kikatiba. Hatua hii inalinda hadhi na heshima ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu

Trial Version www.iliane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya uongozi wa umma;		wa Hesabu za Serikali na Ofisi yake.
	(c) kukiuka Miiko ya Uongozi wa Umma;		
	(d) kukosa weledi; au		
	(e) utovu wa nidhamu.		
	(2) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hataweza kuondolewa kazini isipokuwa kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (3) na (4).		
	(3) Endapo Rais ataridhika kwamba suala la kumuondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali linahitaji kuchunguzwa:		
	(a) atateua Kamati Maalum		

Trial Version
www.riuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ambayo itakuwa na Mwenyekiti na wajumbe wengine wasiopungua wawili na angalau nusu ya wajumbe hao wawe ni Majaji au watu waliopata kuwa Majaji wa Mahakama ya Juu, Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu za Nchi Washirika;		
	(b) Kamati Maalum itachunguza shauri na kutoa taarifa kwa Rais na itamshauri Rais kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe madarakani au la.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(4) Endapo Kamati Maalum itamshauri Rais kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aondolewe madarakani, basi Rais atamuondoa madarakani.		
	(5) Wakati suala la kumuondoa madarakani Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali limepelekwa kwenye Kamati Maalum kwa ajili ya uchunguzi, Rais atamsimamisha kazi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (6) Rais atafuta uamuzi wa kumsimamisha kazi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali endapo Kamati Maalum itamshauri Rais kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za		

Trial version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Serikali asiondolewe madarakani.		
Ibara ya 220: Uwezeshaji wa Nyenzo na Rasilimali.	Serikali itahakikisha kuwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inapatiwa fedha, nyenzo na rasilimali watu ya kutosha ili kulinda uhuru wake katika kutekeleza kazi na majukumu yake kwa ufanisi.	Lengo ni kuweka kwenye Katiba wajibu wa Serikali wa kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili itekeleze kwa wakati na ufanisi.	Sababu za mapendekezo haya ni kumhakikishia kikatiba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupata fedha, nyenzo na rasilmali watu wa kutosha ili kuweza kusimamia matumizi ya bajeti ya Serikali. Wajibu huu ni muhimu na nyeti na hivyo utaratibu huu utaepusha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kukwamishwa kwa makusudi na kumfanya ashindwe kutimiza majukumu yake.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA KUMI NA NNE **MASHARTI KUHUSU FEDHA ZA JAMHURI YA MUUNGANO**			
(a) Mfuko Mkuu wa Hazina na Fedha za Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 221: Mfuko Mkuu wa Hazina.	Kutakuwa na Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano utakaoitwa "Mfuko Mkuu wa Hazina" ambamo fedha zote zitakazopatikana kwa njia mbalimbali zitawekwa, isipokuwa: (a) fedha ambazo zimetajwa katika sheria kuwa zitumike kwa shughuli maalum au ziwekwe katika mfuko mwingine kwa ajili ya	Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Mfuko Mkuu wa Hazina wa Jamhuri ya Muungano.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuwa na chombo kimoja kikuu cha kutunza fedha zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha mapendekezo haya ni kuondoa dhana kwa Wizara na Idara zinazokusanya kodi na maduhuli kudhani kwamba fedha hizo ni zao ila ni za umma na hapana budi kuwasilisha mapato hayo Hazina na kama kugaiwa basi mgao hufanyika

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	matumizi maalum; au		kwa maelekezo ya Bunge.
	(b) fedha ambazo kwa mujibu wa sheria za nchi, taasisi za Serikali zimeruhusiwa kukusanya na kubaki nazo kwa ajili ya kugharamia uendeshaji wa taasisi hizo.		
Ibara ya 222: Masharti ya kutoa Fedha za matumizi katika Mfuko Mkuu wa Hazina.	(1) Fedha zinaweza kutolewa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi, kwa kuzingatia masharti yafuatayo: (a) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa kuwa yatokane na fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina na idhini hiyo iwe imetolewa kwa mujibu wa Katiba hii au	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kuhusu matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina na kuhakikisha kuwa hazitolewi kinyume cha Katiba na sheria zilizotungwa na Bunge.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa usimamizi na udhibiti wa utoaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya Serikali. Aidha mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa fedha hii ambayo ni mali ya wananchi haitumiki bila ya utaratibu uliowekwa ili kuepuka ubadhirifu, ufujaji na wizi wa mapato ya fedha za Serikali.

Trial Version
www.kiuaca.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	sheria za nchi; na (b) fedha hizo ziwe kwa ajili ya matumizi ambayo yameidhinishwa ama na Sheria ya Matumizi ya Serikali iliyotungwa mahsusi na Bunge au sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge.		
	(2) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (1), fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina zitatolewa kutoka Mfuko huo kwa ajili ya matumizi kwa kuzingatia masharti kuwa matumizi hayo yawe yameidhinishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.		
	(3) Fedha zilizomo katika mfuko		

Finance Bill Version
www.kuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	maalum wowote wa Serikali, isipokuwa Mfuko Mkuu wa Hazina, hazitatolewa kutoka mfuko huo kwa ajili ya matumizi isipokuwa kwa mujibu wa sheria inayoidhinisha matumizi hayo.		
Ibara ya 223: Utaratibu wa kuidhinisha Matumizi ya Fedha zilizomo katika Mfuko Mkuu wa Hazina.	(1) Rais atatoa maagizo kwa wahusika kutayarisha na kuwasilisha kwenye Bunge, katika kila mwaka wa fedha wa Serikali, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kipindi cha mwaka wa fedha wa Serikali unaofuata.	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuidhinisha fedha kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya matumizi yaliyopangwa na kuidhinishwa na Bunge.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu mzuri wa kupanga makadirio na matumizi ya fedha kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na kuweka wazi matumizi ya Serikali. Aidha, ni kulipa Bunge mamlaka ya kutoa idhini ya matumizi ya fedha kwa mipango iliyowasilishwa Bungeni na Serikali na kuridhiwa na Bunge kwa kuzingatia maslahi ya taifa na ustawi wa wananchi. Mapendekezo haya yatahakikisha kuwepo kwa uwiano
	(2) Baada ya Bunge kuyakubali makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali yaliyowasilishwa kwa mujibu wa ibara ndogo ya (1), Serikali itawasilisha kwenye Bunge		

Trial Version www.iuane.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali, kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina zitakazogharamia shughuli mbalimbali za Serikali zinazohusu makadirio hayo.		kati ya mapato na matumizi ya Serikali.
	(3) Ikiwa katika mwaka wa fedha wowote inaonekana kwamba:		
	(a) fedha za matumizi zilizoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kugharamia shughuli mahsusi hazitoshi;		
	(b) imekuwa lazima kulipa gharama za shughuli ambayo haikupangiwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria za nchi; (c) kuna fedha ambazo zimetumiwa kwa ajili ya shughuli mahsusi kwa kiasi kinachozidi kiwango cha matumizi kilichoidhinishwa na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuhusu shughuli hiyo;		
	(d) fedha zimetumiwa kulipia gharama za shughuli ambayo haikupangiwa fedha za matumizi kwa mujibu wa sheria za nchi;		
	kutawasilishwa kwenye Bunge makadirio ya matumizi ya nyongeza au, kadri itakavyokuwa, maelezo ya		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	matumizi ya ziada, na baada ya Bunge kuyakubali makadirio ya matumizi ya nyongeza au maelezo ya matumizi ya ziada, kutawasilishwa kwenye Bunge Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali au Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Nyongeza ya Fedha za Serikali kwa ajili ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, na fedha hizo zitagharamia shughuli zinazohusika na makadirio au maelezo hayo.		
Ibara ya 224: Utaratibu wa kuidhinisha matumizi ya Fedha kabla ya Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali kuanza	(1) Iwapo mwaka wa fedha wa Serikali umeanza na Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali inayohusika na mwaka huo haijaanza kutumika, Rais anaweza	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuidhinisha matumizi ya fedha za Serikali kabla ya kupitishwa kwa Sheria ya	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa shughuli za Serikali za lazima hazikwami wakati wa kipindi ambacho mwaka wa Bajeti umekwisha na sheria ya

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kutumika.	kuidhinisha fedha zitolewe kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa ajili ya kugharamia shughuli za lazima za Serikali, na fedha hizo zitatumiwa ndani ya miezi minne tangu mwanzo wa mwaka wa fedha wa Serikali hadi Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali itakapoanza kutumika, kutegemea na lipi kati ya mambo hayo litatokea mapema zaidi. (2) Bunge litatunga sheria kwa ajili ya kuweka masharti ya kuidhinisha matumizi ya fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina kwa kufuata utaratibu ulioelezwa katika ibara ndogo ya (1).	Matumizi ya Fedha za Serikali.	kuruhusu matumizi ya Serikali haijapitishwa.
Ibara ya 225: Mfuko wa Matumizi ya Dharura.	(1) Kutakuwa na Mfuko wa Matumizi ya Dharura ambao matumizi yake	Lengo ni kuanzisha Mfuko wa Matumizi ya Dharura na	Sababu za mapendekezo ni kulipa taifa uwezo wa kukabiliana na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yatawekewa masharti katika sheria za nchi. (2) Sheria iliyotajwa katika ibara ndogo ya (1) itaruhusu Rais au Waziri mwenye dhamana ya masuala ya fedha, pale anaporidhika kuwa kuna: (a) jambo la haraka na la dharura na ambalo halikutazamiwa kutokea na ambalo halikupangiwa fedha, kuazima fedha kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura kwa ajili ya kugharamia jambo hilo; au (b) jambo la haraka na la dharura kama ilivyoelezwa katika aya (a) ya ibara ndogo ya (2), kutumia	kuweka masharti ya matumizi ya fedha kutoka katika mfuko huo. Aidha, ni kuipa Serikali uwezo wa kukabiliana na changamoto za dharura na majanga.	dharura zinapotokea bila ya kusubiri Bunge kuidhinisha fedha za matumizi hayo yanayohitajika haraka. Sababu nyingine ya mapendekezo haya ni kuifanya nchi kujitegemea kwa kuwa na uwezo wa kuchukua hatua za haraka kukabili changamoto za dharura.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya kugharamia shughuli fulani kulipia gharama za jambo hilo. (3) Iwapo fedha zimeazimwa kutoka Mfuko wa Matumizi ya Dharura au fedha zilizotengwa mahsusi kwa ajili ya shughuli fulani zimetumiwa kugharamia jambo la haraka na la dharura, basi kutawasilishwa kwenye Bunge makadirio ya matumizi ya nyongeza, na baada ya Bunge kuyakubali makadirio hayo Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Fedha za Serikali utakaowasilishwa kwenye Bunge kwa ajili ya kuidhinisha matumizi hayo utahakikisha kwamba fedha zozote zilizoazimwa kwenye Mfuko		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wa Matumizi ya Dharura zitarudishwa kwenye Mfuko huo kutoka katika fedha za matumizi yatakayoidhinishwa na Muswada huo.		
Ibara ya 226: Mishahara ya baadhi ya Watumishi kudhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina.	(1) Watumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wanaohusika na masharti ya Ibara hii watalipwa mishahara na posho kama itakavyoelezwa na sheria za nchi. (2) Fedha za malipo ya mishahara na posho za watumishi wa Serikali wanaohusika na masharti ya Ibara hii pamoja na fedha za malipo ya uzeeni na kiinua mgongo, zitatolewa kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina. (3) Mshahara anaolipwa mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kusimamia mishahara, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kwa viongozi na watumishi wa umma walioainishwa katika Katiba na sheria za nchi	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa matumizi ya fedha za umma kwa ajili ya mishahara, malipo ya uzeeni na kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali. Mapendekezo haya ni kuwapa watumishi husika uhakika wa mapato na matunzo yao baada ya kustaafu au kuacha kazi, lakini pia kuepusha watumishi hao kujilipa mishahara na mafao nje ya utaratibu uliowekwa.

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	ya Ibara hii pamoja na masharti yake ya kazi havitabadilishwa kwa jinsi ambayo itapunguza maslahi ya mtumishi huyo baada ya kuteuliwa, isipokuwa kwamba masharti haya hayahusiki na posho anayolipwa mtumishi huyo.		
	(4) Endapo mtumishi wa Serikali anayehusika na masharti ya Ibara hii ana hiyari ya kuchagua kima cha mshahara au aina ya masharti ya kazi, basi kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya ibara ndogo ya (3), mshahara wa kima hicho atakaochagua na aina hiyo ya masharti ya kazi atakayochagua vitahesabiwa kuwa vina maslahi zaidi kwake kuliko kima cha mshahara kingine chochote ambacho anaweza		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuchagua au aina ya masharti ya kazi nyingine yoyote ambayo angeweza kuchagua.		
	(5) Masharti ya Ibara hii yatatumika kwa Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu, Jaji wa Mahakama ya Juu, Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Makamu Mwenyekiti wa Mahakama ya Rufani, Jaji wa Mahakama ya Rufani, Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu, Makamu Mwenyekiti wa Tume ya Haki za Binadamu, Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi, Makamu Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Umma, Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji na Makamu Mwenyekiti wa Tume ya		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na watumishi wengine watakaoainishwa katika sheria za nchi.		
(b) Deni la Taifa na Mikopo ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 227: Deni la Taifa.	(1) Deni la Taifa litadhaminiwa na Mfuko Mkuu wa Hazina. (2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa Ibara hii, deni la Taifa litajumuisha deni la Serikali ya Jamhuri ya Muungano pamoja na deni lolote litakalodhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka chombo cha kudhamini Deni la Taifa ambacho ni Mfuko Mkuu wa Hazina.	Sababu ya Mapendekezo haya ni kutambua kuwa Mfuko Mkuu wa Hazina ndio unaotunza mapato yote ya Serikali ikiwa ni pamoja na mali na madeni ya taifa. Aidha, ni kuendeleza utaratibu huu wa kikatiba unaotumika katika sehemu mbalimbali duniani ambapo Serikali inapokopa, Mfuko Mkuu wa Hazina ndio unaochukua dhamana.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 228: Mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa.	(1) Serikali ya Jamhuri ya Muungano itakuwa na mamlaka ya kukopa fedha ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kugharamia shughuli zilizo chini ya mamlaka yake. (2) Bunge linaweza kutunga sheria ambayo: (a) itaweka masharti ya kuzingatiwa na Serikali wakati wa kukopa; (b) itaweka ukomo wa deni la Taifa na madhumuni ya deni hilo; na (c) itaweka utaratibu wa Serikali kutoa taarifa kwenye Bunge kuhusu mikopo na deni la Taifa.	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kuipa mamlaka Serikali ya Jamhuri ya Muungano kukopa fedha ndani na nje ya nchi na pia kulipa Bunge uwezo kuweka ukomo wa deni la taifa na madhumuni ya deni.	Sababu za mapendekezo haya ni kudhibiti Deni la Taifa ili lisivuke uwezo wa taifa kulipa. Aidha, ni kuhakikisha kuwa mikopo inayochukuliwa ina tija na manufaa kwa maendeleo ya wananchi na kuwa imezingatia misingi ya utawala bora na uwajibikaji. Pia, kutoa taarifa ya madeni Bungeni na kukuza uwazi na uwajibikaji wa Serikali kwa wananchi. Sababu nyingine ni kuepusha kulimbikiza madeni yasiyo na tija na kuwa mzigo kwa vizazi vijavyo.

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (2)(b), taarifa itakayowasilishwa Bungeni pamoja na mambo mengine itaeleza: (a) kiasi cha deni lililopo na riba yake; (b) matumizi yaliyofanywa au yatakayofanywa kutokana na fedha za mkopo husika; (c) utaratibu uliowekwa wa kulipa deni husika; na (d) hatua iliyofikiwa katika kulipa deni husika.	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba kwa ajili ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutoa dhamana kwa mikopo ya Nchi Washirika.	Sababu ya mapendekezo haya ni kutoa fursa kwa Nchi Washirika kukopa ndani na nje ya nchi kwa kudhaminiwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano kulingana na aina na ukubwa wa mikopo. Aidha, mapendekezo haya ni utaratibu wa kushauriana na kukubaliana baina ya Serkali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Nchi Mshirika kuhusiana na dhamana kwa ajili ya mikopo ya aina hiyo.
Ibara ya 229: Mamlaka ya Serikali za Nchi	(1) Serikali ya Nchi Mshirika itakuwa na mamlaka ya kukopa fedha		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Washirika kukopa.	ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano kwa ajili ya kugharamia shughuli zilizo chini ya mamlaka yake. (2) Endapo mkopo utahitaji dhamana, Serikali ya Jamhuri ya Muungano, baada ya kushauriana na kukubaliana na Serikali ya Nchi Mshirika, inaweza kutoa dhamana kwa mkopo unaoombwa. (3) litatunga sheria itakayoweka utaratibu wa Serikali kudhamini mikopo ya Serikali za Nchi Washirika. (4) Katika kipindi cha miezi mitatu tangu kumalizika kwa mwaka wa fedha wa Serikali, Serikali itachapisha Taarifa katika Gazeti la Serikali itakayoelezea mikopo		Sababu nyingine ni kuondoa vikwazo kwa Nchi Washirika kupata fursa ya kukopa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya nchi zao.

Trial Version
www.tuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	iliyodhaminiwa na Serikali katika mwaka wa fedha wa Serikali uliopita.		
Ibara ya 230: Masharti ya kutoza kodi.	Hakuna kodi ya aina yoyote itakayotozwa na mamlaka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano isipokuwa kwa mujibu wa sheria za nchi.	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya utaratibu wa kutoza kodi.	Sababu za mapendekezo haya ni kulipa Bunge pekee uwezo na mamlaka ya kutunga sheria za kutoza kodi.
(c) Vyanzo vya Mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Ununuzi wa Umma			
Ibara ya 231: Vyanzo vya Mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.	Vyanzo vya mapato ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano -vitakuwa: (a) ushuru wa bidhaa; (b) mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na taasisi za Muungano; (c) mchango kutoka kwa Nchi	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka kikatiba vyanzo vya mapato vya Serikali ya Jamhuri ya Muungano.	Sababu za mapendekezo haya ni kuiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake bila ya vikwazo vya kifedha, kuondoa mgongano wa vyanzo vya mapato vya Muungano na visivyo vya Muungano; na kutoa uhalali wa ukusanyaji wa kodi na upatikanaji wa mapato kutokana na vyanzo vya mapato vilivyoainishwa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika; (d) mikopo kutoka ndani na nje ya Jamhuri ya Muungano; na (e) mapato mengine.		katika Katiba. Mapendekezo ya vyanzo hivi vya mapato yamezingatia mapato na matumizi ya Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya Muungano kama yalivyochanganuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC), Taarifa za Makusanyo ya Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na bajeti za kila mwaka zinazopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano na Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Taarifa hizo za kitaalamu zinaonesha kwamba mapato yanayotokana na vyanzo hivi yanatosheleza kuendesha Serikali ya Jamhuri ya Muungano kutokana na uchache wa Mambo ya Muungano yanayopendekezwa na Rasimu hii kusimamiwa na Serikali

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			ya Jamhuri ya Muungano.
Ibara ya 232: Ununuzi wa Umma.	(1) Katika kufanya ununuzi wa umma, Serikali na taasisi zote za umma zitatakiwa kutumia mfumo na utaratibu utakaozingatia haki, uwazi, maslahi ya umma, uwajibikaji, ushindani na thamani halisi ya fedha. (2) Katika kufanya ununuzi wa umma, Serikali na taasisi zake zitatakiwa kutumia au kuweka mfumo ambao utazingatia kununua bidhaa zinazozalishwa au huduma zinazotolewa nchini kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika Ibara hii na sheria za nchi. (3) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti ya usimamizi na udhibiti wa	Madhumuni ya Ibara hii ni kuweka misingi ya mfumo na utaratibu wa kufanya ununuzi wa umma.	Sababu ya mapendekezo haya ni kusimamia na kudhibiti manunuzi ya umma katika Serikali na taasisi zake. Aidha mapendekezo haya yametokana na ukweli kwamba sehemu kubwa ya Bajeti ya Serikali na Taasisi zake inatumika katika ununuzi wa bidhaa au huduma kwa hiyo ni muhimu kuhakikisha kuwa fedha hizo zinatumika vyema na kwa thamani halisi ya fedha.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	manunuzi ya umma.		
	(d) Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano		
Ibara ya 233: Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano.	(1) Kutakuwa na Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano itakayojulikana kuwa "Benki Kuu" ambayo itakuwa na majukumu yafuatayo: (a) kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia mzunguko wa sarafu; (b) kuandaa na kusimamia sera na mipango inayohusiana na sarafu; (c) kudhibiti na kusimamia masuala ya fedha za kigeni; na (d) kusimamia Benki za Nchi	Madhumuni ya Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Benki Kuu ya Jamhuri ya Muungano.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo katika nchi nyingi duniani wa kuwa na Benki Kuu moja inayozisimamia na kuzielekeza benki za Nchi Washirika. Pia, sababu nyingine ni kuweka usimamizi na udhibiti wa sarafu na fedha zote za Jamhuri ya Muungano chini ya Benki Kuu kwa vile utaratibu huu ndiyo unaotumika katika nchi za shirikisho au zilizomo katika umoja wa sarafu ya pamoja (*Monetary Union*) kama vile Nigeria, Umoja wa Nchi za Marekani (*United States of America*) na Ujerumani. Pendekezo hili pia limezingatiwa kwa sababu

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika. (2) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Benki Kuu itakuwa huru na haitaingiliwa ama kwa kupewa maelekezo au kudhibitiwa na mtu au mamlaka yoyote. (3) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo wa Benki Kuu utakaozingatia uwakilishi wa kila upande wa Jamhuri ya Muungano, mamlaka, shughuli na utendaji wa Benki Kuu.		Tanzania ni nchi yenye Sarafu moja.
Ibara ya 234: Benki za Serikali za Nchi Washirika.	Serikali za Nchi Washirika zitakuwa na Benki zitakazokuwa na jukumu la kutunza akaunti ya fedha za Serikali ya Nchi Mshirika husika, kusimamia sera za kifedha na benki za biashara katika mamlaka zao.	Lengo la ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya kuanzishwa kwa benki za Serikali za Nchi Washirika	Katika muundo wa Muungano wenye Mambo ya Muungano na yasiyo ya Muungano na Serikali zaidi ya moja ya kusimamia

Trial Version
www.luance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		na usimamizi wake.	mambo hayo, huhitajika kuwepo kwa Benki za Serikali hizo zaidi ya Benki Kuu. Hivyo, Katiba huainisha na kutofautisha majukumu ya Benki Kuu na kazi na majukumu ya Benki za Nchi Washirika ili kuepusha migongano na kuyumbisha uchumi na thamani ya fedha.
SURA YA KUMI NA TANO **◇ ULINZI NA USALAMA WA JAMHURI YA MUUNGANO**			
Ulinzi na Usalama wa Taifa			
Ibara ya 235: Usalama	(1) Jukumu la ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano ni la kila	Madhumuni ya Ibara hii ni	Sababu za mapendekezo haya ni

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
wa Taifa.	raia.	kuweka kikatiba jukumu la ulinzi na usalama kuwa ni la kila raia wa Jamhuri ya Muungano.	kuendeleza mfumo na utaratibu wa ulinzi na usalama uliopo Tanzania ambao chimbuko na hatma yake ni wananchi wenyewe. Kanuni zilizowekwa zinazingatia kuwa vyombo vya ulinzi na usalama vipo kwa ajili ya wananchi na kwa hiyo ni sehemu ya jamii ya Tanzania. Pia, ni kuhakikisha kuwa Jamhuri ya Muungano, raia wake pamoja na mali zao zinakuwa salama kwa kuzingatia sheria za nchi na sheria za kimataifa na kwa
	(2) Usalama wa Jamhuri ya Muungano unahusu ulinzi wa mipaka yote ya eneo la Jamhuri ya Muungano ikiwa ni pamoja na ardhi, anga na bahari kuu, watu wake, mali zao, haki, uhuru na maslahi mengine ya kitaifa dhidi ya vitisho vya ndani na nje ya nchi.		
	(3) Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano utaimarishwa kulingana na kanuni zifuatazo:		
	(a) ulinzi na usalama wa Taifa unaongozwa kwa mamlaka ya Katiba hii;		
	(b) ulinzi na usalama wa Taifa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	utatekelezwa kwa kuzingatia sheria za nchi na sheria za kimataifa, na kwa kuheshimu kikamilifu utawala wa sheria na haki za binadamu; na		kuheshimu kikamilifu utawala wa sheria na Haki za Binadamu.
	(c) taasisi za ulinzi na usalama wa Taifa zitaheshimu utamaduni wa aina mbalimbali wa jamii katika kutekeleza majukumu yao.		
Ibara ya 236: Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa.	(1) Vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa vitakuwa ni: (a) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania; (b) Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano; na	Madhumuni ya Ibara hii ni kuunda kikatiba vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa katika Jamhuri ya Muungano. Madhumuni	Sababu za mapendekezo hayo ni kutambua kuwa vyombo vya ulinzi na usalama ndio moyo wa nchi na alama inayoonekana ya uhuru na mamlaka ya nchi,

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) Idara ya Usalama wa Taifa. (2) Wajibu wa vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa na mfumo wa usalama ni kulinda mipaka ya Jamhuri ya Muungano, maslahi ya raia na watu wengine, mali zao, haki na uhuru, mamlaka za nchi, amani na umoja wa kitaifa.	mengine ni kumpa Rais mamlaka ya kuunda chombo cha ulinzi na usalama, mamlaka na usimamizi wake, majukumu na wajibu katika ulinzi wa usalama wa nchi.	hivyo, ni vyema vyombo hivyo vikaanzishwa na kikatiba na kuwa chini ya amri moja ya Rais ambaye ni Mkuu wa Nchi kwa nafasi yake ya Amiri Jeshi Mkuu.
	(3) Katika utekelezaji wa majukumu yao, vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa na kila mtumishi wa vyombo hivyo hataruhusiwa -		
	(a) kuwa na upendeleo kwa njia yoyote;		
	(b) kuendeleza maslahi ya chama chochote cha siasa		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au sera zake;		
	(c) kuhujumu maslahi ya kisiasa au mpango wa kisiasa ambao ni halali chini ya Katiba hii;		
	(d) kutishia, kudhulumu au kuwatendea ukatili raia na watu wengine; na		
	(e) kutii amri yoyote isiyokuwa halali.		
	(4) Mtu hataruhusiwa kuanzisha taasisi, kampuni, jumuiya au shirika linalohusiana na ulinzi na usalama wa Taifa au ushirika wa kijeshi, isipokuwa kama inavyoruhusiwa na Katiba hii au sheria za nchi.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(5) Vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa vitakuwa chini ya mamlaka ya Rais.		
	(6) Rais anaweza kuunda chombo cha ulinzi na usalama kwa kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.		
	(6) Bunge litatunga sheria kuweka masharti kuhusu utekelezaji wa majukumu, utaratibu na usimamizi wa vyombo vya ulinzi na usalama wa Taifa. (7)		
Ibara ya 237: Kuanzishwa kwa Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa.	(1) Kutakuwa na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa litakalokuwa na wajumbe wafuatao - (a) Makamu wa Rais;	Madhumuni ya Ibra hii ni kuanzisha kikatiba Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa la	Sababu za mapendekezo haya ni kulitambua kikatiba na kuendeleza utaratibu wa sasa wa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) Rais wa Tanganyika; (c) Rais wa Zanzibar; (d) Waziri mwenye dhamana ya ulinzi; (e) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya ndani ya nchi; (f) Waziri mwenye dhamana ya mambo ya nje; (g) Waziri mwenye dhamana ya usalama wa taifa; (h) Waziri mwenye dhamana ya fedha; (i) Mwanasheria Mkuu wa Serikali; (j) Mkuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania;	kumshauri Amiri Jeshi Mkuu juu ya masuala ya Ulinzi na Usalama kikiwa ni chombo muhimu kwa uhai na usalama wa Taifa.	kuwa na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa. Baraza hili ni muhimu kwa mashauriano ya ulinzi na usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikijumuisha Nchi Washirika kwa kuwa Ulinzi na Usalama ni suala la Muungano. Aidha, chombo hiki kinamkutanisha Rais wa Jamhuri ya Muungano na Viongozi wa Serikali ya Tanganyika na Serikali ya Zanzibar kujadili na kuamua juu ya mambo makubwa ya mustakabali wa Taifa la Tanzania.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(k) Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; (l) Mkuu wa Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na (m) Kamishna Mkuu wa Uhamiaji. (2) Mwenyekiti anaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika kikao cha Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.		
	(3) Kutakuwa na Sekretarieti ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa itakayoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi.		
	(4) Vikao vya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa vitaongozwa na		

Trial Version
www.iluance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Rais. (5) Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa litaweka utaratibu wa mwenendo wa vikao vyake. (6) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.		
Ibara ya 238: Majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa.	(1) Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa litakuwa na majukumu yafuatayo: (a) kuunganisha sera za ndani, sera za nchi za nje na za kijeshi kuhusiana na usalama wa Taifa ili kuwezesha taasisi za ulinzi na usalama wa Taifa	Lengo la ibara hii ni kuweka kikatiba majukumu ya Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.	Sababu za mapendekezo haya ni kuanzisha chombo cha kikatiba cha kumshauri Rais wa Jamhuri ya Muungano akiwa Amiri Jeshi Mkuu kumuwezesha kuamua juu ya mambo makubwa na

Trial Version
www.iuanda.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kushirikiana kikamilifu; (b) kupokea, kutathmini na kuchunguza taarifa kutoka katika vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa na taasisi za Serikali kuhusiana na usalama wa nchi; (c) kutoa maelekezo mahsusi kuhusiana na masuala ya ulinzi na usalama wa Taifa kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali za Nchi Washirika na Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Taifa; (d) kuanzisha sera kuhusu maslahi ya pamoja ya kiusalama ya vyombo vya		mustakabali wa Taifa la Tanzania. Vilevile, kuwezesha na kurahisisha uratibu wa masuala ya usalama katika Jamhuri ya Muungano na Nchi Washirika.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	usalama na kudhibiti usimamizi vyombo hivyo; na (e) kutekeleza majukumu mengine yoyote kama Rais atakavyoagiza.		
	(2) Rais atatoa taarifa kwenye Bunge kila mwaka kuhusu hali ya ulinzi na usalama katika Jamhuri ya Muungano.		
(b)Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania			
Ibara ya 239: Kuanzishwa kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.	(1) Kutakuwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litakalokuwa na jukumu la kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri ya Muungano na kusimamia ulinzi na	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Jeshi moja la ulinzi katika	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua kwamba ulinzi wa nchi ni suala la mamlaka ya Juu ya Nchi na haligawiki hata katika nchi za

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	usalama wa wananchi. (2) Rais anaweza kuanzisha vikosi vingine vya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kama atakavyoona inafaa.	Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambalo ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.	Shirikisho au Muungano. Kwa hiyo, Ibara hii inahakikisha kuwepo kwa chombo kimoja cha ulinzi ambacho ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania ambalo litasimamia masuala yote ya Ulinzi na Usalama wa wananchi na mipaka ya Jamhuri ya Muungano
Ibara ya 240: Uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi.	Kutakuwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.	Madhumuni ya Ibara hii kuanzisha kikatiba nafasi ya Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	Sababu za mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu uliopo wa Jeshi la Ulinzi kuongozwa na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi anayeteuliwa na Amiri Jeshi Mkuu. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu wa wazi wa kikatiba wa kumpata Mkuu wa

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Majeshi ya Ulinzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia Majeshi ya Ulinzi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau wa masuala ya ulinzi na usalama na wananchi kwa ujumla waliopendekeza kuwa na utaratibu wa Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 241: Madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.	(1) Bila ya kuathiri masharti yatakayowekwa na sheria za nchi, Rais kwa nafasi ya madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu atakuwa na mamlaka ya kuyaamuru majeshi ya nchi: (a) kutenda mambo yanayohusika na vita vya ulinzi wa Jamhuri ya Muungano; (b) kuokoa maisha na mali za watu katika hali ya hatari; (c) kusaidia na kushirikiana na mamlaka nyingine wakati wa dharura au maafa; (d) kusaidia mamlaka au uongozi wa Serikali	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua mamlaka ya kipekee ya Amiri Jeshi Mkuu ambaye ndiye mwenye dhamana ya mwisho ya maamuzi juu ya ulinzi na usalama wa nchi. Sababu nyingine ni kumpa uwezo wa kikatiba wa kuyaamuru na kuyapeleka majeshi vitani baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa na kadri itakavyojitokeza kupata idhini ya Bunge.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutuliza ghasia, fujo au kurejesha hali ya utulivu;		Kwa hiyo, ni vyema Katiba ikaainisha kwa ufasaha madaraka ya Amiri Jeshi Mkuu na udhibiti wake.
	(e) kushirikiana na jumuiya ya kimataifa katika ulinzi wa amani pale itakapoonekana inafaa; na		
	(f) kutenda mambo mengineyo ambayo Amiri Jeshi Mkuu ataona inahitajika,		
	na kwa ajili hiyo Amiri Jeshi Mkuu anaweza kuyaamuru majeshi hayo yatekeleze mambo hayo ndani au nje ya Jamhuri ya Muungano.		
	(2) Katika utekelezaji wa masharti ya Ibara hii na kwa kuzingatia sheria za nchi, madaraka juu ya mambo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yafuatayo yatakuwa mikononi mwa Amiri Jeshi Mkuu -		
	(a) kuwateua viongozi katika majeshi ya ulinzi ya Jamhuri ya Muungano;		
	(b) kuwateua wanajeshi watakaoongoza vikosi mbali mbali vya majeshi ya ulinzi;		
	(c) kumwamuru mwanajeshi yeyote asitumie madaraka yoyote aliyokabidhiwa na ambayo yanaambatana na kuwa kwake mwanajeshi; na		
	(d) kulinda uhuru na mipaka ya Jamhuri ya Muungano.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(3) Kwa madhumuni ya Ibara hii, jambo lolote atakalotenda mwanajeshi kinyume cha amri ya Amiri Jeshi Mkuu litakuwa batili.		
Ibara ya 242: Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.	(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania itakayokuwa na jukumu la kusimamia masuala yote ya utumishi katika Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania. (2) Bunge litatunga sheria itakayoweka masharti kuhusu muundo, majukumu na mambo mengine yanayohusu Tume ya Utumishi ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.	Lengo la Ibara hii ni kuweka chombo cha kikatiba cha kusimamia masuala yote ya utumishi wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vyake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau kwamba pawepo chombo cha kikatiba cha kusimamia masharti ya utumishi na maslahi ya wanajeshi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na vikosi vyake. Hii itakuwa ni mara ya kwanza kuwa na chombo kama hiki katika Katiba ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Jeshi

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			la Wananchi wa Tanzania.
(c) Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 243: Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano.	(1) Kutakuwa na Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano litakalokuwa na jukumu la ulinzi na usalama wa watu na mali zao kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. (2) Bunge litatunga sheria kuweka masharti ya utekelezaji wa kazi na majukumu ya Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano kwa kuzingatia haki za kiraia na sheria za kimataifa.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano la Tanzania.	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya Wananchi waliotaka kuwepo kwa Jeshi moja la Polisi litakalosimamia usalama wa raia wote katika Jamhuri ya Muungano ikijumuisha Nchi Washirika.
Ibara ya 244: Misingi ya Utendaji wa Jeshi la	(1) Katika utekelezaji wa majukumu yake, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya	Lengo la Ibara hii ni	Sababu za mapendekezo haya

Final Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Polisi.	Muungano litazingatia - (a) viwango vya juu vya kitaaluma na nidhamu miongoni mwa wafanyakazi wake; (b) ulinzi na ukuzaji wa haki za binadamu; (c) kanuni za uwazi na uwajibikaji;na (d) kukuza mahusiano na jamii.	kuweka kikatiba misingi itakayoongoza utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Polisi kwa ufanisi.	kutambua dhamana kubwa ya Jeshi la Polisi la kulinda usalama wa raia na mali zao. Hata hivyo, pamoja na kuwa ni chombo cha nguvu cha kidola bado kinapaswa kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Katiba, sheria na kanuni zinazokuza na kuimarisha utawala wa sheria na haki za binadamu. Sababu nyingine ni kuweka utaratibu utakaolifanya Jeshi la Polisi kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya kitaaluma, nidhamu,
	(2) Jeshi la Polisi, katika kutekeleza majukumu yake, litashirikiana na vyombo vinavyohusika na kupambana na uhalifu vya Nchi Washirika katika kufanya uchunguzi na kushughulikia makosa ya rushwa na ufisadi.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			kulinda haki za binadamu, kanuni za uwazi na uwajibikajii na kukuza mahusiano ya kijamii.
Ibara ya 245: Uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi.	Kutakuwa na Mkuu wa Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano ambaye atateuliwa na Rais baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama wa Taifa.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba nafasi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau waliotaka Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia usalama wa raia na mali zao katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 246: Uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi.	Mkuu wa Jeshi la Polisi atatekeleza kazi zake kwa uhuru, bila woga, upendeleo wala chuki na kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na sheria za nchi.	Lengo la Ibara ni kuweka kikatiba uhuru wa Mkuu wa Jeshi la Polisi katika utekelezaji wa majukumu yake.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha kuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi anafanya kazi yake kwa uhuru kwa kuzingatia Katiba, sheria za nchi na kanuni zilizowekwa bila ya kushinikizwa au kuingiliwa na mtu au mamlaka nyingine yoyote.
Ibara ya 247: Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi.	(1) Kutakuwa na Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi itakayokuwa na jukumu la kusimamia utumishi wa Jeshi la Polisi. (2) Katika uajiri wa askari wa Jeshi la Polisi, Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi itazingatia kanuni na misingi ya utumishi iliyoainishwa	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi ikiwa ni chombo cha kusimamia masuala yote ya	Sababu za mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau kwamba pawepo chombo cha kikatiba cha kusimamia masharti ya utumishi na maslahi ya

Trial Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika Katiba hii.	utumishi wa askari wa Jeshi la Polisi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	watumishi wa Jeshi la Polisi. Hii itakuwa ni mara ya kwanza kuwa na chombo kama hiki katika Katiba ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
	(3) Bunge litatunga sheria kuweka masharti ya muundo na utekelezaji wa kazi na majukumu ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi.		
(d) Idara ya Usalama wa Taifa ya Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 248: Kuanzishwa kwa Idara ya Usalama wa Taifa.	(1) Kutakuwa na Idara ya Usalama wa Taifa ya Jamhuri ya Muungano itakayoitwa "Idara ya Usalama wa Taifa". (2) Idara ya Usalama wa Taifa itahusika na shughuli za kuimarisha usalama wa Jamhuri ya Muungano na kulinda Katiba	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba Idara ya Usalama wa Taifa.	Sababu za mapendekezo ya ibara hii ni kuanzisha kikatiba chombo kitakachokuwa na dhamana ya kuhakikisha usalama wa taifa na watu wake dhidi ya mataifa ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hii, maslahi ya Taifa na ya watu wake na itatekeleza majukumu mengine kama yatakavyoainishwa na sheria za nchi.		nje na maeneo ya kimkakati na kiusalama ndani ya nchi ikiwa ni pamoja na kuilinda Katiba ya Nchi.
Ibara ya 249: Uteuzi wa Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa.	Rais atamteua Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa baada ya kushauriana na Baraza la Ulinzi na Usalama la Taifa.	Lengo la Ibara hii ni kuanzisha kikatiba nafasi ya Mkurugenzi wa Idara ya Usalama wa Taifa.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuzingatia maoni ya wadau waliotaka Rais kushauriana na mamlaka nyingine katika uteuzi wa Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa lengo la kusimamia usalama wa taifa katika Jamhuri ya Muungano

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			wa Tanzania.
Ibara ya 250: Usalama katika Nchi Washirika.	(1) Bila ya kuathiri masharti ya Sura hii, Wakuu wa Nchi Washirika wanaweza kumuagiza kiongozi yeyote wa Jeshi la Polisi au Idara ya Usalama wa Taifa kuchukua hatua yoyote ambayo ni muhimu kwa ajili ya kulinda au kuimarisha usalama wa eneo lolote la Nchi Mshirika husika. (2) Bunge litatunga sheria itakayoainisha masharti yanayohusu namna bora ya utekelezaji wa ibara ndogo ya (1).	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba yanayowawezesha Wakuu wa Serikali wa Nchi Washirika kuwaagiza viongozi wa Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa kuchukua hatua kwa ajili ya kulinda na kuimarisha usalama katika eneo lolote la Nchi Mshirika husika.	Sababu za mapendekezo haya ni kutambua umuhimuu na mamlaka ya Jeshi la Polisi na Idara ya Usalama wa Taifa kwamba hayagawiki lakini pia kutambua umuhimu wa nchi washirika kuwa na uwezo wa kuvitumia vyombo hivi; na hivyo kupewa mamlaka ya kuwaagiza wakuu au maafisa wengine iwapo kuna haja ya kukabili hali ya kiusalama.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
SURA YA KUMI NA SITA **MENGINEYO**			
Ibara ya 251: Utaratibu wa kujiuzulu katika Utumishi wa Umma.	(1) Mtu yeyote mwenye dhamana ya kazi yoyote iliyoanzishwa na Katiba hii anaweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa iliyoandikwa na kutiwa saini kwa mkono wake, kwa kufuata masharti yafuatayo: (a) iwapo mtu huyo aliteuliwa au kuchaguliwa na mtu mmoja, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa mtu huyo aliyemteua au aliyemchagua, au iwapo aliteuliwa au kuchaguliwa na kikao cha watu, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kujiuzulu katika utumishi wa umma na Mamlaka ya kuarifiwa juu ya uamuzi huo.	Sababu za mapendekezo haya ni kuheshimu kanuni za utawala wa sheria; na kanuni za utumishi kwa kuwa na utaratibu unaoruhusu mtumishi kujiuzulu kwa hiyari yake au kwa kutekeleza maelekezo au maamuzi ya mamlaka za nchi kwa mujibu wa Katiba.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kikao hicho; (b) iwapo mtu huyo ni Rais, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Spika; (c) iwapo mtu huyo ni Makamu wa Rais, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwa Rais; (d) iwapo mtu huyo ni Spika au Naibu Spika wa Bunge, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha kwenye Bunge; na (e) iwapo mtu huyo ni Mbunge, basi taarifa hiyo ya kujiuzulu ataiwasilisha		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kwa Spika.		
	(2) Mtu aliyetoa taarifa ya kujiuzulu kwa mujibu wa masharti ya ibara ndogo ya (1), atahesabiwa kuwa amejiuzulu tangu siku ile ambayo taarifa yake ya kujiuzulu itakapopokelewa na mtu anayehusika au kikao kinachohusika au itakapopokelewa na mtu yeyote aliyeruhusiwa kuipokea taarifa hiyo na mtu anayehusika au kikao kinachohusika, lakini kama taarifa hiyo ya kujiuzulu imeeleza kwamba mtu huyo atajiuzulu tangu siku nyingine baada ya taarifa hiyo kupokelewa na mtu anayehusika au kikao kinachohusika, basi mtu huyo atahesabiwa kuwa amejiuzulu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	tangu siku hiyo nyingine ya baadaye.		
	(3) Endapo mtu yeyote mwenye dhamana ya kazi yoyote iliyoanzishwa na Katiba hii amejiuzulu, ikiwa anazo sifa zote zinazohitajika na kwa kila hali anastahili, anaweza kuteuliwa au kuchaguliwa tena kushika madaraka ya kazi hiyo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii.		
Ibara ya 252: Masharti kuhusu kukabidhi Madaraka.	(1) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhi madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, mtu yeyote mwenye mamlaka, kwa mujibu wa Katiba hii, ya kumteua mtu mwingine kushika madaraka pia	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba wa kukabidhi madaraka katika Utumishi wa Umma.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa Utumishi wa Umma wa kuhakikisha kuwa wakati wote kuna mtu anayeshikilia nafasi ya utumishi ili

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	atakuwa na uwezo wa kumteua kaimu au mtu ambaye atashika kwa muda na kutekeleza madaraka hayo.		kuepusha ombwe na kukosekana kwa huduma au maamuzi kwa wananchi. Aidha, mapendekezo haya ni kuweka utaratibu wa kukabidhi ofisi unaolingana na Utumishi wa Umma.
	(2) Kanuni zifuatazo zitatumika pia kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii kuhusu utaratibu wa kukabidhiana madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano:		
	(a) iwapo kuna mtu mwenye madaraka aliyokabidhiwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii na mtu huyo yupo likizo na wakati huo huo anasubiri kuacha madaraka hayo, basi anaweza kuteuliwa mtu mwingine na kukabidhiwa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	madaraka hayo, bila ya kujali kuwepo kwa yule mtu anayesubiri kuacha madaraka hayo;		
	(b) iwapo kuna watu wawili au zaidi ambao kwa wakati mmoja wote wanashika madaraka kutokana na uteuzi wao uliofanywa kwa mujibu wa Kanuni iliyoelezwa katika aya ya (a), basi katika hali hiyo kukitokea umuhimu wa kutekeleza shughuli yoyote inayohusika na madaraka hayo yule mtu wa mwisho kuteuliwa ndiye atakayehesabiwa kuwa mtu pekee mwenye dhamana ya madaraka		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hayo; na (c) iwapo mtu ameteuliwa, kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii, kuwa kaimu au kushikilia madaraka wakati mtu aliyeteuliwa kushika nafasi ya madaraka hayo ameshindwa kutekeleza shughuli zinazohusika na madaraka hayo, basi haitaruhusiwa kufanya uchunguzi wowote au kutoa hoja yoyote juu ya uteuzi wa huyo kaimu kwa sababu mtu aliyeteuliwa kushika nafasi ya madaraka hayo ameshindwa kutelekeza shughuli zinazohusika na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mmadaraka hayo.		
Ibara ya 253: Baadhi ya Watumishi wa Umma kutoshika nafasi za Kisiasa.	(1) Watumishi wafuatao hawatakuwa na haki ya kugombea, kuchaguliwa au kuteuliwa katika nafasi ya kisiasa hadi utakapopita muda wa miaka mitatu tokea kuacha au kustaafu nafasi ya madaraka aliyokuwa akiishikilia: (a) Jaji Mkuu, Naibu Jaji Mkuu na Jaji wa Mahakama ya Juu wa Jamhuri ya Muungano; (b) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Jaji wa Mahakama ya Rufani; (c) Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba, kuzuia baadhi ya viongozi wastaafu kushiriki kwenye siasa kwa kipindi cha miaka mitatu tangu walipostaafu au kuachia madaraka.	Sababu za mapendekezo haya ni kuondoa mgongano wa kisiasa katika utendaji wa Serikali na kuepusha uwezekano wa mtu kuchukua maamuzi muda mfupi kabla ya kuacha uongozi au kustaafu kwa lengo la kumsaidia kugombea au kupata cheo cha kisiasa baada ya hapo.

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(d) Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano;		
	(e) Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama;		
	(f) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;		
	(g) Katibu Mkuu Kiongozi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano;		
	(h) Makatibu Wakuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; na		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(i) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Wajumbe wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mkurugenzi wa Uchaguzi; (j) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu; (k) Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Maadili ya Uongozi na Uwajibikaji; (l) Mwenyekiti na Wajumbe wa Tume ya Utumishi wa Umma; (m) Msajili wa Vyama vya Siasa.		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Bunge linaweza kutunga sheria kuhusu aina nyingine ya watumishi wa umma ambao hawataruhusiwa kushika nafasi za madaraka ya kisiasa kwa mujibu wa Ibara hii.		
	(1) Katika Katiba hii, isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo:	Lengo la Ibara hii ni kutoa ufafanuzi wa baadhi ya maneno na istilahi za kikatiba zilizotumika ndani ya Katiba.	Sababu ni kuendeleza utaratibu wa kutafsiri istilahi za kitaalam katika utungaji wa Katiba. Pia ni kawaida duniani kote wa kuwa na Ibara ya aina hii katika Katiba.
	"chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichoandikishwa kwa mujibu wa sheria za nchi;		
	"Jamhuri ya Muungano" maana yake ni Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;		
	"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Mahakama ya Jamhuri ya		

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Muungano; "Jeshi" maana yake ni Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano pamoja na chombo chochote kilichoundwa kwa mujibu wa Katiba hii au sheria za nchi na kinachotawaliwa kwa amri ya jeshi; "nafasi ya madaraka" maana yake ni wadhifa, cheo, hadhi, madaraka ya uongozi au mamlaka ya utendaji katika utumishi wa umma; "Mahakama" maana yake ni Mahakama ya Juu na Mahakama ya Rufani; "Mahakama Kuu" maana yake ni Mahakama Kuu za Nchi		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika; "mtumishi wa umma" maana yake ni mtu aliyeajiriwa katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Utumishi wa Mahakama, Utumishi wa Bunge, wakala wa Serikali, utumishi katika taasisi zinazojitegemea ambazo zinafanya kazi za Serikali au zinazomilikiwa na Serikali isipokuwa haitajumuisha utumishi wa kisiasa; "Mwanasheria Mkuu" maaana yake ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano; "Naibu Waziri" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na kukabidhiwa madaraka ya kazi ya Naibu		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Waziri;		
	"Nchi Washirika" maana yake ni Tanganyika na Zanzibar;		
	"Serikali" maana yake ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na mtu yeyote anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali;		
	"Uchaguzi Mkuu" maana yake ni uchaguzi wa Rais na uchaguzi wa Wabunge wanaowakilisha majimbo ya uchaguzi unaofanywa baada ya Bunge kumaliza muda wake;		
	"Waziri" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kushika nafasi ya madaraka ya Waziri na wadhifa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	wa "Naibu Waziri" utatafsiriwa kwa muktadha huo"		
	"Waziri Mwandamizi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa kushika nafasi ya madaraka ya Waziri Mwandamizi kwa mujibu wa Katiba hii; "Waziri Mkaazi" maana yake ni Waziri aliyeteuliwa na Serikali ya Nchi Mshirika kushika nafasi ya madaraka ya Waziri Mkaazi;		
	(2) Kanuni zifuatazo zitatumika kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Katiba hii:		
	(a) kila yanapotajwa madaraka ya Rais, ifahamike kuwa madaraka yanayohusika ni pamoja na mamlaka ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutekeleza shughuli za kazi mbalimbali na vile vile wajibu wa kutekeleza shughuli na kazi mbali mbali kama Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, na pia mamlaka mengine kama hayo au wajibu mwingine kama huo ikiwa imeelezwa katika Katiba hii au katika sheria nyingine yoyote kwamba mamlaka hayo mengine ni ya Rais au kwamba wajibu huo mwingine ni wa Rais;		
	(b) kila yanapotajwa madaraka ya kazi katika utumishi wa Serikali, ifahamike kuwa kazi inayohusika ni kazi		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	katika Utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Mungano isipokuwa kama imeelezwa vingine, na kila inapotajwa Idara ya Serikali ifahamike kuwa idara inayohusika ni idara ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, isipokuwa kama imeelezwa vingine;		
	(c) iwapo kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii kuna jambo lolote linalotakiwa litekelezwe au lishughulikiwe na chama chochote cha siasa, basi, jambo hilo litatekelezwa au litashughulikiwa na chama hicho kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa na chama hicho kwa ajili hiyo,		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na pia kwa kuzingatia masharti ya Katiba hii au sheria ya nchi iliyotungwa kwa ajili hiyo;		
	(d) mtu hatahesabiwa kuwa ana madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa sababu tu kwamba anapokea malipo ya uzeeni au malipo mengine ya aina hiyo kwa ajili ya utumishi wake wa zamani katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya zamani ya Zanzibar, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi la Polisi la Jamhuri ya Muungano na Idara ya Usalama wa Taifa		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	au;		
	(e) isipokuwa kama muktadha utaelekeza vinginevyo, kila anapotajwa mtu mwenye dhamana ya madaraka kwa kutaja madaraka yake, mtu anayehusika atakuwa ni pamoja na mtu yeyote ambaye ni Kaimu au aliyeteuliwa kihalali kushikilia dhamana ya madaraka hayo;		
	(f) kila yalipotajwa mamlaka ya kumwondoa mtu katika nafasi ya madaraka katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano, mamlaka yanayohusika ni pamoja na mamlaka		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yaliyotolewa kwa mujibu wa masharti ya sheria yoyote yanayomtaka mtu huyo au yanayomruhusu mtu huyo kustaafu:		
	Isipokuwa kwamba masharti haya hayatamhusu Jaji wa Mahakama ya Juu, Jaji wa Mahakama ya Rufani au Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; na		
	(g) kila ilipotajwa sheria ambayo inabadilisha au kufuta sheria nyingine, ifahamike kuwa sheria inayohusika ni pamoja na sheria ambayo inarekebisha sheria hiyo		

Tri Current Version
www.tri-nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	nyingine au ambayo inaendeleza kutumika kwa hiyo sheria nyingine, ama bila mabadiliko au baada ya kubadilishwa au kurekebishwa; au sheria ambayo inaweka masharti mapya katika sheria nyingine.		
Ibara ya 255: Jina la Katiba na kuanza kutumika.	(1) Katiba hii itaitwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014. (2) Katiba hii itaanza kutumika itakapozinduliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	Lengo la Ibara ni kubainisha jina na muda wa kutumika kwa Katiba husika.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kitaalam wa kuhakikisha kuwa jina la Katiba ya Nchi linatamkwa bayana ndani ya Katiba na tarehe ya kuanza kwake
Ibara ya 256: Kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inafutwa na, isipokuwa kwa masuala	Lengo la Ibara hii ni kufuta rasmi Katiba ya Jamhuri ya	Sababu ya mapendekezo haya ni kuendeleza utaratibu wa kikatiba

Trial Version
www.huance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
ya Mwaka 1977 Sura ya 2.	yaliyoelekezwa katika Masharti Yatokanayo, Masharti ya Mpito na Masharti ya Muda, haitakuwa na nguvu ya kisheria mara baada ya kuanza kutumika kwa Katiba hii.	Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 pamoja na kuweka Masharti ya Mpito na Masharti ya Muda.	wa Katiba Mpya kufuta Katiba iliyopo ili kuondoa uwepo au mgongano wa matumizi ya katiba mbili kwa wakati mmoja.
SURA YA KUMI NA SABA **MASHARTI YATOKANAYO NA MASHARTI YA MPITO**			
SEHEMU YA KWANZA - MASHARTI YATOKANAYO			
Ibara ya 257: Matumizi ya Baadhi ya Masharti ya Katiba Sura ya 2	(1) Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito yaliyoainishwa katika Sura hii ya Katiba yataanza kutumika tarehe ambayo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 itakapoanza kutumika.	Lengo la Ibara hii ni kuweka utaratibu wa kikatiba kuhusu matumizi ya masharti ya kipindi cha mpito na ukomo wa Katiba	Sababu za mapendekezo ni kuhakikisha kuwa, mabadiliko ya Katiba hayafuti uhalali wa sheria na maamuzi yaliyofanywa chini ya Katiba iliyofutwa na Katiba za

Final Version
www.kuanc.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(2) Kwa kuondoa shaka, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 itakuwa imefutwa na, isipokuwa kwa masuala yaliyoainishwa katika Sehemu ya Pili ya Sura hii, haitakuwa na nguvu ya sheria kuanzia tarehe ya kuanza kutumika kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014.	ya mwaka 1977.	awali zilizofutwa kabla ya hapo. Pia ni kuhakikisha kunakuwa na mwendelezo wa sheria zilizokuwepo kuendelea kutumika chini ya Katiba mpya.
SEHEMU YA PILI - MASHARTI YA KIKATIBA NA SHERIA ZA NCHI			
Ibara ya 258: Kuendelea kutumika Masharti ya Katiba.	(1) Masharti Yatokanayo na Masharti ya Mpito katika Sura hii ya Katiba na yale yaliyowekwa katika Mabadiliko ya "Sheria Maalum" ambayo bado yanaendelea kutumika katika Katiba zilizoainishwa katika Ibara hii,	Madhumuni ya Ibara hii ni Kutambua kikatiba Sheria na maamuzi yaliyofanywa katika katiba zote	Sababu za mapendekezo haya ni kuainisha na kuzipa uhalali Sheria zitakazoendelea kutumika baada ya Katiba mpya kupitishwa ili

Draft Version www.tuanze.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	yataendelea kutumika.	zilizofutwa kuwa halali chini ya Katiba mpya.	kuweka mwendelezo na uhakika wa utawala katika nchi.
	(2) Kwa madhumuni ya Ibara hii, "Sheria Maalum" maana yake ni "the Republic of Tanganyika (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1962, the Interim Constitution (Consequential, Transition and Temporary Provisions) Act, 1965, the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1977, the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1984 na "the Constitution (Consequential, Transitional and Temporary Provisions) Act, 1992".		
Ibara ya 259: Kuendelea	(1) Masharti ya sheria zilizoainishwa	Lengo la Ibara hii ni	Sababu ya mapendekezo haya ni

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kutumika Sheria za Nchi.	katika ibara ndogo ya (2) na ambazo zinatumika kabla ya tarehe ya kuanza kutumika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 zitaendelea kutumika kwa namna ambayo imeelekezwa katika Ibara hii. (2) Sheria za nchi ambazo: (a) zimetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 zitaendelea kutumika kwa madhumuni ya masuala yaliyoelekezwa katika sheria hizo; na	kuweka utaratibu wa kuendelea kutumika kwa sheria za nchi zilizotungwa ili kuweka mwendelezo wa sheria hizo na kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Serikali katika kipindi cha mpito cha utekelezaji wa Katiba ya sasa.	kuhakikisha kuna mwendelezo wa sheria na kuzipa uhalali kutumika baada ya Katiba mpya kupitishwa na kuanza kutumika.

TrialVersion
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(b) zimetungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambazo zinatumika Tanzania Bara zitaendelea kutumika Tanganyika kwa madhumuni ya masuala yaliyoelekezwa katika sheria hizo.		
	(3) Kwa madhumuni ya masharti ya ibara ndogo ya (2) wakati na baada ya Muda wa Mpito:		
	(a) sheria zote zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambazo zinatumika Tanzania Bara na Zanzibar na kwa kuzingatia marekebisho yatakayohitajika, zitakuwa sheria za nchi ambazo		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	zitatumika katika Jamhuri ya Muungano kwa Mambo ya Muungano;		
	(b) kwa kuzingatia mgawanyo wa Mambo ya Muungano na mambo yasiyo ya Muungano yaliyoelekezwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014, sheria zote zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambazo zinatumika Tanzania Bara na Zanzibar, kwa kuzingatia marekebisho yatakayohitajika, zitatumika Tanganyika na Zanzibar kwa mambo yasiyo ya Muungano hadi		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	hapo Tanganyika au Zanzibar itakapotunga sheria kuhusu mambo hayo; na		
	(c) sheria zote zilizotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano ambazo zinatumika Tanzania Bara na kwa kuzingatia marekebisho yatakayohitajika, zitakuwa sheria za nchi ambazo zitatumika Tanganyika.		
	(4) Bila kujali masharti ya ibara ndogo ya (3), Bunge la Jamhuri ya Muungano linaweza kutunga sheria yoyote kuhusu mambo ya Muungano na mambo yote yasiyo ya Muungano yanayohusu		

Draft Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Tanganyika hadi Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania litakapoundwa kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014.		
SEHEMU YA TATU - UTUMISHI WA UMMA			
Serikali ya Jamhuri ya Muungano			
Ibara ya 260: Kuendelea kuwepo kwa Rais madarakani.	Mtu aliyekuwa anashika nafasi ya madaraka ya Rais wa Jamhuri ya Muungano kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, ataendelea kushika nafasi ya madaraka ya Rais kwa masharti ya Katiba hii hadi mtu mwingine atakapochaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kushika nafasi ya madaraka ya Rais kwa mujibu wa Katiba hii.	Lengo la Ibara hii ni kumtambua Rais aliyepo kuwa anaendelea madarakani mpaka atakapomaliza kipindi chake cha Urais na Rais mwingine kuchaguliwa na kushika madaraka	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.

Trial Version www.nuta.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Ibara ya 261: Kuendelea kuwepo kwa Makamu wa Rais madarakani.	Mtu aliyekuwa anashika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, ataendelea kushika nafasi ya madaraka ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa masharti ya Katiba hii hadi Rais wa Jamhuri ya Muungano atakapochaguliwa katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.	Lengo ni kutambua kikatiba kuendelea kuwepo kwa Makamu wa Rais hadi Makamu wa Rais mwingine atakapochaguliwa na kushika madaraka hayo. Aidha, ni kurahisisha utekelezaji wa kazi na majukumu ya Makamu wa Rais katika kipindi ambacho Makamu wa Rais mwingine hajachaguliwa.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.
Ibara ya 262: Kuendelea kwa Waziri Mkuu, Mawaziri na Naibu	(1) Mtu anayeshika nafasi ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ataendelea kuwa katika nafasi ya madaraka hadi	Lengo la Ibara hii ni kuendelea kutambua kikatiba uwepo wa	Sababu ya mapendekezo haya ni kuhakikisha kuendelea kwa uongozi

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mawaziri.	Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 utakapofanyika na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ameshika madaraka. (2) Mtu anayeshika nafasi ya madaraka ya Waziri au Naibu Waziri ataendelea kushika nafasi hiyo ya madaraka hadi Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 utakapofanyika na nafasi hiyo ya madaraka itakoma saa ishirini na nne kabla ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuapishwa kushika nafasi ya madaraka ya Rais.	Waziri Mkuu, Waziri na Naibu Waziri katika kipindi cha mpito.	wa juu wa nchi uliopo mpaka Rais mwingine atakapopatikana kwa Uchaguzi Mkuu unaofuata.
		(a) Watumishi wa Umma	
Ibara ya 263: Kuendelea kwa Watumishi wa	(1) Kila mtu aliyeshika au kukaimu nafasi ya madaraka ya utumishi wa umma katika Serikali ya	Lengo la Ibara hii ni kutambua kikatiba	Kuweka masharti yatakayohakikisha haki za

Trial Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Umma.	Jamhuri ya Muungano, Bunge la Jamhuri ya Muungano au Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano kabla ya tarehe ya kuanza kutumika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014, ataendelea na atatambuliwa kuwa amechaguliwa, kuteuliwa au kuajiriwa kushika au kukaimu nafasi ya madaraka ya utumishi wa umma katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Bunge la Jamhuri ya Muungano au Mahakama ya Rufani ya Jamhuri ya Muungano na kwamba masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2014 au sheria za nchi kuhusiana na kuchaguliwa, uteuzi, ajira na kula kiapo au yamini yamezingatiwa na	kuendelea kwa Watumishi wa Umma waliopo katika utumishi wa umma baada ya Katiba Mpya kutungwa na kuanza kutumika.	Watumishi wa Umma zinalindwa kwa mujibu wa sheria na masharti ya kazi hizo kama ilivyokuwa kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

Final Version
www.iliance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutekelezwa.		
	(2) Kila mtu ambaye kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 au sheria za nchi, atahitajika kuondoka katika nafasi ya madaraka baada ya muda maalum kupita au atakapotimiza umri wa kustaafu ataacha kushika nafasi ya madaraka katika utumishi wa umma baada ya kufika mwisho wa muda maalum au atakapofika umri wa kustaafu.		
	(3) Masharti ya ibara ndogo ya (1) na (2), hayatatafsiriwa kwamba yanaondoa au kufifisha madaraka aliyonayo mtu au mamlaka imepewa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa		

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Tanzania ya mwaka 1977 au sheria za nchi kufuta nafasi ya madaraka na kumvua madaraka au kumwachisha kazi mtu anayeshika au kukaimu nafasi ya madaraka au kumtaka mtumishi wa umma kujiuzulu.		
	(4) Kwa madhumuni ya malipo ya kiinua mgongo au malipo mengine ya uzeeni, muda wa utumishi wa mtumishi wa umma anayehusika na masharti ya Ibara hii, utahesabika kuwa ni pamoja na muda wa utumishi aliokuwa nao kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014.		
	(5) Isipokuwa kama itaelekezwa vinginevyo, masharti ya kazi ya		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	mtumishi wa umma ambaye masharti ya Ibara hii yanamhusu hayatakuwa duni au hafifu ukiliganisha na masharti ya kazi aliyokuwa nayo kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 au sheria za nchi zitakazotungwa kwa ajili hiyo.		
SEHEMU YA NNE - BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO			
Ibara ya 264: Kuendelea kwa Ubunge na Uongozi wa Bunge.	(1) Kwa kuzingatia masharti ya ibara ndogo ya (2) na sheria za nchi kuhusu masuala ya uchaguzi wa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano na uchaguzi wa Spika, Naibu Spika na Viongozi wa Kamati za Bunge, Spika, Naibu Spika, Viongozi wa Kamati za Bunge na Wabunge wataendelea	Lengo la Ibara hii ni kutambua kuwepo kwa Uongozi wa Bunge, wabunge na Watumishi wa Bunge mpaka watakapomaliza kipindi chao.	Sababu ya mapendekezo haya ni kuweka masharti yatakayohakikisha haki za Uongozi wa Bunge na Wabunge zinalindwa kwa mujibu wa sheria na masharti ya kazi hizo kama ilivyokuwa kabla ya kuanza kutumika kwa Katiba Mpya. Kuhakikisha wananchi hawakosi kuwa na wawakilishi wao kwa

Final Version
www.iuanc.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kuwa Spika, Naibu Spika, Viongozi wa Kamati za Bunge na Wabunge, hadi Uchaguzi Mkuu mwaka 2015.		mujibu wa Katiba ya mwaka 1977.
	(2) Masharti ya Ibara ndogo ya (1) hayatatafsiriwa kwamba yanazuia kuondolewa kwa Spika, Naibu Spika, Viongozi wa Kamati za Bunge au Mbunge, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, Sheria ya Uchaguzi wa Taifa na Kanuni za Kudumu za Bunge.		
Ibara ya 265: Kuvunjwa kwa Bunge.	(1) Endapo, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 au sheria za nchi, jambo au suala lolote linahitaji kufanyika au linaweza kufanyika, jambo au suala hilo linaweza kufanyika	Lengo la Ibara hii ni kuwezesha kuitishwa kwa Bunge lililovunjwa wakati Bunge jipya halijaanza kazi	Sababu za mapendekezo ni kuruhusu kuitishwa kwa Bunge lililovunjwa wakati Bunge jipya halijaanza kazi, kutapelekea

Final Version
www.iuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	kutokana au kufuatia kuvunjwa kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.	pale panapohitajika.	Mhimili wa Bunge kuendelea kuwepo na kutekeleza jukumu lolote la dharura litakalojitokeza.
	(2) Ikiwa umuhimu wa kuliitisha Bunge utatokea kabla ya kutangazwa kwa matokeo ya Uchaguzi Mkuu ambao utafanyika baada ya kuvunjwa Bunge la Jamhuri ya Muungano:		
	(a) kwa madhumuni ya kuliitisha Bunge, Spika, Naibu Spika na Wabunge waliochaguliwa kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977, sheria za nchi na Kanuni za Bunge wanaweza kuitwa na watakuwa Spika, Naibu		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Spika na Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano litakaloitishwa; (b) kwa madhumuni ya uteuzi katika nafasi ya madaraka wakati Bunge limevunjwa, mtu anayeweza kuteuliwa sharti awe Mbunge, uteuzi unaweza kufanywa wa mtu ambaye alikuwa Mbunge kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Sheria za nchi zinazohusika.		
SEHEMU YA TANO - MAHAKAMA YA JAMHURI YA MUUNGANO			
Ibara ya 266: Kuendelea	(1) Mahakama ya Rufani ya Jamhuri	Lengo ni kuweka masharti ya	Sababu za mapendekezo haya ni

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
kwa Mahakama ya Rufani na Mahakama Kuu.	ya Muungano na Mahakama Kuu ya Tanzania Bara zitaendelea na zitakuwa na mamlaka ya kusikiliza mashauri na kutoa uamuzi au amri kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria za nchi. (2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), Majaji wa Mahakama ya Rufani na Majaji wa Mahakama Kuu watakuwa na madaraka ya kusikiliza mashauri, kutoa hukumu au amri kutokana na mashauri yaliyofunguliwa au yatakayofunguliwa katika Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu.	kikatiba yanayoelekeza Mahakama na Majaji wa Mahakama za Rufani na Mahakama Kuu kuendelea na kazi zao katika kipindi cha mpito	kuwezesha Mahakama kuendelea na kazi za utoaji haki wakati wa kipindi cha mpito na baada ya hapo.
Ibara ya 267: Kuendelea kwa Mashauri yaliyopo	(1) Shauri lolote ambalo halijakamilika au limekamilika katika Mahakama	Lengo ni kuweka utaratibu	Sababu za mapendekezo haya ni

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mahakamani.	ya Rufani au Mahakama Kuu litaendelea kusikilizwa hadi kukamilika; na hukumu, hati ya kukazia hukumu na amri iliyotolewa au itakayotolewa katika shauri hilo inaweza kutolewa na kutekelezwa na Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu. (2) Kwa madhumuni ya ibara ndogo ya (1), kila hukumu, hati ya kukazia hukumu na amri iliyotolewa na Mahakama ya Rufani au Mahakama Kuu ambayo haijatekelezwa kikamilifu kabla ya kufutwa kwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaweza kutekelezwa kikamilifu baada ya kuanza kutumika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka	wa kikatiba utakaoruhusu kukamilisha kusikilizwa kwa mashauri yaliyofunguliwa kabla ya Katiba Mpya kuanza kutumika.	kuhakikisha kuwa Mhimili wa Mahakama unaendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa haki kwa wananchi katika kipindi chote cha mpito na baada ya hapo. Sababu nyingine ni kuzuia kukata rufaa kwenye Mahakama ya Juu kwa mashauri yaliyotolewa uamuzi katika Mahakama ya Rufani kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1977. Aidha, ni kuondoa mgongano wa utekelezaji wa kazi

Final Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	2014.		za Makahama katika kipindi cha mpito.
	(3) Uamuzi wowote wa Mahakama ya Rufani uliotolewa kuhusu shauri lolote lililofunguliwa kabla ya kuanzishwa kwa Mahakama ya Juu kwa mujibu wa masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2014, hautakatiwa rufani katika Mahakama ya Juu.		
SEHEMU YA SITA - MASHARTI YA MPITO			
Ibara ya 268: Muda wa Mpito.	Muda wa Mpito utakuwa muda wote kuanzia tarehe ya kuanza kutumika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 hadi tarehe 31 Disemba, 2018.	Lengo la Ibara hii ni kuweka kikatiba utaratibu wa mchakato wa maandalizi ya Serikali na vyombo vyake, kuingia katika mfumo mpya wa utendaji	Sababu za mapendekezo haya ni kuifanya Serikali na vyombo vyake iendelee kutekeleza wajibu wake katika kipindi cha mpito cha miaka minne tangu kuanza kutumika kwa Katiba Mpya.

Trial Version www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
		kulingana na Katiba Mpya.	Mambo hayo yatatekelezwa hatua kwa hatua kwa mujibu wa mpango utakaopitishwa na Bunge Maalum au kuwekwa na Kamati ya Utekelezaji wa Katiba katika kipindi cha mpito ikionyesha mambo ya muda mfupi, mambo ya muda wa kati na yale yatakayo kamilika wakati wa ukomo wa kipindi cha mpito. Uzoefu wa nchi nyingine kama vile Kenya, Ghana na Uganda ibara za masharti ya kipindi cha mpito zimewekwa ndani ya

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
			Katiba yenyewe badala ya kutungiwa sheria tofauti kama yalivyokuwa mazoea ya Tanzania yaliyofanya watu wengi wasijue uwepo wa sheria hizo zikiwa sehemu ya Katiba.
Ibara ya 269: Utekelezaji wa Masharti ya Katiba Mpya.	(1) Mambo yafuatayo yatafanyika na kukamilika katika Muda wa Mpito: (a) kutungwa kwa Katiba ya Tanganyika; (b) kurekebisha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ili kuwiana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014;	Lengo la ibara hii ni kuweka katika Katiba mambo yatakayofanyika na kukamilika katika kipindi cha mpito.	Sababu za mapendekezo haya ni kuhakikisha masharti yaliyowekwa na Katiba Mpya yanatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Sababu nyingine ni kutoa muda wa utekelezaji wa hatua kwa hatua kwa masharti ya

Final Version
www.uiano.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	(c) mgawanyo wa rasilimali baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi Washirika;		Katiba Mpya.
	(d) kutunga na kurekebisha sheria mbalimbali za Nchi Washirika ili kuwiana na masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014;		
	(e) mgawanyo wa watumishi wa umma baina ya Serikali za Muungano na Serikali za Nchi Washirika;		
	(f) mgawanyo wa madeni baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali za Nchi		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	Washirika;		
	(g) kuundwa kwa Tume na taasisi za kikatiba zilizoainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014 na kwa kuzingatia masharti ya Katiba hiyo;		
	(h) kufanya uteuzi katika nafasi za madaraka kwa utaratibu ulioainishwa kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014;		
	(i) kufanya maandalizi na kuendesha Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2014;		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	na		
	(j) kufanya maandalizi na mambo yote muhimu kwa ajili ya utekelezaji bora wa masharti ya kikatiba yaliyomo kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 2014.		
	(2) Maoni ya wananchi yaliyokusanywa na Tume ya Mabadiliko ya Katiba yaliyotumika kuandaa Rasimu ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya mwaka 2014 yanaweza kutumika katika kuandika Rasimu ya Katiba ya Tanganyika.		
Ibara ya 270: Kamati ya Kusimamia muda wa	(1) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa masuala yanayohitaji kufanyiwa	Lengo la Ibara hii ni	Katika dhana mpya ya utungaji

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
Mpito.	kazi na kukamilishwa katika Muda wa Mpito, Rais atateua Kamati ya Utekelezaji wa Katiba katika Muda wa Mpito. (2) Kamati ya Utekelezaji wa Katiba itakuwa na: (a) Mwenyekiti; na (b) Wajumbe wengine wanane. (3) Sekretarieti ya Kamati ya Utekelezaji itaongozwa na Katibu na itakuwa na watumishi wa idadi inayotosha katika utekelezaji wa kazi ya kamati kwa ufanisi. (4) Uteuzi wa Mwenyekiti, Wajumbe na watumishi wa sekretarieti utazingatia uwakilishi wa kila	kuanzisha Kamati ya Utekelezaji wa Katiba itakayosimamia muda wa mpito na kuanzisha Sekretariati yake.	wa Katiba ni muhimu kuwa na Kamati ya utekelezaji wa Katiba nje ya Serikali na nje ya Bunge ili kuhakikisha matwaka ya Katiba na hasa yale yatokanayo na masharti ya muda wa mpito yanatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi. Uzoefu wa nchi nyingine umeonesha umuhimu wa kuwa na kamati ya utekelezaji wa katiba ili kuhakikisha mabadiliko yaliyoainishwa katika katiba mpya yanatekelezwa kwa ufanisi na

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	upande wa Jamhuri ya Muungano.		kwa muda uliopangwa.
Ibara ya 271: Kufutwa kwa Masharti yatokanayo na Masharti ya Mpito.	Baada ya kumalizika kwa Muda wa Mpito, masharti ya Sura ya Kumi na Saba yatakoma na hayatakuwa na nguvu ya kisheria.	Lengo la Ibara hii ni kuweka masharti ya kikatiba ya ukomo wa masharti yatokanayo na masharti ya mpito.	Sababu za mapendekezo haya ni kuweka ukomo wa kuendelea kutumika kwa masharti ya mpito na kuondoa utata unaoweza kujitokeza ili kuhakikisha kuwa, mambo yote yaliyoainishwa kufanyika katika muda huo yanatekelezwa kama yalivyopangwa na kukamilika kwa wakati.

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	NYONGEZA **[Imetajwa katika Ibara ya 63]** **Mambo ya Muungano**		
	1. Katiba na Mamlaka ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.		
	2. Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.		
	3. Uraia na Uhamiaji.		
	4. Sarafu na Benki Kuu.		
	5. Mambo ya Nje.		
	6. Usajili wa Vyama vya Siasa.		

Trial Version
www.nuance.com

IBARA	MAELEZO YA IBARA	MADHUMUNI NA LENGO	SABABU ZA MAPENDEKEZO
	7. Ushuru wa Bidhaa na mapato yasiyo ya kodi yatokanayo na Mambo ya Muungano.		

Trial Version
www.nuance.com